# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 23 Mei, 2016

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES J. MLOKA – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha mezani.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI:** Katibu!

**NDG. CHARLES J. MLOKA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo Mbunge wa Nsimbo, sasa aulize swali lake.

Na. 209

**Uchaguzi wa Madiwani katika Kambi ya Katumba**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza: -

Chaguzi za Madiwani zilifanyika katika kambi ya wakimbizi Katumba wa 2015:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha chaguzi za Serikali za Vijiji na Mtaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Katumba, Vijiji ambavyo havijafanya uchaguzi wa Vviongozi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2014 ni 14 na vitongoji 51. Uchaguzi ulishindwa kufanyika kwa sababu Kata hiyo ilikuwa ni kambi ya wakimbizi ambao walikuwa hawajapata uraia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuwapa uraia wananchi wa maeneo hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo inaendelea na maandalizi ya kufanya uchaguzi mdogo katika vijiji na vitongoji hivyo na tayari katika bajeti ijayo ya mwaka 2016/2017 zimetengwa sh. 3,300,000 ili kuwezesha zoezi hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Richard, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nifanye masahihisho kidogo ni Kata ya Katumba siyo Mtumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo ambayo ilikuwa ni makazi ya wakimbizi yalikuwa yanapata ufadhili wa Shirika la Wakimbizi Duniani *(UNHCR)* katika huduma mbalimbali za jamii ikiwemo elimu, maji na barabara. Ningependa kujua Serikali ina mpango gani wa kuhusisha *UNHCR* kwa kuwa makambi yanaenda kuvunjwa, msaada gani ambao watautoa ili kuboresha miundombinu mbalimbali ambayo sasa hivi imekuwa ni hafifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale awali kwamba maeneo haya uchaguzi bado haujafanyika, japo uchaguzi haujafanyika jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha katika maeneo hayo, wanaendelea kupata huduma za kijamii kwa ufanisi kama kawaida. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI jambo hilo tunaliangalia kwa karibu zaidi na kwa kuanza changamoto yetu kubwa ni kuisukuma bajeti hii ambayo sasa hivi imepitishwa kuhakikisha kwamba Halmashauri hii inafanya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni kuhakikisha kwamba, kwanza tunajua katika maeneo hayo huduma za kijamii nyingi zilikuwa zinatolewa na Shirika la Wakimbizi Duniani, sasa hivi ni jukumu la Serikali. Hili ni jukumu letu kubwa na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutapeana ushirikiano wa kutosha ili wananchi wa pale waweze kupata huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo miundombinu ya barabara, huduma ya elimu, huduma ya afya na ifike muda na wao wajione kwamba ni wananchi kama wananchi wengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge pale, swali la nyongeza!

**MHE. MWANNE I. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naitwa Mwanne Ismail Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, tatizo la Wakimbizi wa Katumba linafanana na tatizo la Wakimbizi wa Ulyankulu na kwa kuwa hawakufanya uchaguzi wa Madiwani. Je, Serikali inasema nini, ni lini utafanyika uchaguzi wa Madiwani katika Jimbo la Ulyankulu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hao ni wananchi wake, akiwa Mbunge wa Viti Maalum ana kila sababu ya kuona maeneo hayo yanafanyika uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka swali hili nilijibu katika Mkutano wetu wa Bunge uliopita, nilisema pale kuna takribani Kata tatu uchaguzi haujafanyika kwa sababu za msingi, bado suala zima la utengamano linaendelea na pale sasa hivi bado Jeshi na Wizara ya Mambo ya Ndani wanaendelea kumiliki eneo lile. Utararibu utakapokamilika jukumu letu kubwa watu wa TAMISEMI baada ya ule mtangamano kuwa vizuri zaidi na eneo lile sasa rasmi likishakuwa chini ya TAMISEMI, mchakato wa uchaguzi sasa utaendelea ili watu wa pale wajikute

nao wana Serikali yao halali iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi Namba 292. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la pili, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 210

**Ukarabati wa Barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ni sehemu ya ghala la chakula la Taifa katika mikoa mitano (5) inayolima chakula kwa wingi nchini Tanzania; lakini kikwazo kikubwa ni usafirishaji wa mazao kufikia masoko ya nje ya Wilaya; Halmashauri imeomba ongezeko la bajeti ya barabara kufikia shilingi bilioni 7,969,000 ili kuweza kukarabati barabara zote muhimu na kuwezesha wakulima kusafirisha mazao yao kwa urahisi na hatimaye kuongeza kipato cha Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe:-

Je, Serikali ipo tayari kukubali ombi la Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe la kuongeza fedha katika bajeti ya 2016/2017?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe iliandaa makisio ya bajeti ya shilingi bilioni 7.9 kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Hata hivyo, kutokana na ukomo wa bajeti, fedha zilizoidhinishwa ni shilingi milioni 920 ambazo zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara na ujenzi wa madaraja. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Halmashauri hiyo ilitengewa shilingi milioni 870 na tayari Serikali imepeleka shilingi milioni 157.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Barabara katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ni shilingi bilioni 247.5 ambazo endapo zingegawanywa sawa kwa kila Halmashauri zote 181 zilizopo, kila Halmashauri ingeweza kupata bajeti ya shilingi bilioni 1.3 tu. Hivyo, mara zote mahitaji yamekuwa ni makubwa kuliko uwezo wa rasilimali fedha kukidhi mahitaji hayo, ndiyo maana tunaweka vipaumbele ili kutekeleza mambo machache kwanza kulingana na uwezo

uliopo kibajeti. Serikali itaendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya barabara kadri uwezo utakavyowezekana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba bajeti iliyopita walitenga milioni 870, lakini ni milioni 157 tu ndiyo zimepelekwa. Je, haoni umuhimu wa kuhakikisha pesa iliyobaki inapelekwa.

Swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Rungwe imepata mafuriko na uharibifu wa barabara umekuwa mkubwa sana, naomba Wizara hii itutumie pesa za haraka kwa ajili ya *emergency* kwa ajili ya vijiji kama tisa zaidi ya kilometa 40; kama Kijiji cha Kyobo, Ikuti na sehemu za Lupepo. Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka pesa hizo haraka kwa ajili ya kusaidia barabara na madaraja yaliyoharibika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika majibu yangu ya msingi nilisema bajeti ilikuwa ya shilingi milioni 870, zilizopelekwa mpaka sasa ni shilingi milioni 157, jibu hili nimekuwa nikilitoa kila mahali katika vipindi mbalimbali. Nilisema wazi, ukiachia changamoto ya ujenzi wa barabara, lakini kuna miradi mingi kipindi kilichopita ilikuwa haiendi vizuri. Nilitolea mifano miradi ya maji na miradi mingineyo kwamba upelekaji wa pesa ulikuwa ni tatizo kubwa sana, lakini kulikuwa na sababu zake za msingi. Katika mwaka uliopita pesa nyingi sana zilienda katika matukio makubwa ambayo yalikuwa yamejitokeza kama suala la uandikishaji na uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchakato wa hivi sasa, Serikali imejielekeza zaidi katika ukusanyaji wa mapato, ndiyo maana hivi sasa hata ukiangalia kwa mara ya kwanza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imevunja rekodi katika ukusanyaji wake wa mapato. Nilisema kwamba hata miradi iliyokuwepo mwanzo imesimama, lakini hivi karibuni miradi hiyo inapelekewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yetu ni kwamba, katika kipindi hiki cha bajeti kilichobakia nina imani Serikali itajitahidi kupeleka fedha katika miradi yote iliyosimama nikijua wazi katika maeneo hayo mengine wakandarasi ambao ni wa ndani na wengine wa nje wanaendelea kudai. Kwa hiyo, suala hili tunaweka kipaumbele siyo kwa ajili ya maeneo hayo tu isipokuwa kwa Tanzania nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafuriko na kuharibu miundombinu ya barabara, hili nilisema ni kweli. mwaka huu ukiangalia maeneo mbalimbali tumekuwa na changamoto ya mvua kubwa iliyonyesha. Nimetolea mfano kule Rungwe, ukienda Kyela, ukienda Kilosa na maeneo mbalimbali, yote yameathirika kwa ajili ya mvua na ndiyo maana tulipeleka utaratibu kwamba kila Halmashauri ianishe uharibifu wa miundombinu mara baada ya mvua ile kunyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu kubwa ni kuangalia sasa kile ambacho tunaweza kusaidia kwa kipindi cha sasa. Kwa hiyo, baada ya uharibifu huo, Serikali itachukua jukumu la kusaidia siyo maeneo ya Rungwe peke yake, isipokuwa maeneo mbalimbali ambayo yameathirika na nafahamu hata maeneo ya Morogoro hali ilikuwa mbaya sana na maeneo mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tizeba.

**MHE. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kweli, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa tu kujua baada ya Halmashauri zetu kuleta haya maombi na ilikuwa katika matarajio yetu kwamba uharibifu huu usikutane na msimu mwingine wa mvua kwa sababu uharibifu utakuwa mkubwa zaidi na bajeti tuliyoipitisha inaweza ishindwe kukidhi hayo mahitaji. Sasa, labda ni lini tu Mheshimiwa Waziri watatuona kabla mvua hazijaanza tena hasa sisi tunaotoka kwenye maeneo ya misimu miwili ya mvua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini naomba niseme kwamba hapa siwezi kusema kesho au keshokutwa, kwa sababu tunachofanya ni *needs assessment*. Tuna Halmashauri zipatazo 181, kila Halmashauri ina changamoto yake ya jinsi gani miundombinu ya barabara imeharibika. Kwa hiyo, wataalam wetu wanalifanyia *assessment* katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikopita maeneo mengine ni kweli huo uharibifu umekuwa wa kiwango kikubwa sana. Hivi sasa wananchi wengine wanashindwa hata kufika katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, jukumu letu kubwa ni ku-*fast truck* hii *process* ili angalau kitakachopatikana kidogo tuweze kugawana ili wananchi waweze kupata huduma kwa kipindi hiki cha sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa kwa niaba.

Na. 211

**Askari Kuboreshewa Makazi yao**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. DEVOTHA M. MINJA)** aliuliza:-

Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza wanaishi katika nyumba chakavu zisizokuwa na hadhi ukilinganisha na kazi zao wanazofanya kwa jamii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaboreshea makazi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yalivyowahi kujibiwa maswali kama haya ndani ya Bunge lako Tukufu mara kadhaa kuhusu Askari kuboreshewa makazi yao, Serikali inafahamu kuwa lipo tatizo la baadhi ya Askari wa Jeshi la Magereza na Polisi kuishi katika nyumba chakavu zisizokuwa na hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hili Serikali imeendelea na mpango wa kuzifanyia ukarabati mkubwa baadhi ya nyumba kwenye baadhi ya magereza na kujenga nyumba mpya. Mahitaji ya nyumba hivi sasa ni nyumba 14,500 wakati zilizopo ni 4,221 hivyo kuwepo kwa upungufu wa takribani nyumba 10,279 ambao unalazimisha baadhi ya Askari wa Magereza kuishi nje ya kambi za jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Magereza limesaini mkataba na kampuni ya *Poly Technologies* ya China kwa kujenga nyumba 9,500 kwenye vituo vyote vya magereza nchini. Mgawanyo wa ujenzi wa nyumba hizo ni Makao Makuu Magereza nyumba 472, Mkoa wa Arusha nyumba 377, Dar es salaam 952, Dodoma 356, Kagera 364, Kigoma 272, Kilimanjaro 390, Lindi 233, Manyara 206, Mara 378, Mbeya 622, Iringa 336, Morogoro 669, Mtwara 215, Mwanza 398, Pwani 384, Rukwa 358, Ruvuma 320, Shinyanga 337, Singida 299, Tabora 408, Tanga 382, KMKGM Dar es Salaam 219, Chuo cha Ukonga 115, Chuo cha Kiwira 183, Chuo cha Ruanda 62, Chuo cha KPF 27, Bohari Kuu 82 na Bwawani 84. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Polisi, Serikali inakusudia kujenga nyumba 4,136 katika Mikoa 17; hii Mikoa 17 tunayozungumzia, tafsiri yake ni kwamba Mikoa 15 ya Tanzania Bara na Mikoa mitano ya Zanzibar, wameichukulia Unguja na Pemba kama Mkoa kitu ambacho siyo sahihi. Kwa hiyo usahihi wake ni kwamba Mikoa 15 ya Tanzania Bara na Mikoa 5 ya Zanzibar inafanya kuwa Mikoa 19 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimeona nifanye marekebisho kwa sababu mara nyingi tumekuwa tukizungumza hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kutatua changamoto za uhaba wa nyumba kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo mikopo yenye riba nafuu, miradi shirikishi na kwa kutumia fedha za bajeti ya Serikali kadri hali ya uchumi itakapokuwa ikiimarika. Mkakati huu unakwenda sambamba na mipango ya maendeleo ya Serikali ikilenga kufikia idadi ya nyumba za makazi kwa askari wote waliopo sasa na watakaoajiriwa baadaye. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu ambayo tumeyapata kwa swali hili, kidogo yana mchanganuo ambao unafaa tofauti na mara ya mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza. Dhiki katika Jeshi la Magereza ni uzembe kwa sababu kwa maoni yangu Jeshi hili ni Jeshi tajiri, Jeshi hili lilikuwa na Gereza la Kilimo Songwe ambalo lilikuwa linafanya kazi vizuri sana, Gereza la Karanga lilikuwa na kiwanda kizuri sana cha viatu, Gereza la Ukonga lilikuwa na kiwanda kizuri sana cha nguo; lakini *tender* zinatolewa kununua nguo za Magereza na za Polisi, *tender* zinatolewa kununua viatu vya Polisi na Magereza. Kwa nini, Serikali isiboreshe viwanda vya Jeshi hili, ili Jeshi likafanye biashara na likaweza kutatua matatizo yake pamoja na matatizo ya nyumba na hata kuisaidia Serikali, badala yake inatoa kazi ambazo Jeshi hili linaweza likazifanya kwa watu wengine. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, nashukuru kwa mchanganuo uliotolewa. Naomba kumuuliza Waziri, kwa kuwa Askari Magereza katika Jimbo langu pale Rombo wanaishi katika nyumba zinazoitia aibu Serikali kwa kweli, wanaishi kwenye mabanzi. Je, Waziri yupo tayari kuandamana na mimi akakague nyumba hizo na kwa sababu hiyo, hizi zilizotengwa 390 angalau chache zianze kujengwa Rombo kwa ajili ya kunusuru makazi ya wale Askari pale Rombo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza limepanga kuongeza uzalishaji wa mapato ya kilimo, ushonaji na ufugaji. Kwa hiyo, msingi wa swali lake kwamba Jeshi la Magereza limezembea siyo sahihi, kuna mipango kabambe tu ya kuhakikisha kwamba Jeshi la Magereza linajitegemea kwa chakula, lakini pia linaendeleza ujuzi na rasilimaliwatu ilizokuwa nazo katika kuhakikisha kwamba linachangia juhudi za Serikali za kuweza kuifanya sekta ya viwanda kuchukua sehemu kubwa katika uchumi wa nchi yetu katika miaka inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia utaratibu huo Jeshi la Magereza limeandaa andiko ambalo linaainisha miradi minane. Uzalishaji wenye matokeo makubwa ya haraka *(quick win projects)* na limeshawasilishwa Serikalini ili kuweza kupata fedha. Miradi hiyo ambayo ni ya kokoto Msalato; unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama Mbigili na Ubena; uzalishaji wa mafuta ya alizeti Ushora, Kongwa na Msalato; ushonaji wa viatu Ukonga na Karanga Moshi ambako ni kwa Mheshimiwa Selasini. Halafu kuna mradi wa samani ambao uko Arusha; kilimo cha umwagiliaji Idete Morogoro na kuimarisha kikosi cha ujenzi ili kiweze kumudu na kufanya kazi kubwa za ukandarasi.

Pia Jeshi hilo limeandika mpangokazi wa kujitosheleza kwa chakula ambalo pia limeshawasilishwa Serikalini ili kupata fedha za uendeshaji. Kwa hiyo, Jeshi linatekekeza sera ya uwezeshaji kwa kuingia ubia pia na taasisi mbalimbali binafsi kupitia utaratibu wa *PPP* ili kupata mitaji ya kuongeza uzalishaji. Mpaka sasa Jeshi limeshaingia ubia na kampuni ya *Tabin* ya Uturuki kwa ajili ya kutekeleza kilimo cha mpunga Gereza la Kigongoni. Pia limeainisha maeneo yenye madini na kupata leseni ya uchimbaji karibu 181, hatua za kutangaza maeneo hayo kwa ajili ya uwekezaji zinafanywa. Hilo nadhani lilikuwa ni swali lake la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ametaka kujua kuhusiana na Kilimanjaro. Kilimanjaro tuna aina mbili, mbali ya ile miradi ambayo nimeizungumza, kuhusiana na huo ujenzi wa nyumba 3,500, lakini pia kuna utaratibu ambao Jeshi la Magereza linaenda nao, kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo husika. Kwa Mkoa wa Kilimanjaro tayari nyumba karibu 38 zimejengwa kupitia mradi huo. Kinachofanyika ni kwamba tunatumia rasilimali za nguvukazi zilizopo jeshini pamoja na ujuzi tulionao kuweza kujenga nyumba hizi kufikia katika *level* ya kuezeka halafu baadaye kupitia fedha za bajeti tunafanya *finishing*. Kwa hiyo, kupitia utaratibu huo kwa Mkoa wa Kilimanjaro tumeshajenga nyumba 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kuambatana na Mbunge wakati wowote kwa ajili ya kwenda kuhakikisha kwamba tunatembelea miradi hii na mipango mingine ambayo atakuwa nayo Mheshimiwa Mbunge na

tutashirikiana kwa pamoja. Tunapenda Wabunge wa aina yake ambao wako tayari katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwaarifu kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa nje ya nchi kwa safari ya kikazi kuanzia leo Jumatatu tarehe 23 Mei, 2016, kwa wakati wote ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu hatakuwepo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Katiba na Sheria atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Harrison Mwakyembe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali lingine, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo sasa aulize swali lake.

Na. 212

**Kuongezeka kwa Vifo Vinavyotokana na Ajali za Barabarani**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Kwa miaka ya hivi karibuni vifo vya Watanzania kutokana na ajali za barabarani vimekuwa vingi na kuleta hisia kwamba hali hii sasa ni janga la Kitaifa, ni muhimu Watanzania wakafahamu kwa takwimu kuhusu ukubwa wa tatizo la vifo na majeruhi kutokana na ajali za barabarani badala ya kusikia taarifa ya tukio moja moja:-

(a) Je, takwimu ni zipi na mchanganuo wa matukio kuanzia mwaka 2013 hadi 2015 Kitaifa na Mikoa miwili inayoongoza na yenye ajali chache?

(b) Je, mfumo gani endelevu kama upo, wa wazi ambao Serikali inatumia kutoa takwimu hizi kwa Watanzania badala ya taarifa moja moja pindi inapotokea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 zilitokea ajali 23,842 zilizosababisha vifo karibu 4,002 na majeruhi 20,689. Mwaka 2014 kulitokea ajali 14,260 zilizosababisha vifo 3,760 na majeruhi 14,530 na mwaka 2015 zilitokea ajali 8,337 zilizosababisha vifo 3,464 na majeruhi 9,383.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa ambayo imeongoza kwa ajali kwa mwaka 2013 ni Mikoa ya Kipolisi ya Kinondoni, ambao ulikuwa na ajali 6,589 na Mkoa wa Kipolisi wa Ilala ambao ulikuwa na ajali 3,464 na mkoa ambao ulikuwa na ajali chache ilikuwa ni Simiyu ambao ulikuwa na ajali 67 na Tanga ajali 96. Mwaka 2014 mikoa iliyoongoza kwa ajali ni Mikoa ya Kipolisi Kinondoni ambapo ajali zilikuwa ni 3,086 na Mkoa wa Kipolisi wa Ilala ulifuata kwa kuwa na ajali 2,516. Mikoa ambayo ilikuwa na ajali chache kwa mwaka huo ilikuwa ni Kagera ambayo ilikuwa na ajali 29 na Simiyu ajali 55. Mwaka 2015 Mkoa wa Kipolisi ya Ilala ajali 1,431 na Temeke ajali 1,420 ambayo ndiyo iliyokuwa inaongoza kwa mwaka huo. Mikoa ambayo ilikuwa na ajali chache kwa mwaka 2015 ni Mkoa wa Rukwa ambao ulikuwa na ajali 53 pamoja na Mkoa wa Arusha ambao ulikuwa na ajali 53.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo endelevu wa wazi uliopo wa kutoa takwimu za kupitia taarifa za mwaka za Jeshi la Polisi *(Police Annual Reports)* ambapo kila Mtanzania anaweza kupata taarifa hizo za ajali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oscar, swali fupi la nyongeza.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa idadi ya karibu vifo 12,000 vilivyosababishwa na ajali za barabarani kwa miaka hiyo mitatu vinaweza kulinganishwa na mauaji ya kimbari, mauaji ya halaiki, na majeruhi 44,444 ni sawa na kiwanda cha kutengeneza Watanzania kupata ulemavu wa viungo mbalimbali. Je, Serikali inatueleza nini kuhusu kuja na suluhisho lenye mashiko na kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa ajali za barabarani hasa za mabasi ya abiria zinashiriki sana kwenye kutengeneza vifo na majeruhi, tena kwa kiwango kikubwa kwa mara moja, Je, Serikali ina mkakati gani pia kudhibiti ajali za barabarani zinazohusisha mabasi ya abiria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mipango na mikakati mbalimbali ya muda mrefu na muda mfupi. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, tunajaribu kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Pia Jeshi la Polisi kupitia Askari wa Usalama Barabarani wamekuwa wakifanya doria za mara kwa mara na ukaguzi ili kuweza kuwabaini na kuwakamata wale ambao wanavunja sheria. Pia kumekuwa na utaratibu wa kutumia zile kamera za tochi ambazo zinabaini wale ambao wanakiuka taratibu za usalama barabarani ikiwemo kuongeza kiwango cha *speed* zaidi ya kilichowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa pia tukiangalia mchakato wa kuangalia utaratibu wa utoaji leseni vile vile ili kudhihirisha kwamba kwa kushirikiana na mamlaka nyingine watu wote ambao wanaendesha vyombo vya moto barabarani basi wawe ni ambao wana leseni zilizopo kisheria na isiwe kuzipata kinyemela. Pia kuna utaratibu wa kuchukua hatua stahiki kwa wanaovunja sheria siyo tu wale ambao wanaendesha vyombo hivi, hata wasimamizi wa sheria hizi mara moja inapotokea kutaka kulitia madoa Jeshi la Polisi basi hatua zimekuwa zikichukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mifumo ambayo tumejaribu kuanza nayo sasa hivi, mifumo ya matumizi ya *point* ambayo bado haijaanza ipo katika utaratibu mzuri, nadhani muda siyo mrefu sana tutaweza kutumia ili kuwafanya sasa watu wawe na hofu zaidi ya kuvunja sheria hizo za barabarani. Pia kuna utaratibu wa tozo za papo kwa papo na hii imesaidia sana kiasi fulani kudhibiti ajali hizo. Tuna utaratibu wa kutumia TEHAMA kwa ajili ya kudhibiti ajali za barabarani. Pia tuna mipango, maana alitaka mipango ya sasa hivi na baadaye, tunayo mipango ya matumizi ya kamera ambayo nayo vile vile ipo katika michakato na ukaguzi wa lazima kwa magari yote. Kwa hiyo, hizo ni baadhi ya hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua katika Jeshi la Polisi kupitia kitengo cha Polisi cha Usalama Barabarani kudhibiti hali ya ajali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi fulani imepungua, na ndiyo maana ukiangalia kwenye takwimu nilizozisoma kwenye swali la msingi utakuta ajali za barabarani zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Lyimo, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na sababu ambazo Mheshimiwa Waziri amezizungumza, naamini kabisa baadhi ya ajali, tena ajali nyingi sana zinatokea kwa sababu ya kutokuwa na alama barabarani pamoja na matuta makubwa sana. Tulishasema hapa Bungeni matuta yawe na *standards*. Ni lini Serikali itafanya matuta nchi nzima yawe ya *standard* ili kuepusha ajali ambazo siyo za lazima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kudhibiti ajali barabarani ni suala ambalo ni mtambuka linahusisha taasisi mbalimbali. Kwa mfano, suala ambalo Mheshimiwa Suzan Lyimo amelizungumza ni la msingi, ambalo kwa upande wa Serikali linahusisha Wizara ya Ujenzi na ndiyo maana tukawa na mkakati kabambe wa kushirikisha wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda muafaka utakapofika tunaweza tukauanika mpango huu, tupo katika hatua nzuri ambapo tuna ushirikiano mzuri na *SUMATRA*, Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS, TBS* na shule za udereva pamoja na Polisi, tunakaa pamoja ili tuweze kuwa na utatuzi wa kudumu wa matatizo ya ajali kwa kuunganisha nguvu kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe tu wasiwasi kwamba mambo hayo tunayafanyia kazi na wakati muafaka utakapofika basi tutauweka hadharani.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe sasa aulize swali lake.

Na. 213

**Ndege Zinazoendeshwa na Rubani Mmoja**

**MHE KHALIFA MOHAMMED ISSA** aliuliza:-

Imekuwa ni kawaida kwa ndege ndogo zenye uwezo wa kubeba abiria kumi hadi kumi na sita kuendeshwa na rubani mmoja bila ya kuwa na msaidizi na rubani kama binadamu anaweza kukumbwa na hitilafu yoyote kiafya na kushindwa kumudu kuongoza ndege:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuruhusu ndege kuongozwa na rubani mmoja ni sawa na kuyaweka rehani maisha ya abiria?

(b) Je, sheria za nchi yetu na zile za Kimataifa zinasemaje juu ya ndege ya abiria kurushwa na rubani mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zinazoongoza fani ya kuendesha ndege hapa nchini huongozwa na miongozo inayokubalika Kimataifa na ambayo imeridhiwa hapa nchini na Bunge. Katika taratibu hizo kuna matakwa ya kisheria na kiufundi ambayo yakifuatwa yanawezesha kuwa na uwezekano mdogo sana wa marubani kukumbwa na athari ya kiafya na kushindwa kumudu kuendesha ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marubani hupimwa afya zao na Madaktari Bingwa kila muda maalum kulingana na umri kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 140 mpaka 177 ya *The Civil Aviation Personnel Licensing Regulations,* 2012. Hivyo basi, Serikali inaruhusu ndege kuendeshwa na rubani mmoja kwa kuzingatia taratibu hizo. Aidha, Kanuni ya 32(5) inasema kwamba ndege iliyoandikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuruka kwa shughuli za kibiashara yenye uzito unaozidi kilo 5,700 itakuwa na marubani wasiopungua wawili.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za usalama wa anga nchini zinaongozwa na Sheria Namba 80 *(Civil Aviation Act)* na Kanuni zilizotengenezwa chini yake. Aidha, urushaji wa ndege yenye abiria tisa au zaidi unaongozwa na Kanuni ziitwazo *The Civil Aviation Operation of Aircrafts Regulations,* 2012 ambapo ndege inayotimiza vigezo vilivyowekwa kwenye vifungu Namba (2), (3) na (4) vya Kanuni ya 32 kuwa na uzito wa chini ya kilogramu 5,700 inaruhusiwa kuendeshwa na rubani mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika viwango vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO)* kwenye kiambatisho Namba 19 chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Usafiri wa Anga wa Chicago, hakuna kiwango chochote kinachobainisha wazi kuwa ndege yenye uwezo wa kubeba abiria 10 au zaidi ni sharti iendeshwe na marubani wawili. Pia, hakuna hata mapendekezo ya kiutekelezaji *(recommended practice)* kwenye suala hilo. Aidha, kiambatisho cha sita chenye sehemu tatu kinachohusisha uendeshaji wa ndege *(operations of aircrafts)* ambacho ndicho kinachozungumzia idadi ya marubani katika uendeshaji wa ndege hakuna katazo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa, swali fupi la nyongeza.

**MHE KHALIFA MOHAMMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na jawabu refu sana la Mheshimiwa Naibu Waziri, bado nina maswali mafupi mawili ya nyongeza. Swali la msingi lilikuwa ni *risk*, kuweka rehani roho za abiria. Hii haijalishi ukubwa wa ndege, ubebaji wa abiria wachache au wengi. Jawabu ilikuwa rubani kabla ya kurusha ndege, au vipindi kwa vipindi wanafanyiwa *check-up*.

Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni binadamu katika maumbile yake unaweza kumfanyia *check up* sasa hivi lakini akifika pale hali yake ikawa na mgogoro. Je, haoni kwamba bado suala ni kuweka rehani roho za abiria?

Swali la pili, pamoja na *treaties* nyingi za Kimataifa na kuridhiwa na Bunge, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kulisimamia hili na kukawa na ulazima maalum wa ndege yoyote ya abiria kuweza kuongozwa na rubani zaidi ya mmoja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *risk* inapimwa. Katika eneo hili sheria tulizo nazo za kimataifa ambazo nchi yetu imeziingiza katika sheria zetu na Bunge hili limeidhinisha, hiyo *risk* imepimwa kwa uzito wake na ndiyo maana ni aina fulani tu za ndege zinazobeba abiria kiwango fulani zinazoruhusiwa kuendeshwa na rubani mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuna marubani maalum wanaoruhusiwa kuendesha ndege usiku na wakati ambapo huwezi ukaona uwanja ulivyo, ni aina fulani tu ya marubani ambao wamepitia kozi maalum zinazozingatia leseni za *IFR (Instruments Flights Rules)*. Ndege zile ambazo zinatumia *CFR* ambazo ni kwa marubani ambao hawaja-*qualify* sana hazihitaji masharti hayo na kwa kawaida hawaruhusiwi kuendesha usiku au kwenye kipindi ambacho mawingu ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la afya, ambalo ndilo swali lake la msingi Mheshimiwa Mbunge, nadhani ukiweka hata marubani watatu, wanne, Mwenyezi Mungu kama afya hiyo hakubali nadhani siyo *solution* na ndiyo maana upimaji wa kila mwaka na kwa wale ambao wanarusha ndege za kimataifa za kibiashara upimaji wa kila baada ya miezi sita ni wa lazima. Ndugu zangu niwaambie, na niwaombe Wabunge wote tupime afya zatu. Tukiwa tunapima afya zetu kila wakati *risk* ya kupata labda *pressure* au nini ni ndogo sana. Wataalam wetu wanaotupima tuwaamini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zungu, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na rubani kuwa mmoja na *risk* za ndege hizi zimewekwa kwa mazingira kwa Rubani mmoja anaweza kurusha hizi ndege kwa kitalaam, lakini liko tatizo la baadhi ya viwanja vyetu kutokuwa na mitambo ya *Precision Approach Path Indicator,* kutokuwa na mitambo ya *Visual Approach Slope Indicator* na hizi ni kwa Rubani licha ya kuwa anayo mitambo ya *Eye Rescue* ya ndege yake, lakini anahitaji *Visual Support.*

Je, Serikali sasa itafanya nini kuhakikisha *System* hizi za taa, *visually* kumsaidia Rubani kuweza kutua, kuokoa maisha ya watu na kumuokoa yeye mwenyewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna baadhi ya viwanja vyetu vina matatizo ya vifaa, lakini Serikali tumejipanga kuhakikisha viwanja vyetu vyote ambavyo vinatumika kwa sasa

hivi viwe na vifaa vya kisasa kuhakikisha kwamba kuna usalama wa kutosha kwa ajili ya abiria wetu wanaosafiri katika viwanja hivyo vya ndege.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 214

**Ujenzi wa Barabara ya Nyololo- Mtwango**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Upembuzi yakinifu wa barabara ya kutoka Nyololo hadi Mtwango yenye urefu wa kilomita 40 umefanyika mwaka 2013/2014:-

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa barabara ya Nyololo - Igowole hadi Kibao ilikamilika mwaka 2014 yakiwa ni maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *TANROADS,* itaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka wakati taratibu za kutafuta fedha za kuijenga kwa kiwango cha lami zinaendelea na ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo imeelekeza hii barabara katika ukurasa wake wa 61.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola swali fupi la nyongeza.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, hii barabara ni ya muhimu sana na ni ya miaka mingi sana na bahati nzuri sana hata Naibu Waziri wa Ujenzi mwaka 2015 alifika kule Mufindi na alifanya mikutano miwili na aliwaambia wananchi kwamba, baada ya kumaliza uchaguzi hii barabara itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kufuatana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea viwanda, viwanda kule tayari viko, kuna kiwanda cha Kibwele pale, kuna kiwanda cha Kilima *Factory,* kuna kiwanda cha Lugoda *factory,* hivi ni Viwanda vya Chai na vinategemea hii barabara. Mheshimiwa Waziri aniambie kwa sababu upembuzi yakinifu walishamaliza na Serikali iliahidi na Chama cha Mapinduzi kimeahidi kwamba kitaweka kiwango cha lami. Ni lini hizi fedha zitapatikana na wataanza kujenga kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi walishaambiwa tayari kuna nyumba zao zilishawekewa alama ya *X* na wanatarajia kuhama! Je, Serikali ni lini itaenda kutoa fidia kwa wale ambao walijenga nyumba jirani na barabara na Serikali ilisema itawalipa fidia kwa mfano, wananchi wa Kijiji cha Nzivi, Igowole, Kibao, Mtwango na pale Lufuna, kuna nyumba ziliwekewa *X*, Serikali itaenda kuwalipa lini ili waanze kuhama?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Tunapoongelea ujenzi ni pamoja na fedha za fidia pamoja na fedha za ujenzi wenyewe. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama ambavyo barabara hii ipo katika ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020, namhakikishia ahadi hiyo itatekelezwa, asiwe na wasiwasi!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saumu Sakala, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa tatizo la barabara lipo nchi nzima na katika Jimbo letu la Pangani pia tatizo hili la uharibifu wa barabara limekuwa ni sugu. Licha tu ya barabara inayounganisha Wilaya ya Pangani na mikoa mingine kuwa mbovu, lakini pia barabara zinazounganisha vijiji na vijiji zimekuwa mbovu kiasi ambacho kipindi cha mvua hazipitiki kabisa. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha barabara zile zinapitika kipindi chote cha mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itahakikisha ubora wa hizi barabara unaongezwa na unaimarishwa na tutaweka mipango maalum kuhakikisha magari makubwa ambayo mara nyingi ndiyo yanayoharibu barabara hizi hayataruhusiwa kupita katika barabara ambazo haziruhusu kupita magari yenye kiwango fulani cha *tonnage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hii anayoiongelea iko katika Ilani yetu na tutaendelea kuiimarisha na nichukue fursa hii kuwaomba au kuwaelekeza *TANROADS,* Mkoa wa Tanga kuhakikisha kwamba, kama ambavyo tuliwapa

maelekezo kufungua barabara zingine na hii wahakikishe inafunguliwa na maeneo hayo yote yaliyoharibika yatengenezwe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Habari, Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 215

**Serikali Kuongeza Uwezo wa Kurusha Matangazo Kituo cha TBC- Songea**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

Wananchi wa Tarafa za Hagati, Mbuji na Mkumbi hawapati matangazo ya Redio ya *TBC* kutokana na Kituo cha *TBC*- Songea kutokuwa na uwezo wa kurusha matangazo na badala yake wanapata matangazo ya redio toka nchi jirani ya Malawi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza uwezo wa kurusha matangazo ya kituo cha *TBC*- Songea ili wananchi wa Tarafa hizo wapate habari kupitia *TBC*?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martin Alexander Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matangazo ya Radio ya Taifa kupitia mtambo wa masafa ya kati yaani *Medium Wave* yenye nguvu ya Kilowati 100 yalikuwa yakisikika vizuri katika Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Ruvuma wakati mtambo huo ulipokuwa ukifanya kazi. Tangu mwezi Julai, 2013 mtambo huo haufanyi kazi kutokana na uchakavu na hivyo kuathiri usikivu wa matangazo ya *TBC* katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa wananchi kupata matangazo, *TBC* ililazimika kuhamisha mitambo yake miwili ya Radio yenye uwezo wa Kilowati moja kwa kila mmoja iliyokuwa imefungwa eneo la Mshangano - Songea na kuifunga eneo la juu la mlima wa Matogoro (Songea) ili angalau usikivu wake usambae eneo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufunga mitambo hiyo, matangazo ya *TBC*- Songea yameboreshwa. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo wa mitambo ya *FM* inayotumika kwa sasa mawimbi yake ya sauti hayafiki mbali

sana ukilinganisha na yale ya mitambo ya *Medium Wave* iliyokuwa ikitumika wakati wa awali ambayo yanafika eneo kubwa zaidi la Mkoa wa Ruvuma zikiwemo Tarafa za Hagati, Mbuji, na Mkumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kukabiliana na changamoto za usikivu hafifu katika maeneo kadhaa Mkoani Ruvuma, *TBC* imeshafanya upembuzi yakinifu wa kufunga mitambo ya *FM* yenye uwezo wa kilowati moja katika eneo la Mbamba Bay lililopo Wilaya ya Nyasa ili kuongeza usikivu wa redio na *TBC*. Katika bajeti ya mwaka wa 2016/2017, Wizara yangu imetenga fedha za maendeleo kwa ajili ya kufunga mtambo eneo la Mbamba *Bay*. Kazi hiyo ya uboreshaji wa matangazo katika eneo hilo itaanza mara tu fedha za kununua na kufunga mitambo zitakapotolewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martin Msuha, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa umbali wa kutoka Songea na Mamba Bay - Nyasa bado ni mrefu, Serikali haioni haja ya kufunga mitambo angalau kwenye milima ya Mbuji ili kuongeza usikivu katika tarafa hizo zilizotajwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upembuzi uliyofanyika, huu mtambo utakaofungwa Mbamba Bay utakuja kukutana na mtambo uliofungwa hapa Matogolo na kwa pamoja usikivu utaongezeka badala ya kufunga kwenye Kata ya Mbuji kama anavyosema. Ni upembuzi wa Kitaalam umefanyika na hili likifanyika tutaongeza usikivu katika eneo lake na kwa sababu ni matokeo ya utafiti tunaamini hili likifanyika basi hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayaombea hapa yatakuwa yamefanyika na usikivu utaongezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa, swali fupi la nyongeza.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *TBC* na Radio ya Taifa ndiyo visemeo vya Serikali. Je, wakati mnaboresha mitambo, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapeleka wafanyakazi wa *TBC* na Radio ya Taifa kwenda nje kujifunza ili kusudi waendane na teknolojia ya sasa, kuwapeleka nje kwenda kusoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Ndassa kwa kazi nzuri anayofanya ya kutetea tasnia ya habari kwa sababu na yeye mwenyewe ana *background* ya habari. Pili *TBC* imekuwa na mipango mizuri ya kuwapeleka wafanyakazi wake kwenda kuongeza ujuzi wao nje ya nchi, lakini pia na kuwaalika Wataalam mbalimbali kuja hapa kwa ajili ya kuongeza ujuzi wao. Mfano mzuri, wenzetu wa China wamekuwa wakitusaidia sana, wafanyakazi wengi wanakwenda kujifunza. Hata hivi tunapoongea wako wafanyakazi ambao wanaongeza ujuzi wao China, lakini tunao Wachina ambao wako hapa kupitia ushirikiano wa *TBC* na *Star Times,* nao wanaongeza ujuzi wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini *program* hizi zitaendelea na tutaendelea kuziboresha mara kwa mara ili wafanyakazi wetu waendane na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani.

**MWENYEKITI:** Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 216

**Hitaji la Viwanda vya Kusindika Mazao- Mkoa wa Simiyu**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Vijana wengi wa Mkoa wa Simiyu hawana ajira kutokana na ukosefu wa viwanda mkoani humo na Serikali ilitunga Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda vya kusindika mwaka 1996-2020 itakayosimamia maendeleo ya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya mazao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda vya kusindika mazao katika Mkoa wa Simiyu?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipaumbele vya Serikali hadi mwaka 2020 ni kuhimiza wawekezaji kujenga viwanda vinavyotumia malighafi za ndani hususan kwenye Sekta ya Kilimo na Maliasili, viwanda vinavyozingatia fursa za kijiografia, viwanda vinavyotoa ajira kwa wingi na vile vinavyochochea ujenzi wa viwanda vingine. Kwa sasa Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika maeneo hayo. Aidha, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda kwa kuzingatia

vipaumbele tajwa ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo malighafi ya kutosha inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, tushirikiane kubaini fursa za uwekezaji katika viwanda, tuhamasishe wawekezaji na tuweke mazingira mazuri kwa wawekezaji popote nchini ikiwemo Mkoani Simiyu. Uwekezaji tunaoulenga hasa ngazi za vijiji mpaka wilayani ni ujenzi wa viwanda vidogo sana, viwanda vidogo na viwanda vya kati. Hili ndilo tabaka la viwanda linalotoa ajira kwa wingi, lakini tabaka linaloweza kusambaa kwa urahisi toka mijini mpaka vijijini. Mafanikio ya jukumu hili yanahitaji ushirikiano mkubwa kuanzia ngazi ya vijiji mpaka mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Kurugenzi ya Viwanda na Biashara ndogo pamoja na Taasisi za *SIDO, TANTRADE, TBS* na *EPZA* tuko tayari kushirikiana na mamlaka za Mkoa wa Simiyu ili kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa viwanda watakavyobaini na vile vilivyoahidiwa na viongozi wakuu wa Taifa hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Kwa kuwa vijana ni nguvu kazi ya Taifa, je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo na kuwawezesha vijana wa Mkoa wa Simiyu, wajasiriamali mitaji ya uhakika na kuwatafutia masoko nje ya nchi, ambapo itapunguza ukosefu wa ajira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu swali la Mheshimiwa Mbunge limekuwa mahususi naomba nitoe maelekezo yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, awasiliane na Meneja wa *SIDO* wa Mkoa wa Simiyu, atambue kikundi cha Vijana ambao wanatabia ya ujasiriamali, wataelekezwa biashara ya kufanya na katika mkopo wa *NDF* unaokuja watatengewa fedha kusudi tuwalee na kusudi mje mnipime kwa mwaka mmoja ujao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, akina mama lishe na akina baba lishe pale Temeke wanakaribia kufilisika toka tatizo la bei ya sukari kupanda lilivyoanza! Hawakushawishika kupandisha bei ya vyakula wanavyouza kwa sababu walitegemea tatizo hili la sukari litakuwa ni la muda mfupi, lakini mpaka leo hawajui ni lini tatizo hili litakwisha. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna umuhimu wa yeye kila siku kutoa *status update* ya sukari hapa nchini kila tunapoingia hapa Bungeni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru akinamama lishe kwa kuwa watumishi wa Mungu. Hawana hulka ya kutafuta faida wanatoa huduma, watafurahi duniani na mbinguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la msingi ni kwamba Mwijage nitoe *status* ya sukari, kila siku nakubali kabla hatujaahirisha mchana huu nitatoa *status* ya mgao wa sukari kwa nchi nzima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali fupi la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, swali la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Maswa imekwishatenga eneo zaidi ya heka 110 na tumekwisha kuandika barua kwa *EPZA* kuja kuwekeza Maswa. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini atatusaidia Maswa, *EPZA* kuja ku-*facilitate* maeneo ya uwekezaji ili tuweze kukaribisha wawekezaji kwa maana ya kuwekeza viwanda vidogo vidogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Maswa kama Wabunge wengine ambao wamejitolea kutoa maeneo yao ili kusudi kujenga viwanda vidogo lakini na *Special Economic Zone*. Naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa *EPZA* watafute hii barua ya Maswa, waende Maswa na Mkurugenzi wa *SIDO* wabainishe ni kitu gani kinachoweza kufanyika pale na wanipe jibu ili kusudi nimridhishe Mbunge kabla ya Bunge hili kumalizika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa James Millya Kinyasi, Mbunge wa Simanjiro, naomba sasa swali lake aliulize!

Na. 217

**Soko la Tanzanite Wilayani Simanjiro**

**MHE. JAMES K. MILLYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza wazo la kuanzisha mradi wa *EPZ* ambao umetengewa eneo kwenye Mji mdogo wa Mererani ili kuwezesha kuwepo kwa soko la *Tanzanite* Wilayani Simanjiro ambalo linadhibiti utoroshwaji wa madini ya *Tanzanite* na kuwapatia vijana wetu ajira?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Millya Kinyasi, Mbunge wa Simanjiro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara umetenga eneo lenye ukubwa wa hekta 530.87 kwa ajili ya matumizi ya *EPZ* katika Kijiji cha Kandasikra - Mererani, Wilayani Simanjiro. Pamoja na kwamba juhudi za kutenga eneo hilo zilianza mwaka 2007, bado halikuwa tayari kwa uendelezaji kutokana na taratibu za kuhamisha miliki ya ardhi kuchukua muda mrefu. Taratibu hizo zimekamilika mwezi Julai, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji pia ulichangiwa na kuchelewa kulipwa kwa fidia kwa wananchi sita ambao walikuwa hawajafanyiwa uthamini waliokuwa wanadai jumla ya shilingi milioni 15.05. Mamlaka ya *EPZ* kupitia Halmashauri ya Simanjiro ilifanikiwa kulipa fedha hizo tarehe 31 Machi, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa eneo hilo lipo huru na hivyo taratibu za uendelezaji, ikiwemo kuandaa mpango kabambe wa uendelezaji wa eneo hilo *(Master Plan)* na hatimaye kuanza ujenzi wa miundombinu wezeshi kama barabara, umeme, maji, mifumo ya maji machafu, majengo ya huduma zitafanyika. Maandalizi hayo ya ujenzi wa miundombinu yatafanyika sambamba na uhamasishaji wa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kuwekeza katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Ni masikitiko makubwa kwamba kwa miaka takribani miwili, shilingi milioni 15 imezuia kuanzishwa kwa *EPZ* iliyotarajiwa na Serikali. Mwanzoni mwa mwaka huu mwezi wa Pili, kilo mbili za *Tanzanite,* kilo mbili Waheshimiwa Wabunge ni takribani bilioni mbili, siyo kama *gold,* zilikuwa zinaibiwa kutoroshwa nje ya nchi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba uulize swali fupi tafadhali!

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kujenga nchi hii, msitukimbize!

**MWENYEKITI:** Sawa, lakini kwa mujibu wa Kanuni inabidi uulize swali fupi la nyongeza.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mafupi mawili ya nyongeza. Wahindi hawa wanaoshirikiana na baadhi ya Watanzania waliolelewa na Wahindi walikuwa wanatorosha madini ya *Tanzanite* nje ya nchi, je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi kwamba *EPZ* hii itaanza kujengwa Simanjiro ili madini yetu yasije yakatoroshwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza, Mheshimiwa Rais wakati akifungua Bunge hili alisisitiza kuhusu madini haya, Mheshimiwa Waziri juzi wakati akihitimisha hoja yake alisema kuna matatizo makubwa ya *Tanzanite*. Naomba nitoe takwimu, mwaka 2014…

**MWENYEKITI:** Tafadhali, swali tu, hakuna takwimu. Naomba kama umemaliza Mheshimiwa Waziri ajibu.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali; mwaka 2014, dola za Kimarekani milioni 300 za *Tanzanite* zilitoroshwa India, Kenya milioni 100, lakini Tanzania ikauza milioni 38, je, ni lini Serikali ya Tanzania itakuwa makini ili kuwasaidia Watanzania kunufaika na madini yao, na wachimbaji wadogo kama akina Chusa, wachimbaji wadogo kama akina Onee watanufaika na rasilimali hii kubwa waliyopewa na Mungu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuligeuza eneo la Mererani *Special Economic Zone* na mojawapo ya kuweka eneo lile huru la kiuchumi ni kudhibiti ile malighafi au maliasili inayozalishwa pale. Sasa ninachofanya kwa mamlaka niliyopewa, natafuta wawekezaji kama nilivyosema, ili waje pale watengeneze eneo ambako madini yale na madini mengine yatakuwa yanauzwa pale. Tayari ninao wawekezaji watakaobadilisha Mji ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, wamenipa hekta 500, nataka hekta 1000 nyingine zaidi zifike hekta 1,500. Nitatengeneza *Special Economic Zone,* namwagiza Katibu Mkuu anayeshughulikia uwekezaji wale wawekezaji ambao wanataka kuwekeza Arusha waje Bungeni wafanye *demonstration* yao ili watu wa Kanda ya Kaskazini muweze kuona wenyewe, niwaachie mzigo ninyi mshindwe kutoa ardhi inayotakiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 218

**Tatizo la Maji Mkoa wa Songwe**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Tatizo la maji ni changamoto kubwa sana katika Mkoa wa Songwe na Wilaya zake zote:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondolea adha ya maji wanawake wa Mkoa huu hususan Mji Mdogo wa Tunduma ambako hali ni tete zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua adha kubwa ya tatizo la maji inayowakabili wananchi wa Mkoa wa Songwe hususan wanawake. Katika mpango wa muda mrefu wa uboreshaji wa huduma ya majisafi Mkoa wa Songwe, Serikali imekamilisha usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni kwa ajili ya kuboresha huduma ya majisafi katika Miji ya Mkoa wa Songwe ikiwemo Vwawa ambako ni Makao Makuu ya Mkoa, Itumba, Isongole pamoja na Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha za kutekeleza mradi huo kutoka kwa wafadhili mbalimbali. Kwa sasa Serikali imewasilisha maombi katika Benki ya Maendeleo ya Ufaransa ya kupata mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza mradi wa majisafi Mjini Tunduma. Pia Serikali imewasilisha maandiko ya miradi ya majisafi kwa Miji ya Vwawa na Tunduma kwenda Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kwa ajili ya kutafuta fedha za kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji kwa Miji ya Vwawa na Tunduma, Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya upanuzi wa mfumo wa usambazaji wa maji katika miji hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba usanifu umekamilika katika Miji ya Isongole, Vwawa pamoja na Tunduma, lakini nisikitike kusema kwamba neno usanifu umekamilika bado haliwezi kuleta matumaini kwa akina mama wa Mkoa wa Songwe ambao wanapata shida kubwa sana ya maji. Kwa hiyo, napenda kuomba Mheshimiwa Waziri aniambie kwamba ni lini mradi huo utaanza katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili la nyongeza kama tunavyojua Mkoa wetu wa Songwe ni mkoa mpya na lengo la kuleta Mkoa mpya ni kusogeza huduma karibu na wananchi. Huduma mojawapo ni huduma ya maji ili akinamama wale wa Mkoa wa Songwe waweze kupata huduma kama inavyostahili. Hata hivyo, nioneshe masikitiko yangu makubwa kwamba mpaka sasa, hasa…

**MWENYEKITI:** Naomba uulize swali tafadhali!

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza. Kwa maeneo ambayo ni ya pembezoni, mfano kule Ibaba, Ileje, ukienda Mkwajuni Wilaya ya Songwe, ukienda Iwula, ukienda Kamsamba bado miundombinu ya maji haijakaa vizuri. Naomba kupata jibu la Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini Serikali itajenga miundombinu mizuri ya maji, hasa kwa maeneo ambayo ni ya pembezoni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wake na kwa sababu ni Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum nafikiri wananchi hawakupoteza kura zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameniuliza maswali mawili ya nyongeza, ni lini miradi hii iliyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itaanza. Kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba, tayari sasa hivi Serikali inafanya majadiliano na wafadhili kwa ajili ya kupata mikopo ya masharti nafuu. Hii

miradi ni mikubwa, uwezo wa Serikali tunaendelea lakini bado siyo mkubwa sana kiasi cha kuweza kutekeleza miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba kuna Miji ya Mkoa wa Songwe, Mkoa ni mpya, kuna maeneo mengi bado hayajapata huduma ya maji. Serikali inaendelea, tumeanza programu ya kwanza ya maendeleo ya maji mwaka 2006/2007, programu ya kwanza ya miaka mitano imekwisha mwaka 2015 Disemba. Sasa hivi tumeanza programu ya pili, kwa hiyo ile miradi ambayo haikukamilika, miradi ambayo haikuanza katika awamu ya kwanza, basi tutaianza na kuikamilisha katika awamu ya pili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umemalizika, kwa hiyo sasa naomba niwatangaze wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza, ni Mgeni wa Mheshimiwa Cecil D. Mwambe ambaye ni Padre P. Haule kutoka Jimbo la Katoliki la Mtwara. Padre Haule, karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 45 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline S. Mabula ambao ni wanafunzi na Walimu kutoka *Loreto Girls High School.* Karibuni wanafunzi wetu, pia hao wameambatana na wanafunzi wa *UDOM* wanaotoka Jimbo la Ilemela Mkoa wa Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni 50 wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Mheshimiwa Mashimba Ndaki ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kutoka Mkoa wa Shinyanga. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia H. Mwakagenda kutoka *TGN* Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Tumaini Msauge *(Program Officer)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 13 kutoka Shirika la Ndugu Wafransisko Wakapuchini *(Roman Catholic)* kutoka Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Amina Molel, baadaye Mheshimiwa Maria Kangoye na Mheshimiwa Zacharia Issaay ajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kwanza na mjadala.

**MBUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel!

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara ya Ardhi, kwa sababu mimi pia ni miongoni mwa wananchi ambao wanaguswa na migogoro ya ardhi nikitokea katika jamii yangu ya Wamasai. Kwa hiyo, moja kwa moja naomba nigusie baadhi ya maeneo ambayo kwa namna moja au nyingine yamechangiwa na migogoro hii, hasa kutokana na kwamba Serikali ama viongozi husika kutokuvalia njuga migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya mambo ambayo kwa namna moja au nyingine yamechangia sana migogoro baina ya wafugaji na wakulima ni Sheria ya Utambuzi wa Mifugo ya mwaka 2010 ambayo inashindwa kutambua wafugaji wa asili na hasa katika maeneo yao husika. Pia Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 na yenyewe pia imekuwa ikizuia mifugo katika maeneo ya wanyamapori ilhali maeneo hayo siku za nyuma yalikuwa ni wazi kabisa kwa ajili ya wafugaji na wafugaji hawa walikuwa hawabugudhiwi na kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine pia ni hizi sheria ambazo ni nyingi, mfano Sheria ya Mazingira ya mwaka 2007 na yenyewe pia kwa sababu inaainisha kuwa ufugaji wa asili ni moja ya vyanzo vya uharibifu wa mazingira, hii pia imechangia kuwepo kwa migogoro baina ya wafugaji na wakulima. Maeneo mengi yaliyokuwa yakitumika na kutambuliwa na wafugaji,

nakumbuka tangu nikiwa mdogo maeneo hayo wafugaji walikuwa wakiyatumia na wafugaji hawa wamekuwa wakilisha mifugo yao na kumekuwepo na amani baina ya wafugaji na wakulima, hakukuwepo na migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu sheria hii sasa haiwatambui wafugaji na haithamini ile mifugo yao na kuona kwamba mifugo hii ya asili ni chanzo cha uharibifu wa mazingira, sheria hizi zimekuwa zikichangia migogoro hiyo na kwa sababu haitambui imekuwa ni chanzo cha uharibifu huu au migogoro hii baina ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba yapo maeneo mengi ambayo yametengwa, migogoro hii pia inachangiwa na baadhi ya viongozi, viongozi wa Kiserikali, viongozi wa kisiasa, viongozo wa kimila, viongozi wa kidini, wote hawa wamekuwa wakichangia migogoro hii. Kwa mfano, katika Ranchi ya Manyara ambayo hata wakati huo akiwa Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamini Mkapa, eneo hili la Ranchi ya Manyara lilitamkwa wazi kwamba litumike kwa ajili ya mifugo, lakini mpaka leo hii baadhi ya viongozi wa kisiasa wamekuwa wakilitumia hili eneo na kuwanyima hata wafugaji ambao na wenyewe wanatoka katika jamii hiyo, kuwazuia kulisha mifugo yao na hata wakati mwingine maeneo haya ambayo mifugo inatakiwa ipite na kwenda kunywa maji imekuwa ni shida pia.  Hili ni  eneo la Ranchi ya Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wanasema kwamba kabla ya kutoa kibanzi kwenye jicho la mwenzako, ni vema basi ukatoa boriti kwenye jicho lako. Ijumaa, miongoni mwa walichangia hapa na hasa nizungumzie eneo la Monduli ambako mwaka jana nilipata bahati ya kuzunguka katika Kata zote katika Uchaguzi Mkuu, yapo baadhi ya maeneo ambayo baadhi ya viongozi wenyewe kama nilivyosema wamechangia, lakini pia hata viongozi wengine hao ambao tunaowatarajia na …

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge jamani naomba muongee taratibu, tumsikilize mchangiaji.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na tunapokuja huku tukitarajia kwamba wao ndio faraja kuweza kuishauri Serikali ndiyo wamekuwa hao wanaochangia migogoro. Mfano katika Milima ya Nanja, mmoja wa viongozi ambao wakati huo alikuwa ni Diwani wa CCM na kwa hivi sasa yuko upande wa pili, ameuza eneo hili la Mlima Nanja na hivi sasa eneo hilo linatumika kwa uchimbaji wa kokoto na eneo hili limeuzwa pasipo ridhaa ya wananchi wenyewe. Kwa hiyo, wakati mwingine tunapozungumzia kuhusiana na hii migogoro, ni vema na pia tukajiangalia, je, tumechangia kwa kiasi gani, tumetatua migogoro kwa kiasi gani ili basi tuweze kuwanyooshea vidole wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi katika Wilaya ya Monduli na hasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye mamlaka husika kwa jitihada zake, ambapo Februari na Machi mwaka huu, aliweza kufika Wilayani Monduli katika ziara yake na kufuta baadhi ya vibali 13 vya mashamba ambayo yalikuwa yametelekezwa na mashamba hayo kugawiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona kwamba pamoja na kwamba jitihada hizi zipo, lakini bado tuiombe Serikali yenyewe ili iweze kushughulikia migogoro hii ambayo imekuwa ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na viongozi hao kama nilivyosema, baadhi yao viongozi wa Kiserikali, vile vile viongozi wa kisiasa ambao wamehodhi maeneo makubwa na matokeo yake wananchi wanapata shida ya kuweza kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Wilaya ya Arumeru ambako hasa ndiko huko ninakotoka, yapo mashamba makubwa na hayo mashamba, mfano shamba la *Gomba Estate* na kwa bahati nzuri katika moja ya nakala tulizopewa na Mheshimiwa Waziri yameorodheshwa. Mashamba haya tangu tunakua yamehodhiwa na ukienda hata kwa hivi sasa mashamba haya hayatumiki, wananchi wa kule hawana maeneo wakati mwingine ya kulima na hata juzi tu wananchi moja ya mashamba ambayo yapo katika maeneo hayo ya Malalua, maeneo ya Gomba walijikatia baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vema kama hawa wafanyabiashara au hawa ambao wamehodhi maeneo haya hawawezi kuyamiliki, nafikiri ni vema kabisa huu utaratibu ukaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wanapewa mashamba haya ili waweze kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mashamba haya na hasa ukizingatia mfano kwa Mji wa Arusha ambao kila siku umekuwa ukipanuka. Mji huu na maeneo mengi sasa yamekuwa ni maeneo ambayo wananchi wengi nao wanazidi kuvamia na bado yamehodhiwa na hawa watu ambao hawaitendei haki Serikali. Mheshimiwa Waziri kwa dhamana aliyonayo kama alivyofanya katika Wilaya ya Monduli namwomba pia afike katika maeneo ya Vijiji vya Mlangarini afike katika maeneo ya vijiji, Kata ya Manyire ili aweze kufuta baadhi ya vibali hivi ambavyo vinawakosesha wananchi wetu haki ya kumiliki ardhi, vilevile inawakosesha wananchi wetu kupata maeneo kwa ajili ya kulisha mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda katika Jiji la Dar es Salaam, katika Jiji hili la Dar es Salaam na hasa tukikumbuka mvua za mwaka 2011/2012 ambazo zilileta maafa kwa kiasi kikubwa, Serikali kwa wakati ule iliwatafutia eneo la Mabwepande na wananchi wakaweza kupewa viwanja ingawa bado wako wengine ambao wamerudi tena katika bonde la Msimbazi, wamerudi katika

mabonde ya Mkwajuni, tuangalie kwamba sheria hizi wapo kweli ambao wameshalipwa, lakini wapo kweli ambao miaka nenda miaka rudi wapo maeneo hayo. Tuangalie ni kwa jinsi gani Serikali inaweza kuwasaidia ili kuepusha migogoro hii ambayo kwa namna nyingine imekuwa ikikosesha amani wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba tunafahamu umuhimu wa ardhi, kila mmoja wetu anatambua thamani ya ardhi na ardhi imekuwa ikipanda thamani kila leo. Ili kuepusha migogoro hii ya ardhi, tusiwasubiri wananchi mpaka wanajenga, wanamaliza kujenga halafu bado wanapelekewa huduma zote muhimu, utakuta umeme wamepelekewa ,matokeo yake baadaye wanakuja kubomolewa. Hii inakuwa ni kero kwa wananchi na wananchi wanakosa imani na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu Mheshimiwa Waziri na kwa sababu ameingia katika Wizara hii na ameanza vizuri, hebu naomba arekebishe pia hata hao watendaji ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakisababisha migogoro hii ya ardhi kwa kutoa vibali maeneo ambayo siyo halali kujenga, matokeo yake pia wananchi wamekuwa wakijenga na baadaye wanakuja kuwabomolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nimwombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba, kwanza nimtie moyo kwa kazi nzuri anayoifanya na aendelee kufuta mashamba haya ambayo yamekuwa ni kero na hasa ukizingatia kule Bwawani pia kule Lucy mashamba haya yapo namwomba afike pia katika Kata ya Nduruma ufike pia huko Lucy ufute hivi vibali ili wananchi waweze kumiliki ardhi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina, tunaendelea na Mheshimiwa Maria Kangoye na baadaye Mheshimiwa Zacharia Issaay ajiandae.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu asubuhi hii ya leo, nikushukuru wewe pia kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu wake Dkt. Angelina Mabula kwa kazi nzuri wanayofanya, niwape pole kwa changamoto nyingi wanazokumbana nazo ndani ya Wizara hii, kwani zipo nyingi zikiwemo zile za migogoro ya ardhi ambazo zimekuwa ni za muda mrefu na zenye kuhitaji hekima na busara katika kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *gender sensitivity* nipende kumshukuru na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kumteua mwanamama Dkt. Angelina Mabula kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Baada ya salamu hizi naomba nijielekeze katika kuchangia hotuba iliyoko mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina hekta milioni 88.6 za nchi kavu na kati ya hizo ni hekta milioni 60 ambazo ni mbuga na zina uwezo wa ku-*accommodate* ufugaji. Pamoja na kuwa na eneo kubwa la kututosheleza bado kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na migogoro hii imekuwa ikisababisha ulemavu vifo, upotevu wa mali lakini hata wananchi kuhama makazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua jitihada ya Wizara hii katika kutatua migogoro hii lakini naiomba Serikali ikae itafakari, itafute mbinu mbadala na rafiki kutatua matatizo haya. Hata pale inapowezekana ishirikishe wazee wa kimila katika kuwashawishi wakulima na wafugaji kutumia maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli zao. Niishauri Serikali kutengeneza mifumo ya kuzuia kuliko kutengeneza mifumo ya kupambana baada ya matatizo haya kufumuka. Kubwa zaidi niishauri Serikali kuhakikisha inafanya utafiti ili iweze kujua vyanzo halisi vya migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaisihi Serikali kuona haja ya kutambua ufugaji wa asili katika Sera ya Taifa ya Ufugaji ya mwaka 2006, kwani ufugaji huu umekuwa ukichangia asilimia 7.4 ya Pato la Taifa. Kikubwa ni kutengeneza mfumo madhubuti kuhakikisha kwamba ufugaji huu haugeuki kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Sheria ya Ardhi kumekuwa na changamoto kubwa ya wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha wa sheria hiyo, kumekuwa na tafiti nyingi ambazo zimebainisha kwamba wananchi wanaoishi katika ngazi za msingi hususani vijijini wakiwemo wanawake, wakiwemo wafugaji, wachimbaji wadogo na wakulima wamekuwa wakikosa haki katika kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi zipo mila ambazo zinamkandamiza mwanamke katika kumiliki ardhi, mila hizi zimekuwa zikimwaminisha mwanamke kwamba yeye ni wa kuolewa na kusubiri kurithi ardhi kutoka kwa mume wake. Hii tumeona changamoto yake kwamba, yapo baadhi ya makabila yanasadikika kwamba wanawake wao wanawaua waume zao ili waweze kurithi mali. Hii imekuwa ikiwanyima wanawake haki ya kupata, kutumia na kudhibiti ardhi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweke mpango mkakati wa kutoa elimu ya Sheria hii ya Ardhi katika ngazi ya vijiji ili wananchi waweze kujua haki zao katika kumiliki ardhi. Kama Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 za mwaka 1999 zinavyoainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wawekezaji na ardhi; kumekuwa na tatizo la wawekezaji kuhodhi maeneo makubwa ya ardhi na baadhi yao wamekuwa wakitumia sehemu ndogo tu ardhi hiyo, wapo ambao hawajaendeleza kabisa maeneo hayo na kusababisha mapori katikati ya vijiji na mara nyingi mapori haya yamekuwa yakitumika na wahalifu kama maeneo ya kujifichia. Vijana wa Kitanzania wana uhitaji mkubwa wa ardhi ili kuweza kufanya shughuli za kiuchumi, tukumbuke kwamba vijana hawa wa Kitanzania wamelelewa katika mila na desturi za Kiafrika ambapo mali zote ikiwemo ardhi ni za baba, hata pale wanapojitahidi kwenda shule na kuhitimu vyuo vikuu bado wanakuwa hawana fursa kubwa ya kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara hii isitengeneze utaratibu wa kuwagawia maeneo ya ardhi vijana ili nao waweze ku-*contribute* katika uchumi wa nchi yetu. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumepunguza tatizo ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara la wananchi kuvamia maeneo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu wa kumiliki ardhi, kumekuwa na mlolongo mrefu katika umilikishaji wa ardhi, aidha kwa kupata cheti cha hakimiliki ya kimila ama kwa kupata hati. Hii imesababisha wawekezaji kukosa uvumilivu na kukimbilia katika nchi ambazo zina unafuu katika kumilikisha ardhi. Mlolongo huu mrefu umesababisha Watanzania kuwa wavivu wa kumiliki ardhi kihalali na kwa namna moja au nyingine tumekuwa tukiikosesha Serikali yetu mapato yanayotokana na ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 37(a) inasisitiza kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi. Napenda kuiomba Serikali hii iweze kutekeleza Ilani hiyo ili kuweza kumsaidia Mtanzania kuweza kumiliki ardhi ndani ya muda mfupi. Hili linawezekana kama tu tukiziwezesha Halmashauri zetu za Wilaya kuajiri vijana wa kutosha na Wizara ijikite zaidi katika kampeni nyingi zikiwemo zile za upimaji wa ardhi kuanzia ngazi za Vijiji mpaka za Miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha napenda kuikumbusha Serikali kwamba ilikuja Wilayani kwetu Magu Jimbo la Mheshimiwa Kiswaga ikaomba eneo kwa ajili ya kujenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya wananchi. Napenda kuwataarifu kwamba eneo hilo tayari lipo tunawasubiri tu ninyi mje muwekeze ili wananchi wetu waweze kunufaika kwa kupata nyumba bora kwa bei nafuu. Hata Wilaya ya Maswa Mkoani Simiyu tayari wameshawatengea eneo, tena

eneo lipo halihitaji hata fidia ni kazi kwenu kuja kujenga nyumba hizo ili wananchi waweze kupata nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, napenda kuungana na wenzangu wote kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo fupi hapa linatoka kwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza. Katibu wa Wabunge wote wa CCM, anawaomba Wabunge wote wa CCM kuhudhuria kikao kifupi cha dakika 15 mara baada ya kuahirishwa Bunge katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Zacharia Issay. Mheshimiwa Yussuf Salum na Mheshimiwa Joshua Nassar wajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi anavyofanya kazi kubwa ya kulitumikia Taifa letu na hususani katika kukemea yale yote ambayo yanakinzana na matakwa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza sana mpendwa ndugu yetu Mheshimiwa William Lukuvi kwa kazi kubwa aliyofanya kule Mbulu. Nampongeza sana namwombea kwa Watanzania wote na kazi anayofanya kwa nchi yetu ni kubwa kwa dakika hii ya sasa na jinsi ambavyo ardhi ni eneo lenye matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kuiasa Serikali, mara nyingi tumepata matatizo mengi hasa yale yanayotokea baada ya wananchi kujenga, wananchi wanapimiwa na Maafisa wa Serikali katika maeneo ya hifadhi na maeneo ambayo hayafai kwa makazi, baadaye Serikali inaenda kubomoa bila hata fidia. Naiomba Serikali ianze kuainisha maeneo yote ambayo hayafai kwa matumizi mbalimbali ya wananchi wetu yakiwemo yale ya mikondo ya maji na yale ambayo ni hatarishi kwa maisha yao ili kuepuka hasara kubwa na matatizo mbalimbali yanayotokea baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwataka watu wa barabara na wale wengine wote wanaotumia ardhi, kwa sababu mara nyingi sana tumekuwa na tatizo la kubomoa majengo baada ya wananchi kujenga na wanapata madhara makubwa hasa ya kiuchumi. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali iainishe hata yale ya barabara. Tumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais alipokuwa Waziri wa barabara aliweka alama *X* kwenye mtandao wa barabara zote nchini na kwa hivyo nyumba nyingi hazikujengwa

hadi sasa na zile zilizokuwepo zinaendelea kuchoka lakini pia ione umuhimu wa kufidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuongelea eneo hili la fidia, wananchi wengi wanapata hali siyo nzuri kutokana na kwamba baada ya mtu kujenga anabomolewa jengo, madhara ni makubwa sana na kwa hivyo niitake Serikali iwe inaangalia madhara makubwa yanayompata Mtanzania wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la Watumishi wa Serikali. Wote tunafahamu kuwa wale waliojenga kwenye mikondo ya maji na waliojenga kwenye barabara walipimiwa na watumishi wa Serikali ambao ni wataalam, haijalishi ni mtaalam wa aina gani lakini aliienda kumpimia yule mtu. Leo hii tunapofika hatua ya kwenda kubomoa yale majengo bila fidia bila hali ya kuangalia ni kwa namna gani mwananchi yule anadhurika, hatuwatendei Watanzania haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wengine wamegawa *plot* mara mbili kwa Mtanzania mmoja, hali inayoleta migogoro mikubwa kati ya mtu na mtu au taasisi na taasisi. Naomba Serikali iangalie ni kwa namna gani inajitahidi kuona athari za namna hizi zinachukuliwa hatua za kimsingi na zile za mpango mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwepo na mpango kabambe wa wananchi kupata hati miliki. Hati miliki itaondoa mgogoro mkubwa wa ardhi kwa asilimia kubwa nchini. Iwezekane basi hata namna ya wananchi na Serikali yao kuingia ubia, zipi gharama za Serikali na ipi gharama ya mwananchi ili apate hatimiliki katika ardhi anayomiliki sasa. Kumekuwa na tatizo kubwa la kesi nyingi za ardhi kubadilishwa kutoka kesi ya ardhi kwenda kuwa kesi ya jinai kwa ajili ya uelewa mdogo wa wananchi. Naiomba Serikali itafute njia mbadala ya kuondoa tatizo hili kwa kutenga fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara hii ilipowasilishwa imekuwa ni bajeti ndogo kuliko tulivyotarajia. Tulitarajia tungekuwa na mpango kabambe wa wananchi kupata hatimiliki, lakini kwa ubia wa gharama kati ya Serikali na wao ili kuwezesha wananchi kumiliki ardhi yao na kuondoa migogoro mikubwa inayotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inabidi kukemea hii hali ya rushwa kwenye Mabaraza ya Ardhi. Maana siyo kwamba Wapinzani wakizungumza mambo yote ni ya uongo, mengine ni ya ukweli lazima tutazame na tuone tunafanyaje wakati inapobidi. Serikali isione tu kwamba hali ya kuachia vyombo vya kiutendaji ni hali ya kawaida, inaendesha inavyotaka, inaendesha kwa

mfumo huu wa kidikteta, inaendesha kwa mfumo wa rushwa na wakati huo huo wananchi wanaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niitake Serikali kutazama upya watumishi wote au watendaji wote wa Mabaraza ya Ardhi na matendo yao na kuona ni namna gani wale ambao hawafai kabisa na wanatumia madaraka yao vibaya wanaondolewa kwenye *system* ya utendaji wa chombo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hali hii wananchi wengi wanashindwa kutetea haki yao kutokana na uelewa mdogo wa kisheria. Uelewa wa kutetea haki yao na pale wanapotaka kutetea haki yao wananchi wengi hawana uwezo na kwa hivyo wanashindwa kutetea haki yao lakini hali hii inasababisha madhara makubwa kwa wananchi kukosa haki yao na hatimaye kubaki na hali ya sintofahamu na kupoteza haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Wizara iwe na mpango kabambe wa kuona maeneo yenye matatizo ya ardhi au migogoro ya ardhi, basi wanafanyiwa utaratibu wa kuanzishiwa Mabaraza ya Ardhi yakiwemo yale ya Wilaya kwa ajili ya kupunguza umbali mkubwa na gharama kubwa wanayopata wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wana kipato kidogo, hawawezi kuweka Wakili, hawawezi kwenda kwenye Mahakama ambayo iko mbali na makazi yao na kwa hivyo hawana uwezo wa kutetea haki yao ya kimsingi na wanaacha inapotea bure. Kama itawezekana pia kuwe na utetezi wa Wanasheria wa Halmashauri kutetea kesi zinazoingiliana na zile za Halmashauri na Halmashauri nyingine au kijiji na kijiji kingine kwa ajili ya utatuzi wa kero hizi na migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa sababu muda huu ni mdogo, nimwombe Mheshimiwa Waziri alituahidi kule Mbulu kuanzishwa kwa Baraza la Ardhi Wilayani Mbulu. Namwomba sana katika bajeti hii haionekani, lakini sisi tayari tumetimiza wajibu wetu tutamwandikia barua Wabunge wote wa Majimbo mawili, Baraza hilo kwa mwaka huu lazima liwepo awe na majibu wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimtakie kazi njema Mheshimiwa Lukuvi, niwatakie Watanzania wote utashi mwema wa kuiona nchi yetu inakwenda vizuri na niwashukuru sana kwa jinsi ambavyo Baraza letu la Mawaziri linafanya vizuri sana na wanajitahidi, kukejeliwa ni jambo la kawaida, tunaongezewa *speed,* tuwe na *speed* kali sana. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kukejeliwa ni kuongezewa mwendo wa safari, nawashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia, sasa hivi ni zamu ya Mheshimiwa Yussuf Salum na baadaye Mheshimiwa Joshua Nassar ajiandae.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya leo. Mwenyezi Mungu amesema katika *Quran,* Sura ya 41, aya ya tisa mpaka ya 11 katika juzuu ya 24 kwamba ameitandika ardhi na akaipa neema mbalimbali za ndani ya ardhi na juu ya ardhi, akaipa milima na mabonde, akaipa mito na maziwa, akaipa misitu, akaipa na viumbe hai na madini ili kwayo ituneemeshe na itufaidishe wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha katika ardhi hii ya Tanzania imekuwa kama ni laana sasa kwetu, badala ya heri inakuwa shari. Mwenyezi Mungu ametuambia hayo na turudi katika vitabu vyake ili tujifunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi katika uchangiaji wake, Mwenyekiti wangu Mchakachuliwa, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, alikariri falsafa ya Baba wa Taifa, kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Watanzania tuna ardhi kubwa, tunamshukuru Mungu. Tupo wengi, tunakaribia milioni 50 sasa *Alhamdulillah*, lakini kwa nini tunagombana, tunahasimiana, tunapigana mpaka tunauwana? Ni kwa sababu ya ardhi. Ni kwa sababu ya ama ya siasa safi, uongozi bora ama yote mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa muda wa miaka 54, bado inawaomba tena mkae chini mtafakari, tatizo letu ni nini mpaka iwe ardhi hii haijatuletea tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitu ambacho kinaleta matatizo katika ardhi na kusababisha maafa makubwa ni kukosekana kwa kile kinachoitwa *Integrated Land Information Management System.* Pamoja na mipango mizuri iliyopangwa na Mheshimiwa Waziri na timu yake, pamoja na *World Bank* kutoa pesa zaidi ya Dola milioni 20 kwa ajili ya kazi hii, pesa hizi kwa zaidi ya miaka miwili zimezuiliwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, hili halijatendeka. Watanzania wanauana, wanaumizana, wanahasimiana, kwa nini? Siasa safi, au uongozi bora? Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema kwa miaka 54 hebu wenzetu kaeni chini kuwe na *vision,* leo kila mchangiaji anasimama anakwambia tunamshukuru Mheshimiwa Lukuvi tokea awe Waziri, amejaribu kutatua migogoro. Mheshimiwa Lukuvi ni mwanadamu, ni kiumbe. Hivi akiondoka Mheshimiwa Lukuvi, tunarudi kule kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kaeni chini Serikali ya CCM tuwe na *vision*, yeyote atakayekuja katika Wizara hizi, awe anaanza pale anakwenda mbele. Leo akiondoka Mheshimiwa Lukuvi iwe Wizara hii haipo; akiondoka Mheshimiwa Mwigulu, Wizara ya Kilimo, kwisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Namshukuru Mheshimiwa Profesa Muhongo. Ukienda katika ile Wizara, unajua hasa kwamba anatoka wapi anakwenda wapi, *step by step*. Amejipanga! Kwa hiyo, pale unajua namna gani mtu amejipanga, anatoka wapi, anakwenda wapi. Jamani ukweli lazima usemwe! Kwa hiyo, tunaomba Serikali ya CCM katika Wizara zote tujipange, tuwe na *vision* tujue tunakwenda wapi, siyo kusema kwamba aah, Lukuvi! Lukuvi kiumbe! Lukuvi ni binadamu huyu! Akiondoka huyu jamani, tuwe tunarudi kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba Bunge hili, leo hii, wakati bwana mkubwa anawasilisha huyo, tujue fedha hii iliyotolewa na *World Bank* itatoka lini, wapewe wafanye kazi ili Watanzania wasiuwane na wasihasimiane kwa neema waliyopewa na Mwenyezi Mungu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije la pili. Namwomba Mheshimiwa Waziri Lukuvi, pamoja na kutushawishi sana Wajumbe wa Kamati yake, pamoja na maelezo mazuri sana aliyotutolea, lakini bado tuna wasiwasi na bado mimi binafsi sijakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha miaka nane wananchi wa Kigamboni wamekuwa mayatima, wamekuwa na hofu juu ya hatima ya ardhi yao, Mji wa Kigamboni utakavyokuwa. Pamoja na kupunguza eneo likarejeshwa kwa wananchi, hilo lililobakia la hekta 6000, hadi leo Serikali hii haikupi fedha ya kwenda kufanya hizi shughuli ambazo zinatakiwa kufanywa. Hii miundombinu. Sasa kama hupewi fedha na ardhi ile tayari imezuiwa na wananchi wale wamepewa tu maelezo kwamba mwingie kwenye uwekezaji, mwingie hivi, mwingie hivi, lakini kwa muda wa miaka nane sasa hakuna fedha inayotoka, pale tunategemea nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunasema jamani, Serikali ya CCM tunapanga; lakini tunajitekenya wenyewe, mkicheka wenyewe, kama hamjampa fedha huyo Lukuvi, atafanya nini? Kwa hiyo, kama fedha haijatengwa, wale wafanyakazi na ile Ofisi; wafanyakazi warudi Wizarani na Ofisi ifungwe, mpaka atakapopewa fedha ile itarudi ikae kwa miundombinu, ili ule Mji wa Kigamboni uje katika hilo linalotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika nyumba za gharama nafuu. Kuna wazo zuri, mipango mizuri na kwa kweli namshukuru sana. Kama analipwa hiyo shilingi milioni 40, basi ni haki yake, alipwe Mkurugenzi wa Nyumba na Makazi,

kutokana na kazi anayoifanya. Kwa sababu mtu kama anafanya kazi, basi mwache apewe kwa namna anavyofanya kazi. Anafanya kazi na anastahiki. Tunaiomba Serikali waondoe suala *VAT* katika nyumba za gharama nafuu ili wananchi wanyonge waweze kununua hizi nyumba ziwafaidishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi jamani mtu anayelipwa mshahara wa sh. 150,000/=, ataweza kweli kununua nyumba yenye thamani ya shilingi milioni 45 kwenda juu? Kama hakuna wizi huko nyuma, ataweza? Sasa tunaiomba kodi hii *VAT* iondolewe katika hizi nyumba ili nyumba hizi, lile lengo lililokusudiwa la wale wanyonge kuweza kununua na kuishi katika nyumba hizi ziwafikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mheshimiwa Waziri, Tanzania imekua, Watanzania wanaongezeka, mahitaji ya ardhi yanaongezeka, lakini na teknolojia ya kutumia ardhi inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya upimaji wa ardhi ni ndogo sana. Pamoja na kuruhusu taasisi binafsi, wakawapa vibali wapime ardhi, lakini bado kasi ni ndogo sana hususan huko vijijini. Namwomba Mheshimiwa Waziri, hii kasi iongezeke ili upimaji uendelee kwa kasi na wananchi wa vijijini wamiliki ardhi ziwasaidie waweze kukopesheka kwa faida yao na kwa faida ya nchi yetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika, naomba ukae.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Joshua Nassari na baadaye Mheshimiwa Omar Mgumba akae tayari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukisoma maandiko, Biblia Yeremia 33 mstari wa tatu, inasema, "niite nami nitakuitikia, nami nitakuonesha mambo makubwa na magumu usiyoyajua." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wamelia na wamemwomba Mungu, wamemwita naye amewasikia na sasa hivi yameanza kujidhihirisha, matokeo yake ndiyo haya, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, wanakuja Bungeni kuomba sanamu ya Mashujaa iondoke iwekwe ya Diamond. Matokeo yake wengine wanaongea kwenye Bunge hili, wanasema wana uchungu sana, hawataki Bunge lionekane *live*, halafu siku moja baadaye anakwenda kuomba *exclusive interview* ya Ayo *TV* ili aonekane yeye kwenye *TV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile maombi haya ambayo Watanzania wameomba Mungu, yameonekana leo hii, ndiyo maana Mheshimiwa Rais anafanya *vetting* ya Mawaziri kwa zaidi ya mwezi mmoja, badala yake anatuletea Mawaziri walevi wanaokunywa viroba asubuhi. Hili ndilo tatizo la kukosa sukari kwenye nchi na uongozi thabiti. Ndiyo maana naona Mawaziri wanakunywa viroba. Sasa kama Mawaziri wanalewa, sijui madereva wa bodaboda kule mtaani watafanya namna gani? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nijikite kwenye uchangiaji wa leo kwenye Wizara ya Ardhi. Mwaka 1952, Mtanganyika wa kwanza aliyekwenda Umoja wa Mataifa miaka tisa kabla ya uhuru, alikuwa anaitwa Japhet Kirilo Ngura Ayo, akiwa ni mwananchi wa Meru, baada ya hapo, kilichompeleka *UN* Marekani 1952, New York, ilikuwa ni suala la ardhi na akianzia Meru, kwa sababu ya mgogoro uliokuwepo wa ardhi ndani ya iliyokuwa inaitwa Wilaya ya Arusha Meru miaka hiyo na Kiriro huyo akaja kuwa Mbunge wa kwanza. Wakati wa harakati za uhuru Mwalimu Nyerere amelala sana pale Meru nyumbani kwa Kiriro, alikuwa anakuja kutafuta ushauri, kwa sababu mwezake alikwishafika kabla yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka tisa kabla ya uhuru Kiriro ametumwa *UN*, New York, kwa fedha ambazo zilichangwa barabarani kwenye vyungu ambavyo watu wa Meru waliweka zikamsaidia kwenda yeye pamoja na Mwanasheria *United Nations,* 1952.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata uhuru, ameingia Nyerere, Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne na Awamu ya Tano, bado ardhi ya Meru imeendelea kizungumkuti. Halafu matokeo yake, mnavyotuona sisi kule tunaamua kuchukua sheria mkononi sasa, tukija Bungeni mnaanza kutuambia Mheshimiwa Mbunge unatakiwa utulie, uwe kiongozi, uvae suti vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nivae suti? Kiriro alivaa suti mwaka 1952, mpaka leo ardhi haijarudi. Tumepata uhuru *over 50 years*, bado kilio ni kile kile! Matatizo ni yale yale! Ndiyo maana tunasema Serikali hii kwa kweli imechoka. *You guys are sick and tired!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niulize kwa mfano, amekuja Mheshimiwa Simbachawene Meru mwaka 2014 kama siyo 13, akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Tumeongozana kwenda kwenye shamba la *ACU* la Valesca, Serikali ikakubali kutoa ekari 1500 kwenda kwa wananchi, leo hii ni mwaka 2016, bado zoezi halijawahi kufikia mwisho, bado ni mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Mheshimiwa Ole-Medeye akiwa Naibu Waziri wa Ardhi kabla yake 2012, tumekwenda kwenye shamba la Karamu, mimi na yeye mguu kwa mguu mwaka 2012. Leo ni mwaka 2016, *we are crying a very same, we are singing a very same song*. Kila siku hadithi ni zile zile. Tufanyeje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaishia hapo, Tanzania *Plantation;* na mimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kikubwa kweli! Mheshimiwa Waziri nakushukuru leo umetupa begi kubwa, nafikiri hili begi nitapeleka nyumbani, litatusaidia kufanya kazi za nyumbani. Kwenye kitabu hiki ukurasa wako wa 39 ambao umeonesha hali ya migogoro ya ardhi kwenye nchi, umetaja hapa mashamba yaliyoko Arumeru, umeyataja mengi; Lusi, Dolly Agakhan sijui nini *Tanzania Plantation* na mengine na ukasema chanzo cha mgogoro ni wananchi kuingiza mifugo kwa nguvu bila idhini katika mashamba ya wakulima wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mkononi ninalo Gazeti la Serikali *(Government Gazette),* ambalo limesainiwa na kutolewa mwezi Agosti, 1993 kabla mimi sijaanza Darasa la Kwanza, ambalo linaonesha kabisa kwamba kulikuwa na nia ya Rais ku-*revoke*. Baada ya hapo ikafutwa na likatwaliwa. Leo hii ni mwaka 2016 tangu mwaka 1993, leo unatuambia wananchi wanaingiza mifugo kwenye shamba la mwekezaji mkubwa, eti ndiyo maana kuna mgogoro. Hivi ni nani ambaye amevamia hapa? Ni wananchi au Mhindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi inawekewa mfukoni Mhindi mmoja mwenye uraia wa Uingereza, anaishi Tanzania, anamiliki ardhi, ardhi imefutwa na Rais, leo anaendelea kuimiliki, amegawa, ameuza na anaendelea kuuza. *Who is powerfull in this country? A business person* au *the Government itself? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, nina nyaraka nyingi hapa mkononi na Mheshimiwa Waziri, anajua vizuri kwa sababu kwake mimi nimekuwa ni mgeni wa kila siku. Nimemwomba pengine aje Arumeru akae hata wiki moja au mbili; kama hana sehemu ya kukaa mimi nitam-*host* kama ni chakula mimi nitampa. Aje kwa gharama zangu, siyo kwa gharama ya Ofisi ya Mbunge, tufanye kazi tumalize. Leo naomba nimpe tu *list* ya mashamba ambayo kuna nyaraka zake ziko hapa na nitaziwasilisha mezani kwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ambayo ni kizungumkuti ni Shamba la Valesca ekari 1500, shamba la Karamu, shamba la Tanzania *Plantation*, shamba la Madira ambalo lilitwaliwa na wenyewe na lilipaswa kurudi kwa wananchi na nyaraka zipo hapa nitakupa badala yake tumepewa ekari 200, nyingine akapewa ekari 50 Mbunge mmoja wa Chama cha Mapinduzi alikuwa

wa Vunjo anaitwa Aloyce Kimaro. Wakati huo amekwenda nje huko akadanganya anakuja kujenga hoteli, asaidie ku-*host* Mkutano wa *Sullivan,* leo ni miaka karibu 10 baada ya Mkutano wa *Sullivan,* hakuna hoteli wala nini, ardhi bado imehodhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, achia mbali shamba la Madira, kuna shamba la kwa Hidaya. Mzungu mmiliki hayuko Tanzania, miaka zaidi ya nane, nimekwenda kumtatufa, hayupo. Limeachwa, limekuwa pori hapo, sijui yupo nchi gani huko, tunaangalia. Shamba la kwa Ugoro, mpaka na kesi Mahakamani wananchi walishinda, lakini halirudishwi kwa wananchi. Shamba la kwa Oscar, badala yake linakodishiwa wananchi au watu mpaka leo; nimekuja na risiti ninazo nitaziwasilisha kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hii barua mojawapo hapa, imeandikwa mwaka 2001 na ikasainiwa na mtu anayeitwa T. J. Nkya, Msajili wa Hati Msaidizi, Kanda ya Kaskazini na anaonesha kabisa kwamba shamba la *Arusha Ex Coffee Farm* limekuwa *revoked.* Kwenye barua yake kwenda kwa Kamishina wa Ardhi anasema kabisa kwamba napenda kuthibitisha kwamba hati tajwa hapo juu ilitwaliwa; kwenye mabano ikaandikwa *(revoked)* na Mheshimiwa Rais, tangu tarehe 27 Februari, 1990, *revocation* kusajiliwa tarehe 3 Januari, 1991; chini ya waraka namba 6156. Mpaka leo hii tunavyozungumza lile shamba linamilikiwa na Wazungu na wameuza, wamegawa na wamepata hati, wamefanya *subdivision* Serikali imelala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina nyaraka nyingine tena kwa mtu anayeitwa N. J. Masuwa, Kamishina wa Ardhi, alizungumzia suala hilo hilo na akasema kwamba utaratibu wake ulikwisha, anamwambia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru awagawie wananchi. Mpaka leo hii hakuna kitu. Matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake sasa ni kwamba wananchi wanapojaribu kuingia kwenye shamba hilo kwa nyaraka hizi, wananchi wa Kijiji cha Maksoru mwaka 2015 wakashikwa wakafunguliwa kesi, tena wakapewa kesi ya *armed robbery*. Mimi Mbunge ndiyo nilihangaika mpaka kesi ikabadilishwa wakatoka wako nje leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu mwezi wa Tatu, Arumeru Magharibi kwa Mheshimiwa Gibson hapo, wananchi wengine kwenye lile lile shamba la Tanzania *Plantation* ambalo nimesoma taarifa yake ambayo imekuwa *gazetted* kwenye gazeti la Serikali hapa, wamefunguliwa kesi mwaka huu mwezi wa Tatu wakapewa *armed robbery*. Wengine tena upande wa huku kwangu mwaka 2015 akapewa kesi ya mauaji, kisa tu au chokochoko anadai ardhi. Nataka niulize, Serikali hii mtaweza nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikija hapa sijawahi kuomba kwamba eti naomba kule kwangu sijui kuna shule haina choo au madawati. Kama mnashindwa kusimamia nyaraka, mtaweza kusaidia wananchi wapate madawati nyie! Mtaweza kujenga matundu ya vyoo kwenye shule? Mtaweza kununua ndege? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda na nimeshagongewa kengele ya kwanza, Mheshimiwa Waziri hizi nyaraka zote na nyingine nimeshazifikisha kwake na leo nimekuja nazo nitapeleka kwa Mwenyekiti. Wakati akihitimisha hotuba yake leo, kama asipozungumzia masuala hayo, kwa kweli naomba niweke nia kabisa kwamba nitatoa shilingi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na la mwisho ambalo naomba niliguse kabla ya kengele kulia, Mheshimiwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Nashukuru, lakini ujumbe umefika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba na baadaye Mheshimiwa Sixtus Mapunda, akae tayari.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Ardhi. Kwa sababu kama alivyosema Mwalimu Nyerere, ili tuendelee tunahitaji vitu vinne na ardhi ikiwa ni mojawapo. Siasa safi tunayo ya ujamaa na kujitegemea, watu tunao, uongozi bora tunao unaotokana na Chama cha Mapinduzi na sera zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ni mchakato, hayawezi kuja siku moja kama wenzetu wanavyotaka. Hatukuwepo mwaka 1961 wakati tunapata uhuru, lakini Tanzania ya mwaka 1961 siyo Tanzania ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wenzetu wanaosema kwamba hakuna dira; dira ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tena katika utangulizi tu, imezungumza Wazi kabisa nataka pale kunukuu aya ya 6(b) inasema: "kuongeza kasi ya kupima ardhi yao na kuwapatia hatimiliki za kimila ambazo watazitumia kama dhamana ya kuwawezesha kupata mikopo na kuendeleza shughuli zao za kilimo, uvuvi na ufugaji."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu akisema kwamba hatuna *vision,* achukue Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hii hapa, kila kitu kimo humu ndani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu sasa katika Wizara hii ya Ardhi. Ardhi kama tulivyosema, ndiyo rasilimali muhimu sana kwa Taifa lolote lile ikiwemo Tanzania; ardhi na vitu vyake vinavyopatikana katika ardhi. Inawezekana tumepotoka. Kwa mfano tu, inapogundulika mafuta au madini sehemu yoyote ya ardhi, fidia pale kwa Mtanzania ambaye anaimiliki au kijiji atapewa tu labda kama ana migomba, minazi au nyumba yake, lakini mali ile yote ya pale iliyogundulika chini ya ardhi tunaimilikisha kwa wageni. Mtanzania yule anabaki maskini kwa kisingizio cha uwekezaji au tunasema tutapata mrabaha ambao ni mdogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri katika hili ili kuendeleza kuwaneemesha Watanzania na kutengeneza matajiri wazawa wa Kitanzania ama kwa kumiliki Serikali au kijiji au yule mwenye ardhi pale, popote pale inapogundulika rasilimali hiyo, basi tutengeneze sheria ije kwamba yule ambaye yupo pale apate hata asilimia fulani katika umiliki ule ili utajiri ule uendelee kubaki kwa Watanzania badala ya sasa kubaki na mashimo na michanga isiyokuwa na faida na mrabaha mdogo ambao tunapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusu migogoro ya ardhi. Tena Mheshimiwa Waziri nafikiri labda amepitiwa katika hili. Katika kitabu chake sijaona migogoro yoyote ya ardhi katika Wilaya yangu ya Morogoro katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini na ukizingatia ndiyo tunaongoza kwa mashamba pori yanayomilikiwa na watu wanaojiita wawekezaji, wamekopea tu mapesa, lakini hawayaendelezi. Naomba kama nitaileta tena ile *list* aingize hiyo migogoro ili tuweze kupatiwa majibu na kuweza kurudishwa kwa wakulima waweze kuyaendeleza baada ya hawa wawekezaji kushindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la migogoro ya ardhi kama Mheshimiwa Waziri alipotuambia pale nyuma kwamba wameshaanza kuitatua, kwa mfano, wameanza kule Kilombero na Ifakara, basi kasi hii naomba iongezwe ili tatizo hili liweze kutatuliwa haraka. La sivyo, katika hatari ninayoiona ambayo inakuja mbele yetu, inayohatarisha umoja wetu, mshikamano na amani nchini, basi ni hii migogoro ya ardhi. Wote ni mashahidi, tumeona watu wenyewe, Watanzania sasa hivi wanavyopigana, wanavyouana, kwa hiyo, naomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi itolee kauli hili suala la upimaji wa ardhi na kuwamilikisha ardhi watu wake ili tuweze kuiendeleza tuondoe hili tatizo la migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kutoa ushauri katika hili, migogoro mingi hii inasababishwa na viongozi waliopewa mamlaka kubwa lakini ufahamu

mdogo wa kisheria, hasa viongozi wa vijiji na Mabaraza ya Ardhi, kwa sababu huko ndiko kuna migogoro mkubwa. Pia linachangiwa na kupewa dhamana kubwa wakati hawana posho wala mshahara, matokeo yake wanajikita kwenye vitendo vya rushwa kwa mtu ambaye anataka ardhi kwa sababu anajua hawa Wenyeviti wa Vijiji au Viongozi wa Vijiji ndio wenye mamlaka, anakwenda kuwanunua wanapata ardhi kiujanja ujanja, baadaye inatuletea matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda huko vijijini utakuta mwekezaji au mtu yeyote kapata ardhi bila kuwashirikisha wananchi, lakini unakuwa muhtasari upo na sahihi zipo za *initial* na hati imetolewa mpaka Wizarani kwenye hiyo ardhi. Matokeo yake, hata tukienda Mahakamani, haki hiyo inakuwa hatuipati mpaka labda tumtegemee Rais atengue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, naomba Wizara ya Ardhi, niliwahi kusema hapa kwamba pale Ngerengere sasa hivi ni Mamlaka ya Mji Mdogo; na sera za ardhi zinasema mjini popote hapahitajiki kuwa na shamba, lakini pale tuna shamba la Serikali ya *LMU (Livestock Management Unity)*. Naomba shamba hili tuwape ardhi mahali pengine nje ya mji, ili shamba hili tuweze kulitumia kwa matumizi ya makazi na huduma za kijamii, lakini pia tuweze kuliendeleza kama ukanda wa viwanda vidogo vidogo ndani ya Halmashauri yetu kwa sababu ndiyo sehemu ambayo ina miundombinu mizuri lakini pia lipo karibu na Dar es Salaam, itakuwa ni rahisi sana kupata wawekezaji kwa ajili ya kuendeleza viwanda, kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kwenda uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kujielekeza kwenye *National Housing Corporation -NHC*. Sasa hivi *NHC* wamejikita sana kwenye miji mikubwa na matokeo yake kutokana na ushindani uliopo, hata nyumba nyingine zinaanza kukosa wapangaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna Wilaya mpya, Halmashauri mpya na Mikoa mipya na tuna matatizo makubwa ya miundombinu ya majengo na wateja ni Serikali, wapo wa uhakika! Basi tunaomba kama wangeweza kuja kujielekeza huko kuanza kujenga nyumba kwenye mikoa mipya, Halmashauri mpya na Wilaya mpya ili tuweze kwenda kwa kasi na sisi tuwe na majengo na kuwa na ofisi na tutawalipa pango lao kwa kupitia Halmashauri zetu na Serikali Kuu kwa sababu jukumu hilo linatakiwa ni Serikali kujenga miundombinu. Nina uhakika wateja wa uhakika pale wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kujielekeza kwa Mheshimiwa Waziri kumwomba tena kwa mara nyingine aje katika Halmashauri yangu ya Morogoro ili kutatua mgogoro mkubwa wa Mkoa wa Pwani na Morogoro katika Kata ya Magindu Pwani na Kata ya Seregete ‘B’ kuhusu mpaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo ni la muda mrefu ambapo wenzetu wa Magindu wanaleta mifugo katika Halmashauri yetu na wanawauzia wawekezaji bila kufuata taratibu, matokeo yake inaleta migogoro mikubwa sana na uhasama kati ya watu ambao ni ndugu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje katika Kata ile ya Kidugaro katika Kijiji cha Seregete hapo Magindu atusuluhishe kwa sababu tumeshakaa muda mrefu wenyewe hatujapata muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgumba, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda na baadaye Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ajiandae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi ya leo. Awali ya yote, nichukue fursa hii kama walivyosema waliotangulia kumshukuru sana na kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, *Comrade* William Vangimembe Lukuvi. Kwa kweli ukiitazama Wizara yake, ukitazama majukumu yaliyopo katika Wizara hiyo na jinsi anavyofanya kazi na ile *flexibility* yake ya kwenda kwenye migogoro ya ardhi, kwenye masuala yanayohusu ardhi kila kona ya nchi yetu, kwa kweli inatupatia matumaini makubwa. Huenda mwarobaini wa migogoro ya ardhi ndani ya nchi yetu umeshapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya ya utangulizi, naomba nijielekeze kwa kifupi kwenye mambo matano ambayo naomba Serikali iyatazame kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya nchi yetu ipo vile vile ila inapungua kutokana na shughuli za bahari, *size* inapungua, lakini binadamu wanaongezeka kila kukicha. Kwa hiyo, watu wanazaliana, wanaongezeka, lakini ardhi bado ipo vile vile. Tusipokuwa na mpango mahususi wa kuitazama Tanzania ya leo, ya kesho na ya miaka 50 ijayo, tutakuja kuzalisha migogoro ya ardhi ambayo tutashindwa kabisa kuja kuituliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona miji inakua, sasa hivi Jiji la Dar es Salaam limekua katika kiwango cha hali ya juu, sasa linatusumbua jinsi ya kupanga. Wapi upitishe barabara, ni shughuli! Wapi upitishe maji safi, ni shughuli! Wapi upitishe maji taka, ni shughuli! Wapi upitishe nguzo ya umeme, ni shughuli! Hata sasa tunapotaka kwenda kwenye huo mpango wa gesi ambapo inapita kama mtandao wa maji, tutashindwa kwa sababu kila utakayemgusa, utalazimika kumlipa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Dar es Salaam lingekuwa ni kosa letu la mwisho kufanya kwenye miji mikubwa na miji inayofuata yote isiwe na matatizo ambayo yametukuta Dar es Salaam. Sasa tunaona majiji yanayokuja tena, yanapita kwenye matatizo yale yale ya Dar es Salaam. Nenda kaangalie Tanga, matatizo ni yale yale; Arusha inakuja kwa kasi, matatizo ni yale yale; Mwanza ndiyo kabisa, tena itafungana kuliko Dar es Salaam; nenda kaangalie Mbeya, matatizo ni yale yale. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali, hii miji inayokua na ambayo mingine tuna-*predict* baada ya miaka 10 itakuwa miji mikubwa, tumalize mpango wa ramani ya miji. Miji ijulikane itakuwa na sura hii, tusirudi tena kwenye migogoro iliyopita huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unaenda kutatua mgogoro wa Kigamboni; Kigamboni imekuwa darasa zuri sana kwenye mipango miji. Tupange mji, barabara itapita wapi, nyumba itakuwa wapi, uwanja utakuwa wapi na ikiwezekana twende kwenye hatua ya pili; na ramani ya nyumba pale iweje? Sasa atakapofika mtu apate kiwanja chake ajenge nyumba kwa mujibu wa ramani jinsi ilivyo. Tunazunguka nchi za watu, tunaona haya mambo yapo, siyo mageni. Namwomba Mheshimiwa Waziri alipe kipaumbele hili suala, litaweza kuja kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hii Wizara ina changamoto kutokana na *centers* nyingi za *decision making* kwenye ardhi. Kijiji kina mamlaka, Halmashauri ina mamlaka, Wizara ina mamlaka. Ukiondoka kwa upande mwingine, unakwenda kwenye Wizara nyingine, ina mamlaka vile vile kwa mujibu wa sheria kwenye ardhi hiyo hiyo. Sasa matatizo ya Wizara moja au matatizo ya sehemu moja yenye mamlaka kisheria, yanaweza yakapelekea madhara kwenye eneo lingine.

Kwa mfano, migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji na hifadhi, unakutana na Wizara tatu ziko kwenye sakata moja; unakutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, unakutana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; unakutana na Wizara ya Maliasili na Utalii; unakutana na TAMISEMI tena nao wapo humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Wizara nne zisipokaa zikajadili kwa kina, zikaona baadhi ya sheria nyingine ambazo tunaona zinaleta migongano ya kimaslahi, migongano ya kimadaraka zifutwe, hatutatoka hapa. Leo hii ninavyoongea, kule Mbinga tuna mgogoro wa ardhi. Halmashauri inamiliki ardhi ina mamlaka ya kupima kama kawaida kwa mujibu wa sheria; kijiji kimemkaribisha mwekezaji kwenye ardhi ambayo wapo pale wanakijiji. Baadhi ya wanakijiji wamekubali kumpokea mwekezaji, wengine hawataki. Imekuwa ni mivutano mikubwa. Sasa Wizara huku juu wanaweza wakadhani kule chini mambo yanakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kigonsera, Kijiji cha Mihango, Waziri anaweza akaja akapatiwa maafa ambayo kwa kweli yatakuwa hayawezi kuelezeka kwa sababu pale wanakijiji wapo juu wanakasirika kwa nini mwekezaji anakuja? Tunatambua kwamba wawekezaji ni muhimu sana katika Sekta ya Kilimo, nami na-*encourage* sana waendelee kuwepo kwa sababu kweli kuna mambo mengi tunayapata kupitia hawa watu, isipokuwa uelewa wa watu wetu, ukoje. Hii mifumo ya mamlaka katika ardhi inakuwa ni kikwazo kikubwa sana kuiwezesha Wizara yako kufanya kazi *smoothly* katika *speed* ya Mheshimiwa Waziri. Nawaomba wafanyeni watakaloweza kulifanya, hao wanne ambao ni wadau wakubwa wa ardhi, wakae, wapange mpango mzuri, tukitoka hapo mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, migogoro mingi ya ardhi ndani ya nchi yetu ina uhusiano na nani mmiliki? Nani kapima? Kapima wapi? Kwenye Halmashauri zetu, wana mamlaka ya kupima ardhi, lakini uwezo wao wa kupima ardhi ni mdogo. Naiomba Wizara itengeneze *program* maalum ya kutafuta vifaa vya upimaji kwa nchi nzima. Ikishapata hivyo vifaa vya upimaji kwa nchi nzima, kwa sababu kila Halmashauri tuna Maafisa wa Mipango Miji, waende wapime ardhi yote kusiwe na mgogoro, eneo la makazi mtu akitaka kununua kiwanja aende sehemu tayari kimeshapimwa, akalipie apate hati yake, ajenge aendelee na maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwangu pale maeneo ya Lusonga, Mji sasa unakua ardhi haijapimwa. Ukienda Lusewa, Mji wa Mbinga unakua, hakuna kupima. Ukienda Mateka, Kilimani, Tanga, Luwaita, haya maeneo yote ya miji hayajapimwa. Kesho mji utakuwa mkubwa, tutakuja kwenye migogoro mikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nadhani litakuwa la mwisho, nisemee kuhusu ujenzi wa hizi nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Serikali kwa kuifufua sasa *National Housing Corporation* i-*operate* katika kiwango cha hali ya juu. Tunaona nyumba zinajengwa lakini zile nyumba hazinunuliki. Mtu wa kawaida hawezi akanunua kabisa, ni ghali! Mbaya zaidi, tumeingia katika *mortgage financing,* mtu anakwenda kukopa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba akajisitiri, anaenda kwenye mkopo wa riba kwenye hiyo nyumba; yaani unanunua nyumba una riba, *Nationa Housing Corporation* wamechukua vifaa kwa ajili ya ujenzi wa ile nyumba, wanakatwa *Value Added Tax* kwenye yale mambo, ukiyaweka yale yote gharama zinakuwa kubwa sana. Hii siyo njia sahihi ya kumsaidia mtu kwenye ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kitu kimoja kifanyike. Kama Serikali, tumeamua sasa tujenge nyumba za bei nafuu, twende kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tuiwezeshe *National Housing Corporation* ijenge kwa pesa zake, iuze na ipangishe. Zile nyumba zilizokuwepo miaka ya 1960 na 1970 mbona ilikuwa hakuna mambo kama haya tunayoyaona leo! Tuna *flats* zipo kila sehemu, ukiuliza wanasema hii ya *National Housing Corporation,* kila Mkoa zilikuwepo! Namwomba Mheshimiwa Waziri, najua haya mambo anayaweza. Kaa na *National Housing Corporation,* wasikilize changamoto zao, waweke vizuri wajenge nyumba za bei nafuu ili kila Mtanzania sehemu ya kulala isiwe tatizo tena.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mheshimiwa Riziki Shahari pamoja na Mheshimiwa Joseph Selasini wakae tayari.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima. Pia nawashukuru wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kuniona mimi niweze kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa umahiri wake, kwa uchapakazi wake, hatimaye kuirudishia heshima Serikali yetu. Naomba pia niwapongeze Mawaziri wote na Manaibu kwa uchapakazi wao mzuri. Hakika kweli tuna majembe na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja nikitaka ufafanuzi wa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa uliiunga mkono Serikali hii kwa kukipatia Chama cha Mapinduzi kura nyingi sana za kishindo. Sasa nipe nikupe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanapata shida sana hasa kwenye suala la ardhi. Suala la ardhi limekuwa ni shida upande wa shamba la *Efatha*. Imekuwa ni kizungumkuti kwa shamba la *Efatha* kwa sababu mpaka sasa hivi hatujajua Serikali ina mpango gani na wananchi wanaolizunguka lile shamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanapata shida sana, wamekuwa maskini, hawawezi kusomesha watoto wao kwa sababu tu ya hili shamba limechukuliwa na mtu mmoja ambaye anaitwa *Efatha*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefikia wapi juu ya mgogoro huu? Huu mgogoro umekuwa wa siku nyingi sana, Wabunge wa Mkoa wa Rukwa wote wamelipigia kelele sana hili suala, lakini mpaka sasa hivi halijapata ufumbuzi wowote. Je, Serikali ina mpango gani na hili shamba? Kuna tatizo gani kulikomboa hili shamba kuwarudishia wananchi? Naiomba sana Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Lukuvi, hili shamba lirudi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia wananchi wanaoishi uwanja wa ndege wa Sumbawanga Rukwa. Wale wananchi walifanyiwa tathmini za nyumba zao na ziliwekewa *X* muda mrefu, zaidi ya miaka saba. Wananchi hawa hawana urafiki tena na mabenki, wanashindwa kufanya shughuli zao za msingi kwa sababu tu hizi nyumba ziliwekewa *X*, wanashindwa kuzipangisha. Naomba sana Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma hawa wananchi wa Vijiji vya Bangwe, Izia wanaozunguka uwaja ule wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee pia hizi nyumba za *National Housing*. Kabla Serikali haijaanza kujenga, inatakiwa ifanye utafiti kwanza kuangalia vipato vya wananchi ili ipange bei kulingana na vipato vya wananchi. Wananchi hawawezi kuzinunua zile nyumba kwa sababu vipato vyao ni vidogo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iliangalie suala hili. Nawapongeza sana kwa kujenga zile nyumba, lakini zile nyumba gharama yake ni kubwa sana kiasi kwamba wananchi hawawezi kuzinunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa haya machache, naomba Serikali iyafanyie kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali na baadaye atafuata Mheshimiwa Joseph Selasini.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara hii. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi, aliyenijaalia mimi na ninyi wote kuwa na afya njema na kuwemo humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache vilevile ya kuchangia kama wenzangu wengi walivyosema, labda nami nianze nalo hilo hilo kwamba, pamoja na makandokando yake yote kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi, lakini naona hii Wizara anaiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa yale yaliyosemwa na hotuba ya Kambi ya Upinzani kwamba tunachohitaji ni *system,* lazima uwepo mfumo! Siyo tu kama alivyosema Mheshimiwa Yusuph kwamba Mheshimiwa Lukuvi yeye ni binadamu, lakini pia kawekwa na binadamu. Nani anajua kwamba atakaa hapo miaka yote mitano? Anaweza akahamishwa kesho kutwa. Je, akihamishwa wakati yuko katikati ya hii mikakati yake, tutafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisisitize hilo kwamba tunahitaji mfumo na huu mfumo sijui unatoka wapi! Usidhani Waziri mwenyewe anaweza akasema mfumo nimeutengeneza huu na utafuatwa na wengine wanaokuja, kwa sababu historia haituoneshi hivyo, imekuwa kila awamu ikija, inakuja na misamiati yake na taratibu zake na mambo yake na mbaya zaidi ni kama vile inafumua lote lililokuwa kabla ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kusema, limesemwa pia na wachangiaji wengine kadhaa kuhusu masuala ya mipango Miji. Taratibu, akili ya mwanadamu iliyo sawa huwa anarudia lile lililokaa sawa, wenye lugha yao wanasema kuna *success stories.* Sasa unapokuja kufanya mambo, unafuata zile *success stories.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wameimba sana hapa kuhusu Kigamboni *Development Agency,* mpaka mwanafunzi wangu Mheshimiwa Mary Mwanjelwa akasema *this is a non starter,* yaani hakuna pa kuanza, hakuna pa kuelekea. Hivi tuliigiza nini tukaweka ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CDA* ime-*fail for more than 40 years.* Miaka 40 *CDA* haijulikani kama inatambaa au imekaa kitako au inasimama dede wanasema, lakini bado tukaanzisha mamlaka nyingine kwenye eneo dogo halafu na hotuba zote zimesema mpaka ya Kamati kwamba mmeanzisha dude halifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hiyo hiyo ndogo iliyopo tunasema tunabana matumizi, tunapeleka kule kule; pesa inatumika hakuna *productivity.* Sasa sijui ndiyo siasa safi na uongozi bora! Sijui, lakini kuna kasoro kubwa katika

haya. Tunahitaji kujiangalia kwa kina na tuseme hasa na tuamue tunataka nini kwenda mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka nimeanza kuja hapa Dodoma Bungeni kila nikitoka kichwa changu huwa kinapata wasiwasi na mpaka juzi nadhani, sikumbuki nilikuwa na nani, nikamwuliza hivi hili jengo la Bunge kuwekwa hapa, nani aliamua? Hii ndiyo barabara!

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kile kikao cha kwanza nilipofika, nimekaa pale nje getini, nikaona mabasi yanapita yanafuatana. Nikasema haya mabasi yanakwenda wapi? Wakasema hii ndiyo barabara kuu, ndiyo hiyo ulipotokea Dar es Salaam, ndiyo huko inakwenda *stand* hapo. Naambiwa na jengo la Bunge liko hapa. Kwa nini liliwekwa eneo kama hili? Sasa nikauliza, wana mipango ya kuhamisha watu wa huku au wana mipango ya kuhamisha hili lipelekwe huko mbele ya safari? Jamani, tunafanyaje mambo kama haya? Tunapangaje? Hivi kweli wanaoitwa wapangaji, hawa watu wanaotupangia haya nao wamesoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku baba mkwe wangu aliniuliza, akaniambia wewe mama ulikwenda kusoma Marekani, umesoma umefaulu kweli au? Kwa sababu anachosema yeye kwamba, tukisharudi huku na *degree* za huko huko, bado tunawaita wale wataalam tuliosoma nao kule kuja kutusaidia huku. Sisi wenyewe hatuwezi. Kuna tatizo hapa, halafu watu tunakaa tu kama vile mambo yamekaa sawa. Jamani mambo haya hayajakaa sawa. Bado kunahitajika kazi ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijui, kwa sababu hatujaingia huko na wala hamtushirikishi kwenye mambo yenu, tunaona tu *vision* na misamiati ya hapa kazi, ya kasi zaidi, kasi mpya lakini tunabaki pale pale. Sijui tunahitaji kufanya nini, lakini ilikuwa vizuri tu mngekuwa waadilifu 2015 mngetupisha kwa sababu naamini UKAWA tulifanya *performance* nzuri sana na hii ingekwenda vizuri kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine ambalo limegusa suala mahususi kuhusu Jimbo langu la Mafia. Naishukuru Serikali na Wizara hii kwa kwenda kutusaidia angalau shamba moja kati ya mawili ambayo Wilaya ya Mafia tulikuwa na migogoro nayo. Mafia jamani ni ndogo, anapokuwepo mwekezaji sijui au mmiliki mwenyewe wa shamba pori hili la ekari karibu 4,000 na kitu kwa miaka tu linakaa hivi hivi, wananchi wanakuwa hawana mahali; sasa angalau mmetusaidia kwenda na nimeona kwenye taarifa humu kwamba shamba lile limerudishwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, Mheshimiwa Waziri atusaidie uhamisho huu ukamilike. Kwa sababu tunapozungumza sasa hivi, huyo mwenye

nalo ameshatushtaki, kwa hiyo, tuna kesi na kwa bahati mbaya ni kesi ambayo inabidi tuje kuisemea Dar es Salaam na kwa bahati mbaya Mafia hatusafiri ila kwa ndege kwa sababu hatuna meli ya kuaminika. Ndiyo pale nikagomba sana kuhusu sh. 400,000/= mlizotupangia TAMISEMI kama usafiri, kwa sababu ile ni safari moja tu na nusu kwa sababu ndege sisi tunalipa *return* kwa 350,000. Sasa ni wazi kabisa hii kesi sisi itatushinda. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri achukulie hii kama *special case* ili jambo hili liishe haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza katika hilo, liishe pia kwa kutuwekea mipaka ya vijiji vyote vitano vinavyozunguka pale, kwa sababu nimeona kwenye hotuba humu ya Mheshimiwa Waziri, amesema ni vijiji vitatu, sasa pia sivijui ni vijiji gani. Lile shamba la Tumaini linagusa Vijiji vya Jojo, Kirongwe, Baleni, Gonge na Kithinge. Sasa sijui vitatu vipi vimepimwa na viwili vipi vimebaki, lakini ingekuwa ni vizuri zaidi hili tukalikamilisha liishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna hiyo pia ndiyo itakuwa mwendo mzuri sasa wa kushughulikia masuala, tusiwe tunafanya hii nusu nusu; tunagusa, halafu tunaacha halijakamilika, tunaliachia katikati. Kwa hiyo, naomba tena kwa msisitizo kabisa, suala hili likamilike kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba nizungumze kidogo kuhusu masuala ya huduma ya upimwaji ardhi. Sijui kwa nini niliposoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri naona hata hao wahitimu kwenye fani hii ni wachache. Najiuliza ni kwa nini? Sikuona, labda kama ipo, wahitimu wa Chuo Kikuu cha Ardhi, sikuona. Nimeona Chuo cha Morogoro na Tabora nadhani. Ni wachache mno! Hawa watu wanahitajika, tatizo ni nini? Hatuwafundishi. Vyuo hivi havina miundombinu ya kutosha kusomesha watu wengi au ni nini hasa tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lingine niulize, hivi Serikali inashindwaje kubeba jukumu la kutoa huduma hii? Tatizo ni nini mpaka tunaletewa sasa wapimaji binafsi ambao nao wanakuja na masharti magumu sana, wananchi wanashindwa? Utaambiwa shamba lako kama ni ekari tatu, watakwambia sijui watakutumia heka ngapi uwape na wao sehemu ama wanakutajia pesa nyingi na wananchi wanashindwa. Nilidhani hii ni huduma ya msingi kabisa Serikali ibebe na ifanye kwa taratibu kabisa. Kwani Serikali inashindwa nini kusema mwaka huu tunapima labda mikoa miwili, mwaka ujao mikoa mengine! Kwani nchi yenyewe ni kubwa ya kiasi gani Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana suala hili la ardhi hebu lishughulikiwe kama walivyosema wengi kwamba ardhi ndiyo kila kitu. Tunahitaji ardhi tuwekeze, tunahitaji ardhi tuishi tu humo kwenye majumba yetu na mambo mengine yote yanahitaji ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tu nami nimalizie kwa kusema tena kwamba, naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa sababu imeonesha *reality* na tuifuate. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Selasini na baadaye Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Stephen Ngonyani wajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Ardhi. Awali ya yote niseme kwamba Bunge hili liliunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza migogoro ya ardhi na kwa bahati nzuri, nilikuwa miongoni mwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Spika wa Bunge la Kumi kuingia kwenye Kamati hiyo kwa ajili ya kazi mahususi ambayo Bunge liliagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Lukuvi pamoja na wasaidizi wake, kwa sababu kadri ninavyofuatilia utendaji wao ni kwamba yale mapendekezo ya ile Kamati Teule yanaendelea kutekelezwa hatua kwa hatua. Moja kati mapendekezo tuliyotoa ni kwamba Wizara ijaribu kuzi-*coordinate* Wizara zinazoshughulika na masuala ya ardhi; Wizara ya Mifugo, Wizara ya Maji, ili kuweza kuratibu vizuri matumizi ya ardhi yetu maana yake tuligundua kila Wizara inafanya mambo yake kuhusu masuala haya ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona ni kwamba, hili linafanyika na mambo yanakwenda vizuri. Vilevile tulitoa pendekezo kwamba, lazima watumishi wa Wizara hii wapewe nafasi ya kwenda kujifunza, kwa sababu migogoro ya ardhi haipo Tanzania peke yake, iko nchi nyingi. Nchi zetu za Afrika Mashariki na Kati, migogoro hii ni mingi sana na wenzetu kwa mfano, Ethiopia wamejaribu kuitatua kwa namna ambavyo imeleta muafaka kati ya wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, tulipendekeza watumishi hawa wapewe nafasi ya kwenda kujifunza namna wenzao walivyotatua migogoro hii na kuleta amani katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lingine ambalo tulitoa ni hili ambalo linazungumzwa sasa hivi kuhusu upimaji wa ardhi. Migogoro haiko kwa wakulima na wafugaji peke yake au kwa wakulima na hifadhi peke yake au na wawekezaji peke yake, lakini hebu tazameni; ukitoka Dar es Salaam kuja Dodoma, sasa miji hii inaungana, maana yake kuna ujenzi holela wa ovyo ovyo tu. Dar es Salaam imeshaungana na Chalinze; Chalinze imeshaungana na Morogoro; Arusha imeungana na Bomang'ombe; Bomang'ombe imeungana na Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachia hali hii iendelee, maana yake ni kwamba huko tuendako Taifa hili litakosa ardhi ya kilimo, kwa sababu kila anayefikiria kuweka jengo lake analiweka mahali popote anapotaka. Ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Lukuvi hili atalizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na upimaji, Wizara ilikuwa na mfuko maalum ambao ulikuwa unazisaidia Halmashauri kukopa ili kuweza kufanya upimaji katika Halmashauri zao. Ulikuwa unaitwa *Plot Development Revolving Fund.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi watu wa Rombo tulipeleka maombi yetu Wizarani kwa ajili ya kukopa fedha hizi ili tuweze kufanya upimaji, mpaka leo hatujajibiwa na nadhani pengine Mfuko umekufa. Nadhani hiki kilikuwa kitu kizuri. Wizara iangalie namna ya kuboresha huu Mfuko ili Halmashauri ziweze kukopa fedha kwa ajili ya kusaidia kupima katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, ni hiki kilio cha kila Halmashauri kirejeshewe mapema ile *retention* wanapokusanya kodi ya ardhi. Mara nyingi inachelewa, sasa matokeo yake ni kwamba zile Ofisi za Ardhi katika Halmashauri zinakuwa kama zimefungwa miguu na mikono, hazina nyenzo, hazina fedha, kwa sababu hiyo upimaji unakuwa ni mgumu sana na utekelezaji wa majukumu yao pia unakuwa ni mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, nizungumze kidogo kuhusu Jimbo langu. Katika Jimbo langu kuna eneo la Ziwa Chala. Hili ni ziwa pekee katika Afrika kama siyo dunia. Ni ziwa pekee ambalo maji yake hayajachafuliwa kwa asilimia 85. Sasa hivi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinafanya utafiti wa namna tabianchi ilivyobadilika kwa miaka 500,000 iliyopita kwa kutumia lile ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sijui Halmashauri au Wizara, ilikwenda ikakabidhi watu iliyowaita wawekezaji eneo la lile ziwa na kuwamilikisha. Pamoja na hayo, ardhi inayozunguka lile ziwa ni ardhi ambayo wananchi wa Kata ya Holili, Chala, Mamsera, Ngoyoni na Mengwe walikuwa wamemilikishwa zamani na iliyokuwa inaitwa *Land Board*. Sasa wananchi wa Kata hizi wanazuiwa kwenda kwenye maeneo yao, wanapigwa, wanadhalilishwa na wenzao wawili matajiri ambao ni Warombo kule kule waliokwenda kumleta Mzungu wakamweka pale kwa kigezo kwamba ile ardhi ni mali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara kwa sababu waliopewa hiyo ardhi walikuwa viongozi katika Serikali ya Chama cha Mapinduzi, mwone kwamba jambo kama hili linawachafua. Kata nilizotaja ni karibu tano, wazee wanapigwa, akinamama wanapigwa na watu wachache waliopewa ardhi yao wanadai kwamba ni mali yao. Naamini Mheshimiwa Lukuvi kwa kasi

aliyoonesha na kwa usikivu alioonesha, nami niseme ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, siyo dhambi kumpa pongezi Mheshimiwa Lukuvi. Siyo dhambi hata kidogo, kwa sababu hata mimi binafsi niseme tu kwamba, kuna mambo aliyonitendea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhulumiwa kiwanja Tegeta tangu mwaka 1994. Nimekwenda kwenye haya mnayoita Mabaraza za Ardhi, nimehangaika sikupata haki yangu; lakini Mheshimiwa Lukuvi ameingia, haki yangu nimepata. Sasa ndiyo maana nasema siyo dhambi kama jambo zuri likifanyika lisemwe. Nami ningesema na wengine waige mfano wa Mheshimiwa Lukuvi wa kutatua mambo kwa haraka. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba hata hili la Ziwa Chala Mheshimiwa Lukuvi atalifuatilia na alitatue kwa masilahi ya watu wangu wa Rombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, pale Tarakea kuna kiwanja cha vijana cha kucheza mpira, watu wamefanya siasa tu, wakampa mfanyabiashara mmoja anaitwa Maulidi, kajenga hapo jengo lake. Sasa kwa uhaba wa ardhi tuliyonao Rombo, vijana wetu hawana mahali pa kuchezea, lakini tajiri kaweka jengo pale, liko limesimama naye anatumika kwa ajili ya kukisaidia Chama chenu kwenye kampeni, anatoa pesa za kampeni. Matokeo yake kwa kuwa anatoa pesa za kampeni, hakuna mtu anayemgusa. Ni imani yangu kwa kasi hiyo hiyo pia Mheshimiwa Waziri atakwenda pale aangalie jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kata ya Mengwe, hili nililisema kwenye Wizara ya Ujenzi, tuna kiwanja pia cha watoto cha kucheza mpira. Wameweka hapo matingatinga tangu mwaka gani sijui, yako pale, vijana hawana mahali pa kuchezea, hebu Mheshimiwa Lukuvi aangalie namna ya kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niseme tu, Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla tuna matatizo makubwa sana ya ardhi. Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro nao ni Watanzania, nimesikia tukizungumza hapa kuhusu mashamba ambayo Serikali inayarejesha kwa wananchi. Naomba kama unaweza ukawekwa utaratibu hata wananchi wa maeneo ambayo ni *highly populated* kama Rombo, vijana wana moyo wa kufanya kazi ya kilimo, lakini hawana maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wapo tayari kwenda kwenye maeneo mengine ya nchi ambayo wakipewa ardhi kwa utaratibu fulani wanaweza wakaendeleza kilimo. Nami niko tayari kuwaorodhesha vijana kama hao na kuwapeleka ofisini kwa Mheshimiwa Waziri ili kama kuna shamba fulani la Serikali watalitoa, basi na wale vijana wanufaike kwa sababu nao ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua, huu utaratibu wa kupima ardhi ambazo tunapata hati zile za kimila, sijui namna gani, kwa mashamba ya kimila kama ya Kilimanjaro, vile vihamba ambavyo vina makaburi, tunaambiwa hatuwezi kukopa kwa sababu mashamba yetu yana makaburi, upimaji wake unafanyika namna gani. Sisi tutakosa hiyo haki kwa sababu siyo dhambi sisi kuzika kule kwenye vihamba vyetu, ni kwa sababu ya ukosefu wa ardhi. Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kutusaidia ili wale wananchi waweze kupata manufaa ya ardhi yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Joseph, muda umemalizika. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Flatei Massay, halafu Mheshimiwa Stephen Ngonyani pamoja na Mheshimiwa Moshi Kakoso wajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini pia namshukuru Mungu sana kwa kupata afya nzuri ya kusema hapa sasa. Kwanza nianze kushukuru sana Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa nini nasema haya? Kimsingi namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi na Naibu wake kwa kufanya kazi hii ambayo imekuwa kero sana kwa wananchi wetu hasa kwenye migogoro ya ardhi. Mheshimiwa Lukuvi amejitahidi sana kwa kweli kama wachangiaji waliotangulia walivyosema, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake binafsi zinazoonekana na Wizara yake kwa ujumla kuonesha moyo dhahiri kabisa wa kutatua matatizo ya ardhi; hasa amefika kule kwetu Mbulu, alisaidia Halmashauri ya Mji kwa kweli kurudishiwa ardhi yake na amesaidia kwenye Bonde la Yaeda Chini kutatua mgogoro ulioko pale ambao nimeuona pia ameuandika katika kitabu chake hiki cha migogoro kwenye ukurasa wa 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kwamba kwa kuwa sasa Sheria ya Ardhi inataka watu wengi au *majority* kupiga kura ili kutoa adhi, lakini kuna maeneo mengine wapo watu ambao ni *minority,* naomba wale pia wazingatiwe. Kwa mfano, kwenye eneo letu kule kuna watu wanaoitwa Wahadzabe; wale mara nyingi wanakula kwa kufanya kitu kinachoitwa uwindaji. Kwa hiyo, wana tabia ya kuhama na kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba waangaliwe, kwani ardhi yao katika lile bonde ni ndogo sana. Nashukuru kwanza kwa kufanya hatua ile, lakini angalau wale watu wawe *considered* katika ardhi ambayo kimsingi iko kule ambayo ni eneo pekee katika maeneo ambayo wanayo katika Mbuga ile ya Yaeda Chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amezungumza Mbunge mwenzangu wa Mjini, kama kuna maeneo yenye migogoro Tanzania hasa ya ardhi, nafikiri ni kule kwetu Mbulu. Namshukuru Waziri kwa kweli kwa kutusaidia na kutuambia kwamba yuko tayari sasa kuja kuanzisha Baraza la Ardhi ambalo litafanyika kule kwetu Mbulu. Nami nimwambie kabisa, jana Jumapili nilikuwa nyumbani, wamekubali, wameshapanga majengo ya kumpa kuanzisha Baraza la Ardhi na Halmashauri imeshamwandikia barua, nafikiri ataipata na nafikiri mwenzangu amezungumza, sina sababu ya kuendelea na hilo, lakini nakushukuru sana, Mungu ambariki kwa sababu kwa kweli akileta maendeleo yale ya kusikiliza kero za wananchi kwa haraka, migogoro yote itakuwa rahisi kutatulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kuishauri Wizara hasa katika upimaji wa ardhi. Ili kuondoa migogoro, ni vyema basi Wizara ikajielekeza kuipima ardhi hasa ardhi yote ya Tanzania, pawe na *Land Bank* ambayo itaondoa kitu kinachoitwa migogoro mingi. Ardhi ya Tanzania ikipimwa ni rahisi kuondoa migogoro; tutaelewa kabisa huu ni mwisho na mpaka wa mji na hapa panaelekea kuwa kwa wafugaji na hapa ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi yetu ikipimwa, kwa sababu sasa hivi kuna *GPS*, kwa hiyo, ni rahisi sasa kutumia *GPS*, kwa mfano ile ya Tume ya Uchaguzi, hivyo, ni rahisi sana kupima ardhi yote ya Tanzania. Ardhi ile ikipimwa ni rahisi pia kujua nani anaishia wapi, migogoro mingi itapungua kwa ajili hii. Kwa hiyo, naishauri Wizara yetu hii ya ardhi, pamoja na kazi nzuri inayofanya, ipime ardhi hizi na ardhi ikishapimwa basi, inaweza kutatua migogoro kwa wingi sana kila mtu akijua mipaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie jambo la utaratibu wa kupata hatimiliki. Naiomba Wizara ifupishe kidogo utaratibu au iende kasi ya upatikanaji wa hatimiliki kwa wananchi wetu. Maana sasa hivi ukitaka kupata hatimiliki, kwa kweli unatumia utaratibu mrefu sana mpaka kuipata hati hii. Kupata wapimaji kwenye maeneo yetu ni kazi. Kwa mfano, katika Mkoa wa Manyara hasa Wilaya ya Mbulu, hatuna wapima ardhi, kwa hiyo, inachukua muda mwingi sana mpaka mtu apate hatimiliki ya kiwanja chake ili aweze kukiendeleza au kuombea mkopo au kufanyia maendeleo fulani. Nashauri haya, basi Wizara ijitahidi katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna jambo lingine ambalo napenda kulieleza. Kuna upimaji wa miji na upimaji wa miji midogo. Niombe sasa Wizara ijikite na ielekeze namna nzuri ya upimaji wa miji. Miji ikipimwa; kwa mfano, miji midogo ikipimwa na miji ikapimwa itakuwa rahisi sasa matumizi bora ya ardhi kufanyika. Sasa hivi maeneo mengi yanavunjwa kwa sababu hatuna *plan management* ya ardhi katika miji yetu midogo na mikubwa. Kwa hiyo, naiomba

Wizara ijikite katika hali hii ya kupima miji yetu ili pawe na *plan* ya mji wowote unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule kwetu kuna Miji ya Haidom ambao sasa tumeuombea kuwa mji na Mji wa Dongobesh ambao unazidi kuwa mji na Mji wa Mbulu ambao kimsingi ni wa siku nyingi, lakini una ramani nyingi ambazo nashukuru Mheshimiwa Waziri alipokuja alisema kabisa kwamba atatusaidia kutupatia mpima atakayesaidia kupima ule Mji wa Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa miji hii midogo ambayo sasa inakua, ufanyike upimaji mahususi wa mwanzo na miji mingine Tanzania ili migogoro isiwepo kwa sababu Maafisa wengi wa ardhi wanapata shida. Maeneo mengi hasa ya makorongo, maeneo ya kutoa maji yanaleta shida sana katika maeneo haya, kama ardhi isipopimwa hasa kwenye miji hii ambayo tunategemea kuwa miji mikubwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hela ambazo zinaitwa *retention* ambazo kimsingi Halmashauri zinakusanya kama maduhuli na zinakuja Wizarani, basi Wizara ihakikishe zile hela zinarudishwa kule ili Halmashauri zetu ziweze kujiendesha kwa kutumia hela za *retention* ambazo Serikali kuu inakusanya kupitia Hamashauri zetu. Maana Halmashauri zetu pia hicho ni chanzo cha pato na ni pato mojawapo ambalo likirudishwa kule kwa haraka basi, Halmashauri zinaweza kujiendeleza, zikaendelea kufanya mpango wa upimaji katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, napenda kujielekeza kwenye habari hii ya nyumba zenye bei nafuu. Tumeona mpango mzuri wa Mheshimiwa Waziri; kwanza nampongeza sana. Nina *Bag* hapa, yuko mchangiaji alisema hapa, sitaki kumtaja jina, anasema Wizara haikujipanga. Wizara imejipanga. Nimelisoma hili *Bag!* Yaliyomo humu ukiyasoma kama Mbunge ukayaona yalivyokuwa yanaelekeza, ni rahisi kuona kuwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wamejipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko Sheria za Ardhi huku, tukasome tuelewe tuwasaidie wananchi wetu ili waelewe. Sisi kama Wabunge tunaweza kuwa rahisi kuwaelekeza wananchi, kuwafundisha katika maeneo ili angalau waweze kuondoa migogoro. Hiyo itakuwa ni rahisi kuliko kulaumu kwamba Serikali haijajipanga. Serikali imejipanga, wametuletea mambo yako humu, migogoro imepangwa, Mheshimiwa Waziri ameandika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Serikali tusaidie sasa kueleza wananchi wetu ile namna bora, maana hakuna Serikali mahali popote duniani inayoweza kufanya kazi kwa upande mmoja tu. Ni lazima upande mwingine wa sisi Wawakilishi tufanye kazi ya kuelimisha watu wetu ili migogoro hii nayo ipungue

tufikie katika hali ambayo itasaidia Wizara na Serikali kwa ujumla, maana Serikali tu haiwezi kutatua migogoro kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro pia inatatuliwa na Wanasiasa ambao ni sisi wenyewe. Nasi Wanasiasa yaani Wabunge na wengine wanaotusikia wanaochaguliwa, tusaidie kuelekeza watu ili wasiwe wa kwanza kuvunja sheria. Maana tukianza kuvunja sheria, tutakuwa wa kwanza kuilaumu Serikali, kwa sababu mpaka Serikali ije inatumia muda mwingi na gharama nyingi, watu wengi wamefariki, wamepoteza maisha kwa migogoro hii ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba pia, Serikali kwa upande mwingine ijitahidi. Wakuu wa Wilaya; namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, anatatua migogoro kwa kuiona mwenyewe *physically*. Natoa rai yangu kwa Wakuu wa Wilaya wa maeneo mengine, Wenyeviti wa Vijiji, ni tatizo. Inafika mahali wako Matajiri wanaotaka ardhi kwa muda mwingi, lakini inafika mahali wakipewa kitu kidogo, yaani rushwa wanachanganyikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufika mwenyewe na hadanganywi. Hadanganywi kwa sababu anaiona ile migogoro inavyokwenda, anaona jinsi ya uhaulishaji wa ardhi na wakati huo basi anafika mahali anaweza kustopisha zile ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri, lakini naomba pia, amalizie ile migogoro ambayo kimsingi iko Manyara na Mbulu. Naamini Mungu atamsaidia, atakuja tena. Najua Tanzania ni kubwa na lazima tuongee *worldwide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naipongeza Wizara, pia naunga mkono hoja hii. Nakuachia pia muda uendelee na Mungu akubariki sana. ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Massay. Tunaendelea na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na baadaye Mheshimiwa Moshi Kakoso ajiandae.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuniona na vilevile nianze kumshukuru Mheshimiwa Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Pombe Magufuli kwa safari hii kutuchagulia Mawaziri majembe. Mheshimiwa Lukuvi wewe ni jembe na Mawaziri wote waliochaguliwa safari hii na Mheshimiwa Dkt. Pombe Magufuli wote ni majembe, mnafanya kazi kwa kujitolea sana, Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Shirika la Nyumba. Shirika la Nyumba linaendeshwa na Mkurugenzi mzuri asiyekuwa na majivuno, mchapakazi mzuri asiyekuwa na makundi. Mungu ambariki sana pale alipo. Nataka kutoa maoni yangu, kwamba katika Shirika la Nyumba kuna matatizo makubwa ambayo inatakiwa Serikali hii ya sasa yashughulikiwe sana. Kuna nyumba ambazo zimejengwa kwa gharama nafuu na kuna nyumba ambazo zimejengwa kwa gharama nafuu ambazo haziwasaidii Watanzania maskini, zinawasaidia watu matajiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu leo hii Wabunge tuliopo hapa ndani ni asilimia 70 ambao wamekuja wapya na kuna asilimia 30 tu ya Wabunge waliokuwepo Bunge lililopita. Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wanakaa kwenye nyumba za Shirika la Nyumba. Leo hii nyumba zile kuwapa Wabunge wapya waingie hawataki, wanakodisha kwa watu. Naomba mlishughulikie suala hili. Kama umeshakuwa Mbunge na umetoka, ukishatoka hapa huna mkataba wa kurudi Bungeni. Ni kwamba mkataba wako umekwisha na ulipewa nyumba na Shirika la Nyumba ili ukae kwa muda ule utakaokuwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge leo anakaa *Guest* au hotelini wakati kuna majumba hapa yamekodishwa kwa watu, wanafanyia biashara ambazo hazina mbele wala nyuma! Naomba Mheshimiwa Waziri hebu fuatilia Shirika lako la Nyumba hasa kule walikotoka Wabunge wa zamani. Zile nyumba ambazo walikuwa wanakaa wenzetu, wapewe Wabunge wapya, wakae na wao waone faida ya hili Shirika. Tunalitetea Shirika hili, lakini halina msaada kwa Wabunge. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kwamba, nyumba nyingi zilizoko Dar es Salaam zimechukuliwa na matajiri. Badala ya kuwasaidia maskini, wanawapangisha matajiri wenzao, wao wanakaa kwenye nyumba zao, zinakuwa ni nyumba tu ambazo zimekaa hazina faida yoyote kwa Watanzania. Sasa maana ya kusema tunajenga nyumba kwa ajili ya Watanzania, faida yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kuna maeneo ambayo wenzetu wa Shirika la Nyumba wamebomoa; maana ya kubomoa maeneo haya ni kwa ajili ya kujenga nyumba mpya. Nashangaa zinakwenda kujengwa nyumba nyingine leo hii Dar es Salaam, Magomeni, kumekuwa pori. Wezi wakiiba usiku, wanakwenda kujificha pale. Si muanze kujenga lile eneo pale ambalo mlibomoa kwa ajili ya kujenga nyumba nyingine!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo pale Tanga. Tanga wamekuja wamebomoa ambazo wazee wa kimaskini walikuwa wanakaa, wakaambiwa kunajengwa nyumba mpya. Leo mwaka wa nne karibuni, nyumba

hazijajengwa. Sasa maana yake ni nini? Kama tunataka kujenga nyumba, basi anzeni kutakasa kwenye miji mikubwa ili ile miji mikubwa iwe mizuri halafu mnarudi huku katika maeneo ambayo mnafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja katika suala la ardhi. Mheshimiwa Waziri, ni msikivu. Tumekuja hapa kuleta malalamiko kwa ajili ya ardhi, siyo kwamba kule kwetu Wakurugenzi wanashindwa kufanya kazi. Kwenye Jimbo langu nimebadilishiwa Wakurugenzi mara sita. Huyo Mkurugenzi atakayefanya kazi ya kuchunguza ardhi hii mpaka aorodheshe alete hapa, akitaka kuleta hapa anaambiwa ahame. Sababu za kuhamisha Wakurugenzi hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika Tanzania nzima, Jimbo ambalo linaongoza, ambalo lina mashamba makubwa ambayo hayaendelezwi ni Korogwe Vijijini. Nashangaa maeneo mengine yanagaiwa. Watu wanapewa maeneo, wanaambiwa hapa Serikali imechukua, Korogwe Vijijini kuna tatizo gani? Kwani haya maeneo kule ni ya nani ambayo Serikali inashindwa kuyatoa kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati alikuja Waziri wa Kilimo wakati ule, alikuja akatoa hati kwamba wananchi wachukue Shamba la Chavda. Leo hii shamba la Chavda limekaa zaidi ya miaka 15 kuwapa watu wa Korogwe waendee hata kulima ni masharti. Leo hii kuna mashamba ya mkonge. Mashamba ya Mkonge ilikuwa ni kuendeleza mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, badala ya kuendeleza mkonge, watu wanafanya biashara zao. Wanaleta watu wengine wanakuja kufanya kazi, wanakuja kupanda mkonge; tena afadhali watengeneze wao. Wanachofanya wao ni kwamba wanangoja wakulima wadogo wadogo wamelima, wao wanakuja kupanda mkonge. Maana yake nini, kama siyo dharau? Serikali sikivu kama hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri, mara ya kwanza niliuliza swali hili na nikaomba kwamba nitoke na Mheshimiwa Waziri aende kule Korogwe akaangalie haki inavyotendeka. Leo hii watu wa Magoma hawana mahali pa kuzikana, shamba wamezungukiwa. Leo hii kuna mgogoro wa kijiji na kijiji, Kata ya Mkomazi; Kata ya Mnyuzi haina mahali, Kata ya Mswaha haina mahali; Makalamo na maeneo mengi. Mashamba 18 mtu mmoja kwenye shamba lao, halafu tunasema wakati huu ni wa Kilimo Kwanza. Watalima wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana na namwamini sana. Tusifanye kazi kwa mazoea. Yeye hafanyi kazi kwa mazoea, ndiyo maana leo hapa kila Mbunge wa Upinzani, kila Mbunge wa CCM anamuunga mkono. Siyo tunakuunga mkono kwa sababu ya sura, bali kwa

muda mfupi ambao smekaa katika Wizara hiyo, smeifanyia kazi nzuri kiasi ambacho hata sisi Wabunge tukimpinga ni kama tunajipinga wenyewe. Nimeona nimwambie suala hili hasa katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga ulikuwa ni mkoa wa zao la mkonge, lakini baadaye mkonge hamna. Leo hii nenda Morogoro, kuna watu wamezuia mashamba makubwa, yasiyokuwa na faida, mtu anakwambia huyu alikuwa ni Waziri. Waziri wakati watu wanakosa ardhi? Kama Waziri alikuwa amechukua shamba, haliendelezi, watu wa Morogoro wanalalamika, wanagombana kila siku kwa sababu ya ardhi na mtu mmoja huyo huyo ana eneo zaidi ya hekta 1,000 na hajapanda hata mahindi; Serikali mna ugumu gani kuyachukua maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nenda Kilimanjaro, watu wanapata shida kama Ndugu yangu Mheshimiwa Selasini alivyosema hapa. Leo hii nimetoka Bukoba, watu wana ardhi nzuri, watu waende kule wakaendeleze ile ardhi kuwasaidia watu wa Bukoba wapande vitu, vionekane. Tusiangalie tu mji mkubwa wa Dar es Salaam, Arusha na Mbeya, angalieni na mikoa midogo midogo ambayo Watanzania wengi wako huko ambapo kuna ardhi ya kutosha lakini hawana mahali pa kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijenga nyumba pale Bukoba Kijijini kwa rafiki yangu Rweikiza unaweza kupata wapangaji wengi tu, lakini watu wanang'ang'ania tu Dar es Salaam, Tanga na sehemu nyingine. Hizi sehemu nyingine kama Wilaya ya Korogwe, hizi Wilaya ndogo ndogo kwa ndugu yangu kule Mheshimiwa Nassari, kuna eneo kubwa kule ambapo nimemsikia hapa, naomba sana Serikali yangu sikivu, kama kweli mnataka kuwasaidia Watanzania, kwanza zichukueni zile nyumba za Wabunge wote ambao hawakurudi ili Wabunge hawa wapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunaomba sana, ile ardhi ambayo imechukuliwa na watu ambapo wanakaa, watu hawana faida yoyote, hawaleti faida yoyote kwa Watanzania, Watanzania maskini wanalalamika kila wakati, hawapati msaada wa aina yoyote, tena ukienda ukiingia unapelekwa Mahakamani na ukifika kule unanyimwa dhamana. Sasa hii biashara ni kuoneana au ndiyo ubinadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngonyani. Tunaendelea na Mheshimiwa Moshi Kakoso na baadaye Mheshimiwa Maulid Mtulia akae tayari.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie kwenye Wizara muhimu ya ardhi. Awali ya yote, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ambaye amefanya kazi nzuri. Tunaamini kazi hii anayoifanya ni kwa manufaa ya Watanzania. Namwomba aongeze jitihada hasa aelekeze na maeneo ambayo yako pembezoni kama Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo migogoro ya ardhi kwenye Mkoa wa Katavi. Mkoa wa Katavi ni mkoa ambao asilimia kubwa sana umemilikiwa na hifadhi za misitu na hifadhi ya Taifa ya Katavi. Karibu vijiji vingi ambavyo vimezunguka mkoa huu viko kwenye migogoro ya ardhi, lakini ni mkoa ambao una ardhi kubwa sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu sana kuelekeza nguvu kwenye maeneo haya ili aje aangalie migogogro ambayo ipo. Ipo kwenye vijiji kadhaa ambavyo viko kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kijiji cha Kabage na Kijiji cha Nkungwi. Vijiji hivi vina migogoro miwili.  Moja, ni mgogoro wa mashamba kati ya wananchi waliomilikishwa ardhi kinyume na utaratibu. Wamechukua ardhi kubwa sana ambayo hawaiendelezi matokeo yake wananchi ndio wanaolima na wanabughudhiwa na wanauawa. Naomba aelekeze nguvu kwenye Kijiji cha Kabage. Yapo mauaji yamefanyika kwa matatizo ya ardhi; ayafuatilie kwa karibu ili tupate suluhisho la mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kwenye Kijiji cha Nkungwi. Kijiji hiki kina tatizo la mgogoro wa ardhi wa Mpairo. Mpairo ni ardhi ambayo imemilikwa na wananchi wachache. Ipo kwenye Serikali ya Kijiji na Serikali ya Wilaya ilishatoa maelekezo lakini bado mgogoro huu ni mkubwa sana. Naomba Serikali iweze kuingilia mgogoro huu ili tuweze kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Nkungwi. Vijiji hivi ambavyo viko kwenye Tarafa ya Mwese, vina tatizo sana la migogoro ya ardhi kati ya Serikali za Vijiji na *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa nia njema iliweka hifadhi kwa manufaa ya Watanzania, lakini bado Serikali hii sikivu imeweka utaratibu wa kuangalia *WMA* kuwashirikisha Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali hasa kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuja, afike Mpanda akamilishe tatizo la migogoro ya ardhi hasa inayosababishwa na *WMA* kuwa na kiburi bila kuwashirikisha wananchi wala kushirikisha Serikali, wanafanya wanavyotaka wao. Hili akilishughulikia atakuwa ametatua tatizo la Vijiji vya Mkabage, Mkungwi, Kasekese, Sibwesa, Kapalamsenga na Kaseganyama. Maeneo haya na mengineyo mengi kwenye Mkoa wa Katavi yana tatizo kubwa hili ambalo atakuwa amesaidia kutoa utatuzi kwenye eneo hili la migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lipo eneo la Vijiji vya Kapanga, Lugonesi na Lwega. Ni tatizo la migogoro ya ardhi ya mipaka ambayo kimsingi kama utatoa maelekezo kama Mheshimiwa Waziri, lina nafasi kubwa sana ya kuweza kutekelezwa kwa sababu ni usimamizi tu unaotakiwa ili kuweza kutoa tatizo hili kwenye vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa amefanya ziara kwenye Mkoa wa Katavi, ajitahidi sana kushirikisha Waheshimiwa Wabunge wamweleze migogoro ya ardhi ambayo ipo. Nikumbushe, wakati wa harakati za kuomba nafasi ya ridhaa ya Uchaguzi Mkuu wa 2015, alikuja na Mheshimiwa Rais, yeye ni shahidi; alisimama eneo moja la Luhafu ambalo lina wakazi 25,000, mpaka sasa wananchi wanaendelea kukaa bila kuwa na amani kwa sababu Serikali imeshindwa kutoa utatuzi wa ardhi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana kutoa maelekezo ya Serikali yatakayowapa manufaa wananchi kwenye maeneo yale ambayo yeye mwenyewe ni shahidi, alifika na alisikia kilio cha wananchi na Mheshimiwa Rais alizungumza na akatoa ridhaa kwa wananchi, akatoa matumaini makubwa sana. Naomba hilo alifuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Shirika la Nyumba. Kwanza nampongeza Mkurugenzi wa Shirika hili kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kizalendo. Naomba sasa Shirika libadili mwelekeo wa kuelekeza ujenzi wa nyumba kwenye maeneo ya Miji Mikuu tu. Namwomba aelekeze kwenye mji ambao unakua sasa hivi, Mji wa Katavi. Tunajua Shirika lipo linafanya kazi vizuri, lakini tunaomba kulishauri shirika hili; kwanza, lijenge nyumba ambazo zitakuwa na thamani inayofanana na watu wanaojengewa nyumba, waweze kumudu gharama za upangishaji au gharama za manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika limekuwa likijenga nyumba kwa gharama kubwa sana kiasi kwamba sasa wanaojengewa nyumba hizi ni baadhi ya wale wachache tu ambao wanaweza wakamudu gharama hizo. Naomba Shirika liangalie mwelekeo mpya ili liweze kujenga nyumba ambazo wananchi wataweza kumudu kukaa na wataweza kuzinunua kwa gharama ambazo zinafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana, kwenye eneo lingine kuna tatizo la uhaba wa wataalam wa ardhi. Kumekuwa na tatizo kubwa sana la uhaba wa wataalam. Eneo la kwetu Mkoa wa Katavi ni sehemu ambayo kuna tatizo kubwa sana la wataalam wanaohusika na suala zima la ardhi na ndiyo maana unakuta miji mingi inajengwa kwa uholela kwa sababu wataalam wanakuwa hawapo na hata kama wapo vitendea kazi vinakuwa havipo.

Naiomba Serikali ielekeze nguvu, itenge fedha za kutosha ili iweze kutoa tatizo la upimaji wa ardhi kwa manufaa ya wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie eneo la hatimiliki. Tunapotaka kuwasaidia wananchi na walio wengi wanaoishi vijijini, ni lazima Serikali ije na mkakati wa kuwezesha wananchi kumiliki ardhi ambayo itawasaidia kuweka masuala yao katika hali nzuri, hasa kwenye dhana ya kukopeshwa. Wananchi wengi wa vijijini hawakopesheki kwa sababu ardhi walizonazo hazijamilikishwa kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ije na mpango wa kuweza kuwasaidia wananchi wapate hatimiliki, hata zile za kimila ziharakishwe kutengenezewa mazingira ili wananchi waweze kumiliki ardhi yao. Maeneo mengi wananchi wanalima, wanafanya shughuli zao za uvuvi lakini hawana kitu ambacho kinaweza kikawasaidia kuwezeshwa na Serikali. Naomba eneo hili lipewe kipaumbele sana kwa sababu ni eneo ambalo linaweza likawasaidia na likawainua wananchi walio wengi, wanaokaa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hotuba ya Waziri wa Ardhi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maulid Mtulia!

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima. Pili, nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba siku ya Alhamisi sawa na tarehe 19 kaka yangu Iddi Mohamed Azzan kwa hiari yake aliamua kufuta kesi ya uchaguzi ya Jimbo la Kinondoni. Namshukuru sana Mungu, namshukuru naye kaka yangu kwa ukomavu, maana sisi watu wa Pwani tunasema "mtu mzima akivuliwa nguo, basi huchutama." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wametoa sifa nyingi sana kwa Mzee wangu, Mzee Lukuvi. Imenipa tabu hata mimi mchangiaji nisije nikaharibu shughuli hii nikaonekana kituko. Kabla sijafika huko, nianze na maswali mawili ambayo naomba Mheshimiwa Lukuvi wakati akifanya majumuisho ayagusie. La kwanza, ujenzi wa mji wetu mpya wa Kinondoni *status* yake ikoje? Wananchi wa Kigamboni wana mashaka, hawajui. Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri atuondoe shaka hii katika majumuisho atakayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, anaonaje; mimi nina mashaka kidogo na hasa ukizingatia sasa tunatarajia au tumeshapitisha kuwa na Manispaa au Wilaya ya Kigamboni. Sasa tutakuwa na *Kigamboni Municipal Council,* lakini vile vile kuna kitu kinaitwa *Kigamboni*

*Development Agency*: Je, hatutakuwa na vyombo viwili vyenye mvutano ili kuhakikisha Kigamboni yetu inakuwa nzuri? Mheshimiwa Waziri naomba anisikilize vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kinondoni, nimekumbwa na suala la bomoa bomoa. Bomoa bomoa ile imenikuta kwenye Kata yangu ya Magomeni, Mtaa wa Kwasuna, Kata yangu ya Hananasif Mtaa wa Kawawa; tena Mtaa umepewa jina la Mzee wetu, namheshimu sana; amepewa Mtaa wa Mabondeni ambapo Serikali wameona pale hawastahili kukaa watu, wakaenda kuvunja bila kujali jina lake walilompa yule mzee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi, siku mbili, tatu nimemsikia kaka yangu Mheshimiwa Waziri January Makamba alikuwa na mkutano wa hadhara kule Segerea, amesema Serikali haina mpango tena wa kuendelea na bomoa bomoa. Vile vile ikasemwa kwamba Serikali ina mpango wa kufanya mabadiliko ya sheria ya mazingira ya kupunguza mita 60 baada ya kuona kwamba utekelezaji wake umekuwa mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo hoja yangu. Hoja yangu ya msingi; hawa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kinondoni nyumba zao zimevunjwa na mbaya zaidi kuna wengine mpaka leo wanaishi pale kwenye vile vibanda. Mheshimiwa Waziri, kibinadamu Serikali lazima ije na suluhisho. Kwa sababu ninavyojua, jukumu la Serikali pamoja na mambo mengine ni kuhakikisha watu wake wanapata mahali pazuri pa kuishi. Sasa wale watu wanaishi kwenye vijumba vibovu pale. Tumevunja nyumba zao nzuri, tumewabakishia vijumba vya mabati. Lazima Serikali itumie au itekeleze wajibu wake kuhakikisha wale watu wanapata mahali pazuri pa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wale watu waliovunjiwa nyumba zao, lazima Serikali ije na mpango, tunawapeleka wapi? Hatuwezi kuwa na Serikali ambayo inapomkuta mtu ana nyumba ya vyumba vitatu na *sitting room,* inamvunjia halafu anabaki kwenye kibanda cha bati. Tulisema tunawavunjia nyumba zao kwa ajili ya usalama, lakini leo wanaishi katika mazingira magumu zaidi kuliko zile tulizovunja. Mheshimiwa Waziri kama atapenda, nina takwimu za watu waliopata maradhi ya shinikizo la damu kutokana tu na nyumba zao kuwekewa *X* na waliopoteza maisha. *(MakofI)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali inatakiwa ihakikishe wananchi hao wanapata mahali pazuri pa kuishi. Nami napenda kushirikiana na Mheshimiwa Waziri katika maeneo yafuatayo:-

Moja, tuna maeneo ya *squatters* kwenye Kata ya Hananasif na Kata ya Tandale. Tukiamua kufanya maendeleo tukabadilisha kutoka *squatters*

tukafanya mji wa kisasa tukajenga majumba marefu, maana yake hawa watu wote waliokaa mabondeni wanaweza kupata mahali pazuri pa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nafikiri Serikali ifike mahali hasa sisi Wabunge wa Mjini ambao hatuna mashamba ya kupewa na Serikali wala sitakuja hapa nikaomba shamba Mheshimiwa Waziri, najua hana shamba la kunipa. Ninachokitaka, ni lazima Serikali tuje na mpango wa namna gani ya kubadilisha makazi yetu haya ya *squatter* tuwe na majumba yaliyokuwa kwenye mpango na majumba ya kwenda juu. Aliweza Mheshimiwa Mzee Karume! Mzee Karume kafanya Zanzibar, sisi tunashindwa kwa sababu gani? Kama tutashindwa kufanya Kinondoni, tunataka tukafanye wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana Shirika lake la Nyumba. Hili Shirika limebadilishwa kabisa kutoka kutengeneza nyumba kwa ajili ya wananchi wanyonge, mpaka sasa wanatengeneza nyumba za kibiashara. Unaambiwa nyumba ya bei nafuu ni sh. 40,000,000 ya bei nafuu ni sh. 60,000,000. Kwa wananchi wetu wenyewe wana uwezo wa kujenga nyumba kwa sh. 30,000,000 ikawa bora kuliko hiyo ya sh. 40,000,000 inayojengwa na Shirika. Sasa kama Shirika hili nalo limekuwa kama la kibepari ambalo lengo lake ni kupata faida, imetokana na lengo la msingi la kuhakikisha wananchi wanapata makazi bora, tena wananchi wanyonge. Kwa kweli Shirika limetoka kwenye mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliwahi kusema Shirika lisijenge tena nyumba za kibiashara, lakini lazima Shirika lirudi lijenge nyumba za bei nafuu kweli ambazo wananchi wa hali ya chini wanaweza kukaa. Siyo nyumba za bei nafuu za kiini macho za sh. 30,000,000 au sh. 40,000,000 ambazo wananchi hawawezi kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ikiamua kutekeleza haya naogopa kusema, Mheshimiwa Lukuvi namheshimu sana mzee wangu, lakini namwomba sana, wale watu wanaoishi pale Kinondoni Mkwajuni wanaiaibisha Serikali yetu. Siyo wa kwenda kuwafukuza! Lazima sasa Serikali ionane na mwakilishi wa wananchi; tuje na mpango wa namna gani tutawaondoa pale ili nao wapate mahali pa kuishi, wasikie. Wakisikia Mheshimiwa Lukuvi ana roho nzuri, anapendwa, anapigiwa makofi na Waheshimiwa Wabunge, nao waone sababu ya Mheshimiwa Lukuvi kupigiwa makofi na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kinondoni niko tayari kushirikiana na Serikali, niko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Waziri kuhakikisha tunalitatua tatizo hili ambalo naamini linanitia aibu kama Mbunge, linamtia aibu yeye kama Waziri na linaitia aibu Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Serikali ya wananchi, madaraka yake imepata kutoka kwa wananchi na lazima itumike kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana na naunga mkono hoja ya Upinzani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtulia. Tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Willy Qambalo na baadaye Mheshimiwa Augustino Masele ajiandae.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuonesha masikitiko yangu kwa Mheshimiwa Waziri. Nimeona kwenye kile kitabu cha migogoro ya ardhi, Wilaya ya Karatu haipo. Nilimkabidhi mmoja wa wahudumu wa hapa ndani orodha ile na nikamsindikiza kwa macho yangu, Mheshimiwa Waziri alikuwa amekaa pale, alimkabidhi na aliisoma. Simlaumu, nimemwandalia orodha nyingine hii hapa ambayo ni *more comprehensive*. Nitampatia baadaye, ikibidi nipige picha ili nipate ushahidi kwamba nimemkabidhi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri imeainisha mamlaka tatu ambazo zinashughulikia masuala ya ardhi. Ziko mamlaka za Halmashauri za Vijiji, iko mamlaka za Halmashauri ya Wilaya na Mji na iko pia Wizara yake. Namwomba Mheshimiwa Waziri asiogope, asihofu. Akiona tunakuja kwake iwe ni kiashiria tosha kwamba wale walioko kule chini wameshindwa. Pia ionekane kwamba inawezekana wale walioko kule chini pia wanachangia katika matatizo yaliyopo. Kwa hiyo, tunakuja kwake kwa kuwa tumeshakata tamaa na wale ambao walipaswa kutusaidia kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo migogoro mingi ya ardhi na migogoro hii mingine imesababishwa na sera. Tunayo ile sera iliyokuja mwaka 1975 ya Operesheni Vijiji, imeleta mkorogano mkubwa sana. Pia migogoro mingine imesababishwa na sisi viongozi wa kisiasa. Pia iko migogoro mingine na ndiyo mingi zaidi, imesababishwa na baadhi ya Watendaji katika ngazi mbalimbali za utendaji wao; Mabwana Ardhi wa Wilaya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, akiona tunakuja kwake awe na amani kabisa. Tuna nia njema, amejaribu, nami naamini hatabadilika, aendelee na kasi hiyo. Tuna imani kiasi fulani kwamba amejaribu na ataendelea na kasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo migogoro mingi sana ya ardhi. Wamesema Wabunge wengine, shida kubwa ya ardhi ya nchi hii, haijapimwa. Kuna shida gani kupima ardhi ya nchi hii na kuwamilikisha wale ambao wanayo? Kitabu cha Waziri kimesema ni asilimia 15 ya ardhi ya Tanzania ndiyo imepangwa na imepimwa, nami naamini hii ni ardhi iliyoko mijini, ardhi kubwa iliyoko vijijini inaonekana haina mwenyewe, lakini ile ardhi ina mwenyewe, yuko yule ambaye ameikalia hadi sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na naishauri Serikali, kama kweli tuna nia ya dhati ya kumaliza migogoro hii au kuipunguza kwa kiwango kikubwa, Serikali ije na mpango madhubuti wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kisheria. Bila kufanya hivyo, migogoro ya ardhi, leo utatatua, kesho utazaliwa mwingine. Kwa hiyo, kila kukicha utaendelea kupata migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana mpango mzuri anaoufanya kule Ulanga na Kilombero; *program* ya upimaji wa ardhi katika zile Wilaya tatu, ni mpango mzuri, lakini atamaliza Tanzania baada ya miaka mingapi? Kama kwa miaka mitatu anafanya mpango wa majaribio katika Wilaya tatu. Anahitaji zaidi ya miaka 50 kupima ardhi ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri na ameandika pale, amesema mpango ule ukifanikiwa utasambaa katika nchi nzima. Majibu anayo, mpango ule lazima ufanikiwe, ikibidi akahamie kule yeye mwenyewe asimamie ile kazi ili ule mpango ufanikiwe ili ardhi ya wananchi ipimwe na wamilikishwe kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la mashamba ya wawekezaji, nchi hii inawaabudu sana hawa watu wanaoitwa wawekezaji. Nimeangalia kwenye kile kitabu iko jumla ya karibu ekari milioni 5.6 ambazo hawa waheshimiwa wamezikalia. Sisi kule Karatu tunayo mashamba 40 ambayo yana jumla ya ekari 45,000 hainingii kwenye akili kwanza kwa nini hawa watu walipewa mashamba haya? Kwa sababu, mashamba mengi wamepewa kwa ajili ya kulima na kufuga, wengi wa hawa ni watu waliotoka nje, hivi tulikuwa tunahitaji mtu atoke Ulaya kuja kufuga hapa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wafugaji wazalendo ambao sasa hivi maisha yao ni kutangatanga na kuhamahama kutafuta malisho kwa sababu, ardhi kubwa imechukuliwa na hawa waheshimiwa. Hawa wawekezaji wamepewa maeneo ambayo ni *very prime,* yana maji, yana rutuba na yana mvua za uhakika. Wananchi wetu wamesukumwa wamekaa maeneo ambayo mvua ni kidogo sana na nimeona mashamba mengine karibu muda ule wa miaka 99 au 71 unakaribia kwisha, naomba hiyo miaka ikiisha mtushirikishe sisi watu wa maeneo hayo wasipewe tena maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hebu atusaidie hivi hawa wawekezaji wanailipa Serikali shilingi ngapi kwa kuwa na maeneo hayo? Kwa sababu, baadhi ya wawekezaji hao badala ya kufanya yale ambayo wamekubaliana kufanya, leo wameyapangisha au kukodisha mashamba hayo kwa watu wengine na wana-*charge* hela nzuri tu! Kule kwetu Karatu eka moja ya shamba hilo lililoko kwenye maeneo mazuri unalikodisha kwa sh. 200,000/= kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipiga mahesabu ya harakaharaka kwa eka 45,000, ungeweza kupata shilingi bilioni tisa kutoka Karatu tu. Mheshimiwa Waziri mashamba yale 40 ya Karatu yanakuletea shilingi ngapi? Nadhani watakuwa wanaletea kidogo sana. Kwa hiyo, niombe na wengi wa hawa wawekezaji wanakaa nje ya nchi, yaani wanakuja tu kupumzikia kule wakati wa baridi kwenye nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mashamba mawili ambayo yamekuwa ni tatizo katika Wilaya ya Karatu; liko shamba la mwekezaji anayeitwa *Acacia Hill* au *Ndamakai Estate*. Mheshimiwa Waziri nina uhakika anayo taarifa ya shamba hili, Mkuu wa Mkoa anazo taarifa, Mkuu wa Wilaya anazo taarifa na hata Mheshimiwa Waziri alipopita Karatu kwa muda mfupi aliambiwa habari ya shamba hili. Huyu bwana ni mbabe, ni katili, ni mkorofi na hata haijui Serikali. Ni mtu wa ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu bwana anamiliki zaidi ya eka 3,840 lakini robo tatu ya eneo hilo halijaendelezwa, limekuwa ni mapori bubu ya kufugia wanyama tembo na wale wengine. Sasa siku hizi ni lazima asubuhi wototo wa shule wasindikizwe ili wasikutane na wanyama hao. Sasa mtu ana eka 3,840 ameendeleza tu robo, tena ameendeleza kwa kahawa ambayo imekwishazeeka, maeneo mengine yote ni pori! Mheshimiwa Waziri lile shamba ni *size* yake naomba aje autengue umiliki wa yule bwana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huyu bwana pia, kwa ukorofi niliousema amediriki kuwanyima wananchi barabara. Barabara ya mita sita kwa kilometa tano ukifanya mahesabu ya eneo ni karibu eka sita. Barabara ambayo inaokoa muda na gharama ya kwenda kijiji cha jirani ambacho ingebidi utumie karibu muda wa masaa mawili kwa umbali wa kilometa karibu 50, yaani kwa kukatiza pale unahitaji dakika 20, lakini huyu bwana kwa ukorofi wake amewanyima wananchi eneo hilo. Kwa hiyo, inabidi wazunguke kutoka Kijiji cha Mang'ola Juu kwenda Kijiji cha Makumba, mtu anaingia gharama ya kwenda kilometa 40 kwa sababu ya ubabe na ukatili wa bwana huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba huyu bwana ashughulikiwe kabla wananchi hawajachukua hatua, kwa sababu yeye anapotaka kwenda mjini anapita kwenye maeneo ya wananchi. Tutamfungia kule kwenye kisiwa na

ataishia kule! Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua za haraka kumnusuru huyu bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko shamba lingine jirani na hapo Mang'ola Juu linaitwa Tembotembo, lina matatizo hayo hayo ni mashamba ambayo yameendelezwa kwa kiwango kidogo sana. Kwa bahati mbaya taarifa ambayo halmashauri imeandaa na taarifa ambayo iko kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri zinakinzana, lakini naamini tutashirikiana, ili kupata taarifa ambazo ni sahihi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri haya mashamba mawili naomba ayachukulie hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la uhakiki wa mipaka ya Ngorongoro.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda umemalizika. Haya, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Allan Kiula na baadaye Mheshimiwa Rashid Shangazi akae tayari.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Ardhi ambayo ni Wizara nyeti kwa sisi ambao bado tuko nyuma kimaendeleo na ambao tunahitaji huduma ya Wizara hii. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na kama walivyotangulia kusema wenzangu, ule mkoba tulioupata una elimu kubwa sana, tukiutumia ule mkoba vizuri, tukasoma, tunaweza tukapata elimu ya kutosha na ikatusaidia sisi kuweza kuwahudumia wananchi wetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ambavyo nimekuwa nazungumza katika uchangiaji wangu wa awali, wilaya mpya zina changamoto kubwa sana. Wilaya ya Mkalama ambayo ni wilaya mpya hatuna Afisa Ardhi Mteule, ambalo ni jambo muhimu sana, tunamhitaji. Tunaye ambaye amehamishiwa pale lakini hajateuliwa kwa hiyo, namwomba Waziri aidha, tupate mwingine kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI au huyo aliyepo ateuliwe, atakuwa ametutendea haki na atakuwa amewatendea haki wananchi wa Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, huduma za Baraza la Ardhi tunatumia kwa wenzetu wa Iramba ya Magharibi, sisi wilaya yetu ilikatwa kutokea huko, kwa hiyo, tuna shida hatuna Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi. Wananchi wangu wa

Mkalama wakitaka kupata huduma hiyo inabidi wasafiri waende Kiomboi walale huko wapate hiyo huduma. Kwa hiyo, tunaomba jambo hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wakati jambo hilo linafanyiwa kazi, tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe kibali au atoe maelekezo, Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi awe anakuja kufanya mashauri hayo kwenye Wilaya yetu ya Mkalama, inaweza ikatusaidia zaidi, ili kuwapunguzia wananchi gharama. Pia na haki kutendeka kwa sababu, wananchi wanaona wao wamekuwa *neglected* kwamba hawapati haki kikamilifu wanapokwenda kule na wala hawasikilizwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo iko migogoro wamezungumza wenzangu hapa migogoro mingi, lakini katika mazingira ya kawaida na kama *machinery* za Serikali, *organ* za Serikali zikiwa zinafanya kazi kawaida haya mambo hayakutakiwa kufika Bungeni wala hayakutakiwa kuzungumziwa hapa, wala hayakutakiwa kufika kwa Mheshimiwa Waziri. Haya mambo tunayozungumza kama Wataalam wangekuwa wamefanya kazi yao vizuri iko migogoro ambayo ingeshamalizwa. Migogoro hii ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya, wakati tunasema tunataka Wilaya au Mkoa upanuke lazima iwekwe miundombinu na wataalam wapelekwe na jambo hilo walimalize na wawashirikishe wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu kuna migogoro mikubwa sana; kuna mgogoro kati ya Wilaya ya Mkalama na Mbulu, kuna mgogoro kati ya Mkalama na Hanang, kuna mgogoro kati ya Mkalama na Singida Vijijini. Jambo hilo limekuwa ni kero kubwa, lakini pia kwa sababu jambo hilo halijafanyiwa kazi kikamilifu unakuta Wilaya moja inakwenda kujenga shule mpakani au inakwenda kujenga kwenye Wilaya nyingine. Sasa imeleta mkanganyiko mkubwa sana tunaomba kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu wako tunawaamini jambo hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iko migogoro ya ndani ya Wilaya nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, wameleta orodha ya migogoro lakini swali nililokuwa najiuliza kuna watu walipewa kazi hii ya kubainisha migogoro mbona migogoro mingine haikuingia? Tafsiri yake ni nini, inanipa picha kwamba, sasa jambo hili linatakiwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe avae viatu aingie vitani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyokuwa tunapiga kampeni, unakumbuka mgombea Urais na Makamu wake walikwenda majimboni, mwingine kushoto mwingine kulia, wanaweza kabisa mwingine akaenda kushoto mwingine kulia na wataalam wao jambo hili katika kipindi hiki likamalizika, kwa maana ya Tanzania nzima watu wenye migogoro. Kwa

sababu, mambo haya hayahitaji *rocket science,* ni mambo ya kiutawala, yanahitaji wafike pale penye mgogoro na wawaelimishe watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko shamba la mifugo linaitwa Makomit, linaleta mgogoro sana katika vijiji vitatu; Kuna Kijiji cha Ishenga, Kijiji cha Kinyangiri na Kijiji cha Kikhonda na nasema ni mgogoro kwa sababu Mbunge siku zote anapita barabara hiyo. Kama walivyosema Wabunge wengine waliopita hapa ni kwamba, viongozi waliokuwepo si Wakuu wa Wilaya ama Wakurugenzi, wanakuja wanafanya kazi, wanafanya mikutano ya ujirani mwema, wanahama. Wanapohama mgogoro wanauacha palepale, anapokuja mtu mpya au kiongozi mpya, mtaalam mpya anaanza jambo hilo upya, sasa jambo hilo limekuwa gumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nafikiri wale watu hawana *muscles* za kutatua hii migogoro, sasa *muscles* hizo ziko Wizarani, Wizara tunaomba itume watu makini waimalize hii migogoro na sisi tuwe Wabunge kwa amani kwa sababu, moja ya changamoto ambayo tunapata ni jinsi tutakavyoimaliza hiyo migogoro. Tusipoimaliza inakuwa ni changamoto kubwa sana, hilo ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, wamezungumza wenzangu suala la sehemu zinaitwa *business centres,* hizi *business centres* zinakua kwa haraka sana, maeneo hayo yaje yapimwe, mipango miji iwekwe kwa sababu, baada ya muda nako vijijini kutakuwa na *squatters* kama zilivyo Dar-es-Salaam na maeneo mengine, lakini ni jambo ambalo linaweza likafanyiwa kazi mara moja na lenyewe likamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza Hati za Kimila; Hati za Kimila zitolewe turasimishe hayo maeneo ili hao ndugu zetu, wananchi wetu tunaowaongoza waweze kukopesheka, lakini pia, waweze kutambuliwa na tuweze kumaliza migogoro midogo midogo ambayo inazunguka mazingira yetu. Mambo haya yanawezekana kabisa kwa makabrasha mliyotupa hapa, inaonekana Wizara ya Ardhi ina wataalam wa kutosha na tuna imani hiyo na katika Serikali hii ya Awamu ya Tano tunataka tuone hayo mabadiliko ili na sisi tuwe tunatembea vifua mbele tujue migogoro hiyo imemalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, “yuko mtani wangu mmoja anaitwa Mheshimiwa Waitara” anafikiri Dar-es-Salaam anakaa peke yake. Mimi nakaa Dar-es-Salaam vilevile na nakaa Kimara, eneo la Kimara lirasimishwe watu wapewe maelekezo maeneo yao yatambuliwe. Maeneo yao yakitambuliwa labda wanatakiwa kuhama waambiwe kwa sababu, huwa linakuja suala watu tunaanza kubomolewa nyumba zetu kule na mimi nina nyumba kule tunaanza kuleta mgogoro. Kwa hiyo, tunaomba jambo hili na lenyewe liweze kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uko mgogoro mwingine kati ya sisi na Simiyu, ule Mto Sibiti unahama kwa hiyo, mto unapohama na mpaka unahama vilevile. Kwa hiyo, ni muhimu wananchi wetu wakaelekezwa mpaka uko wapi na pande zote mbili hizo zikashirikishwa na sisi kama Wabunge wa maeneo yote niliyoyataja hapa tuweze kushirikishwa ili tuweze kukaa kwa amani na tuweze kuwatumikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba na lenyewe tunalialika waje Mkalama, wilaya ile ni mpya kuna wafanyakazi wengi, zaidi ya wafanyakazi 100, hawana mahali pa kuishi. Mkija mkijenga kule na eneo tutawapatia, mtakuwa mmetusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hizi nyumba zinazojengwa zinazouzwa wanazoziita za gharama nafuu ziangaliwe, ziko nyumba zimejengwa pale Singida zimebananabanana, unajua utamaduni wa mikoani na mjini uko tofauti, *designing* ibadilike; halafu thamani ya milioni 40 au milioni 50 ionekane, kwamba hii ni milioni 40 na hii ni milioni 50. Bado *opportunity* iko kubwa wanaweza wakapanuka zaidi na Shirika letu la Nyumba likaweza kusaidia zaidi Taifa letu hili na watu wanaona kazi ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ujumbe wangu umefika, maana tunasema ni muda wa kazi tu, hatuna mambo mengi sana hapa, unafikisha hoja zako unatulia. Naunga mkono hoja, asanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Allan. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Kiteto Koshuma na baadaye Mheshimiwa Daniel Mtuka ajiandae.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuipongeza Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na hasahasa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Lukuvi pamoja na Mheshimiwa Mama yangu Mama Angelina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea suala zima la *National Housing,* kama walivyochangia Wabunge wengi kuhusiana na suala la *National Housing* kujenga nyumba ambazo zinaonekana ni nyumba za bei nafuu kwa kinadharia tu, lakini nyumba hizi si kwa ajili ya wale wananchi wasiojiweza kwa sababu, nyumba hizi za *National Housing* ni nyumba ambazo ni za gharama sana. Kwa mfano, katika Hotuba yake Mheshimiwa Waziri *page number* 58 mpaka *page number* 61 ameonesha kwamba nyumba za *National Housing* zinajengwa ili kuweza kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia hapa mfano Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Ilemela tunazo nyumba za *National Housing* ambazo zimejengwa Buswelu. Nyumba hizi zilikuwa ni nyumba nzuri, lakini sasa zinauzwa bei ya juu, zinauzwa kwa gharama ya shilingi milioni 80, sasa najiuliza je, mwananchi wa hali ya kawaida, hali ya chini, anao uwezo wa kununua nyumba ya shilingi milioni 80?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwambia kwamba, aende kuchukua mkopo benki, tunafahamu wote kwamba, unapoenda kuchukua mkopo benki unaulipa kwa riba. Hivi kweli, je, tunaposema hii nyumba inauzwa milioni 80 mwananchi huyu aende kuchukua mkopo benki unakuwa umemsaidia mwananchi wa hali ya chini au unakuwa sasa umezidi kumgandamiza. Hii ni kwa sababu, anapokwenda kuchukua mkopo benki riba itakuwa ni kubwa; akikopa milioni 80 anaweza akarudisha milioni 120 kwa hesabu za harakaharaka kwa sababu, mimi pia ni mtaalam wa masuala ya benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi naishauri Serikali iweze kusaidia shirika hili. Kwa mfano, shirika hili ukiangalia mara nyingi wanasema kwamba, nyumba hizi zinakuwa ni za gharama kwa sababu ya kupitisha miundombinu kwa sababu halmashauri zinakuwa zimewapa eneo lakini miundombinu kama vile maji, umeme, barabara, inakuwa haipo. Kwa hiyo, nashauri kwamba, basi Serikali au Wizara husika isaidie kupitisha miundombinu ya barabara, maji pamoja na umeme, ili pale shirika hili linapoanza kujenga hizo nyumba basi ziwe za bei rahisi, ili kuweza kuwakwamua wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, niweze kuishauri Serikali kwamba, Shirika la *National Housing* liweze kujenga nyumba za bei nafuu kwenye makazi ya vijijini kwa sababu, vijijini ndiko sehemu ambako tuseme asilimia kubwa ya wananchi hapa nchini Tanzania wanaishi, lakini makazi yao bado ni duni sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali kupitia Shirika lake hili la *National Housing* kujenga makazi ya bei nafuu huko vijijini.

Mheshimiwa Mweyekiti, lakini pia, ukiangalia sehemu nyingi za vijijini tayari kunakuwa kuna makazi yamekwishajengwa pale, kulikoni Serikali iende kujenga sehemu nyingine, naishauri Serikali kwamba, itumie lile eneo la kijiji husika kubomoa zile nyumba zilizopo kwa  kuwapa elimu wananchi kwamba, ni kwa nini nyumba zinabomolewa, lakini kuweza kunyanyua majengo aidha ya magorofa au majengo ya kawaida, ili wananchi wa eneo hilo waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maeneo mengi ya watu wanaoishi vijijini ni wakulima. Kwa hiyo, watakapokuwa wamejenga nyumba zile wananchi wanaweza wakapangishwa au wakauziwa kwa bei nafuu na wakulima hawa

wakaweza kulipa kidogo kidogo hatimaye kumaliza deni na nyumba kuwa za kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la *squatters, squatter* imekuwa ni suala ambalo ni sugu sana hapa nchini Tanzania. Naishauri Serikali kwamba, izisaidie fedha Halmashauri, ili ziweze kusaidia kurasimisha makazi na hii inaweza ikasaidia Serikali pia kupata mapato kwa sababu, katika hizi *squatter* hawa wananchi wanalipa tu mapato kwa Halmashauri lakini Serikali inakosa mapato kwa kupitia *property tax.* Kwa hiyo, nashauri Serikali iweze kuzisaidia halmashauri hususan Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Ilemela, watusaidie fedha kwa ajili ya kurasimisha makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia wakazi wa Mkoa wa Mwanza wanaishi sana kwenye milima, matokeo yake tunaona *disaster* zinatokea, wananchi wanaangukiwa na mawe. Kwa hiyo, utaona kama maeneo yale yakiweza kupimwa na Serikali na kuweza kurasimishwa kwa wananchi kihalali, basi tutakuwa tumeondokana na hizo *disaster* za wananchi kuangukiwa na mawe pia hata kuondoa hili suala zima la bomoabomoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikijiuliza, kuna tatizo moja limetokea hapo Mkoani Mwanza, Wilaya ya Ilemela, kuna rada imejengwa katika Mlima wa Kiseke, rada ile imesababisha makazi 500 sasa yatakwenda kubomolewa ili kupisha rada hiyo ya Mlima huo wa Kiseke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza, hivi wakati hawa wananchi wanaanza kujenga kuanzia nyumba ya kwanza mpaka zimefika nyumba 500 na sasa zinahitajika kubomolewa, Serikali ilikuwa wapi? Haikuwaona hawa wananchi toka wanaanza kujenga nyumba moja mpaka zinafika nyumba 500? Leo hii waseme kwamba, wanataka kuzibomoa nyumba hizo, ili wananchi hawa wapishe eneo hilo la rada, kwa sababu, kwa kweli ni eneo ambalo limekuwa ni hatarishi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri sana Serikali, wananchi wanapovamia sehemu moja kwenda kujenga, basi mwananchi wa kwanza anapoanza kujenga ile nyumba moja, Serikali iweze kutoa elimu kwa wale wananchi, ili wasiendelee kuathirika pale nyumba zinapokuwa nyingi na hatimaye kubomolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, mtakapokuja kuhitimisha hoja hii mnisaidie tu kunipa majibu kwamba, je Wananchi wale wa Kiseke wategemee nini? Je, watalipwa fidia? Kama watalipwa fidia, ni vigezo gani vitatumika kuangalia katika kulipa fidia hizo? Hilo naomba sana mnisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuongelea suala zima la hizi mashine ambazo zilitolewa na Shirika la *National Housing,* mashine za kufyatulia matofali kwa vijana wetu. Ukiangalia mashine hizi za kufyatulia matofali kwa kweli zina malengo mazuri tu; kwanza ni kupata ajira kwa vijana, lakini pili, kujenga nyumba ambazo ni za bei nafuu na pia ni imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vijana hawa wameshindwa kupata soko la kuuza haya matofali ambayo wamepatiwa hizo mashine na hatimaye hata kuna mikoa ambayo iliathirika na wakanyanganywa hizo mashine kwa mfano Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini je, Serikali kwa nini inashindwa kuwasaidia hawa vijana ili wanapokuwa wanafatua yale matofali basi wapate tenda hususani kwenye halmashauri zetu, wapate tenda za kujenga. Lakini unakuta kwamba kwenye halmashauri wanatoa tenda kwa watu wengine na wanatumia matofali haya ya kufyatua ya kawaida. Hivi hawa vijana ambao mmewapa hizi mashine kwa nini Serikali isiwasaidie ili na wao waweze kujiendeleza? Pia na hizi Halmashauri nazisihi kwamba ziendelee kutoa mitaji kwa hawa vijana ambao wamegawiwa hizo mashine za kufyatua matofali ili waweze kusaidia kufyatua matofali mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sikuwa na mengi, ni hayo tu, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiteto na sasa namwita Mheshimiwa Daniel Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii kutoa mchango wangu mdogo. Niseme tu jambo moja kwamba nimepitia hotuba ya Bajeti ya Wizara hii, nimepitia hili begi ambalo tumepewa, nilikesha, nimesoma vizuri sana. Nimepata matumaini makubwa sana kama mtaalam wa ardhi tumetukanwa kwa miaka mingi kwamba hatufanyi chochote, kazi zetu ni kusababisha migogoro, kuuza viwanja na kadhalika, lakini nimepata matumaini makubwa niliposoma makabrasha haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kitu kimoja kwamba nimeridhika sana na kitabu hiki cha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi. Hili ndilo suluhisho pekee, hiki kitabu ndilo suluhisho pekee la migogoro na kila mmoja sasa tukitekeleza hili tutaishi kwa amani katika nchi hii na kila mmoja atafaidi kipande cha Ardhi ambacho atapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri yafuatayo ili kutekeleza mpango huu:-

Kwanza, naomba tutunge sheria moja tu inayo-*govern* suala la ardhi. Hatuhitaji Sheria ya Ardhi namba tano ya Vijiji, sheria namba tano ya vijiji tunaomba tuifute, inaleta migogoro mingi na ardhi ya vijiji ni sehemu kubwa kuliko hata ile nyingine iliyobaki. Hatuwezi kusema ardhi ya vijiji, ya mjini ardhi ni ardhi tu, tafadhali sana tukishatunga sheria hii utekelezaji wa sheria ufuatwe. Kila mmoja wetu, Mbunge, watendaji, wale watu wa vijijini naomba tutekeleze Sheria ya Ardhi, tusimamie utekelezaji wa ardhi. Sheria nyingi nzuri zimetungwa ziko kwenye makabrasha, sheria nyingi nzuri lakini bila utekelezaji, ni kazi bure, naomba hili mlishike sana wenzetu mliopewa dhamana hii kwa maana ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye mpango huu, tuajiri wataalam wa kutosha wanaoshughulikia mambo haya. Vyuo vyetu vimetoa watu wa kutosha, Chuo Kikuu cha Ardhi, Morogoro, Tabora wametoa wataalam wa kutosha, wako mitaani tunawaona. Ajirini wataalam hawa waje kusimamia mpango huu. Inatia mashaka na inasikitisha sana mnapounda mabaraza vijijini mnakamata tu wazee pale kwamba wewe mzee ndiyo utakuwa Mwenyekiti. Hivi unaweza ukaenda *dispensary* pale ukakuta tu mzee anatibu hajasomea uganga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kule mahakamani unakuta tu mtu anatoa hukumu hajasoma mambo ya Sheria? Kwa nini tunakabidhi suala hili zito la ardhi watu ambao hawajasoma? Yaani ardhi tunaidharau kiasi hiki? Ardhi ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wataalam wa-*play* kila mahali kuanzia vijijini mpaka huku Taifa. Watu wamesoma, hii ardhi ni taaluma hatuwezi kucheza na ardhi, hatuwezi kukabidhi mtu ambaye hana ajira na hana *liability* yoyote yaani hatuwezi kumbana. Unapomwajiri mtu ambaye ni mtaalam atakuwa anasema mimi ni mtaalam, lakini pia nimeajiriwa, nalinda kibarua changu. Sasa unampa tu mtu unamkamata barabarani wewe utakuwa mshauri kwenye Baraza la Ardhi haiwezekani, *liability* iko wapi, lazima atavuruga tu ndiyo maana ya kwenda shule, naomba tulizingatie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishakwenda kwenye mpango huu maana yake ni kwamba, sasa tukapime ardhi ya nchi nzima. Nimepitia kwenye mpango huu nadhani kuna *pilot project* kwenye wilaya karibu 63, mmeweka mipango hii, lakini nasema hivi tukapime nchi nzima, siyo wilaya kadhaa, wala manispaa kadhaa , wala halmashauri kadhaa, twendeni tukapime nchi nzima, tutumie wataalam wetu kwenye halmashauri zetu, wapo wataalam, kama hawapo tuajiri kama nilivyosema tukaipime nchi nzima ipimwe sasa siyo kupima maeneo mengine na maeneo mengine kuachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimefurahishwa kwenye mpango huu, jambo ambalo litatuondolea migogoro ni kwamba, tupime ardhi kwa uwiano hasa ardhi ya kilimo na ardhi ya ufugaji ipimwe kwa uwiano. Fanya sensa ya mifugo mahali, angalia ardhi iliyopo pima ile ardhi wagawiwe wafugaji kwa mujibu wa idadi yao na idadi ya mifugo na ardhi iliyopo. Hesabu wakulima wako wangapi, pima ardhi iliyopo kwa ajili ya kilimo kwenye eneo husika kama ni wilaya kama ni kijiji igawe ardhi kwa uwiano wa idadi ya wakulima waliopo hilo litaondoa migogoro, tugawe ardhi kwa uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nadhani tukienda hivyo migogoro haitakuwepo na iwekwe kwenye sheria hii ambayo tunakwenda kuitunga hasa kwenye kilimo na ufugaji kumekuwa na mgogoro mkubwa sana, gaweni ardhi kwa uwiano. Siyo mfugaji mmoja anayemiliki maekari na maekari na wengine hawana ardhi. Mkulima mmoja anamiliki maekari na maekari wengine hawana ardhi katika kijiji, tugawe ardhi sasa kwa uwiano, kwa mujibu wa sheria na tusimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *change of land use*, hasa nazungumzia eneo ambalo limepimwa. Suala hili limekuwa na mgogoro mkubwa sana, sheria zimetenga kabisa upimaji ule kwa mfano kwenye miji umetenga maeneo mazuri, maeneo ya makazi, ya biashara, ya viwanda na ya kumwaga takataka. Zile *plan* zinakuwa vizuri mnapoanza. Kwa mfano, mradi wa viwanja 20,000 ukiuangalia zile ramani ziko vizuri lakini ukienda sasa hivi kwenye utekelezaji yaani ile *plan* imeshavurugika tayari watu wanabadilisha matumizi ya ardhi bila utaratibu. Sheria ipo ya kubadilisha matumizi kwa kufuata sheria na kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nenda kwenye makazi ya watu miziki inadundwa mpaka saa nane, saa tisa za usiku kwenye maeneo ya makazi. *Petrol station* zinajengwa kwenye maeneo ya makazi kinyume na ile *plan* ya zamani. Watu wabadilishe matumizi ya ardhi kutokana na sheria na sheria ipo tulinde *plan* zetu maeneo ya wazi yameshajengwa, yanavamiwa hovyo. Eneo lilitengwa kwa ajili ya shule, watu wamejenga maeneo ya biashara tunakwenda wapi, mbona sheria zipo? *Enforcement of laws* ni jambo la muhimu sana katika ku-*plan* mambo ya ardhi, naomba sana tuzingatie.

Mheshimiwa Mwenyekitii, mwisho, kule kwangu Manyoni kuna mgogoro wa ardhi, kati ya wananchi na Hifadhi ya Muhesi-Kizigo, ndiyo haya mambo niliyokuwa nayazungumza. Mgogoro wetu ni tofauti kidogo na maeneo mengine, sisi tunagombana na hifadhi kwa sababu ile hifadhi walitunyanganya lile eneo wakapanua ule mpaka wakala kijiji, wakala maeneo ya malisho ya mifugo, wakala maeneo ya kilimo kule Manyoni. Huo ndiyo mgogoro wetu, sisi hatuombi kuongezewa kumega hifadhi hapana, tunaomba mpaka wetu ule wa zamani urudishwe, hilo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha huu mgogoro wa Muhesi Kizigo na wananchi wa Manyoni wanaoishi pembezoni mwa ule mpaka, wanaomba sana warudishieni ule mpaka wa zamani, yale mashamba yao yamebanwa, hawana pia maeneo ya kulisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna unyama mkubwa sana wa hawa wenzetu wanaolinda yale maeneo, nadhani hili linamhusu Profesa Maghembe, hili eneo Wizara ya Maliasili na Utalii kile kikosi wanaenda kinyume kabisa na sheria za kibinadamu. Unakuta mtu amejenga nyumba, ameweka makenchi yake, wanapanda juu wanashusha makenchi, hizo kenchi unajuaje kama mtu alinunua mbao zimegongwa mihuri wa kibali au hapana mtu amepandisha kenchi wewe unaenda unashusha, kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ameshachonga madirisha mnakwenda mnachukua yale madirisha mnapiga watu, mama tu ameingia kuchukua kuni pale anapigwa mpaka anazimia na anakwenda kufunguliwa kesi. Ninazo kesi nyingi pale Manyoni yaani kuna watu wamejaa pale kwenye mahabusu ya Manyoni. Hivi ni balaa kupakana na hifadhi? Naomba tafadhali sana hebu tufuate sheria na toeni pia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ule mpaka haujulikani, yaani ukienda nioneshenі mpaka hifadhi ni wapi inapoanzia na kile kijiji kinapoanzia hawawezi kuonesha. Kwa hiyo, naomba sana wana Manyoni wanasema rudisheni ule mpaka wa zamani kule ambako ulikuwepo, muwaachie mashamba yao na eneo lao la kulima. Pia wekeni ule mpaka unaoonekana, pandeni hata miti, kule Bukoba wanaita *bilamla*, kule Manyoni tunaita *machito*, weka mpaka hata chimbia hata miti, hata vile vinguzo, panda hata minyaa angalau kuwe na mpaka unaoonekana kwamba hapa ndiyo mwisho, hii itapunguza sana migogoro.

Mheshimiwa Mweyekiti, mwisho kabisa, nirudie kwa kutoa wito kwamba mpango huu ni mzuri tujipange vizuri kama nchi twendeni tukaipime Tanzania, tuiweke kwenye ramani, tuepushe migogoro, mpango huu unatekelezeka na ni mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda siyo rafiki sana tutaendelea na wachangiaji wengine jioni na tutaanza na Mheshimiwa Kunti Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Dkt. Godwin Mollel na huku wengine tutaendelea na Mheshimiwa

Zainabu Katimba, Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mheshimiwa Felister Bura, Juliana Shonza na Mheshimiwa Rose Tweve.

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa tena kikao cha muhimu cha Wabunge wote wa CCM mara baada ya kuahirisha Bunge kwenye ukumbi wa Msekwa. Pia Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla anawatangazia matokeo ya mechi iliyochezwa siku ya Jumamosi kati ya Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wa Bunge, kwamba Waheshimiwa Wabunge kwa mchezo wa mpira wa miguu tulitoka sifuri na wafanyakazi wa Bunge walipata moja.

Kwa hiyo niwapongeze wafanyakazi wa Bunge ingawa na Wabunge wamejitahidi pia. Vile vile kwenye mpira wa *Netball* Waheshimiwa Wabunge tulipata magoli 22 na wafanyakazi wa Bunge 20. Kwa hiyo, Wabunge akinamama tumeweza, hongereni sana. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda umefika mwisho, naomba nisitishe Bunge hadi saa kumi kamili leo jioni.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka*
*Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na mjadala, wachangiaji wetu wa jioni hii, nitaanza na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kupata fursa ya kuchangia Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi. Naomba nianze kuchangia Wizara hii, kwenye suala zima la migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la migogoro niseme tu Mheshimiwa Lukuvi amepata pongezi nyingi, lakini kwa Mkoa wa Dodoma kwa kweli kazi bado anayo. Nasema kazi bado anayo kwa sababu Mheshimiwa Lukuvi, atasema mambo kadhaa nitakayoyazungumza hapa hayahusiani na Wizara yake, lakini yeye ndiye tunajua Wizara yake inahusika na suala zima la makazi, bila ardhi makazi hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa yetu ya Dodoma, kuna kitu ambacho kinataka kuja kutengenezwa kinachofanana na kinachokuja kutengenezwa hapa *KDA*. Sisi Dodoma tuna msalaba unaitwa *CDA*, hii *CDA* ilianzishwa mnamo mwaka1973 kwa madhumuni na malengo ya kwenda kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kuja Manispaa ya Dodoma ama Mkoa wa Dodoma. Yapata leo miaka 43 makao makuu yapo ya chama tu, ya Serikali hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize Serikali mko hapa *team* nzima, huyo Waziri Mkuu yuko hapa mwakilishi wake, lakini Wizara mbalimbali ziko hapa. Wana Manispaa ya Dodoma wanataka kujua, kama suala zima la uanzishwaji wa kitu kinachoitwa *CDA*, ilikuwa dhumuni lake na malengo yake ni kwa ajili ya kuleta, Makao Makuu Dodoma imeshindikana, kwa nini hii *CDA* isirudi Dar es Salaam ambako ndiko kuna makao makuu ya nchi? Badala yake kuendelea kuwatesa na hao Watanzania wasio kuwa na hatia yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CDA* ilikuja ili ipange mji wetu vizuri, igawe viwanja vyetu lakini pili, iweze kuwapatia wananchi wa Manispaa ya Dodoma ardhi, waweze kuiendeleza, waweze kupata makazi yaliyo bora. Leo wananchi wa Manispaa ya Dodoma, hawana ardhi ambayo wamemilikishwa na *CDA* badala yake wamegeuzwa kuwa watumwa ndani ya wilaya yao, wanaitwa wavamizi kila kunapokucha wanabomolewa nyumba zao. Inasikitisha sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, wananchi hawa bila huruma *CDA* imekuja tangu mwaka 1973 kuna watu walikuwepo tangu mwaka 1959 kabla hata ya Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Njedengwa pale walienda kuwavunjia watu wakampa eneo mtu mmoja tu, anaitwa Maimu, wakavunja nyumba 127, wakampatia maekari mtu mmoja anaitwa Maimu pale. Wananchi wetu wakawaacha hewani, wanateseka halafu leo wanataka kuendelea kuwashawishi Watanzania wa Manispaa ya Dodoma wabaki na *CDA,* hawaitaki *CDA* chukueni pelekeni kwenu, mnakoona kunafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii nimeona hapa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, migogoro iliyoripotiwa ni migogoro miwili tu, (d) *center* na (c)*center*, si kweli. Nami nimshukuru Mheshimiwa Waziri hili begi lake alilonipa nimeweka haya ma-*document* ya *CDA,* ya wananchi haya, yako humu yamejaa haya humu, haya nimemletea. Mimi hili begi kazi yake nitakuwa nabeba makablasha ya wananchi, wanaoandika barua kwenye Ofisi zenu hamuwajibu, mnaitetea *CDA*, mnaenda mnakaa kwenye vikao vya Bodi ya *CDA* mnawaangamiza Watanzania wa Manispaa ya Dodoma, wamewakoseeni nini? Kwa nini mnawanyanyasa hawa watu kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapimieni ardhi, wapeni ramani zenu, wapeni waende wakajenge, watu wanahangaika barabarani wanauza machungwa akinamama wajane, wana watoto wanasomesha, wanakwenda wanajijengea nyumba zao, mnaenda mnawavunjiwa, mnawaambia wavamizi. Mnachotaka ni nini, kuwaua? Waueni basi tujue moja kama hamuwataki, watu hao hao ndiyo wanaendelea kuwasitirini ninyi kupata kura, halafu bado mnaleta blabla hapa, za kuendelea kuwanyanyasa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii mlipiga magoti na kupiga *push up* mwaka 2015 mwaka jana, 2020 nahisi mtaruka kichura chura. Kwa sababu hawa watu hawako tayari kuendelea na mateso haya na mwakilishi wa Waziri Mkuu aliyeko hapa, wananchi wa Kata zote 41 za Manispaa ya Dodoma, wanahitaji kukutana na ofisi ya Waziri Mkuu, ili waeleze manyanyaso na mateso wanayoyapata na hawa watumishi wa *CDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CDA* haisimamiwi na mtu yeyote ipo tu ina-*hang* hapo, inajifanyia mambo inavyotaka, inafunga ofisi tarehe 2 Februari, wamefunga ofisi eti kisa mfagizi kafiwa na mume wake, sisi mbona huwa hatuahirishi Bunge hapa mama yangu Stella amefiwa, mbona hatujaahirisha Bunge ili twende tukamzike mama yake Stella. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mume wa mfagizi wa *CDA* kafiwa wamefunga ofisi ambayo inahudumia zaidi ya watu 40,000 kweli ni mateso gani mnayowatesa hawa watu. Wana kikao tu cha kawaida cha kikazi wanafunga ofisi eti wamekwenda kwenye kikao, hawa watu kwa nini mnawaendekeza kiasi hiki? Hiki kiburi mnawapa ninyi Serikali. Laiti mngeamua kuwasimamia na mkawaambia lengo na madhumuni ya kuanzishwa kwa *CDA* wangeshika adabu, wangefuata Kanuni na taratibu za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wetu wanakwenda wanachukua ardhi zao, wakichukua ardhi badala ya kwenda kuwafanyia maboresho ya ardhi pale wawapimie watu mahali walipo, hawawapimii mahali wanawaambia tunapima upya. Wanawafukuza kwenye maeneo yao, wanaenda wanapima vile viwanja, wakipima viwanja wanawalipa fidia laki tano, kiwanja kinaenda kuuzwa milioni tano ama milioni nane, mwananchi gani anaenda kupata hiyo milioni nane ya kununua kiwanja. Ardhi umemkuta nayo mwenyewe, wana mashamba yao yaliyokuwa enzi na enzi, walikuwa wanayatumia kulima ardhi ya Dodoma hii haiongezeki inapungua, ila watu tunaongezeka. Kwa hiyo, ni lazima *CDA* muiambie na itambue, kwamba wanahitaji siku ngapi wakamilishe upimaji wa ardhi Manispaa ya Dodoma wafungashe vilago vyao waende wanakotaka kwenda, sisi Dodoma hapa tumechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawezi kufanya hiyo kazi, Mheshimiwa Lukuvi na Waziri Mkuu, wananchi wa Dodoma watakachokuja kukifanya wasije wakaleta lawama, wamechoka kunyanyaswa na mateso ya *CDA*. Hilo nimemaliza kwenye *CDA,* naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wangu wanataka kukutana na Waziri Mwenye dhamana na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu Wabunge wa Majimbo hususani Jimbo la Dodoma Mjini, mmekuwa mkiwafunga midomo wasisemee suala la *CDA*. Alianza hapa Malole mwaka juzi mkamfunga zipu, eti ooh usiongee kwani ni ya nani, kama ni ya kwenu si mseme, kama na ninyi mnanufaika humo semeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro ya Swagaswaga ambayo najua iko kwa Mheshimiwa Maghembe, lakini suala lile la Swagaswaga, Mkungunero Dagram A mgogoro wa uliopo katika mpaka wa Chemba na Kiteto. Tunahitaji mpaka ule Waziri akautatue. Bunge la mwezi wa Pili, wazee wa watu walitoka Wilaya ya Chemba, wakaja kumwona Mheshimiwa Waziri wakamwelezea hali halisi iliyoko pale kati ya mgogoro wa Chemba na Kiteto, Mheshimiwa Waziri hata ile wakawapa maneno matamu, wakawarudisha wazee wa watu na wakawaahidi Waziri Mkuu anakwenda. Mpaka leo Waziri Mkuu hajawahi kukanyaga, wala harufu tu ya kusikia kwamba atakuja kwenda haipo, kwa nini wanawadharau hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawawezi kushughulikia, wawambie wajichukulie hatua wenyewe watajua nini cha kufanya huko, mpaka wasubiri watu wafe ndio wataona ving'ora na magari 42 yanafukuzana yanakwenda kuangalia maiti za watu kule. Kwa nini mnafanya namna hii ninyi? Wananchi wa Dodoma wamewakoseeni nini? Tuambieni kama kuna makosa ambayo tumewakosea tuwaombeni radhi, ili na sisi tuweze kupata haki ya kuhudumiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kama maeneo mengine.

Maeneo mengine umefanya, Dodoma kwetu wewe ni sifuri na mbaya zaidi ulikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma hii, usichokijua ni nini wewe Mheshimiwa Lukuvi, kipi usijchokijua kwa Dodoma hii ambayo umekaa kimya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ongea na kiti, elekeza kwenye kiti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ni mzuka tu! Suala la nyumba huko Swagaswaga na wapi huko niwaombe tu mwende wananchi wale, wazee wa watu wanalalamika huko, dharau hawazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba, wakati Kamati zinaundwa nilikuwa mjumbe wa Kamati hiyo kabla sijabadilishwa, nilikwenda kuona nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba, nyumba zile sijui maana yake

tulipoziona zilikuwa hazijaisha lakini tukaambiwa zikiisha zitakuwa nzuri, sasa sijui zinakuwaje nzuri kabla ya kwisha sijaelewa, chumba kinachokwenda kuwekwa mtu pale ukiweka kitanda cha futi tatu na nusu, utaweka na meza ndogo ya kuwekea mafuta ya kupaka, labda na kitana na dawa ya mswaki. Chumba huwezi kuweka kitanda cha tano kwa sita, nani siku hizi analeta biashara ya mbanano kwenye vyumba, vyumba vya kulala havina hadhi… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Anafuatiwa na Mheshimiwa Halima Jemes Mdee na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa natoa mchango wangu nitambue mchakato unaoendelea Chasimba, wananchi wangu wameanza mchakato wa kupatiwa hati, kwa hiyo kwa hili mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, nampongeza sana Mheshimiwa Lukuvi kwa hili, kwa sababu wananchi wale takribani elfu ishirini walikuwa wanatakiwa kuondoka, lakini sasa hivi wameanza kupata matumaini na wanapatiwa hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile natambua mradi mkubwa wa Shirika la Nyumba unaoendelea Jimbo la Kawe, eneo lililokuwa la Tanganyika Packers, baada ya mapambano ya muda mrefu, kuokoa lile eneo kutoka kwa wanyang'anyi wanchache, tumefanikiwa limerudishwa chini ya Shirika letu la Nyumba. Vile vile wako pamoja na mwekezaji, kuna maendeleo wanafanya pale, kwa hiyo na hiyo pia natambua mradi mkubwa unaoendelea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutamsifu sana Mheshimiwa Lukuvi hapa, lakini tusipompatia fedha ni sawa na bure, Mheshimiwa Lukuvi mwaka jana bajeti yake ya maendeleo aliyopata bilioni tatu *point* tano mwaka huu anaomba bilioni ishirini, kumi za nje kumi za ndani. Wakati Lukuvi anaomba hii fedha taarifa ya *review* ya miaka mitano ya Mpango wa Miaka Mitano inatuambia ni asilimia 10 tu ya Watanzania ama nyumba ambazo zina hati za kimila na hati za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 10, miaka 54 baada ya uhuru, tunampa huyu jamaa bilioni 20. Inawezekana ana dhamira njema, lakini hiyo dhamira njema, haiwezi kuishia kwa kutatua migogoro, jukumu la Waziri sio kutatua migogoro, ndiyo maana tuna vyombo mpaka ngazi ya kijiji, huyu anatatua migogoro kwa sababu mfumo umefeli, anakwenda kufanya kazi ambayo kimsingi siyo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 54 baada ya uhuru asilimia 20 tu ya ardhi ya Tanzania, imewekewa mpango, iko *planned.* Hivi kweli migogoro ya ardhi itakwisha? Hivi kweli wakulima na wafugaji wataacha kuuana. Mtakumbuka miaka minne iliyopita, alipokuwa Waziri mama Tibaijuka nilileta hoja, nikasema sasa hivi tumepewa hivi vitabu, lakini nitawaambia hizi takwimu zilizokuwa humu na uhalisia uliopo kule chini, ni vitu viwili tofauti, tunafanya kuhisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema kwa nia njema kusaidia nchi hii, naomba Mheshimiwa Lukuvi anisikilize na alifanyie kazi, tunahitaji kufanya *land auditing,* ili tujue kila kipande cha ardhi ya nchi hii kinafanya nini, nani ana nini, kiko wapi, kinafanya nini, mali ya Serikali Kuu ni ipi, mali ya vijiji ni ipi, mali ya halmashauri ni ipi. Ili tukishajua thamani ya kila kipande, tutajua na juu ya kila kipande kuna nini, kuna majengo gani, hayo majengo yanasaidia nini katika uchumi wa nchi. Kwa hiyo, tukitumia fedha nyingi, tukafanya kitu kimoja, kitu kikawa kina tija kwa Taifa; kitajibu kodi ya ardhi, kitajibu mipango ya nchi, kitajibu *property tax,* tutajikuta biashara ya kuzungumzia mapato haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikaenda kikarudi, zikapigwa danadana, miaka minne baadaye, hakuna kitu kinachoendelea. Sasa swali linakuja Mheshimiwa Lukuvi kazi yakoeitakuwa ni kutatua migogoro? Hivi nikimuuliza leo kama Waziri wa Ardhi ni vipande gani vinafaa kwa ajili ya kilimo cha kumwagilia maji atakuwa anaotea, nikimwambia nani ana nini, atakuwa anaotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikimuuliza Mheshimiwa Mwijage hapa anazungumza eti biashara ya viwanda na yeye kwenye ukurasa wa 45, amezungumza utengaji wa maeneo ya viwanda. Tunajua, juzi kwenye hotuba yake ya viwanda na biashara, alivyobanwa kwenye maeneo ya *EPZ* na *SEZ* alikuwa anang'atang'ata meno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaambiwa Tanzania ya viwanda, ardhi ya *EPZ* ya *SEZ* karibu hekta 31 hakuna fidia iliyolipwa, elfu kumi ndiyo inafanyiwa tathmini, hiyo elfu kumi Serikali ilitakiwa ilipe bilioni 60, Serikali haina fedha, sasa hivi katika zile elfu kumi Serikali mnatakiwa mlipe bilioni 190, bilioni 130 zaidi. Hivi hizo kweli ni akili jamani, hapo bado zile hekta elfu ishirini na moja bado hazijafanyiwa tathmini. Halafu tunasema oooh Tanzania ya viwanda, ardhi

yenyewe huna, hujalipa fidia, Sheria za nchi zinamlinda Mtanzania dhidi ya kulipwa fidia ili aweze kuondoka, tunapigana maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Lukuvi, tuisaidie hii nchi, tufanye *land auditing, let us do that.* Tulivyopendekeza aliyekuwa Waziri akaenda akakagua hayo mashamba yaliyokuwepo. Sijui mashamba 964, ekari karibu laki tisa sijui na ngapi mwenyewe anakuja kugundua yale mashamba kwamba kwa wastani wageni wanamiliki ekari, 6,300, wazalendo wanamiliki ekari 280 kwa wastani. Wageni 6,000 wazalendo 200, kwa hiyo tukiwa na hizi taarifa tutajua tunaipeleka wapi nchi, tukiwa hatuna hizi taarifa, tutabakia tu tunafikiria hapa puani, hatufikirii kizazi cha sasa, kijacho na cha kesho kutwa. Nimwombe tena tutasaidia mpango wetu wa kilimo, tutasaidia mipango yetu ya viwanda, tutasaidia mambo ya kodi, tutaweza kuisogeza nchi mbele, tutakuwa na takwimu ambazo ni *tangible. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba, hili shirika tumshukuru kijana wetu ameli-*transform,* Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni na Watanzania tujifunze kuwalipa watu kutokana na uwezo wao wa akili, tuache fikira za kimaskini. Nchi za wenzetu wako tayari kumlipa mtu hela nyingi kama ataweza kurudisha kitu chenye tija, sasa leo tunawalaumu Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje tu kodi wanazolipa na naomba nitaje tu, hili shirika tunaambiwa wajenge nyumba za maskini. Asilimia 10 ya mapato yao ya mwaka yanatakiwa yapelekwe Mfuko Mkuu wa Hazina, wanatakiwa walipe kodi ya makampuni asilimia 30, wanatakiwa walipe gawio milioni 300, wanatakiwa walipe riba ya mikopo wanayojengea asilimia 16 hakuna cha ruzuku ya Serikali. Wanatakiwa walipe kodi ya ardhi, kodi ya jengo, kodi ya zuio, kodi za Halmashauri *Civil Service Levy*, kodi ya *VAT,* hawa hawa wananunua ardhi kwa bei ya soko, hivi kutakuwa kuna nyumba ya bei nafuu hapo? Hakuna! Wenzetu huko mnakokwenda kutembea kila siku, haya mashirika yanawezeshwa na Serikali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu huko mnakoenda kutembea kila siku haya mashirika yanawezeshwa na Serikali zao kama kweli hizi lugha mnazosema, tunataka ooh, tusaidie maskini, Waziri atujibu hapa, ana mpango gani wa kupunguza huu mzigo kwa shirika, ili hao maskini wasaidiwe tunaojifanya tunaimba kwa maneno wakati kwa vitendo hatulisaidii Shirika letu. *(Makofi)*

Mheshimimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tuwape moyo lakini tuwasaidie huu mzigo wote wa haya makodi kumi niliyoyataja hapa, yote yanabebwa na mlaji. Mwaka 2014 hawa mapato yao ya mwaka yaliyokuwa

bilioni 176 ukitoa tu asilimia 10 ya *withholding* wanatakiwa wapeleke Serikalini bilioni 17, wanasema ile pesa walioipeleka Serikalini walikuwa na uwezo wa kupata mkopo wa bilioni 101 ya kujenga nyumba nyingine. Yaani badala mfikirie vyanzo vipya vya kodi mkiona tu amekuwa *creative* pesa zinaingia mnataka mvune, hebu jiongezeni basi. Nimewaambia fanyeni *land auditing*, msifikirie uchaguzi, yaani shida yetu sisi Watanzania huwa tunawaza uchaguzi na tukiwa tunafanya mambo kwa kuwaza uchaguzi tutakuwa tunawaza puani, hatuwazi mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri asijali hata kama itam-*cost ten million* kufanya *auditing* nchi nzima, anaweza akaziagiza hata halmashauri kwa sababu ndiyo maana tunakuwa tuna mfumo wa utawala, aagize halmashauri tunataka mtupe taarifa kwenye halmashauri zenu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba nawakilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Conchesta Lwamlaza atafuatiwa na Dkt. Godwin Aloyce Mollel.

**MHE. CONCHESTA L. LWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache kuhusu hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongea kuhusu halmashauri kuweza kupima viwanja na kupanga miji. Ni kweli halmashauri zimepewa jukumu la kupanga miji, kupima mashamba, kupima viwanja, kuweka makazi kwa ustawi wa watu wao, lakini kwa muda mrefu halmashauri hizi nchini zimeshindwa kufanya kazi hii kwa sababu ya ukosefu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nyuma halmashauri zilikuwa zina *retain* pesa yake ile asilimia 30 inayotokana na kodi za ardhi na hivyo wanapata uwezo wa kufanya kazi ya kupima viwanja. Baada ya kuwaondolea mapato hayo kwenda katika Wizara ya Ardhi, fedha hizi hazirudi na kama zinarudi zimechelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nafuatilia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa tisa umeweza kutuonyesha mapato ambayo yametokana na kodi za ardhi. Ametuambia kwamba wameweza kukusanya bilioni 54.35, lakini tukienda ukurasa wa 83 unaotuonyesha mgao uliorudi katika

halmashauri wa asilimia 30 yaani utaona maajabu, asilimia 54 bilioni zimekusanywa, lakini halmashauri 138 zimepata bilioni nne nukta nne. Kwa hiyo, naweza kuangalia uwiano na nimekwenda mbali nikaangalia Mkoa wa Kagera ambao ni mkoa wangu mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mgao wa mwaka huo tumeweza kupata milioni 113 na *point*, lakini unaweza kuona katika *trend* hii ni namna gani halmashauri zinaweza kupata fedha ya kuweza kupima viwanja. Siyo hivyo, nashauri Serikali itazame upya hata hii asilimia 30 ni sawa hata kwenye barabara halmashauri zinapewa hela ndogo, lakini kama ni sheria ibadilishwe ili hawa watu waweze kupata angalau hata asilimia 40 hata kama ni nusu kwa nusu kwa sababu kazi nyingi ziko ndani ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupima viwanja ndani ya halmashauri kuendana na ubia hata kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Wizara inafikiria au tayari imeanza kufanya ubia. Halmashauri nyingi zinakopa pesa kwa ubia tuseme na *UTT*, lakini fedha hizo ambazo mara nyingi halmashauri wanakopa nani anazisimia. Kumekuwa na malalamiko katika hali hii ya Wizara ya Ardhi, haieleweki maana yake inasimamiwa na TAMISEMI, Wizara ya Ardhi inasimamia vyake, kwa hiyo, matokeo tunakuwa na mkanganyika mkubwa. Halmashauri ziko TAMISEMI zinakwenda kukopa pesa, pesa hiyo inatumika vibaya, nani anasimamia mikopo hiyo? Wizara ya Ardhi inawekaje mikono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, naweza kukupa mfano katika halmashauri yetu ya Manispaa ya Bukoba, kulizuka mgogoro mkubwa nafikiri mlihusika wanakopa pesa za kulipa fidia, lakini fidia zinazolipwa wanalipwa wale watu ambao wana ardhi na hata *CAG* aliendа kukagua akaona kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye Kamati ya TAMISEMI tulienda kuona hivyo hata Lindi imefanyika hivyo, kwa hiyo fedha zinakopwa. Je, nani kati ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi ambao wanaweza kusimamia mikopo hii ili fedha zitumike kadri inavyotakiwa. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie hili maana yake TAMISEMI wanasema wao mikopo ipitie kwao, Wizara ya Ardhi ni vipi, kwa hiyo, naona kuna mkanganyiko hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende moja kwa moja kwenye kodi ya majengo. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani upande wa ardhi amejaribu kusema, yeye anafikiria na sisi kambi kwamba inawezekana mnapenda kutuchonganisha na hizi halmashauri zetu ambazo tunasimamia kama upinzani lakini siyo hivyo. Kwa mfano, tuchukue Dodoma hapa hii halmashauri ni ya Chama cha Mapinduzi, mnafikiri mnaondoa majengo hii manispaa itajiendesha namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri msipeleke ushuru au kodi ya majengo kwa Serikali Kuu. Miaka miwili ya mwisho kwenye Bunge nilikuwa kwenye Kamati ya TAMISEMI tumekwenda pale Dar es Salaam tuliona jinsi *TRA* walivyoshindwa kukusanya kodi ya majengo walikuwa wanafanya uthamini wa upendeleo yaani yule mwenye kajumba kadogo ndiyo anawekewa fedha nyingi nani atafanya uthamini ili kwa kweli kupata hali halisi ya mapato ya majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* walishindwa na kama walishindwa kipindi hiki mimi sioni sababu, mnakwenda kuua halmashauri hizi hata za kwenu ambazo sio za upinzani peke yake zote mtakwenda kuziua. Kwa hiyo, mwangalie kwa makini kwamba kodi za majengo zirudishwe, halmashauri ziweze kujiendesha kama kweli mnakwenda kufanya *D by D* na kwamba kweli hapa Halmashauri zifanye nini ziweze kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye wawekezaji, Wabunge wengi sana wamelalamika kuhusu wawekezaji lakini wawekezaji hawa wako hata wanasiasa ambao nao wanakwenda kwa ulaghai wao, wanakwenda kuhodhi ardhi kubwa katika maeneo ya halmashauri zao. Mfano katika Mkoa wa Kagera tuna mgogoro mkubwa katika Wilaya ya Muleba, mgogoro huo nina uhakika uko mezani kwa Mheshimiwa Waziri, kama haupo nina *documents* hapa akihijtaji kama hana nitampa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Kitene, Kata ya Kasharunga uko mgogoro kati ya kijiji na aliyekuwa Waziri wa zamani marehemu Edward Barongo. Mwaka 1990 aliomba kijiji kimpe ardhi eka 2000 sasa hivi ana eka zaidi ya 11,000. Tuje kwa aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sijui nimtaje jina, aliyemfuata huko nyuma, Mheshimiwa Waziri anamjua. Yeye kwenye kata hiyo hiyo katika Kijiji cha Kamyora aliomba ardhi eka 1098 sasa hivi anahodhi ardhi zaidi ya eka 4000, kwa hiyo, uko mgogoro mkubwa.

**MBUNGE FULANI:** Mtaje.

**MHE. CONCHESTA RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namtaja si Profesa Tibaijuka ni dada yangu si kwamba namsema ndani ya Bunge, lakini nakataa hii tabia ya kila kitu changu, kila kitu changu, hapana. Ukiwa kiongozi wakati mwingine na wewe uwaachie wengine. Kama ni kiongozi huwezi kuhodhi ardhi, watu wanakuja kukodi kwako au watu hawawezi kufanya nini, ni tabia mbaya ambayo lazima tuikemee. Hatujasema kwamba kiongozi wa siasa hawezi kumiliki lakini, naomba tumiliki kwa ustaarabu, tumiliki ili tuwaachie na wenzetu wale ambao tunawaongoza, ndiyo hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachomwomba Mheshimiwa Waziri, mgogoro huu tunaomba waende wapime upya hiyo ardhi ili kusudi kama mtu

aliomba eka 1098 abaki na hizo, ili zile zinazobaki wananchi wapate maeneo ya kutumia. Hivyo hivyo katika kile Kijiji cha Kitene, japokuwa marehemu Edward Barongo, alishafariki, Mungu amweke mahali pema, lakini ana watoto wake. Kwa hiyo, kama aliweza kuomba eka 2000, kwa nini ahodhi eka 11,000? Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri aende kwa kutumia vyombo vyake wakapime upya hiyo ardhi ili haki iweze kutendeka na migogoro hii iweze kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nimalizie kuhusu wataalam wa ardhi ni kweli mna vyuo lakini vyuo hivi wataalam hawatoshi. Nimegundua kwamba inawezekana watu hawaoni maana ya kwenda shule kujifunza haya mambo ya ardhi. Mwendeshe kampeni maalum, vijana wetu waweze kuona kwamba wanastahili kwenda kusoma mafunzo haya na muwahakikishie ajira ili kusudi vijana wetu wa Kitanzania waende kwenye vyuo hivi, wasome wapate utaalam ili muweze kuajiri wataalam wengi katika halmashauri zetu. Kusema ukweli halmashauri hazina wapimana hazina wachora ramani. Kwa hiyo, tunaomba kwa hayo machache muweze kutangaza watu waende wasome na waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Godwin Aloyce Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainabu Athman Katimba.

**MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa kupata nafasi. Kwanza nakubaliana na wenzangu wanaosema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni nami niseme tu katika migogoro ambayo nimewahi kumletea Mheshimiwa Waziri kuhusu ardhi ndani ya Wilaya yetu ya Siha, nimeeleza hata ya kufanya na kuyafuatilia na amefika katika Wilaya ya Siha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona wanavyoshirikiana na Wizara ya Kilimo kutatua migogoro iliyoko eneo la Ushirika. Vile vile niseme kwamba leo tujielekeze zaidi wapi atakapokwenda kukwama wakati anafanya shughuli zake ili ajipange mapema zaidi na nimwombe anayemwakilisha Waziri Mkuu, ili aweze kunisikiliza kwa makini na kumfikishia ujumbe huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Wilaya ya Siha, tuna migogoro ya mipaka kati ya Arumeru na Longido, lakini sikuwepo siku mbili ,tatu hizi wananchi kati ya Arumeru na Siha wamebomoleana nyumba upande wa Arumeru wamebomoa nyumba moja lakini Siha kwa sababu Mkuu wa Wilaya kafika pale tena kafika amelewa, lakini alipofika pale ame-*provoke* wananchi kati ya

pande zote mbili zimebomolewa nyumba nne za Arumeru, lakini ikabomolewa na ofisi ya mtendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda pale kazi ilikuwa ni rahisi, ilikuwa tu kukutanisha wananchi pande zote mbili na kuwaelewesha na kukaa chini mkondo wa sheria ufuate sehemu yake, lakini Mkuu wa Wilaya ya Siha alitaka nguvu zitumike kuliko akili. Niseme tu nimshukuru *OCD* Meru na Siha, lakini na Mkuu wa Wilaya ya Meru angalau anasimama kwenye nafasi yake kama tunavyotaka aende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapoongea hivi najua migogoro ambayo nimewaandikia, lakini migogoro ambayo ameandika Mkuu wa Wilaya ya Siha baada ya maagizo ya Mheshimiwa Waziri, mgogoro ambao nimekuwa nikiusisitiza kila siku, leo tunapoongea hivi matrekta mawili yamebomolewa na wananchi, nimepata meseji sasa hivi lakini gari la polisi limevunjwa kioo, huyo ndiyo Mkuu wa Wilaya tuliyenaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanasemaje? Wananchi wanasema na baadhi ya watumishi, wananchi walipoona yule mwekezaji kwenye Kata ya Songu, alipokuwa anaenda kwenye Kata ya Songu kulima hilo eneo ,wananchi walimzuia. Walipomzuia wakamtaka Mkuu wa Wilaya na uongozi wamzuie kwa sababu bado wana mgogoro, wao wanasema eneo ni lao na wenyewe wawekezaji wanasema eneo ni lao, wakataka tu kwamba azuiliwe na yeye asilime ili waendelee na mchakato wa kawaida, lakini Mkuu wa Wilaya akaagiza polisi waje wakamate watu. Polisi wakatumia nguvu nyingi wakakamata na viongozi, ndiyo yaliyofikia, hayo sasa ndiyo matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana nashukuru Mheshimiwa Waziri alikwenda kwenye Wilaya ya Siha, lakini nimwambie kuondoa Mkuu wa Mkoa ambaye alikwenda naye baba, wengine wote ni watuhumiwa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi na hata juzi tulimuuliza amekodisha heka nyingi ambazo haziruhusiwi, tena *beacon* zimepimwa amewapa watu viwanja, halafu wakaenda tena kukodishwa halafu zikalimwa wakang'oa zile *beacon,* anatuambia tutafute shilingi milioni mia moja kwa ajili ya kurudishia *beacon,* hiyo ndiyo Serikali ya Wilaya tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe na nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Waziri wa Kilimo, twende ili wathibitishe ninayosema kwa maneno yao hawathubutu kumwambia ukweli. Akienda cha kwanza kiongozi akifika pale anaambiwa yule Mbunge ni mkorofi, ana fujo, lakini kiukweli mimi sina fujo wala huwa mimi siyo mkorofim isipokuwa nataka watu waende kwenye *focus* ambayo ndiyo tunaitaka nchi hii ifike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana kwamba, tunataka kuipeleka Tanzania iwe ni nchi ya pato la kati, hamna namna yoyote tutakuwa nchi ya pato la kati na narudia tena, ni lazima kama tunajenga viwanda, basi watakaotengeneza malighafi kwa ajili ya hivyo viwanda wawe ni Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukatengeneza kiwanda, sawa tunakubali na mwekezaji wa kiwanda awe na sehemu ya kutafuta malighafi, lakini ili kuwapeleka nao Watanzania waweze kumiliki uchumi wa nchi yao, ni lazima nao waweze kuzalisha malighafi ambayo itatumika kwenye hivyo viwanda, ndicho tunachokisema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Wilaya ya Siha, nilisema tena hapa tunaweka 130,000, hivi tungesema tunatoa eka 10,000 tunahakikisha nao watu wa Siha wanamiliki au Watanzania wanamiliki, sio lazima watu wa Siha wakamiliki zile 120,000, tukawekeza tutapunguza migogoro. Leo umeona Mheshimiwa lile shamba la maparachichi ni zuri, lakini ndani ya Wilaya ya Siha ni mojawapo ya wilaya hazina pato, inasemekana baraza lao livunjwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ukienda kwa wawekezaji wanakwambia kwanza tumechoka viongozi wako wa Wilaya sisi ndiyo tunatengeneza magari, sisi ndiyo tunawapa hela na vitu vingine, tunakuomba uende ukasema tuwe tunadaiwa kile tunachostahili, tena tupeleke kwenye maendeleo yaonekane na wananchi. Kama mimi nasema uwongo, naombeni twende tuthibitishe haya ninayosema na niko tayari kuwajibika kama nasema uwongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, tukiwamilikisha namna hiyo tutapunguza migogoro, kama mkulima mwekezaji amewekeza kwenye zao fulani, nao wakulima wakawekeza kwenye zao hilo hilo kwa kupewa ardhi, kwa sababu wanatumia soko moja na wakatumia eneo moja kuuza, urafiki utakuwepo na migogoro haitakuwepo na upendo kati ya wawekezaji na wananchi utakuwa mkubwa sana. Hicho ndicho tunachokisema, hatusemi hatutaki wawekezaji, sisi tunasema tunataka wawekezaji lakini tunataka tunapofikiria uwekezaji tufikirie *sustainability* ya uwekezaji wenyewe kwamba uwekezaji wenyewe utadumu vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu huyu huyu Mkuu wa Wilaya nilishawahi kumwambia, wala mimi siyo Mbunge wakati huo nilikuwa mfanyakazi wa kawaida tu. Nikamwambia migogoro wa Endarakwai ambao ameandika hapa eka 5,000 wakati ni eka 11,000, nikamwambia fanya hivi, fanya hivi, akakataa akasema yeye ni dola na hatuwezi kumfundisha. Tuliona kilichotokea, nyumba zimechomwa na mabilioni yamepatikana na ni aibu kwetu kama nchi na ni aibu kwetu kama wilaya, wawekezaji kuvamiwa halafu

inarushwa nje, je, na tunataka tuwekeze, tukitaka tuwekeze wakati tunatangaza sehemu zetu za uwekezaji, watu waki-*google* wakiona wawekezaji wamevamiwa tunakosa uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka watu wenye hekima ambao wanajua kupeleka uwekezaji pamoja na wananchi bila kuwa na migogoro ili watu waipende nchi yetu. Nilikuwa naangalia leo hata Ujerumani wanatangaza wanaomba wawekezaji watoke nje, hata sisi tunawahitaji, lakini tunawahitaji kwa namna ambayo itamfanya Mtanzania afaidike, mwekezaji afaidike lakini na mtu ambaye anakaa katika eneo husika afaidike, ndiyo uwekezaji tunaousema. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri anaona hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie watu hao wasimkwamishe kwa sababu hapewi ukweli. Leo shamba ambalo limechomwa matrekta hajawahi kwenye ofisi yake kuambiwa, lakini siku zote tunasema kwa sababu wana maslahi. Mashamba ya ushirika alikuja Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mkuu wa Wilaya wananchi walimzomea kwa masuala ya ardhi, lakini kwa nini ndani ya mashamba ya ushirika ni wao wanalima wananchi hawapati mashamba? Kama nasema uwongo twendeni halafu niko tayari wala msiseme nimesema kwenye Bunge siwajibiki, niwajibike kama nasema uwongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe hili limfikie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, sisi tunapenda hiyo nafasi ya Ukuu wa Wilaya, lakini huyo ambaye anakaa mpaka saa nane *bar*, dereva anakaa kwenye gari na gari la Serikali la kodi ya wananchi, sisi tumechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki mtu anayesababisha Serikali idharauliwe, tunataka Serikali ya Tanzania iheshimike, watu waheshimu Serikali ya Tanzania. Unapokwenda kwa wawekezaji Mkuu wa Wilaya mzima unaongoza Serikali halafu unapewa vitu vidogo vidogo unaidhalilisha Serikali yetu na hatutakuwa tayari. Nilimwambia Mkuu wa Mkoa, huyu Mkuu wa Wilaya anatusumbua na tukamweleza, nikamwambia nitakuja kuomba hapa ahamishwe ikishindikana wananchi wa Siha hatupo tayari Serikali ya Tanzania kuaibishwa, tutamtoa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kwa sababu anatudhalilisha, anafanya vitu ambavyo ukienda kwa mzungu akikuona mweusi anakudharau, hatuko tayari. Kwa hiyo, niseme bila kuathiri juhudi nzuri zinazo… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. kwa mchango wako.

**MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Zainab Athmani Katimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Aloyce Bura na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii adhimu ya kuweza kuchangia katika hotuba hii. Ningependa kuendelea kupongeza jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali. Pia ningependa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwakilishi wa vijana sisi vijana tunatambua kazi kubwa ambayo inafanywa na Shirika la Nyumba la Taifa yaani *NHC,* lakini tungependa kuiomba Serikali kwa kuzingatia kwamba takwimu zinaonesha uwiano wa jumla ya idadi ya watu, vijana ndio wanaochukua asilimia kubwa; lakini pia kwa kuzingatia asilimia 59 ya nguvu kazi ya Taifa ni vijana. Basi vijana waweze kutengenezewa utaratibu wa kipaumbele wa kupata nyumba hizi za *NHC* lakini za bei rahisi. Kwa wale vijana ambao wanaanza kufanya kazi, wanaoajiriwa, wanakuwa na kazi basi na wenyewe watengenezewe utaratibu wapate hizi nyumba za bei nafuu. Hiyo bei nafuu iwe kweli bei nafuu na isiwe bei nafuu kwa kiwango fulani ambacho vijana watashindwa kuzimudu bei zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuishauri Serikali yangu sikivu juu ya umiliki wa ardhi. Sheria namba nne ya ardhi na sheria namba tano ya ardhi zinaeleza kwamba mmiliki wa ardhi ya Tanzania atakuwa ni Mtanzania na sio mgeni na kama mgeni akitaka kumiliki ardhi atamiliki ardhi kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* na kuna utaratibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria namba nne kifungu cha 20(4) kinaeleza bayana kwamba kampuni inayokuwa na *shareholders* wa kigeni yaani *share* nyingi kwa mtu ambaye ni mgeni, kampuni hiyo inakuwa ni kampuni ya kigeni na kampuni ya kigeni kwa sheria za Tanzania hairuhusiwi kumiliki ardhi ila pasipokuwa tu kwa kupitia *TIC* yaani kwa maana ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna utaratibu ambao wageni wanautumia; wageni wanakuja wanashirikiana na wazawa wanasajili kampuni lakini katika *share structure* ya hiyo kampuni inaonesha kwamba wazawa ndio wana-*share* nyingi zaidi lakini baadaye, baada ya kumiliki ardhi wanakuja wanabadilisha ile *share structure* na *share structure* inaonesha kwamba yule mgeni anakuwa ana *share* nyingi zaidi, yaani ni *majority shareholder.* Kwa hiyo, inaifanya ile kampuni inakuwa ni *foreign company,* yaani kampuni ya kigeni

lakini inakuwa bado imemiliki ile ardhi. Kwa hiyo, inakinzana na hii sheria ambayo inasema mgeni na kampuni la kigeni haliruhusiwi kumiliki ardhi Tanzania pasipokuwa kwa utaratibu maalum ambao umewekwa chini ya Kituo cha Uwekezaji *(TIC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali itengeneze utaratibu yaani Msajili wa Makampuni *BRELA* pamoja na Kamishna wa Ardhi kuwe kuna mawasiliano ili kuweza kubaini mabadiliko haya ya *share structure* ili kuhakikisha kwamba makampuni ya kigeni au wageni wasitumie makampuni haya kwa kuchezesha hizi *share structure* kutumia kumiliki ardhi ya Kitanzania tofauti na utaratibu na sheria za nchi yetu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa sana kuishauri Serikali yangu kuhusiana na sheria yetu hii kwa mfano Sheria ya Ardhi namba tano, kifungu cha 18 kinaeleza bayana kwamba, ardhi au haki yaani *customary right of occupancy* ina hadhi sawa na *granted right of occupancy* yaani haki miliki ya kimila ina hadhi sawa na hati miliki ya kupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii ipo kisheria, iko pia kama yaani sera au kama sheria, lakini kiuhalisia hizi hati za kimila hazina haki sawa na hizi hati miliki ya kupewa. Kwa sababu mtu ambaye ana hii *customary right of occupancy* ambayo ni hati miliki ya kimila hawezi kwenda benki akataka kuikopea au kupata mkopo ku-*mortgage* kwa sababu atapata kipingamizi, itaonekana haifai, haitoshi, haina kiwango sawa pamoja na hii hati miliki ya kupewa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunajua vijana wetu wengi waliopo hata huko vijijini wana hizi ardhi na wangependa kutumia hii ardhi waliyoletewa na Mwenyezi Mungu katika Taifa hili kwa ajili ya manufaa yao wao wenyewe na kuboresha uchumi wa Taifa. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kuangalia kwamba hii *section* 18 ya *Village Land Act* iweze kuwa na uhalisia kwa sababu ipo tu *academically* lakini kiuhalisia hati miliki ya kimila haina hadhi sawa na hati miliki ya kupewa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kushauri kuhusu Mabaraza ya Ardhi; Mabaraza ya Ardhi yalianzishwa ili kusaidia kupunguza migogoro ya ardhi, lakini kuharakisha hii migogoro ya ardhi iweze kwisha kwa wakati. Tofauti na matarajio kimsingi haya Mabaraza ya Ardhi yanaonekana yameelemewa; kesi zimekuwa nyingi, zinachukua muda mrefu hadi miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu kwa Serikali, kabla sijakwenda nataka nisome Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kabla sijaenda huko nilikuwa napenda ifahamike Mabaraza haya ya Ardhi ya Kata yanasimamiwa na Wizara ya TAMISEMI; lakini Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya

yanasimamiwa na Wizara hii ya Ardhi, lakini ukija kwenye mahakama unakuta mahakama inasimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta kwamba kuna Wizara tatu tofauti ambazo zimepewa mamlaka ya kusimamia jambo ambalo ni moja. Ukisoma Katiba, Ibara ya 107(a) utakuta imetamka bayana kwamba mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni mahakama. Sasa haya Mabaraza ya Ardhi yanafanya kazi ya kutoa haki ambacho ni kinyume na Katiba nadiriki kusema. Kwa sababu mahakama ndiyo chombo cha mwisho cha kutoa haki na sisi tunajua haya Mabaraza yanachukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama yameshindwa hii kazi na naweza kudiriki kusema naona yameelemewa, basi hii kazi ya kutoa haki irudishwe katika mfumo wa mahakama, kuanzia Mahakama za Mwanzo mpaka kufika mwisho katika mfumo wa mahakama. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia Ibara ya 113 ambayo imeelezea majukumu ya Tume ya Utumishi wa Mahakama, inasema, jukumu mojawapo la Tume ya Mahakama ni kuajiri Mahakimu na kusimamia nidhamu yao. Kwa hiyo, katika mfumo wa mahakama hawa Mahakimu wanasimamiwa na sheria na nidhamu zao zinasimamiwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, wana mamlaka ya kuwawajibisha lakini hawa viongozi wanaokaa katika Mabaraza ya Kata, ya Wilaya hamna mamlaka ya kushughulikia nidhamu zao. Hakuna bodi ambayo ina-*deal* na *ethics* zao, hivyo, ningeomba sana Serikali iweze kuleta Muswada kwa ajili ya kurekebisha hizi sheria zilizoanzisha haya Mabaraza ya Ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba mahakama ina uwezo mkubwa sana wa kuendelea kutekeleza au ku-*solve* haya matatizo na changamoto za ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba pia Waziri wakati anahitimisha aweze kutoa kauli juu ya uhalali wa kukopesheka kwa hati hizi za kimila kwa sababu vijana sisi tunajua wengi wetu tunazo hizi hati; tunataka ziweze kutumika kwa ajili ya manufaa yetu, sheria inatamka kwamba zina haki sawa pamoja na hizi hati za Kiserikali. Kwa hiyo, tunaomba Waziri atamke ili ifahamike na ziweze kutambulika kwamba zina hadhi sawa katika mabenki ili tuweze kukopa kwa kuzitumia hizi hati za kimila. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu wangu kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi pamoja na timu yake kwa kazi nzuri anayoifanya, hakika Mheshimiwa Lukuvi anatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia juu ya Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi. Nadhani wakala ilianzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi na hasa wale wenye kipato kidogo; lakini ofisi za wakala ziko Dar es Salaam, wakala hana ofisi wilayani, mikoani lakini wananchi wenye shida ya kujenga nyumba zenye gharama nafuu wako wilayani, wako vijijini, wako mikoani. Sasa sijui ofisi hii inafanya nini Dar es Salaam na hata katika wilaya zetu hatujawahi kuwaona wala kusikia habari zao, tunazisoma habari za kwenye vitabu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wakala hawa waje Dodoma; Dodoma tuna mahitaji makubwa ya kujenga nyumba za gharama nafuu na hasa kwa matofali haya ya kufungamana; vijana wapo watapata ajira kutokana na kazi hii ya kufyatua hayo matofali, watajenga nyumba za kudumu, nzuri ambazo hazitawasumbua kujenga tena baada ya kipindi kifupi. Naomba wafanye kazi hiyo Dodoma kama mkoa wa mfano na wananchi watafaidika na shughuli watakazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie pia pale alipoachia Zainab kuchangia kwamba mabaraza yetu yanahudumiwa na Wizara tatu; Mabaraza ya Kata yapo chini ya TAMISEMI, Mabaraza ya Wilaya yapo chini ya Wizara ya Ardhi, lakini mwananchi anapokata rufaa anakwenda Wizara ya Sheria na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria waliwahi kufanya kazi hii na walileta mapendekezo Serikalini, sasa Waziri atatuambia mapendekezo yalifanyiwa kazi? Mabaraza yetu ya Kata hawana mafunzo, hawana hata vitabu rejea yaani ukiwaambia warejee kwenye kesi ambayo iliwahi kutokea hawana pa kurejea. Kwa hiyo, wanafanya kazi kutokana na mazoea na akili ya mtu inavyomtuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kuna haja ya Sheria namba tano kufanyiwa marekebisho makubwa. Pia hawa Wajumbe wa Baraza hata ukisema Mwenyekiti anapokwenda kwenye eneo la tukio la baraza hawana

ulinzi hawa watu. Kwa hiyo, wananchi wanaweza wakawafanyia fujo na kuwapiga hata kuwafanyaje wanavyoweza kwa sababu hawana ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia Mahakama ya Ardhi wapangiwe muda wa kumaliza kesi. Mahakama ya Rufaa zingine wamepangiwa muda wa kumaliza kesi; kesi 200 kwa mwaka, lakini Mahakama ya Ardhi hatujui na hawajapangiwa muda wa kukamilisha kesi zao na kusikiliza kesi kwa sababu Mahakama ya Ardhi kuna kesi nyingi sana zinazosubiriwa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa wa Ardhi na wa Mipango Miji; hapa ndiyo kuna majipu ya kutumbuliwa. Mheshimiwa Lukuvi hapa ndiyo kuna majipu yaliyoiva kwa sababu Maafisa Ardhi wanagawa ardhi eneo ambalo wanajua ni eneo la wazi, wanagawa ardhi eneo ambalo wanajua watajenga shule, wanagawa ardhi maeneo ambayo ni ya soko; lakini wanafanya makusudi na ndiyo maana watu wanavunjiwa bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu alievunjiwa analeta hati yake kuonesha kwamba anamiliki kihalali eneo hilo, lakini Maafisa Mipango Miji wapo, Maafisa Ardhi wapo. Nikimsikia Mheshimiwa Waziri amewatumbua hawa watu nitafurahi sana kwa sababu wapo ambao wanafanya makusudi na kuwapa wananchi hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hati ya umiliki wa ardhi ipo hata kwa Serikali zetu. Safari hii ripoti ya *CAG,* Halmashauri zetu walipata hati za mashaka kutokana na halmashauri zetu kutokuwa na hati miliki ya maeneo yao. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hili lifanyiwe kazi haraka sana ili halmashauri zetu wawe na hati za kumiliki mali hasa ya ardhi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Dodoma, Dodoma tuna suala la Mkungunero halikuhusu sana lakini linakuhusu kwa sababu wewe ndiye Waziri wa Ardhi. Mkungunero pale vita vilishawahi kutokea, watu wakapigana, watu watatu wakauawa. Wananchi wa Mkungunero walishaandika barua kwa Waziri Mkuu, Mawaziri waliopita kabla yake walikwenda Mkungunero, tulikwenda nao, lakini mgogoro wa Mkungunero haujakwisha mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro mkubwa kati ya Hifadhi ya Mkungunero na vijiji 17 vya Chemba na Kondoa. Sasa hivi wananchi wa Kondoa hawawaruhusu Maafisa Wanyamapori kufanya kitu pale. Kilomita 50 tu tuliomba ili wananchi waweze kulima, lakini imekuwa kazi miaka nenda rudi, miaka nenda rudi hili suala halijakwisha. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri suala la Mkungunero liishe sasa. Tumewaalika Mawaziri wa Maliasili, Waziri Mkuu alikwenda, yeye mwenyewe tunamwomba aende ili suala la Mkungunero na

wananchi liishe Vijiji 17 wanagombea ardhi pale, wanaomba kilomita 50 tu waweze kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Dodoma Mjini, suala la *CDA* na Manispaa tumechoka nalo, wananchi wamechoka nalo. Inawezekana limetuchosha kwa sababu *CDA* hamuwapi fedha za kutosha, wanabomoa nyumba za watu bila fidia, wanachukua ardhi za watu bila fidia, wanalipa fidia kwa ardhi waliyotwaa kwa tathmini ya mwaka 2002, 2005 sio haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimsihi na nimwombe Mheshimiwa Lukuvi anajua sana suala la *CDA* na suala la ardhi ya manispaa, Mheshimiwa Rais alipokuja hapa wakati wa kampeni alisema *CDA*, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na halmashauri watakaa na kushughulikia suala la ardhi ya Manispaa ya Dodoma, nimsihi sana na Waziri wa TAMISEMI kama hayupo Naibu wake yupo na Mheshimiwa Jenista yupo, niwaombe sana washughulikieni suala la *CDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Dodoma wanaipenda sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi na ndiyo maana tunapata kura nyingi, lakini sasa hili la *CDA* halijashughulikiwa, namsihi sana Mheshimiwa Waziri ashughulikie hili suala la *CDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo la Kongwa, Kata ya Dabalo na Kata ya Segala wana ugomvi mkubwa sana na watu wa Kongwa mpaka kati ya Kata ya Dabalo na Segala na watu wa Kongwa, ni mgogoro wa muda mrefu. Wananchi wameacha kulima pale kwa ajili ya mgogoro ule unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mkoa mmoja lakini mgogoro ule umedumu kwa muda mrefu hakuna namna ya kumaliza mgogoro ule. Nakusihi ndugu kwa ndugu hawaongei, ndugu kwa ndugu wanatafutana, ndugu kwa ndugu wamekasirikiana kwa sababu ya mgogoro uliopo pale Kata ya Dabalo, Kata ya Segala na Wilaya ya Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiw;a Waziri ana uwezo huo,aumetatua migogoro mingi katika nchi yetu, huu mgogoro hautamshinda, nimwombe na ikiwezekana twende pamoja kwani kuna shida gani, twende pamoja mimi na yeye Mheshimiwa Lukuvi tukamalize suala hili, tukamalize mgogoro wa wananchi. Mimi nipo tayari, Mheshimiwa Lukuvi anajua kwamba nipo tayari kwenda pamoja naye. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Upate idhini yangu kwanza. *(Kicheko)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa suala la *National Housing*. *National Housing* wamefanya kazi kubwa na inayoonekana. Kabla ya mwaka 2007/2008 *National Housing* walikuwa wanapata ruzuku

kutoka Serikalini, lakini baada ya kuingia Mkurugenzi Mchechu, *National Housing* imebadilika kwa kiasi kikubwa. Wanajenga nyumba mijini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako, tunaendelea.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini wapunguzieni *VAT* ili tununue nyumba za *National Housing*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Papian atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa kazi anayoifanya kwenye Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naomba kumshukuru Waziri kwa kunipa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kiteto. Tumekuwa na migogoro mingi kwa muda mrefu Kiteto lakini sasa ameshatupa Baraza la Ardhi, tunakushukuru sana na tunakupongeza sana. Tunakuomba meza na vifaa vingine vya ofisini halafu uje ulifungue lianze kuchapa kazi, hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi wamefanya kazi kubwa sana. Mpaka leo Kiteto hali ya amani inayoendelea ni kwa sababu waliweza kupima baadhi ya vijiji, mipaka ikabainishwa na watu wakaweza kuishi kwa amani kwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyobaki Kiteto si kubwa sana. Namuomba Waziri aje na wataalam wake atusaidie kupima ardhi yote ili *finally* migogoro yote iweze kufika mwisho. Wafugaji wapate pa kukaa, wakulima wapate pa kukaa, kila mtu ajue kipande chake cha ardhi, mwisho wa siku itapunguza muingiliano ambao kwa sasa umekuwa unatuletea migongano ya kila wakati. Najua ni gharama kubwa, lakini kwa mazingira na hali iliyojitokeza kiteto tunaomba tupewe *priority* ili tusirudi huko tulikokwishatoka, hilo ni jambo la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ile Tume ya Waziri Mkuu ya Askofu Mhagachi, ilifanya kazi Kiteto ikamaliza, ripoti imekaa. Tunaomba mumshauri Waziri Mkuu ile ripoti ije, Waziri Mkuu afike, tumalize ule mgogoro, watu wajue nini kilitokea katika ripoti ile na hatimaye watu waweze kujua wapi wanatakiwa wasimamie na nini kifanyike kwa watu wote na atakayeyasababisha matukio mengine basi aweze kushughulikiwa kulingana na ile *document* itakavyokuwa inaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kiteto kuna *NGOs* nyingi ambazo zinanitia mashaka. Siku nyingine tutakuja kukuta Tanzania ilishauzwa hatujui na hivi vibali vinatolewa Serikalini. Kwa kweli *NGOs* ni nyingi, unashtukia *NGO* imezaliwa asubuhi watu wanafukuzwa asubuhi wanasema ni *CBOs,* jioni ni *WMAs* na hifadhi, sasa tumeshindwa kuelewa kipi ni kipi. Watu wameshalima mashamba, wamejenga, ni vijiji asubuhi wanakuambia hii ni hifadhi au ni *WMA*, hawa watu tutawapeleka wapi? Asubuhi watu wanaanza kushikiana mikuki na mapanga. Haya siyahitaji Kiteto, naomba Waziri aje hizo *NGOs* nyingine azipunguze, zifutwe na zijulikane zinafanya nini. Kwa sababu *NGOs* hizi zinafanya chokochoko za chini na ndizo zinazoibua migogoro ya wakulima na wafugaji Kiteto na kupelekea watu kupigana wakaisha. Tunaomba zifanyiwe kazi zile ambazo hazifanyi kazi vizuri zifutwe na zile zinazofanya kazi vizuri basi ziendelee na ziratibiwe kwa nini zinafanya kazi hizo na vyanzo vyao vya mapato vinatoka wapi ili tuweze kujua hawa watu wanakwendaje na wanatoka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hati miliki za kimila. Tunataka tujue, hizi hati miliki za kimila wananchi wetu wamepewa, wanajua mipaka ya maeneo na ni *title*, benki haziwakopeshi watu hawa, hazizikubali hizi *title*. Tunaomba Waziri mwenye dhamana azibane benki zinazokataa hizi *title,* azidhibiti, iende Serikalini, itungwe sheria, wasipewe vibali vya kufungua matawi mengine kama wanakataa hizi *title*. Tunahitaji watu wetu wapewe mikopo kutokana na *title* walizonazo kwa sababu ardhi ni yao, wana hati miliki kwa nini wasipewe mikopo kwa kutumia hizo *documents* zao kwa sababu wana haki nazo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri amejitahidi katika kunyang'anya watu ardhi ambao hawaitumii, kutatua migogoro kwenye maeneo mbalimbali, kwa kweli Mheshimiwa Waziri Lukuvi amethubutu lakini naomba niishauri Serikali, Mheshimiwa Lukuvi apewe ulinzi. Akienda na kasi hii Mheshimiwa Lukuvi watampiga mshale, haki ya Mungu, mshale hauna leseni, mshale haulipiwi kodi, anaweza kutembea huko maporini Kiteto na sehemu nyingine ambako watu wana hasira wakampiga mshale kwa sababu anachapa kazi, hongera sana, amethubutu kufanya hayo. Tuombe Mawaziri na viongozi wengine na Wabunge hebu tumuunge mkono Mheshimiwa Lukuvi, tumsaidie kumtatulia migogoro na sisi, kule tuliko na sisi tufanye, tusiwe ni *part* ya *complain.* Viongozi wengi wanalalamika sana, tuko kwa wananchi, migogoro mingine inamalizwa na Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto leo iko *stable* kwa sababu niko pale, hata kama kuna *differences* zozote zile lazima iwe *stable*, lazima itulie, wameniamini lazima watii kwa mamlaka na sheria za nchi. Wabunge twende kwa wananchi tukachape kazi, migogoro mingine ni *differences* tu za makabila, tabaka, uchumi, tumezidiana, amelima pakubwa, amelima padogo, ana ng'ombe wengi, unakaa chini, mnavuta tumbaku, mnakunywa pombe, msivute ile sigara

nyingine kubwa, tatua migogoro ya wananchi kabla haijaenda kwa Waziri, kabla haijaenda kwa Mkuu wa Mkoa, kabla haijaenda huko juu kwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia *National Housing*. Nashukuru sana kuna mchangiaji mmoja amesema *National Housing* ina kodi kubwa, ina vitu vingi inavyolipa lakini naomba ni-*create awareness, National Housing* kuna siku moja inaweza kuanguka, ikashindwa kulipa mikopo. Tuwapongeze wamechapa kazi, lakini naomba ni-*create awareness* kwa Serikali, Marekani iliwahi kuanguka benki zikatingishika ika-*shake* mpaka dunia nzima na Afrika tukapata shida. Napenda kuwaambia leo wana-*flow* ya mikopo mikubwa, wana hizi riba na kodi wanazotakiwa kulipa, nimshukuru Waziri mwenye dhamana alishaona na amewasimamisha kuendelea na *development,* wajenge hizo walizonazo wakae chini, wa-*plan* upya kwa maana kwamba watengeneze *vision* wakijua kabisa kwamba wana mikopo ya kulipa, waone *capability* yao ya kuilipa bila baadae kuja kuitegemea Serikali na kuwa mzigo. Mheshimiwa Lukuvi naomba ulisimamie hilo na uliangalie sana kwa sababu inaweza kutokea ukawa mzigo kwa Serikali, leo ni safi, kesho shimo. Naomba muangalie sana kwa sababu wana amana za mabenki wanaweza kusababisha yakaanguka, huo ni ushauri mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine naomba nishauri Mheshimiwa Waziri, migogoro mingi ya ardhi imekuwepo lakini tukubaliane kwamba katika maeneo mengi watendaji wa Serikali wanaolipwa mishahara, Maafisa Ardhi wanahamisha *beacon*. Kiteto watu wamekwisha kwa sababu wali-*divert beacons* za hifadhi wakasababisha watu kuendelea kugombana. Maeneo ya wakulima yakasogea ndani watu wakaanza kupambana, huyu anasema ni hifadhi huyu anasema ni mashamba, mwisho wa siku watu wakamalizana. Hawa Maafisa Ardhi wako wahuni tunaomba uwaondoe wakae pembeni, ajiri vijana wapya, wako mtaani wana vyeti kwapani, tunaomba uwasaidie hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nishukuru, nimuombe Mheshimiwa Angeline Mabula, Naibu Waziri, amsaidie Mheshimiwa Lukuvi, kwa kazi namjua akiwa Muleba alikuwa anachapa kazi, kulikuwa na migogoro mingi Kagoma alisimama kidete akaeleza ukweli hadharani wananchi wanakukumbuka sasa chapa kazi kwa Tanzania nzima. Pia kuna Dkt. Yamungu, Katibu Mkuu wa Wizara, ni mchapakazi, chini yake kuna Makamishna tunawapongeza, chapa kazi nchi isonge mbele migogoro ipungue hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushukuru na kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii kwa mara nyingine niweze kutoa mawazo yangu katika kuunga mkono hotuba nzuri ya Waziri wetu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Waziri Lukuvi aingie katika Wizara hii tumeona mabadiliko makubwa na tuna matarajio makubwa ya kuona mambo mengi yakiwekwa sawa hasa suala zima la maandalizi ya kuipanga upya nchi yetu. Nchi yetu imeingiwa na tatizo moja ambalo kimsingi tulikuwa tumeepukana nalo la mapigano ya sisi kwa sisi. Suala la ardhi limeonekana kuwa ni chanzo cha migongano baina ya wananchi, wafugaji na wakulima. Jambo hili lisiposhughulikiwa vizuri linaweza likawa chanzo cha vurugu nchini, chanzo cha kutoweka kwa amani iliyojengeka kwa muda mrefu katika nchi yetu. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Lukuvi na wataalam wako nashauri kwa kweli *speed* uliyoanza nayo endelea nayo. Kwa wale watu ambao wanakuwa na ardhi ambayo wanaimiliki bila kuiendeleza basi hatua unazochukua za kuwanyang'anya ardhi na kuwapatia wananchi ambao hawana ardhi uendelee nazo na kasi yako isirudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba yapo maeneo mapya ya utawala, tuna Mikoa mipya ya Geita, Katavi, Simiyu na sasa Njombe pamoja na Mkoa mpya wa Songwe. Naomba maeneo haya ambayo yameanza upya pamoja na Wilaya zake mpya basi Wizara iyatazame kwa upya ili kusudi yawezeshwe kuwa na *master plan* pamoja na upimaji wa kisasa, tusije tukajikuta tena kwamba maeneo haya yameanza upya lakini yakapata athari ile ile ambayo imeikuta mikoa mingi kabla ya utaratibu huu mzuri ambao umekuja nao wa kuwa na hii unayosema ni *Integrated Land Management Information System*. Jambo hili ni la kisasa ina maana kwamba kutakuwa na takwimu nzuri kabisa za matumizi mazuri ya ardhi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kusema tu wazi kwamba Wizara hii ni mama ambapo kila Wizara na Idara ya Serikali haiwezi ikafanya kazi zake bila kushirikiana na Wizara hii ya Ardhi. Iwe Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Mazingira, zote zinategemea uwepo wa mipango mizuri ya matumizi ya ardhi inayofanywa na Wizara yetu hii ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba nchi yetu sasa imekuwa ni kitovu cha wawekezaji, watu wengi wanavutiwa kuja katika nchi yetu. Ni jambo jema na ni la kheri lakini kheri inaweza ikapata tena kikwazo pale inapotokea mwekezaji amekuja kama mgeni wetu lakini anafika mahali anaanza kuwa ni chanzo cha ugomvi baina yake na wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili naomba sasa Serikali yetu kupitia Wizara yetu ya Ardhi ilitilie maanani kwa kuanzisha utaratibu wa kuwa na benki ardhi kwamba kuwepo na maeneo ambayo yametunzwa kama *Special Economic Zones* ambapo mwekezaji yeyote anayekuja aelekezwe mahali ambapo atafanya kazi zake kwa amani. Hali hiyo itatujengea heshima kwa wageni wetu na kwa mataifa mengine ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo niishie hapo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niwapongeze tu ndugu zangu Mawaziri na sisi kama Wabunge tuko pamoja na tuko nyuma yao. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Naomba niende moja kwa moja, niunge mkono hoja ambayo imeletwa leo hapa mbele yetu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya kuongoza na kusimamia wizara hii nyeti. Matunda ya kazi yao kweli yanaonekana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *personally* naomba nimshukuru Mheshimiwa Lukuvi kwa kuwa mfano wa kuigwa hasa kwangu mimi nikiwa kijana kiongozi. Amedhihirisha ni jinsi gani tunatakiwa kuwajibika pale tunapopewa majukumu yetu, ahsante sana Mheshimiwa Lukuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Ardhi ya kuhakikisha Watanzania wanapata hati zao na kutatua hii migogoro inayojitokeza katika maeneo mbalimbali, napenda kushauri suala la elimu ya ardhi litiliwe mkazo. Watanzania lazima watambue haki na thamani ya ardhi yao. Hili limekuwa ni tatizo kubwa linaendelea kujitokeza hususan kwenye Mkoa wangu wa Iringa. Kumekuwa na wajanja wachache ambao wanafika kwenye maeneo ya vijijini na kuwashauri hawa wanavijiji kuwauzia haya maeneo, moja kwa bei ya chini na pili wengine wamediriki kuwashawishi hadi kuuza maeneo yao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea hawa wanavijiji wanakosa hata maeneo ya kuzalisha mazao ambayo yanaweza kuwasaidia wao kuendelea kupambana na kukidhi mahitaji ya familia zao. Kwa hiyo, hili suala la elimu Mheshimiwa Lukuvi naomba tulipe kipaumbele sana. Hii elimu isitoelewe tu kwa wale wanakijiji lakini hata hawa wawekezaji wanaokuja kununua haya maeneo

kule vijijini waambiwe kuwa wanapopewa yale maeneo wahakikishe hawa wananchi wanaachiwa eneo ambalo wataendelea kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nakazania hii elimu? Tumesema tunataka Tanzania sasa iwe nchi ya viwanda na wote tulikubaliana kuwa hawa wakulima wadogo wadogo, hii asilimia 75 ambao wako kijijini wanaotegemea kilimo ndiyo wangetumia hiki kilimo kuzalisha *raw materials* ambazo zitapelekwa kwenye hivi viwanda. Kama haya maeneo yote yatakuwa yamebebwa na hawa watu chache, tutakapoanzisha hivi viwanda watakaonufaika ni wale ambao watakuwa na maeneo makubwa ya kuzalisha hizi *raw materials* na hii dhana nzima ya kuwasaidia hawa wakulima wadogo wadogo waweze kufikia ule uchumi wa kati itakuwa ni vigumu kufikiwa. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza lazima suala la elimu lipewe kipamumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hati miliki hasa hizi za kimila limechangiwa kikubwa sana na Wabunge hapa ndani na mimi ningependa niongezee. Naomba hizi hati miliki za kimila zipewe uzito na ziwe zinatambuliwa kisheria. Hata nchi za wenzetu zilizoendelea, mtu anayemiliki ardhi anapewa heshima kubwa na hiyo heshima inatokana na kuwa ile hati yake popote anapokwenda, hata kwenye hizi *financial institutions* anaweza kukopesheka lakini hapa nyumbani kwetu bado ni changamoto kubwa sana hususan kwa wanawake. Sisi ni asilimia kubwa hapa nchini, *population* yetu ni zaidi ya asilimia 51 lakini ni asilimia 19 tu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kwa heri, dakika tano zako zimekwisha mlikubaliana kugawana dakika na mwenzako Mheshimiwa Juliana Shonza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza dakika tano.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nishukuru kwa kupata nafasi hii. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. Vilevile tuwashukuru sana kwa sababu wameweza kutupatia taarifa zote ambazo zinahusu Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua Mkoa wetu wa Songwe ni mpya na changamoto kubwa ni kwamba maeneo mengi hayajapimwa na wananchi wake wanamiliki ardhi kwa hati za kienyeji. Suala hili kwa Mkoa wa Songwe imekuwa ni changamoto kubwa sana. Kama tunavyojua sasa hivi

Wilaya yetu ya Mbozi imeweza kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe ambapo wananchi wengi wanamiminika kwenda mahali pale kwa ajili ya kupata ardhi. Hata hivyo, ardhi wanauziana kienyejienyeji kwa sababu hakuna mpango wowote wa kuweza kurasmisha ardhi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi kuomba Wizara ya Ardhi kwa kutambua kwamba Mkoa wa Songwe ni mpya wahakikishe kwanza wanakomboa ile ardhi ambayo inamilikiwa na wananchi lakini ukienda kuangalia katika mpango wa Mkoa unakuta sehemu zingine zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Kwa hiyo, naomba Wizara hii iweze kuliangalia hili suala ili waweze kukomboa yale maeneo ambayo yanamilikiwa na wananchi lakini kiuhalisia yametengwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Wananchi wale wa Wilaya ya Mbozi walipwe fidia waweze kuyaachia maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, kama tunavyojua katika Wilaya yetu ya Momba, katika Mji wa Tunduma, mji ule unakua kwa kasi kubwa sana lakini mpaka sasa hivi mipango miji ya Mji wa Tunduma kwa kweli haieleweki. Mji ule ni mji wa wafanyabiashara, *population* iliyopo pale ni kubwa sana na nyumba zimejengwa kiholela holela na pale ndiyo taswira ya Tanzania kwa nchi hizi za Kusini. Mtu anapokuwa anatoka Zambia akifika pale, ile ndiyo picha halisi ya Tanzania, mtu anapotoka *South Africa* akifika pale ile ndiyo picha halisi ya Tanzania lakini mazingira ya pale Tunduma kwa kweli hayaridhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuomba Wizara ya Ardhi, nimuombe sana Mheshimiwa Lukuvi aweze kuangalia eneo lile la Tunduma. Tumeshuhudia katika nchi zingine kwa mfano China, wenzetu waliweza kubadilisha miji yao wakajenga maghorofa, wananchi wakapata nyumba ambazo ni makazi mazuri. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii iweze kutupia jicho katika Mji ule wa Tunduma ili basi yale maeneo yote ambayo ni *squatter* yaweze kuondolewa. Yakishaondolewa waje na mpango wa kutujengea majengo ya ghorofa ili basi wananchi wa pale waweze kuishi katika makazi salama. Naamini hili kwako Mheshimiwa Lukuvi linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo tukijenga majengo ya ghorofa katika eneo lile, moja kwa moja Serikali itakuwa imepata ardhi ya wazi ambayo najua kabisa itatumika kwa ajili ya matumizi mengine ya Serikali. Kwa mfano, katika mji ule suala la miundombinu ya barabara haieleweki, barabara kuu ni moja tu kwa sababu nyumba zimejengwa kiholela. Kwa hiyo, naomba Wizara hii iweze kutupia jicho pale Tunduma, wahakikishe eneo lile linapimwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Unga, unga.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mhehsimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kupongeza Wizara hii ya Ardhi ambayo kwa kweli imeonyesha umahiri katika utendaji wake wa kazi, naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, nitazungumzia zaidi Jimbo la Njombe. Katika Mji wa Njombe kuna tatizo moja kubwa sana, wakati wa Wizara ya Ujenzi niliongea na leo Wizara ya Ardhi naomba niongee. Ninaloliongelea mimi ni zile alama za 'X', zimewekwa alama za 'X' kwenye nyumba ambazo Wizara ya Ardhi imetoa hati halali kwa wale wananchi. Matokeo yake ni kwamba zile hati walizonazo wale wananchi wanaendelea kuzilipia na kodi ya ardhi wanalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo ni kwamba mji ule sasa hivi ni mchafu kwa maana ya kwamba majengo yamechakaa na watu wanashindwa kuziendeleza zile nyumba zao. Kama tunavyofahamu kila mahali penye mji maana yake ndiyo mahali pa biashara, zile nyumba nyingi ni za wafanyabiashara, wanashindwa kutumia zile nyumba kama dhamana katika mabenki kwa sababu tu zina alama za 'X'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ya Ardhi kwa kuwa na yeye ni mnufaika na kodi ya ardhi ambayo wananchi wale wanalipa, waone ni namna gani watafanya kutatua tatizo hilo wakishirikiana na Wizara ya Ujenzi. Vinginevyo tukubaliane, barabara ile pale mjini ipunguzwe *size,* zile alama za 'X' zifutwe ili wale wananchi waendelee kuzitumia zile nyumba zao kama dhamana katika mabenki kwa ajili ya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nyingi kwa Wizara ya Ardhi, liko tatizo la asilimia 30 za Halmashauri ambazo hazirudishwi. Halmashauri yangu ya Mji wa Njombe inadai zadi ya shilingi milioni 60 haijawahi kurudishiwa. Niombe sana Wizara hii iangalie na iweze kurudisha hiyo fedha ambayo Halmashauri imekusanya imeipelekea Wizara na Wizara haijarudisha ile asilimia 30 kwa Halmashauri. Tatizo tunalolipata pale ni kwamba hata kuwahamasisha wananchi waweze kuendelea kulipia kodi hiyo haiwezekani kwa sababu Mkurugenzi hayuko tayari kutoa fedha yake nyingine ili tuhamasishe wananchi walipe kodi ya ardhi ni kwa sababu tu Ardhi wenyewe kama Wizara hawarudishi ile asilimia 30. Kwa hiyo, nikuombe sana kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi

turudishie hiyo asilimia 30 ili ndugu zako tujenge zahanati kule na wadogo zako waendelee kutibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine tulilonalo Njombe ni bustani za mabondeni maarufu kwa jina la vinyungu. Nafikiri kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi unafahamu vizuri sana sheria hii ya mita 60 Njombe inatuathiri sana kwa sababu kwanza mji wenyewe uko milimani halafu wananchi wale walio wengi ni wakulima wanatumia bustani kama sehemu ya kipato kwao. Kwa hiyo, tunapokuja kuwaambia wasilime tayari tunawaathiri kiuchumi na tunavuruga kabisa utaratibu wao wa maisha. Najua hii ni sheria lakini naomba tuangalie jinsi ya kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sababu zinazotolewa wakati mwingine zinakosa mantiki ya kisayansi. Watalaam wanatuambia tusilime mabondeni kwa sababu tunavuruga mfumo wa maji, tunasababisha maji sijui yafanye nini lakini tukumbuke kwamba tumekuwa tukilima kwa muda mrefu, sisi tumezaliwa tumekuta wazazi wanalima maji yale hayajawahi kukauka na yapo vilevile. Sasa hiyo hoja ya kuambiwa tunapungaza maji, tunapunguzaje maji? Kama kuna mahali yamepungua maji ni huko yalikopungua lakini siyo Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ambalo ni la kitalaam kwamba maji yanatunzwa mlimani, zamani Maafisa Ugani walihamasisha wananchi walime kwa matuta ili kutunza maji kusudi mvua ikinyesha maji yakifika kwenye tuta yatulie yaweze kuzama kwenda chini. Kwa hiyo, yakizama kwenda chini yale maji ndiyo baadaye yanakuja kutoka kule bondeni. Sasa leo tunaambiwa huku juu tulime kwenye sesa au tambarare lakini kule mtoni tusilime, kisayansi hiyo haikubaliki. Naona watalaam wa sayansi warudie tena kufanya utafiti wao ili sisi watu wa Njombe Mjini watuache tuendelee kulima vinyungu kwa ndiyo vinasababisha watu wa mjini mle chipsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Njombe Mjini tuna tatizo lingine linalohusiana na ardhi. Uwanja wa ndege wa Njombe Mjini uko mjini kabisa. Katika lile eneo la uwanja wa ndege wako wananchi wana nyumba zao pale na wanashindwa kuendeleza nyumba zao kwa sababu tu wanaambiwa wako eneo la uwanja wa ndege na hawalipi maduhuli yoyote ya ardhi.

Naomba Wizara hii ifanye utaratibu tuone kama wale wananchi ni kweli wako ndani ya eneo la uwanja wa ndege waambiwe rasmi wako ndani ya uwanja wa ndege na kama kuna fidia walipwe waondoke. Kama hawapo ndani ya eneo la uwanja wa ndege basi wapewe hati za ardhi ili kusudi waendeleze yale makazi yao na wazitumie zile nyumba zao kwa ajili ya uchumi. Kinyume cha hapo wale watu tunawafanya wanakuwa maskini, nyumba zinachakaa, wanaishi maisha ya wasiwasi wakiamini kwamba kuna uwanja wa

ndege pale na wenyewe watu wa uwanja wa ndege hawasemi lolote juu ya maendeleo ya ardhi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo na mimi niseme kidogo kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa. Shirika la Nyumba la Taifa walifika Njombe kutafuta eneo la kujenga nyumba na wakaonyeshwa eneo lakini kwa bahati mbaya sana ninasikitika kwamba Shirika la Nyumba hawajarudi tena Njombe. Taarifa niliyonayo ni kwamba walihitaji wapewe eneo la bure sasa Njombe eneo la kutoa bure halipo. Kwa hiyo, niwaombe sana Shirika la Nyumba, wakiona eneo lina thamani maana yake hata nyumba watakazojenga zitakuwa na thamani hivyo hivyo. Naomba waje tena Njombe wachukue lile eneo ambalo tumelitenga kwa ajili yao lakini watulipe fidia kwa sababu eneo la bure halipo na wao kwa upande mwingine zile nyumba si wanaziuza, kwa hiyo ni biashara. Kwa hiyo, wasione kwamba wanatakiwa wapewe eneo la bure kama fidia ya gharama za uendeshaji wa shirika lao, hapana, wasifanye namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Shirika la Nyumba hilo hilo wengi wamesema kwamba nyumba zao ni za ghali sana, ni kweli nyumba zao ni ghali sana. Hatufahamu sana ni gharama gani wanaingia lakini nafikiri shirika lijipange vizuri tu ifike mahali liwe na mifuko miwili, mfuko wa kuuza hizo nyumba za gharama lakini liwe na mfuko kwa ajili ya nyumba za wanyonge. Kwa hiyo, lijenge nyumba za wanyonge ili wanyonge wapate nyumba. Tusipofanya hivyo shirika litaendelea kulaumiwa lakini na lenyewe linashindwa kufanya vinginevyo. Niwaombe sana Shirika la Nyumba wasife moyo, wajitahidi lakini wasisahau kufika Njombe tuwape eneo lile lakini watulipe fidia ili waweze kujenga nyumba zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme na mimi naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nyingine tena. Na mimi kutoka mwanzo niseme kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kukubali kwamba viongozi wa Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wengine wote wamejitahidi sana hasa katika eneo la kuondoa migogoro. Tunawapongeza na tunaomba muongeze bidii. Mimi namfahamu Waziri, Mheshimiwa Lukuvi tulikuwa naye Ofisi ya Waziri Mkuu na najua jinsi anavyochapa kazi, endelea kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ndiyo rasilimali kuu ya Tanzania na pengine nchi hii ya Tanzania imejaliwa kuwa na ardhi yenye rutuba lakini ardhi inakuwa na thamani pale tu ambapo imepangwa, imepimwa na kumilikishwa. Bila ya kuwa na vipimo, bila kuwa na hati miliki, ardhi kwa kawaida pamoja na kwamba ni rasilimali muhimu lakini inakuwa haina thamani. Mpaka sasa hivi ni asilimia 15 tu ya ardhi ya Tanzania imepimwa na imemilikishwa. Kwa hiyo, asilimia ile yote 85 maana yake haina thamani. Kama Tanzania tunataka kuondokana na umaskini inabidi kwa kweli tuipe rasilimali hii muhimu thamani inayotakiwa kwa kupangwa, kupimwa na kumilikishwa. Wananchi wanapokuwa na hati miliki au haki miliki wanaweza wakaitumia ile ardhi kwa shughuli za uchumi lakini ikatumika vilevile kama dhamana kukopa kuweza kutumia ile ardhi vizuri zaidi. Kwa hiyo, ndugu zangu nawaombeni kipaumbele kipelekwe kwenye kupima ardhi hii ya Tanzania na kumilikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi zaidi ya dhamana wanaweza wakatumia ardhi hii ikiwa na hati miliki kama hisa na kuungana na wenye mtaji wa fedha ili ardhi hii itumike katika uwekezaji. Watanzania wanashindwa kuwekeza kwa sababu ardhi waliyonayo haina thamani na kwa hivyo hawawezi kuwa na hisa kwenye uwekezaji. Kwa kiingereza inaitwa *land for equity* ambapo alipokuwa Waziri Mheshimiwa Anna Tibaijuka na mimi tuliibuni ili Watanzania wawe na uwezo wa kushiriki kwenye uwekezaji bila ya kutafuta fedha, wanaweza wakatumia hiyo ardhi kwa kukopa au wanaweza kuwa na hisa kwenye uwekezaji kupitia ardhi hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwa wawekezaji na nataka nijielekeze Hanang. Hanang ni eneo la kilimo na mifugo na ardhi ipatayo heka 70,000 iko mikononi mwa wawekezaji. Wawekezaji wenyewe wale hawaitumii ardhi ile kama inavyopaswa. Kwanza wametumia sehemu tu ya ardhi ile waliyopewa wakati watu hawana ardhi ya kutosha wanaingalia ile ardhi na kuitamani, napenda tuwasimamie wale ili waitumie hiyo ardhi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, sioni sababu ya mwekezaji kutoka nje achukue ardhi ya Tanzania, kwa mfano pale Hanang watu wa Hanang wanazalisha ngano nyingi zaidi kwa heka moja kuliko wawekezaji waliokuja na ina-*defeat the whole purpose* inakuwa haina maana. Kwa hiyo, naomba tuangalie na tija katika uwekezaji ili tupate faida ya kutosha kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hivyo kutokana na uwekezaji kwenye ile ardhi, wawekezaji walituahidi kufanya mambo mbalimbali. Siwezi kuorodhesha, lakini moja ambalo nalijua ni kujenga mabwawa makubwa kwa ajili ya umwagiliaji na wananchi kuweza kunufaika lakini mpaka sasa limechimbwa bwawa moja na halijakamilka. Nataka na ahadi zile zote nazo ziweze kutekelezwa ili watu wa Hanang wanufaike na uwekezaji ule na kama

hawalimi vya kutosha, kuna wengine wana mashamba zaidi ya moja, mashamba yale ambayo hawawezi kuyalima yarudi mikononi mwa wananchi. Mimi najua wananchi wa Hanang wanaweza kulima ardhi ile na kuweza kuleta manufaa ambayo wawekezaji hawaleti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ndugu zangu migogoro ya ardhi iko mingi Wilayani Hanang. Kuna migogoro ya mipaka kati ya kata na kata, vijiji na vijiji na hata wilaya na wilaya zingine zinazopakana na Hanang hata Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Singida, Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine tunakuwa na migogoro. Namuomba Waziri Mheshimiwa Lukuvi aje Hanang na Mkoa wa Manyara ili migogoro ile itatuliwe maana kila wakati kumekuwa na vifo kupitia migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wale wawekezaji watimize ahadi yao moja ambayo wameahidi ya kujenga *branch* ya *university* ya Sokoine kwenye yale mashamba, mpaka sasa imebakia ahadi tupu hakuna utekelezaji wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo nataka kuongelea kuhusu ardhi ni kwamba jamani bila ya kupima hii ardhi na kuiweka kwenye shughuli mbalimbali, mifugo, kilimo, biashara, huduma za jamii, migogoro itaendelea kuwepo. Migogoro itaendelea kuwepo kati ya wafugaji na wakulima, migogoro itaendelea kuwepo kati ya wakulima, wafugaji na hifadhi mbalimbali, migogoro itaendelea kuwepo kati ya wawekezaji na wananchi wa Tanzania. Kwa sababu bila ya kujua wafugaji wawe wapi, wakulima wawe wapi, wawekezaji wawe wapi, jamani hatuwezi kuondokana na mambo haya hata tukiwa na *operation* ngapi haitasaidia. Ukiwatoa wananchi kutoka kwenye hifadhi na haijulikani wapi wanakwenda kwa ajili ya kuhakikisha ng'ombe wao zinabakia kuwa hai watavizia kurudi kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nathamini hifadhi za Tanzania na ni mmoja wa watu ambao nitakuwa wa mwisho kabisa kuondoa hifadhi lakini lazima tuone kwamba wakulima na wafugaji wana maeneo ya uhakika la kufanya shughuli zao. Wakijua eneo lao ni hekta ngapi watahakikisha ng'ombe wanaoweza kubaki kule watabaki na wengine watauzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna nyingine ya kuwasaidia ni kuwa na masoko mbalimbali tushirikiane pamoja kushughulikia suala hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza Wizara zile zikae mara moja ili kuona kwamba wananchi wavyotolewa kutoka kwenye hifadhi, wananchi wanavyogombania ardhi kunakuwa na mahali mahsusi pa wale wananchi kwenda kama ni wafugaji au wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Nyumba, mambo ya msingi kwa binadamu ni chakula, mavazi na makazi. Shirika la Nyumba linafanya kazi nzuri lakini kama lilivyoundwa zamani baada ya uhuru ilikuwa ni kuwapatia maakazi watu wanyonge zaidi kuliko wale wanaojiweza.

Kwa hiyo, naombeni sana Shirika la Nyumba lifanye kazi hiyo ya kuona watu wa Manzese, Keko wamepata nyumba, watu wa maeneo ya chini wamepata nyumba. Maeneo yale ya matajiri wajenge wenyewe kwa sababu wana mali ya kuweza kuweka dhamana kwenye benki na kujenga nyumba zao, sisi tujielekeze kwa Watanzania wanyonge, wana haki ya kukaa kwenye nyumba na hakuna mtu ambaye ana fedha yake mwenyewe asijenge, lakini ni kwa sababu ya kukosa mali ya kuweka dhamana hawawezi kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie pongezi zangu na shukrani zangu za dhati kwa Wizara na viongozi wa Wizara, watendaji na taasisi ambazo zipo kwenye Wizara hii. Na mimi nashukuru sana migogoro inapungua, tuendelee kupunguza migogoro hii hadi inapokwisha. Sisi wengine tumekaa kwenye migogoro tukiona watu wanakufa na hatutaki kuendelea kuona watu wetu wanakufa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, wafuatao kwa hiari ya moyo, dakika tano, tano, kama hawawezi waniambie, Mheshimiwa Joseph Kakunda dakika tano na Mheshimiwa Shally Raymond dakika tano.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Naomba niende moja kwa moja kwenye masuala machache, sasa hivi Wizara inafanya mapito makubwa ya sera ya ardhi na tunaona huko mikoani inaendelea. Naomba kwa hatua hii Wizara isifanye makosa waliyofanya mwanzoni pale. Baada ya sera ya mwaka 1995 waliandaa sheria halafu baadae ndiyo wakaja kuandaa mkakati wa kutekeleza sheria. Kilichokuwa kinatakiwa ni kwamba baada ya sera unaandaa mkakati wa Taifa ambao unakwenda sambamba na programu ya Kitaifa ya kutekeleza sera, halafu ndiyo unakuja unamalizia na sheria. Kwa hiyo, naomba safari hii wazingatie huo mfuatano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utekelezaji wa sera tunahitaji mambo mawili makubwa, kwanza *awareness* ya wadau wote waielewe sera, lakini pili tunahitaji rasilimali, rasilimali watu hiyo ni ya kwanza kabisa na rasilimali fedha. Kwa miaka mingi fedha ambayo imekuwa ikitengwa au inaombwa na Wizara hii imekuwa ni kidogo mno. Ndiyo maana Wizara hii ina upungufu mkubwa wa

Maafisa Ardhi, Maafisa Mipango Miji, Wapima, Wathamini, Wachora Ramani, Wakadiriaji Majengo na kadhalika. Kwa kifupi ina nguvukazi kidogo sana, sidhani kama hiyo nguvukazi inaweza kutekeleza sera kama wanavyotaka. Vilevile rasilimali fedha imekuwa inapangwa kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukiangalia taarifa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri viwanja vilivyopimwa mwaka huu 2015/2016 ni 112,000 tu angalau wangepima 400,000 ingekuwa ni afadhali kwa nchi yetu. Kati ya hivyo viwanja 112,000 viwanja 38,700 vyote vimepimwa Dar es Salaam na Pwani ambayo ni asilimia 35, huu ni upungufu mkubwa sana. Hati miliki zilizosajiliwa 25,000 tu angalau wangekuwa na uwezo wa kusajili hati 100,000 kwa mwaka ingetusaidia kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *trend* ni hii ina maana kwamba hata hii mipango kabambe ya majiji, manispaa na miji yetu inayoandaliwa haitaweza kutekelezeka kwa sababu ya ufinyu wa rasilimali fedha na upungufu wa rasilimali watu. Naomba sana Wizara ijipange ili kwenye mwaka mwingine unaokuja baada ya mwaka ujao (2017/2018), waje na mkakati wa maombi ya fedha za kutosha ili utekelezaji ufanyike vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa nguvu kazi au upungufu wa uwezo wa kutumia fedha. Katika mwaka huu wa fedha walipanga kutumia shilingi bilioni 3.45 kwa ajili ya miradi ya maendeleo wamepata shilingi bilioni 3.43 ambayo ni sawasawa na asilimia 99, lakini hotuba ya Waziri inatuambia wametumia milioni 745 tu ambayo ni asilimia 21. Ina maana hata kama tukiwapa pesa kumbe uwezo wa kutumia fedha yaani ile *absorption capacity* inavyoelekea kwa Wizara hii ni ndogo sana, sasa sijui watajipangaje. Mheshimiwa Waziri atakaposimama atueleze vizuri wamejipangaje, hivi uwezo wa kutumia fedha tufanyaje, sisi Wabunge tumsaidie vipi ili Wizara hii iwe na uwezo wa kutumia fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni Shirika la Nyumba la Taifa, utekelezaji wake nao ni mdogo sana. Mahitaji ya nyumba kwa nchi yetu ni 200,000 kwa mwaka, lakini wao wamepanga kujenga nyumba 5,000 tu kwa mwaka ukilinganisha na nyumba 200,000 yaani ni upungufu mkubwa sana. Mahitaji ya jumla ya nchi yetu sisi tunahitaji nyumba 3,000,000, tutafikia lini malengo haya?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond dakika tano.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi naungana na wenzangu kuendelea kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache lakini sitaweza kumaliza ila nianze tu na yale ambayo ni muhimu zaidi. Kwenye ukurasa wa 43 kwenye kile kifungu cha 58 kazi mojawapo au shughuli aliyotuambia ni pamoja na programu ya Taifa ya kurasimisha na kuzuia ujenzi holela mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sizungumzii hayo anayokwenda kufanya nazungumzia miji ilivyo sasa hivi. Ni kweli miji yetu ilikuwa imepangwa hasa ili miji ya awali kwamba kuna maeneo ya *residential, industrial areas,* miji na kadhalika. Kilio changu ni hali tuliyofikia sasa, eneo kama Oysterbay ni *residential area* lakini sasa unakuta Oysterbay kumekuwa ndiyo kwenye *pubs,* vilabu, ndiyo kwenye kelele usiku na mchana, Oysterbay. Leo Mwalimu angefufuka angesema nini? Sasa sijui jinsi gani yeye Waziri ambaye anashughulikia makazi analizungumzia hili na anafanya nini ili Halmashauri zisiruhusu kujenga hivyo? Sasa hivi Oysterbay hakukaliki, ni fujo tupu. Namuomba Waziri huyu mhusika aweze kuona ni jinsi gani sasa watu watalala usiku na kuamka mapema wakafanye kazi zao. Oysterbay na kwingineko kumeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu huu Mji wa Dodoma, ni mji mtarajiwa kuwa Mji Mkuu au Jiji la Taifa, lakini kuko hovyo, Dodoma haijakaa namna hiyo na Dodoma ndiyo yenyewe yenye *Capital Development.* Iweje watu wa Nigeria walivyokuja huku, walichukua zile ramani zetu wakati wakitaka kuhamisha Lagos kwenda Abuja, wameweza kutekeleza, mji ule umehama na ni kuzuri tu. Si kweli kwamba hawa Mawaziri wetu hawajasafiri, kabla hujatua nchi yoyote ndege ikianza kutua unaona miji ilivyopangika, kwa nini wanakwenda tu wanang'azang'aza macho hawatuletei huo ujumbe. Sasa hivi Lagos imeshahamia Abuja na kumepangika, kwa nini siyo Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nalotaka kuzungumza ni makazi ya watu wa kawaida. Ni miaka mingapi sasa, hamsini na ya uhuru bado watu wanaishi kwenye tembe, zile nyumba ambazo tukiwa tunakuja Dodoma tunaziona, bado watu wanaishi kwenye makuti, bado watu wanaishi kwenye nyumba ambazo hata huwezi kujua kama bado tuko Tanzania. Mabati yameshushwa bei watu wajenge nyumba nzuri, haiwezekani, Waziri mhusika anasemaje, anatoa semina lini kwa watu walio vijijini wajue maana ya kuishi katika nyumba bora? Tunataka kuona anatoa semina, watu waishi kwenye nyumba zenye mabati, zenye kuta nzuri na wasaidike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda ni mfupi sana na nakosa amani kabisa kwa vile hakika ni mambo mazuri ningetaka kuongea lakini nizungumzie mkoa wangu. Mkoa wa Kilimajaro sasa hivi hatuna tena mahali pa kuishi vihamba vimegawiwa limebakia eneo la makaburi tu. Naomba huyu Waziri wetu kila inapowezekana tuonyeshwe eneo jipya ili vijana wetu wahamie huko sasa wakaweke makazi mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu Dodoma, tulikuja lile Bunge la Tisa tukakuta viwanja vimepangwa ukutani tukajichagulia viwanja, tumepelekwa Itega, mpaka leo kule Itega hawajapeleka maendeleo. Mimi ni mmojawapo ambaye nimeathirika, nilinunua kiwanja shilingi milioni nne lakini nakwendaje kujenga Itega, hakuna juhudi zozote za kuwezesha watu kujenga makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie *National Housing.* Ni Shirika ambalo limefungua watu macho na hata hapa Dodoma wakaone ghorofa za Medeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. OMAR A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mungu kutuamsha salama. Na mimi naomba nitoe ushauri wangu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Lukuvi kwa maamuzi yake mazito ya kubomoa lile ghorofa kubwa pale mjini, ila napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri asiishie hapo, azidi kupambana kwa kuwa majengo ambayo hayana ubora yatakuwa mengi sana, hivyo katika kuokoa maisha ya watu, napenda kuhimiza wataalam wetu wasikae ofisini, waende *site* na kukagua kila hatua ya ujenzi inayojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kuangalia watumishi wake kwa karibu zaidi ili kuhakikisha migogoro ya ardhi inapungua kwa kiwango kikubwa. Malalamiko ya ardhi yanasababishwa na watumishi wa Wizara ya Ardhi kwa uuzaji holela maeneo ya wazi, utoaji wa hati mara mbili mbili ambayo siyo ya kujengea. Tukirekebisha hili, hali hii ya migogoro mijini na vijijini itakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, nadhani wengi hawana elimu ya sheria *especially* wafugaji. Utakuta

mfugaji mmoja ana ng'ombe 5,000. Kwa idadi hii lazima atagombana na wakulima kwa kuwa eneo lake haliwezi kumtosha. Elimu ya sheria ya kuwa na idadi ya mifugo inatakiwa itolewe sana na isimamiwe kwa makini na kwa ukaribu. Pia wafugaji wapewe elimu ya kupanda nyasi, ikiwezekana Serikali ianze kwa mashamba ya mfano. Hii itapunguza kasi ya wafugaji kuhamahama kwa kutafuta malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri na watumishi wake, nyumba nyingi zinazojengwa mijini hazifuati sheria ya *parking,* ni vizuri sheria kali ikatipitishwa kwa yeyote asiyefuata kanuni ya ujenzi mijini. Pia napenda kuishauri *NHC* kuangalia upya mpango wa kodi zao na hili linaweza kurekebishika kwa kupunguza kodi na linawezakana kama watasimamia vizuri ukusanyaji wa kodi za sasa hasa katika taasisi kubwa ambazo zinaongoza kwa kutolipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali Na. 2 *page* ya 83, marejesho ya asilimia 30 ya makusanyo ya Halmashauri kwenye mkoa wa Tanga kuna Handeni tu; na sasa kuna majimbo mawili; Handeni Mjini na Handeni Vijijini. Naomba unisaidie ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, napongeza utendaji wa Wizara kwa kazi inayoendelea kutendeka. Nkasi Kusini kuna vijiji kadhaa ambavyo vinadaiwa na *Lwanfi Game Reserve* kuwa viko ndani ya *reserve* yake, vijiji hivi vilikuwepo kabla ya hata *reserve* kuanzishwa. Vijiji hivi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kijiji cha Kasapa, Kata ya Sintali;

(ii) Kijiji cha King'ombe, Kata ya Kala;

(iii) Kijiji cha Mlalambo, Kata ya Kala;

(iv) Kijiji cha Ng'undwe, Kata ya Wapembe; na

(v) Kijiji cha Namansi, Kata ya Ninde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vijiji pia vimepakana na Lwanfi na kuna migogoro ya hapa na pale kama vile kijiji cha Nkata na kijiji cha China, Kata ya Kate. Kwa msingi huo, naomba Waziri achukulie hii ni migogoro na sijaiona ndani ya kitabu chake cha migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalopenda kuchangia ni kuhusu mashamba ya wawekezaji. Mipaka ya mashamba ya wawekezaji wawili Jimboni Nkasi Kusini ina migogoro na wananchi wanaozunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba hayo yanamilikiwa kihalali lakini kutokana uhaba wa ardhi wananchi wanakosa ardhi ya kutosha kulima. Mashamba hayo ni yale ya Nkundi na China. Ni mashamba makubwa, Serikali ione namna ya kuzungumza na wawekezaji hawa ili kuwaachia wananchi sehemu za mashamba hayo kutokana na uhaba wa ardhi walionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi ya Kalambo inapakana na vijiji vya Nkana, Sintali, Mkomanchindo na Kasapa, pamoja na sera ya kugawa vitalu kwa waliobinafsishiwa, vitalu havitumiki vizuri na wananchi hawana ardhi. Nashauri ardhi hii igawiwe kwa wananchi kwa sababu hawana ardhi katika vijiji nilivyovitaja, hii ni muhimu sana.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fikra za kuchangia kwa maandishi. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa tena kuongoza Wizara hii muhimu ili aweze kutimiza azma yake kwenye sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu napenda niuelekeze kwa Mheshimiwa Waziri na nitamtaka wakati wa kufanya majumuisho nipate majibu ya maswali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, Bunge la mwaka 2010 akiwa Waziri wa Wizara hii alisimamia Kamati ya Ardhi, Maliasili kwenda nchini Uganda kujifunza ni namna gani Uganda wamefanikiwa katika sekta ya ardhi. Pia Kamati ilijifunza ni namna gani na muda gani wananchi wa Uganda wanapoanza mchakato wa kumiliki ardhi na jinsi zoezi hilo linavyokwenda haraka yaani si zaidi ya wiki moja mwananchi wa Uganda anakuwa amemiliki ardhi. Kamati ya Ardhi iliyopita nikiwa mmoja wa Wajumbe tulishauri Serikali kupitia Wizara hii kufanya jambo hili. Je, kwa sisi Tanzania na ili jambo hili liweze kupunguza kero na msongamano kwenye ofisi za ardhi limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati iliyopita ilienda nchini Dubai kujifunza kwenye Shirika lao la Nyumba. Kamati ilishauri Shirika la Nyumba lipewe mamlaka yake, lijitegemee na lijiendeshe. Je, suala hili hadi sasa limefikia wapi ili Shirika la Nyumba lifanye shughuli zake kwa ufanisi zaidi? Ahsante sana.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba hii kwa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri kwa mikakati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida ya Serikali yetu tatizo kubwa linaanzia pale ambapo Serikali inaposhindwa kutoa fedha zilizotengwa katika bajeti hii. Wizara ya Ardhi kwangu mimi ni kama Wizara mtambuka kwani migogoro mingi husababishwa na maingiliano ya sera kama vile sera ya kilimo, sera ya mifugo, sera ya madini na kadhalika ambazo zote zinaihusu ardhi lakini ni nani anasimamia sera ya ardhi kwa upana wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi na umaskini wa watu wetu. Watanzania wengi hasa wa vijijini wanakuwa maskini kutokana na kushindwa kwa Serikali kuwamilikisha ardhi. Hivyo watu hawa hushindwa kuaminika na taasisi za kifedha, hawakopesheki na pale mwananchi anapoomba kupimiwa ardhi yake ili aweze kuwa na hati miliki gharama huwa ni kubwa sana na kuwa na milolongo mingi inayosababishwa na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanashindwa kuwekeza vijijini kwani kikwazo kikubwa ni vijiji vingi kutokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kijiji ambacho hakijapimwa kwa matumizi bora ya ardhi kinakosa wawekezaji eti kwa kuwa kijiji husika hakijaingia kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi. Mfano ni jimboni kwangu Liwale wawekezaji wengi wameshindwa kusajili biashara zao kwa kuwa vijiji walivyowekeza havijapimwa kwa hiyo hao wawekezaji kukosa leseni za biashara zao. Yuko mwekezaji ameshindwa kusajili shule kwa kukosa hati miliki ya ardhi kutokana na kijiji kukosa matumizi bora ya ardhi. Vilevile kuna mwekezaji ameshindwa kusajili zahanati kwa kuwa kijiji hakijaingia kwenye matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba mkubwa wa watumishi wa kada hii kunafanya gharama ya kupima ardhi na viwanja kuwa ghali sana. Mfano Mji wa Liwale hulazimika kukodi wapimaji toka Wilaya jirani ya Nachingwea hivyo kufanya bei ya viwanja kuwa juu sana na watu kuendelea kukaa maeneo yasiyopimwa. Namuomba Waziri atuongezee watumishi ili kuhakikisha upimaji wa ardhi Jimboni Liwale unafanyika ili kuharakisha maendeleo ya Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro wa ardhi. Wilaya ya Liwale ina mgogoro wa muda mrefu kati ya wanakijiji cha Kikulyungu na Hifadhi ya Mbuga ya Selous. Mgogoro huu umeshaleta maafa tayari watu wanne (4) wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upimaji wa vijiji; Serikali iharakishe upimaji wa vijiji ili wawekezaji wanapokwenda vijijini wakute kijiji tayari kimeshafanya mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia kuhusu shamba la Malonje. Ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa shamba la Malonje kati ya wananchi na mwekezaji? Mgogoro huu umekuwa ni wa muda mrefu, wananchi wameteseka kwa kukosa ardhi ya kulima. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kuna maeneo kadhaa yenye migogoro Waziri huyu ameimaliza huu unamshindaje au kuna mikono ya wakubwa? Naomba maelezo kwani wananchi wamechoka na ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa na Serikali. Naomba Serikali imalize haraka mgogoro huu kuepusha shari inayoweza kutokea. Ahsante.

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutumbua majipu, kwa hilo hongera sana. Pia naomba kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri anayoifanya na kuliongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishauri Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwamba zile za nyumba za *National Housing Corporation* zilizopo Dar es Salaam ambazo zinakodishwa kwa shilingi 370,000 kwa mwezi kwa kweli bei hiyo ni kubwa mno ukilinganisha na kipato cha wananchi kilivyo. Walio wengi hawamiliki fedha hizo na wakati mwingine nyumba hiyo ikiharibika unaambiwa fedha hakuna, inakubidi utekeleze mwenyewe kazi ya matengenezo au upakaji wa rangi. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii ipunguze kiwango hicho ili wananchi walio wengi wafaidike asimilia mia.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie mchango wangu katika Wizara hii. Nimepitia kitabu cha bajeti katika kusoma nimeona uendelezaji wa miji sijaona Mji wa Tunduma. Kila mmoja anajua kuwa Mji wa Tunduma unakua kwa kasi kubwa na ni lango kuu la kuingilia nchi za Kusini na kati mwa Afrika. Hivyo, kutokuweka Mji wa Tunduma katika miji itakayoendelezwa ni kutokuitendea haki Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Kasi ya ujenzi katika Mji wa Tunduma ni kubwa sana na hatuna kiwanja hata kimoja kilichopimwa hivyo sasa ujenzi ni holela. Pamoja na kutokuona Mji wa Tunduma katika kitabu cha bajeti, naomba Waziri atuingize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika miaka mawili iliyopita tulifanya mchakato wa kutafuta namna ya kukopa katika taasisi za fedha na baadaye turejeshe baada ya kuuza viwanja, lakini tulikataliwa na TAMISEMI. Hivyo, tunaomba Wizara itusaidie kupata fedha katika taasisi za fedha ili kupima haraka Mji wa Tunduma kabla haujaharibika sehemu zote. Wananchi wanahitaji

viwanja, hata leo ukipima viwanja 5,000 ndani ya miezi miwili hutapata kiwanja watakuwa wamemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba sana Wizara itupatie pesa ili tupate *master plan* ya Mji wa Tunduma ili kurahisisha kazi za upangaji wa mji wetu wa Tunduma. Nashauri Halmashauri zote nchini zipate *master plan* katika kurahisisha kupima na kupanga miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua mpango wa kurasimisha makazi (MKURABITA). Mwaka 2012-2013 walikuja Tunduma na kupima baadhi ya maeneo kama Kata ya Maporomoko na Kaloleni katika mitaa ya Kaloleni, Danida, Kastamu, Nelo, Migombani na wakawahamasisha wananchi kufungua akaunti wakaanza kukusanya pesa na kuziweka katika akaunti ile mpaka leo hakuna kinachoendelea pamoja na kuchimba mawe yaani kuweka alama ya kuwa eneo limepimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini mpango huu uliowaacha njia panda wananchi wa kata hizo bila kujua nini kitaendelea utamalizika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Tunduma kuna migogoro ya ardhi kati ya wananchi wenye mashamba na Halmashauri baada ya Afisa wa Ardhi Mteule wakati bado tuko Mbozi kupima maeneo ya watu bila kuzungumza nao na bila kuwalipa fidia na kuwauzia wananchi wengine katika Kata za Mpemba, Katete, Chapwa na Chipaka huo ulikuwa mwaka 2011 na 2012. Hivyo tunaomba pia Waziri afike katika Halmashauri yetu awasaidie wananchi kwani wanamsubiri kwa hamu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mpaka wa Tanzania na Zambia ni tatizo. Nyumba zimeingiliana, Watanzania wameingia Zambia na Wazambia wameingia Tanzania hivyo kuzua sintofahamu kwa wananchi wetu pamoja na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. MBARAKA S. BAWAZIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusaidia sana katika kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji katika Jimbo langu la Kilosa. Nashukuru sana kwa ushirikiano mliotupa japokuwa bado kuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mashamba ya Usagala A&B yaende kwa wakulima. Mashamba hayo yanamilikiwa na *SINO Development Tanzania Limited (Usagara Sisal Estate).* Wafugaji wapewe *Mkata Ranch, Kandoro Ranch* na *Lukumai Ranch* kwani maeneo haya yanafaa sana kwa wafugaji. Hali kwa sasa sio nzuri, watu wanalinda usiku na mchana mazao yao kuogopa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali pamoja na mambo mazuri waliyoyafanya katika Jimbo la Kilosa wazingatie ushauri wangu kwa maslahi ya wananchi wa Kilosa. Naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matatizo makubwa nchini juu ya ulipaji wa fidia kwa wananchi pale Serikali inapotoa/kuchukua ardhi kwa maendeleo na kuwa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya jeshi yamekuwa na migogoro kwa jeshi kutokuwa na hati za ardhi zao na wao kusema wamevamiwa na wananchi. Nashauri majeshi yote Polisi, Magereza na JWTZ wapewe hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba *(NHC);* nashauri mikataba yote ya nyumba iliyoingiwa na *NHC* na wawekezaji wengine ikaguliwe upya. Wasiwasi wangu imekabidhiwa kwa mkataba wa muda mrefu na kwa gharama kubwa mpaka Serikali itakapopata faida itakuwa ni miaka mingi.

Kuhusu maeneo ya wazi, Wizara ikague na kuwanyang'anya wale wote waliopewa maeneo ya wazi na kuyarudisha kwa wananchi. Maeneo mengi ya michezo na kupumzika yametekwa na waporaji wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa ardhi. Halmashauri nyingi zimekuwa zinatoa *tender* kwa wadau kuweza kupima viwanja, nadhani ni kuiibia Serikali mapato yake na kuongeza gharama kwa wananchi. Ninachoomba Wizara ipewe pesa ya kutosha kuweza kusaidia huduma hii kuendelea na kufanya kazi zake kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ofisi za kanda; kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi katika mikoa hasa ya wakulima na wafugaji na maeneo ya vijijini mfano Kijiji cha Mpuguso, Wilaya ya Rungwe, wamenyang'anywa ardhi yao ya kijiji na kujenga zahanati huku wakiwa na hukumu ya halali lakini bado wako kwenye usumbufu. Hivyo, naomba wahusika hasa ofisi ya kanda ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iwe makini kwa hati zinazotolewa kwa wawekezaji ambao wengi wanaingia na *gear* ya kuoa Watanzania ili waweze kupata ardhi. Kwa kushirikiana na Uhamiaji Wizara inaweza kuwabaini wawekezaji hao.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Wizara ya Ardhi ikiongozwa na Waziri Mheshimiwa William Lukuvi kwa kuonyesha nia ya kutatua migogoro ya ardhi kwa kushirikisha wadau wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri wa Ardhi na Waziri wa Maliasili kwa kuonyesha uongozi na nia ya kumaliza mgogoro wa ardhi katika msitu wa Kazimzumbwi uliopo katika Kata za Chanika, Zingizwa, Buyuni na sehemu ya Pugu ambao umedumu tangu mwaka 1994 kutokana na kupunguza mipaka mwaka 1954.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kumaliza mgogoro wa Bonde Msimbazi hasa maeneo ya Kinondoni, Segerea na Ukonga ambapo nyumba za wananchi zimewekwa alama ya "X" na zingine kubomolewa, huko ni kuwarudisha nyuma wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Mheshimiwa Waziri kumaliza mgogoro wa Kipawa Kipunguni, eneo la Uwanja wa Ndege. Pia mgogoro wa ardhi kati ya watu wa kutoka Kipawa na Kipunguni waliopelekwa Kinyerezi Pugu na Buyuni katika Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kulinda maeneo ya umma kama vile shule, zahanati, masoko na polisi; ni muhimu upimaji na kulinda maeneo ya huduma za jamii liwe shirikishi kwa viongozi wa mtaa, kata, Wabunge na wananchi ili kuondoa mianya ya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za upimaji ni kubwa sana kiasi kwamba wananchi wengi wanashindwa hivyo kuishi bila kupima maeneo yao. Ni vema Wizara ikaangalia namna ya kupunguza kero hizo ili wananchi walio wengi au wote wapime ardhi yao ili kujipatia manufaa ikiwemo uwezekano wa kukopesheka katika vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Ardhi iongeze kasi ya kuondoa migogoro ya ardhi na hasa maeneo ya maliasili ili watu wetu waishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Wizara ya Ardhi walau kwa kuweka mipango shirikishi na kuanza kumaliza baadhi ya migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Waziri kwa hotuba nzuri kuhusu sekta ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi. Pili, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

(i) Wananchi waelimishwe kuhusu matumizi bora ya ardhi na kutambua mipaka yao ya ardhi wanayoimiliki.

(ii) Wananchi wanapata shida kutembea mwendo mrefu kufuata Baraza la Ardhi. Nashauri Serikali ianzishe Baraza la Ardhi kila Wilaya ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa.

(iii) Wawekezaji wasichukue ardhi ya wananchi bila kulipa fidia.

(iv) Kwa kuwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa hukopa fedha kwa ajili ya kupima viwanja ni vema warejeshe mikopo hiyo mapema ili Halmashauri zingine nazo zikope *(revolving fund)*.

(v) Serikali isimamie ujenzi holela wa miji yetu *(squatters)* na kila mji lazima uwe na *master plan* kabla ya kuanza kujenga.

(vi) Serikali itenge fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo badala ya kutegemea wafadhili ambapo hakuna uhakika wa kuletewa fedha zote.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuwasilisha mpango na bajeti ya mwaka 2016/2017. Sekta hii ni muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa Taifa letu, ardhi ni msingi wa shughuli zote za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu migogoro ya ardhi. Narejea Jimbo langu la Muleba Kaskazini, tunayo migogoro mikuu miwili katika Kata za Mayombwe na Muhutire kati ya wananchi na kambi ya Jeshi la Wananchi Kaboya. Jeshi la Wananchi kwa maslahi ya Taifa waliamua kuongeza ukubwa wa eneo lao. Mgogoro huu umepitia ngazi zote za uongozi wa nchi ukiondoa mahakama. Uamuzi wa Wizara ya Ardhi na ile ya Ulinzi kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Kikwete na Rais wa Awamu ya Tano ni kuwa Serikali iwalipe fidia wananchi wa maeneo yote yatakayotwaliwa, lakini mpaka sasa fidia haijalipwa na wananchi wamezuiwa kuendeleza maeneo yao kwa miaka sasa. Katika mwaka 2016/2017, Wizara ya Ardhi ibebe jukumu la uongozi na kumaliza mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa pili ni katika Kata ya Rutoro. Eneo hili kampuni ya *NARCO* iligawa vitalu vya ufugaji kwa wawekezaji kwa kuwapatia wawekezaji hao maeneo ambayo tayari vilikuwepo vijiji tena vinavyotambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limeanza tangu miaka ya 2005, Kamati nyingi zimeundwa kutatua tatizo hili, zilileta mapendekezo bila utekelezaji. Moja

ya Kamati iliyotoa mapendekezo yaliyolenga kuleta suluhu ni Kamati ya Makatibu Wakuu wa Wizara sita iliyoteuliwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli, wakati huo alikuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Kamati za Bunge mara mbili zimefanyia kazi suala hili na kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Kikwete wa Awamu ya Nne aliamua kutwaa hati ya *NARCO* inayohusu eneo la Kata ya Rutoro, iliagizwa eneo hilo ligawiwe upya kwa kubainisha eneo la vijiji na lile la wafugaji. Uongozi wa Mkoa umejaribu kutoa mapendekezo namna ya kutatua mgogoro huo kwa kuazima mapendekezo ya Kamati mbalimbali nilizozitaja hapo juu. Nakubaliana na mapendekezo hayo kwa asilimia 49, sikubaliani na mpango huo pale unapotaka kurudia makosa ya kutoa maeneo kwa watu ambao si raia wa nchi hii na pale wanaposhindwa kutambua kuwa wananchi wa Rutoro ni wakulima na wafugaji. Mgogoro huu hapa ulipofikia ni rahisi sana kuutatua, tuwe *objective* bila kupendelea upande wowote, tulenge maslahi ya Taifa, tumalize mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umbali wa mita 60 kutoka ufukwe wa bahari, kingo za mito, mialo ya maziwa, maeneo yote tengefu na maeneo hatarishi *(hazardous land)* yazingatiwe kama sheria zinavyotaka. Kwa mujibu wa *section 7(1)(d) of Land Act No. 4 of 1999* au *section 7* kwa ujumla wake inaelezea kwa kirefu namna ya kuyabaini na kuyatangaza katika Gazeti la Serikali. Naomba Wizara isiishie hapo, waweke alama inapoishia mita 60 kama walivyofanya *TANROADS* na *TANESCO* wameweka vigingi vya zege kuonyesha mwisho wa mipaka ya maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote ya wazi kwa mujibu wa *cadastral surveys* wapewe watu vibali siyo hatimiliki kama waangalizi. Kwa kibali maalum cha Wizara wataruhusiwa kufanya *beautification* kama kupanda maua *(lawn grasses),* kutengeneza miundombinu ya kuchezea watoto kama bembea na kadhalika. Tahadhari wasijenge majengo ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo yote yaliyotengwa kwa taasisi kama viwanja vya kujenga majengo ya shule, nyumba za ibada, mabenki, vituo vya polisi na huduma nyingine kama vituo vya mafuta, Wizara au Halmashauri zihakikishe unawekwa utaratibu kila mwananchi ayatambue maeneo haya na wawe walinzi wa maeneo haya yasivamiwe. Vichimbiwe vibao vikitaja maeneo haya ili ku-*prohibit* uvamizi wa maeneo haya.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, upungufu wa Maafisa Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ni mkubwa sana kiasi kwamba inasababisha maeneo mengi kutokupimwa kwa wakati na watu kujenga holela. Hata hivyo, wafanyakazi waliokuwepo wanashiriki kwa namna moja au nyingine na kujihusisha na rushwa kwa kupima maeneo ya wazi hata maeneo ya hifadhi ya barabara kama ilivyojitokeza kwa mwekezaji mmoja anayeitwa *Cross Road Petrol Station* kujenga *petrol station* eneo la barabara. Kwa mujibu wa mchoro wa awali sehemu hiyo iliwekwa kwa ajili ya kutengeneza *junction* ya barabara kuu ya Masasi - Tunduru - Songea na barabara ya Bomani jambo ambalo limesababisha mgogoro mkubwa na mkandarasi anayejenga kwa lami barabara ya Tunduru - Matemanga ambapo mwekezaji huyo anadai fidia kwa vile ana hati miliki ya eneo hilo ingawa ni sehemu ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ucheleweshaji wa michoro/ramani za viwanja vilivyopimwa ni kero kubwa sana. Tangu mwaka 2012 mchoro wa viwanja vilivyopimwa bado haujarudi kutoka Wizarani ili walionunua viwanja waanze kutafuta hati ya viwanja vyao. Kwa hiyo, ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Tunduru. Mimi nikiwa mmojawapo nimeshindwa kupata mkopo kwa kukosa hati ya nyumba yangu kwa vile mchoro bado haujapitishwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tatizo la viwanja vilivyopimwa kupewa watumishi badala ya wananchi wa kawaida. Watumishi hao baadaye huviuza viwanja hivyo kwa bei ya juu kwa wananchi wa kawaida wakati wao wamevinunua kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, mipaka ya vijiji inavunjwa sana na watumishi wa ardhi kwa kusogeza na kutoa *beacon* zilizowekwa wakati vijiji hivyo vimeanzishwa na kusababisha migogoro ya kijiji na kijiji. Kwa mfano kijiji cha Namasalau na Kitando, Semli na Chikomo/Mchesi/Muungano suala hili limeleta ugomvi wa wakulima kwa wakulima kutokana na Ofisi ya Ardhi kutotoa ramani za awali za vijiji hivyo. Hivyo, ni vyema Ofisi ya Ardhi wakatoa ramani ya Wilaya ya Tunduru kwa kila kijiji ili wajue mipaka yao ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, mikopo ya nyumba kwa wafanyakazi. Mikopo mingi ya mabenki kwa wafanyakazi inatolewa kwa walio Dar es Salaam tu, wa mikoani ni wachache sana ambao wanafanikiwa kupata mikopo hiyo. Hivyo ni vyema Serikali ikasimamia mabenki waweze kukopesha wafanyakazi waliopo mikoani na wilayani ili waweze kujenga sehemu za kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Shirika la Nyumba ya Taifa lijielekeze kujenga nyumba wilayani na mikoani ambako mahitaji ya makazi kwa ajili ya wafanyakazi ni makubwa sana. Shirika lijielekeze huko badala ya kuendelea kujenga nyumba Dar es Salaam na miji mikuu ya majiji na manispaa pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, nashauri Wizara iondoe wafanyakazi wasio waadilifu wanaotoa hati mbili katika kiwanja kimoja; wanaopima maeneo ya wazi na kubadilisha matumizi bila utaratibu; wanaodai rushwa ili kuwapa huduma wananchi ya kupatiwa hati ya viwanja vyao kwa mkoani na wilayani. Pia kupata hati ya kiwanja ni gharama kubwa sana na inachukua muda mrefu sana, naomba nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, maeneo yanayochukuliwa na Halmashauri wananchi walipwe kutokana na thamani ya ardhi kwa wakati huo badala ya kuangalia mazao pekee yaliyoko kwenye kiwanja hicho.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba na kuileta hapa Bungeni. Kwa dhati nampongeza Waziri kwa mipango mizuri, utendaji mzuri na mikakati mizuri ya kuhakikisha ardhi ya nchi hii inatumika vizuri na kuwepo kwa mpango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo tabia ya wananchi kuanzisha miji midogo midogo kiholela pembezoni mwa barabara kuu kila kona. Ukipita barabara kuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kuna miji midogo mingi isiyokuwa na ramani yoyote. Naomba Waziri aeleze Bunge hili ni mikakati gani inapangwa kudhibiti uanzishaji miji kiholela halafu wanadai huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kaliua, Kata ya Ushokola wananchi walichukuliwa mashamba yao ya asili kwa lengo la kupimwa viwanja kwa ajili ya makazi na huduma nyingine tangu mwaka 2000 mpaka leo hawajalipwa haki zao. Mashamba hayo yamepimwa viwanja na watu wanauziwa lakini wamiliki hawaambiwi hatma ya haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 watendaji wa *TANROARDS* waliweka mawe ya alama za barabara kwenye viwanja na miji ya watu. Mpaka leo hakuna lolote linaloendelea wala hawaambiwi lolote kuhusiana na mawe hayo yaliyowekwa. Maeneo yaliyowekwa mawe ni Kata ya Ushokola na Zugimlole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya ardhi inasababishwa na watendaji wabovu, wala rushwa katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya na Manispaa. Maafisa Ardhi ndiyo chanzo cha matatizo kwani ndiyo wanauza viwanja mara mbili mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro unaongoza kwa migogoro ya ardhi. Afisa Ardhi Mteule pale Manispaa ya Morogoro ni chanzo cha matatizo kwa muda mrefu yupo pale na hachukuliwi hatua yoyote. Kwa nini Serikali inashindwa kuchukua hatua za nidhamu kwa watu kama hawa na kuwaacha kuendelea kuwatesa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi kwa ngazi ya Kata na Wilaya ni muhimu sana kusaidia kutatua migogoro ya ardhi kwa gazi za Wilaya. Serikali ihakikishe Mabaraza ya Ardhi yanaundwa katika wilaya zote hapa nchini. Aidha, Wajumbe wa Mabaraza haya wapewe posho yenye tija ili wafanye kazi zao kwa ufanisi na waache utaratibu wa sasa wa kudai fedha kwa wale wenye matatizo ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya migogoro ya wafugaji na wakulima itakwisha kwa Serikali kuhakikisha kwamba makundi haya yanatengewa maeneo ya mifugo na maeneo ya kilimo. Maeneo hayo yakishatengwa yaheshimiwe na kulindwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uwekezaji inaeleza wazi kuwa wawekezaji wote wanaofika nchini na kuhitaji ardhi kwa lengo la kuwekeza watapata ardhi kwa kufika Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* lakini wapo wanaokwenda moja kwa moja vijijini wanawapa viongozi wa vijiji fedha, wanawapa ardhi ya wananchi tena bila kutumia mkutano na wananchi. Serikali itoe mwongozo wa maandishi kwa ngazi za vijiji, kata na wilaya kuhakikisha sheria zinafuatwa ili kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wananchi wake wanapata makazi na nyumba bora ni vyema sasa Serikalii ikaondoa *VAT* kwenye vifaa vya ujenzi kwa Shirika la *NHC*. Pia Serikali ipeleke miundombinu ili kupunguza gharama za nyumba ili wanyonge au wananchi wa kawaida waweze kuzimudu/kuzinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Serikali inapoona wananchi/mwananchi anajenga nyumba eneo ambalo siyo sahihi mara moja asimamishwe na sio kusubiri akamilishe ndiyo abomolewe. Suala la kubomoa linaathiri sana familia, watoto na kusababisha mzigo mkubwa wa mawazo na watu kupoteza maisha.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nijielekeze moja kwa moja kwenye migogoro mbalimbali iliyopo katika Jimbo langu la Mikumi ambapo pamoja na mimi mwenyewe kuileta kwenye Ofisi ya Waziri wa Ardhi mkono kwa mkono lakini cha kusikitisha ni kuwa sio tu kwamba haijaorodheshwa kwenye kitabu cha Waziri alicholeta na kukigawa kwa Wabunge, lakini pia migogoro hiyo haijatajwa kabisa mahali popote.

Naomba Mheshimiwa Waziri akija kwenye majumuisho anipe majibu ni lini na ni nini hatma ya migogoro hii ya ardhi na mashamba pori yafuatayo ambayo yapo kwenye Jimbo la Mikumi na kusababisha Watanzania wenzetu wazalendo kukosa ardhi na nyingi kupewa wanaoitwa wawekezaji ambao wameyafanya mashamba pori na mengine kuyabadilisha matumizi.

(i) Kata ya Mikumi - mgogoro kati ya wananchi wa Kitongoji cha Vikweme na JWTZ na wananchi wa Kikwalaza na Hifadhi.

(ii) Kata ya Ruhembe – mgogoro wa wananchi wa Kitete Msindazi na Hifadhi; wananchi wa Ruhembe na Hifadhi; wananchi wa Kielezo na Hifadhi na wananchi wa kijiji cha Kidogobasi na wavamizi wa ekari 98.

(iii) Kata ya Kilangali - mgogoro wa muda mrefu kati ya Kijiji cha Kilangali na Kijiji cha Tindiga; mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Mbamba na Kijiji cha Kiduhi ni wa muda mrefu sana; mgogoro wa kijiji cha Kilangali na Shamba la Mbegu la ASSA, huu nao ni wa muda mrefu sana na mgogoro wa wakulima na wafugaji kwenye Kata nzima ya Kilangali.

(iv) Kata ya Uleling'ombe - kuna mgogoro mkubwa sana kati ya wananchi wa Uleling'ombe na Msitu wa Ukwiva ambapo eneo hili lilihamishwa mpaka mwaka 1972 na wananchi wanaomba warudishiwe mpaka wa zamami (awali) wa mwaka 1957 ili wapate maeneo ya kulima na kujiletea maendeleo.

(v) Kata ya Ulaya - mgogoro wa ardhi kati ya Basso Masumin na Serikali ya Kijiji cha Ng'ole; mgogoro wa ardhi kati ya wafugaji na wakulima wa Kijiji cha Mbuyuni; mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Ng'ole na Mbamba; mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Ng'ole na Ulaya Kibaoni, mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Ng'ole na Mhenda na mgogoro wa mpaka kati ya Kijiji cha Ng'ole na Nyalanda.

(vi) Mgogoro mkubwa wa shimo la mchanga kati ya Kata ya Ruaha na Kata ya Ruhembe (Kijiji cha Kitete).

(vii) Mgogoro wa ardhi kati ya Kijiji cha Kitundueta (Mhenda) na Kijiji cha Ihombwe kilichopo Mikumi.

(viii) Kata ya Kidodi - mgogoro wa mipaka kati ya Kijiji cha Lumango na hifadhi.

(ix) Kata ya Tindiga - mgogoro mkubwa sana na unaopoteza maisha ya Watanzania wengi sana kati ya wakulima na wafugaji na umedumu kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda Mheshimwa Waziri atuambie ni lini mashamba makubwa yaliyotelekezwa na wanaoitwa wawekezaji yatarudishwa kwa wananchi. Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilileta orodha ya mashamba pori 38 kwenye ofisi ya Waziri wa Ardhi bila mafanikio. Baadhi ya mashamba hayo ni:-

(i) Kata ya Kilangali - shamba Na.120 la Kivungu.

(ii) Kata ya Kisanga - shamba la *SAS* (Kisanga).

(iii) Kata ya Masanze - shamba la Miyombo; shamba la Dodoma Isanga na shamba la Changarawe.

(iv) Kata ya Ulaya - shamba la Ulaya.
(v) Kata ya Tindiga - shamba la Sumagro.

(vi) Kata ya Ulaya - shamba la Nyaranda

(vii) Shamba la Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu kilicholetwa na Mheshimiwa Waziri hakina takwimu shahihi ukilinganisha na hali za mashamba pori hayo yaliyopo Jimboni Mikumi. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri aje mwenyewe Jimboni Mikumi ili ashuhudie mapori makubwa yasiyoendelezwa wala kulimwa kama ambavyo amepewa taarifa na kusababisha wananchi wengi kukosa sehemu za kujiletea maendeleo na kuleta tija na maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza sana naomba Mheshimiwa Waziri anipe ahadi ya kwenda pamoja na mimi Jimboni Mikumi ili akajionee mwenyewe. Ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazochukua katika kusimamia ardhi ya nchi hii pamoja na dhamira ya dhati katika kutatua migogoro mbalimbali ya ardhi nchini kwetu. Nimepitia hotuba hii na kuona dhamira ya Wizara hii na ilivyojipanga kuona namna gani ambavyo Serikali yetu inasimamia ardhi yetu kwa kuithaminisha kwa taratibu na sheria zilizopo, hili ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia juu ya migogoro ya ardhi. Suala hili limekuwa likichukua muda mwingi wa wananchi wa kufanya shughuli za kiuchumi badala yake wanakuwa wakitumia kutatua migogoro ya ardhi. Mfano mzuri ni mgororo wa ardhi wa mpaka baina ya Wilaya ya Kilindi na Kiteto, mgogoro huu umechukua muda mrefu sana. Naomba kauli ya

Mheshimiwa Waziri hivi ni lini mgogoro huu utakwisha. Naamini mgogoro huu umeasisiwa na watumishi wa Halmashauri wasio waaminifu walioshirikiana na baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kiteto. Ili wananchi waone Serikali yao inawajali muda umefika sasa kupata suluhu ya kudumu ya mgogoro huu. Nashauri Serikali iwachukulie hatua watumishi wote waliobadili ramani ya mipaka ya Wilaya hizi mbili kwani awali mgogoro huu haukuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kuna migogoro ya wafugaji na wakulima, hii pia imekuwa ni migogoro ya muda mrefu. Wafugaji wamekuwa wakigombana na wakulima mara kwa mara kwa wafugaji kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na wakulima kulima maeneo ya wafugaji. Nashauri maeneo haya yapimwe na wafugaji wawe na maeneo yao na wakulima wawe na maeneo yao ili kupunguza migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uwepo utaratibu wa kuwa na maeneo ya kufuga na kunyweshea ili wafugaji wapate malisho ya uhakika kwani imeonekana hili ndilo tatizo kubwa kwa sababu wafugaji wamekuwa wakihamahama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kutafuta malisho ya mifugo yao. Vilevile wafugaji wasihame na mifugo yao kutoka Wilaya moja kwenda nyingine bila kuwa na kibali maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la watumishi hasa wale wanaopima maeneo ya ardhi. Nashauri watumishi hawa wasikae kwenye vituo vyao vya kazi kwa muda mrefu. Mfano katika Kata ya Newiro watumishi wa Halmashauri wameuza kwa wafanyabiashara maeneo mengi ya kata hii, leo hii hakuna hata eneo la wazi, maeneo yote yameuzwa. Wasiwasi wangu vizazi vijavyo vitakosa mashamba ya kulima. Mashamba haya yamepimwa na Wizara kutoa hati. Nitaleta hati hizo zenye maeneo makubwa ambayo hayakufuata utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba Wizara hii ifute hati ya shamba la *Tanzania Leaf Tobacco Company Ltd.*, lenye ukubwa wa hekari 2,133 lililopo Kata ya Kwadibona. Shamba hili limetelekezwa kwa muda mrefu sana, takribani miaka 20 bila kuendelezwa. Nashauri hati hii ifutwe ili eneo hili litengwe kwa ajili ya wawekezaji. Barua ya kufuta hati hii imekwishafika Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kujibu kilio cha muda mrefu sana cha Baraza la Ardhi. Kwa niaba ya wananchi wa Kilindi tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kitongoji cha Mchangaji au kwa jina jingine Ishinizya Kijiji cha Senga, Kata ya Kamsamba Wilaya ya Momba Mkoani Songwe, kuna tatizo kubwa sana la mpaka kati ya Mkoa wa Rukwa (Wilaya ya Sumbawanga Vijijini-Kwela) na Wilaya ya Momba maana kijiji hicho cha Mchangani/Ishinizya kila upande unadai ni wake kwa sababu za mipaka. Naomba Wizara yako ikalitatue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kukosa mamlaka ya moja kwa moja kuyawajibisha Mabaraza ya Ardhi imekuwa kero na kufanya wananchi kudhulumiwa haki zao na Mabaraza haya kwa sababu ya rushwa na uonevu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kupitia Wizara hii iangalie upya sheria iliyounda Mabaraza haya ikiwemo na namna ya kuyawajibisha ili wanaojiona miungu watu wanaoweza kufanya chochote badala ya kupunguza migogoro badala yake wameongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi katika kitabu sijaona Ukerewe kama sehemu inayokabiliwa na migogoro ya ardhi, hivyo naomba Wizara itambue kuwa Ukerewe kuna migogoro kadhaa ya ardhi ikijumuisha ifuatayo:-

Mpaka wa kijiji cha Nampisi na majirani zake, kijiji cha Muriti *vs* kijiji cha Kitangaza, mipaka katika vijiji vya Buzegwe *vs* Murutanga, kijiji cha Bulamba *Vs* Musozi, kijiji cha Bukindo *vs* Kagunguli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ya maeneo yaliyotwaliwa ya vijiji vya Bugegwe, Kakerege, Nyamagana, Selema, Kasulu - Nakoza itolewe.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na umuhimu wa Wizara ya Ardhi napenda kushauri mambo yafuatayo ili kuepukana na migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara katika Mkoa wa Rukwa na nchi nzima kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi yaboreshwe kulingana na utendaji wanapokuwa katika Mabaraza ya Ardhi. Kutokuwa na elimu ya kutosha kumepelekea kupata migogoro mingi katika Halmashauri zetu. Hati za kimila, mara nyingi zimekuwa hazitambuliki kwa baadhi ya watendaji katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Manispaa ya Sumbawanga iliyopo katika Mkoa wa Rukwa na Wilaya zake, kata na vijiji pamoja na mitaa na vitongoji vyake. Serikali ina mkakati gani wa kuwapa semina watu hawa ili kuondoa migogoro, kuwawezesha Maafisa Ardhi, kwa kuwapa vitendea kazi. Maafisa Ardhi hawa wamepelekea migogoro mikubwa sana katika Halmashauri zetu kwa kutomaliza mogogoro kwa wakati na mahali pengine kutokea migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kati ya wawekezaji na wananchi, kulingana na migogoro hii kutokea kila eneo katika nchi yetu, nashauri Serikali kutafuta njia sahihi ya kumaliza migogoro hii ya wawekezaji na wananchi kwa kuweka njia shirikishi kuanzia ngazi ya chini ili kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro kwa wananchi wa Isesa na mwekezaji, huu ni mgogoro wa muda mrefu uliopo katika Manisapaa ya Sumbawanga Mjini na Vijijini, suala hili limechukua muda mrefu hata kwenye kitabu cha Waziri mgogoro huu haupo, naomba Wizara ichukue hatua haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia kutokuwa wazi, kutokuwalipa wananchi fidia kwa muda muafaka inapelekea migogoro mingi katika Halmashauri zetu kutokana na taarifa tufauti na kupelekea migogoro isiyo ya lazima, nashauri Serikali kutoa fidia kwa wananchi na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kutoa hati kuchukua muda mrefu, kutokana na hali hii kushamiri hasa katika Mkoa wa Rukwa, Manispaa ya Sumbawanga na ili kuondoa tatizo hili Serikali imegundua tatizo hili, imegundua ni nini linalochelewesha? Pia migogoro kati ya wakulima na wafugaji nashauri Serikali kupima maeneo nchi nzima ili kuepukana na tatizo la migogoro inayoendelea na kupelekea vifo mbalimbali vinavyotokana na migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya ardhi katika Manispaa ya Sumbawanga kulingana na suala hili kuwa na hali ya kutokuwa na usimamizi mzuri wenye uwazi ili kuondoa migogoro isiyokuwa na tija. Suala la ushirikishwaji ngazi za mitaa, hali hii ya kutokushirikishwa hasa kupewa ramani na kuyajua maeneo ya wazi ili kuondoa migogoro inayoweza kujitokeza bila sababu.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni dhahiri kwamba kipimo cha mtu yeyote kinapimwa kutokana na makazi yake anayoishi na hatopimwa kwa mlo wake kwani hii inakuwa ni siri yake mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usajili wa hati na nyaraka za kisheria; kumekuwepo na malalamiko makubwa ya kukatisha tamaa kuhusiana na urasimu katika Halmashauri zetu hususani katika Mji Mkuu kama vile Dar es

Salaam. Tatizo la njoo kesho, njoo kesho kutwa linakatisha tamaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria kwanza mtu atakwenda Halmashauri kufuatilia kiwanja chake anatumia zaidi ya saa sita linatafutwa faili halionekani, kwa siku ile anakosa kazi nyingine kutafuta riziki ya chakula. Siku nyingine akienda atapewa ahadi ya kuwa anatakiwa afike mwezi ujao, mwezi ukiisha ataambiwa kila kiwanja kimeongezeka ukubwa unatakiwa ulipe fedha ya ziada ili utengenezewe hati au sehemu ile iko katika shamba la mzungu! Mheshimiwa Waziri nina ushahidi naomba Serikali iwaangalie sana watendaji ambao wanataka kukwamisha juhudi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upangaji wa makazi ya vijiji. Mheshimiwa Waziri hili ni jambo zuri la mradi huu wa MKURABITA lakini bado jamii/wananchi hawajaelimishwa kuhusiana na jambo hili. Hivyo MKURABITA watoe elimu ya kutosha hasa kwa akina mama ambao bado wanatawaliwa na mila na desturi potofu zinazowagandamiza wanawake. Kwa mfano, katika makabila mengine wanawake hawawezi kuongea mbele ya wanaume na wala hawawezi kujiamulia kitu chochote wala kumiliki mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itilie mkazo MKURABITA watoe elimu stahiki kuhusiana na malengo yao. Hatimiliki ziwe na hadhi ya kuwafanya waweze kukopa katika mabenki kama zilivyo hati nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wafikiriwe kupunguziwa bei ya ardhi kulingana na vipato vyao, kwani wanawake ndiyo maskini wa mwisho, wanawake wana watoto na wao ndiyo walezi wa watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udalali wa Maafisa Ardhi hili ni tatizo, ukitaka kiwanja maeneo ya mji ukifuata utaratibu wa kisheria huwezi kupata kiwanja, utaandika barua ya maombi lakini kupata kiwanja haiwezekani ila ununue barua kutoka kwa Maafisa wa Ardhi ndiyo uweze kuendelea na utaratibu. Serikali iangalie suala hili ili kuweza kuwafanya Watanzania wawe na imani na Serikali yao. Naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza uteuzi wa Waziri na Naibu Waziri kwa Wizara hii na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, kwani ni watendaji wenye weledi mkubwa kwa kujituma kwao na kujitoa kwao katika kupatikana utatuzi wa mambo yanayowakera wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuendelea kujipanga na kuandaliwa sheria maalum ya kuwawezesha wawekezaji kutoa mchango wa maendeleo

ya huduma za jamii kwenye vijiji vinavyomzunguka hilo liwe mojawapo ya sharti maalum kwa mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinaongezeka ndani ya Wizara hii kwenye maeneo yetu ya vijiji, miji na majiji ni upungufu wa watumishi ukizingatia hadi sasa ni asilimia 24 tu kati ya mahitaji yanayohitajika kuanzia Halmashauri hadi Wizara. Ushauri kwa Serikali ni uwepo uthibitisho wa kuthubutu kuongeza ajira na matumizi ya vitendea kazi vya kisasa vinavyoendana na mtandao wa dunia. Angalau kwa asilimia 50 ya watumishi, wanaohitajika tupate ufanisi katika nyanja zote na tuepukane na migogoro iliyokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wamekuwa na migogoro ya wawekezaji na vijiji, panaposhindikana kulipwa kwa fidia ndani ya muda wa uthamini, ni vema Serikali kuona mwelekeo wa kuwapimia wawekezaji nje ya maeneo ya wananchi kwani wao wana uwezo wa kuweka huduma zote za jamii, popote watakapowekwa kuliko kuwachanganya wananchi na kuwazorotesha maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu kuliko yote na kuwezesha yote yaliyopangwa kutekelezwa ni kuhakikisha fedha zilizopangwa kutolewa kwa wakati na katika ukamilifu kama Bajeti iliyopangwa na kuidhinishwa na Bunge hasa shilingi 20,000,000,000 kwa miradi ya maendeleo, kwa nini tumekuwa na viporo vingi vya miradi ndani ya nchi yetu ambayo inawadhoofisha wananchi. Ingawa kiasi hicho hakitoshelezi kwa maendeleo ya jumla kwa Wizara hii. Naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kuchangia hotuba hii kwa kumshukuru Mungu aliyeniwezesha kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tumbatu, kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao, natambua imani kubwa waliyonayo kwangu na naahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, napenda kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kuonesha imani na uwezo mkubwa wa kuiongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, napenda kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Baraza lote la Mawaziri kwa kuonesha umahiri wa kuongoza katika Wizara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa migogoro ya ardhi nchini yanaongezeka siku hadi siku. Hii inasababishwa pamoja na mambo mengine, uhaba wa ardhi inayosababishwa na ongezeko la watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ongezeko la watu namshauri Mheshimiwa Waziri achukue hatua ya kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kuangalia kwa makini uingiaji wa wakimbizi ambao nao pia wanasababisha ongezeko la watu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia ya habari katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 27 (36) amezungumzia juu ya teknolojia hii, ni teknolojia inayohitaji ujuzi mkubwa. Ushauri wangu ni kwamba kazi hii pamoja na kupewa makandarasi, Wizara ichukue juhudi za makusudi kuwaelimisha wafanyakazi wazalendo ili kwa baadae kuepuka na hasara za kuwapa kazi makandarasi badala yake kazi hizo zifanywe na wafanyakazi wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipaka ya Kimataifa, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 34 (46) Waziri ameelekeza namna ya juhudi inayochukua juu suala hili la mipaka ya Kimataifa. Mheshimiwa Waziri ameeleza kukwama kwa upimaji wa mipaka kati ya Tanzania na Burundi. Namuomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni kiasi gani kazi hiyo imeathiri zoezi hili kutokana na hali aliyoieleza kuwa ni ya kisiasa.

Mheshimwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa binafsi nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti ya Wizara yake pamoja na hotuba yake nzuri iliyojaa mazuri na mambo ambayo yametoa kiu za wananchi. Pamoja na *style* yake ya kutoa mabegi yaliyojaa mambo yote yanayohusu Wabunge na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri sina budi kumshukuru kwa kunipatia Baraza la Ardhi katika Wilaya ya Lushoto ambalo lipo kwenye Jimbo langu kwani mchakato huu niliufuatilia wakati tupo kwenye Kamati yako ya Ardhi. Hivyo hujasita kuondoa kiu yangu na ya wananchi wa Lushoto kwa kiujumla na kuahidi kuja kufungua Baraza hilo mwezi wa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi, Mheshimiwa Waziri migogoro ya ardhi ipo katika nchi nzima lakini ndani ya Jimbo la Lushoto kuna migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima hasa maeneo ya Bwei, Kilole

na Mlola, yote haya yanasababishwa na eneo dogo lililopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mwekezaji wa kiwanda cha mbao kinachoitwa *Mombo Saw Mill*. Kiwanda hiki kilikufa takribani miaka 20 iliyopita, lakini Mheshimiwa Waziri eneo hili linapakana na shule ya sekondari ya *St. Mary's* - Mazinde Juu na shule hii ni ya *boarding* kwa ajili ya wasichana. Mheshimiwa Waziri eneo hili limekuwa ni kichochoro cha watu kuingia katika eneo la shule ukizingatia eneo hilo linapakana na shule hiyo na upande lilipo ndiyo mabweni ya wanafunzi. *Father* amemfuata mwenye eneo lakini hakuonesha ushirikiano kwa sababu mwenye eneo hili anashirikiana na watu wabaya ambao hawana nia nzuri ya shule hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninakuomba Mheshimiwa Waziri kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa, suala hili uliingilie kati, eneo hili liweze kurudi ili liungane na eneo la shule. Ninashauri hivyo kwa ajili ya kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza, sambamba na hilo eneo hili halijalipiwa kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ningeomba Mheshimiwa Waziri Mungu akikujalia kufika Lushoto kufungua Baraza la Ardhi, utembelee eneo hilo la Magamba na shule ya sekondari Mazinde Juu kwa ajili ya kupata maelezo ya kina kwenye uongozi wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Lushoto kuna muingiliano mkubwa wa watumishi wa ardhi, hii imepelekea ujenzi holela na urasimu wa kupata hati ni tatizo kubwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimtakie Mheshimiwa Waziri utumishi uliotukuka huku wananchi wa Lushoto wakiendelea kukuombea kwani wana imani kubwa sana na wewe.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha baadhi ya mambo muhimu ambayo yanatakiwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka katika Jimbo la Iramba Mashariki, Wilaya ya Mkalama, Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkalama imekuwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Hatuna Afisa Ardhi Mteule – yupo Afisa Ardhi lakini hajapata uteule, hivyo tunaomba ama tupatiwe Afisa Ardhi Mteule au aliyepo ateuliwe ili shughuli za upimaji ziweze kuanza.

(ii) Wilaya haina Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na tunaomba tupatiwe kwani wananchi wa Mkalama wanapata shida kufuata huduma hiyo Wilaya ya Iramba na kusababisha usumbufu mkubwa wa gharama na muda.

(iii) Migogoro ya mipaka kati ya Wilaya na Wilaya; Mkalama *vs* Mbulu, upo mgogoro wa mpaka katika Kata ya Mwangeza kijiji cha Iramoto na Kata ya Eshgesh na Mbulu.

(iv) Hali ya usalama ipo mashakani kwa sababu wananchi wa Eshgesh sasa wameamua kujenga shule ndani ya eneo la Wilaya ya Mkalama na watu wa Iramoto hawapo tayari kuona jambo hilo.

(v) Mgogoro wa ardhi Mkalama *vs* Hanang, jiwe la mpaka kati ya Wilaya hizi mbili limewekwa katikati ya kijiji cha Singa "B" Kata ya Hilbadau, jambo ambalo limezusha mgogoro mkubwa na manung'uniko kutoka kwa wananchi wa Wilaya ya Mkalama.

(vi) Mkalama *vs* Singida Vijijini katika eneo la Kata ya Kihonda wananchi wa Singida Vijijini wameamua kujenga shule ndani ya Wilaya ya Mkalama hivyo kuhamisha mpaka bila idhini ya mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna migogoro ya ndani ya Wilaya, baadhi ya migogoro hiyo inayohitaji Wizara iingilie ni hii ifuatayo:-

(i) Shamba la Mifugo la Makomoti, mipaka ya shamba hili inadaiwa kupanuliwa/kuongezwa bila idhini ya vijiji husika na baadhi ya wananchi wamejenga ndani ya mipaka mipya na wanalima, hivyo kuanzisha mgogoro mkubwa, vijiji husika ni, Ishenga, Kihonda, Kinyangiri. Tunashauri Wizara iingilie na wataalam wa Wilayani wasihusike kwani wanadaiwa kuwa na maslahi binafsi na eneo hilo.

(ii) Kijiji cha Iramoto kilichopo Kata ya Mwangeza yupo mwekezaji kwa jina la Mr. Afrika ambaye anapewa ekari 700 ambazo ndani yake kuna Kaya 80 hivyo wananchi wanalalamika.

(iii) Kijiji cha Msiu, Kata ya Mwanga yupo mwekezaji anayedaiwa kuwa na haki ya kupewa ekari 200 lakini amehodhi ekari 500 na mahakama imeshindwa kwa makusudi kutoa hati ya mwekezaji huyu kuja kupewa ekari 200 anazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini naishauri Serikali bajeti inayotengwa itolewe yote na kwa wakati hasa ikizingatiwa Wizara hii inakabiliana na changamoto nyingi zinazohusiana na migogoro ya ardhi na maendeleo yanayohusiana na upimaji na uboreshaji wa mipango Miji na Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu ikamilishe haraka mchakato wa ununuzi wa vifaa vitakavyotumika kwenye mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za ardhi yaani *Intergrated Land Information Management System*, kutofanya haraka kunazorotesha ufanisi katika utawala wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya kuna mlundikano wa kesi nyingi kutokana na kushindwa kuhimili, kushughulikia zaidi ya Wilaya nne. Kwa mfano, Baraza la Ardhi la Korogwe linashughulikia Wilaya za Kilindi, Handeni, Lushoto, Korogwe Vijijini na Korogwe Mjini. Kwa kushika zaidi ya Majimbo na Wilaya tano kunasababisha uwepo wa rushwa jambo ambalo linazuia haki za wananchi.

Naishauri Serikali kuanzisha Mabaraza mengine kwa Wilaya ya Kilindi, Handeni, Korogwe Vijijini iwe na Korogwe Mjini na Lushoto iwe peke yake kulingana na ukubwa wa Wilaya hiyo yenye Majimbo makubwa matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uendelezaji Mji wa Kigamboni haujatekelezwa muda mrefu na hata haina bajeti ya maendeleo zaidi ya kuwa na bajeti ya mishahara na ulipaji wa pango la ofisi bila ya uwepo wa majukumu ya kufanya. Naishauri Serikali kuifunga ofisi hiyo na watumishi wapelekwe maeneo mengine yenye upungufu wa watumishi wa ardhi kwenye Miji na Majiji hadi Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuanza kuona umuhimu wa kutoa maeneo ya wawekezaji nje ya maeneo ya mashamba ya wananchi au makazi ya wananchi ili kuepuka ulipaji wa fidia. Wawekezaji wanaofaidika kupata maeneo kwenye Vijiji au Halmashauri wawe na mahusiano mazuri na wananchi katika maeneo yao kwa kuvisaidia vijiji huduma za jamii kwa maendeleo ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa *master plan* za vijiji, miji na majiji ni vema elimu ikatolewa kwa wananchi kabla ya ujenzi holela ambao unapoteza maana ya miji kwa kutokuwa na miundombinu ya barabara mifereji ya maji taka, maji ya mvua mabomba ya maji, viwanja vya michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze juhudi za *NHC* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ujenzi wa nyumba bora na kauli mbiu yao ya maisha ni nyumba. Naishauri Serikali shirika hili lianze kuona umuhimu wa kujenga nyumba

zenye bei nafuu ili kuwawezesha hata wale wenye kipato cha chini waweze kununua nyumba hizo. Aidha, Serikali ione namna itakavyoweza kuondoa *VAT* kwenye vifaa vya ujenzi wa nyumba hizi za *NHC* kwa lengo la kuwawezesha kufanikisha ujenzi wa nyumba zenye bei nafuu.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuisimamia Wizara hii, Wizara ambayo kwa muda imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi sana kiutendaji na kimfumo. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kuwa rasilimali ardhi ina umuhimu wa kipekee kwa uhai na maendeloe ya binadamu. Aidha, kwa uchumi wa Taifa letu ambalo wanancni walio wengi wanategemea sana kilimo, sekta muhimu katika kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Ni kutokana na ukweli huu rasilimali ardhi inabeba sifa ya kuwa haki ya kila Mtanzania na kwamba kumnyima Mtanzania yeyote haki ya kumiliki na kuitumia ni uvunjaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wimbi la kuwepo kwa migogoro ya mipaka na uvamizi wa ardhi katika maeneo ya vijiji limekuwa tatizo kubwa katika nchi yetu. Tatizo hili ni kikwazo kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Migogoro hii imeendelea kusababisha upotevu wa mali, vifo na kuendeleza uhasama kati ya jamii na jamii na hivyo kuwafanya wananchi kubaki maskini na kuishi maisha duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uwepo wa mashamba makubwa yasiyoendelezwa ni chanzo kingine kikubwa cha migogoro ya ardhi nchini. Kwa muda mrefu, mfumo wetu wa kufuta miliki ya ardhi isiyotumika ipasavyo kwa mujibu wa makusudio ya umiliki wa ardhi husika umetumika kutoa mwanya wa watu wachache kuhodhi ardhi bila kuitumia na kuwaacha wananchi wengi kutaabika kwa kukosa ardhi. Naipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa zinazofanyika sasa kuhakikisha mashamba yaliyotelekezwa yanafutiwa hati za umiliki na hatimaye kugawanywa kwa wananchi. Hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia vyema jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkinga ni miongoni mwa Wilaya zinazokabiliwa na migogoro ya umiliki wa ardhi na uwepo wa mashamba yaliyotelekezwa kwa muda mrefu. Kwa nyakati tofauti ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga na mimi binafsi tumewasilisha Wizara ya Ardhi, mapendekezo ya Wilaya kuhusu utatuzi wa migogoro hiyo. Wakati mapendekezo ya ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga yaliwasilishwa Wizara ya Ardhi mapema mwaka 2007, wakati huo Mkinga ikiwa bado ni sehemu ya Wilaya ya Muheza; Ofisi yangu iliwasilisha tena maombi hayo kupitia barua yenye Kumb.MB/MKN/Ardh01/2011 ya tarehe 17 Novemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi mara kwa mara nilikuwa nakumbushia jambo hili kwa michango kwenye hotuba za bajeti za Wizara, na barua. Pamoja na jitihadi hizi bado changamoto hizi hazijapatiwa ufumbuzi. Mheshimwia Waziri nilifarijika sana kupata barua yako iliyotaka Wabunge kuorodhesha migogoro ya ardhi katika Majimbo yetu. Hivyo basi, natumia fursa hii kuikumbushia Wizara juu ya maombi haya ambayo kimsingi yamechukua muda mrefu kupatiwa ufumbuzi:-

(i) Shamba la Kilulu - shamba hili ndipo sehemu ambayo Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga yamejengwa. Shamba hili kwa mara ya kwanza lilimilikishwa kwa Ndugu Van Brandis na Bibi Mary Van Brandis hadi 31/10/1959 ambapo umiliki ulihama kwenda kwa Ndugu Akberali Walli Jiwa. Mmliki huyu hakuendeleza shamba hili lenye ukubwa wa ekari 5,699.9 hadi umiliki wake ukafutwa mwaka 1972. Baada ya kufuta umiliki, Serikali ililipa fidia na shamba likawa chini ya Serikali.

Baadaye Wilaya ya Muheza ilipokea maombi ya kumilikishwa shamba hilo toka Kampuni ya *M/S Arusha Farms Ltd. (CHAVDA)*. Taratibu zote zilifanyika na alimilikishwa ekari 2,699.9 na ekari 3000 walipewa wananchi wa vijiji jirani vya Vuo, Mwachala na Purungu Kasera waliokuwa na shida ya ardhi. *M/S Arusha Farms Ltd* walipewa barua ya toleo *(leter of right of occupancy)* ya tarehe 10/05/1991 ambayo ilisajiliwa na Msajili wa Hati tarehe 13/05/1990 kwa *Land Office Number 125127.*

Mmiliki huyu aliomba mkopo kutoka *CRDB* kwa kuweka rehani barua ya toleo. Aidha, alishindwa kurejesha mkopo huo na *CRDB* waliuza shamba kwa *M/s Mbegu Technologies Ltd.* tarehe 27/03/2004 ambao walilipa mkopo huo, lakini pia hakuweza kuliendeleza shamba hilo. Ndugu Akberali Jiwa licha ya kunyang'anywa shamba hilo na kulipwa fidia aliwasilisha ombi lake la kurejeshewa umiliki wa shamba hilo. Ombi lake liliwasilishwa katika kikao cha Kamati ya kugawa ardhi tarehe 10/10/1996 na iliazimiwa liwasilishwe katika Kamati ya Ushauri ya Ardhi Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hiyo chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa iliridhia Ndugu Akberali Jiwa apewe shamba hili kwa vile *M/s Arusha Farm Ltd.* wameshindwa kuliendeleza. Halmashauri ya Muheza ilitoa barua ya toleo kwa miliki ya miaka 99 kuanzia tarehe 1/10/1998 kwa Akberali Jiwa kwa jina la Kampuni ya *Kilulu (2000) Ltd.* Baada ya tatizo hilo la *double allocation* kujitokeza, Halmashauri ya Muheza iliandika barua yenye Kumb Na. MUDF/3844/63 ya tarehe 2/4/2007 kwenda kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya kuomba kufuta miliki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Halmashauri hadi leo Halmashauri haijapata majibu yoyote licha ya ufuatiliaji uliofanywa wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi kwa sasa ni kwamba eneo hili lina michoro ya mipango miji minne, mitatu iliandaliwa na Katibu Tawala wa Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kabla ya kuanzishwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga na mchoro mwingine umeandaliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga. Aidha, eneo hili limepimwa jumla ya viwanja 400 kwa matumizi mbalimbali ikiwemo, taasisi, majengo ya Serikali, majengo ya umma, viwanja vya michezo, maeneno ya kuabudia, makazi biashara na maeneo ya wazi. Kwa mara nyingine tena naiomba Serikali ifute milki ya *Kilulu Plantation* kwa manufaa ya umma.

(ii) *Moa Estate* - shamba hili lina ukubwa wa ekari 15,739.60 na linamilikiwa na *Mkomazi Plantations Ltd.* ya S.L.P 2520 Dar es Salaam ambayo baadaye ilibadilisha jina kuwa *Mao Plangation and Aquaculture* ya S.L.P 364 Dar es Salaam, kwa hati Na. 2468, 9780 na 9781. Halmashauri ya Wilaya ilituma notisi ya kuwafutia hati miliki yao kwa kutelekeza shamba na kulipia kodi. Baada ya hapo Halmashauri ya Wilaya iliwasilisha barua ya mapendekezo kwa Kamishna wa Ardhi yenye Kumb. Na. MKG/LD/F/2/54 ya tarehe 28/07/2009. Taratibu za ufutaji hati miliki ziliendelea Wizarani lakini Halmashauri ilipokea barua ya mmiliki ikieleza kuwa jina la umiliki lilibadilika na kuwa *Moa Plantation and Aquaculture* wa S.L.P 364 Dar es Salaam na kwamba wanataka kuendeleza shamba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ilikwishawasilisha Wizarani barua ya mapendekezo ya kufuta hatimiliki, ililazimika kumwandikia Kamishna wa Ardhi barua yenye Kumb. Na. MKG/LD/F/2/56 ya tarehe 09/06/2001 kumweleza kupokea barua hiyo na kwamba shamba hilo lina vijiji vinne ambavyo vimeanzishwa na kusajiliwa Moa, Ndumbani, Mayomboni na Mahandakini. Aidha, vijiji hivyo tayari vina huduma za jamii kama shule, zahanati, barabara na kadhalika. Katika maeneo hayo hivyo aendelee na taratibu za ufutaji hatimiliki au kama atasitisha ufutaji basi wamiliki wakubali kumega maeneo yanayokaliwa na vijiji na kuendelezwa na wananchi. Kamishna wa Ardhi kwa barua Na. LD/70503/76 ya tarehe 23/11/2011 alisitisha ufutaji huo kwa masharti kwamba walipe kodi ya ardhi kuanzia mwaka 1996 hadi 2011/12 na kumega maeneo ambayo yenye vijiji tajwa. Hata hivyo, hawakutimiza masharti hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo, Halmashauri iliandika barua kwa Kamishna wa Ardhi yenye Kumb. Na. HW/MKG/LD/F/2/62 ya tarehe 27/07/2012 ili aendelee na taratibu za ufutaji. Kamishna wa Ardhi kupitia barua yenye Kumb. Na. LD/70503/76 ya tarehe 23/11/2011 alisitisha ufutaji huo kwa masharti kwamba walipe kodi ya ardhi kuanzia mwaka 1996 hadi 2011/2012 na

kumega maeneo ambayo yenye vijiji tajwa. Hata hivyo hawakutimiza masharti hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo, Halmashauri iliandika barua kwa Kamishna wa Ardhi yenye Kumb. Na. HW/MKG/LD/F/2/62 ya tarehe 27/07/2012 ili aendelee na taratibu za ufutaji. Kamishna wa Ardhi kupitia barua yake Kumb. Na. LD/70503 ya tarehe 15/01/2013 iliitaka Halmashauri kuwasilisha vielelezo jambo ambalo Halmashauri ilifanya. Aidha, barua ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi yenye Kumb. Na. LD/NZ/12931/18/DW ya tarehe 15/04/2013 kwenda kwa Kaimu Kamishna wa Ardhi nayo inahusika akishauri ufutaji wa hati hizo uendelee. Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya inasubiri uamuzi wa Kamishna wa Ardhi.

(iii) *Mwele Seed Farm* - shamba hili lina ukubwa wa hekta 954, mmiliki ni Wizara ya Kilimo. Wakati ambapo shamba hili lilikusudiwa kuwa shamba la kuzalisha mbegu, hali halisi ni kwamba kwa kipindi cha takribani miaka 15 sasa shamba hili limeshindwa kutumika kama ilivyokusudiwa na sehemu kubwa kubaki kuwa pori. Wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hili Mbababakofi, Maramba A, Maramba B na Lugongo ndiyo wamekuwa nguvu kazi ya kulifanyia usafi shamba hili pale wanaporuhusiwa kufungua mashamba mapya na kulima mazao ya muda mfupi kila msimu mpya wa kilimo unapowadia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 21/09/2007, Halmashauri ya Wilaya iliandika barua kwa Kamishna wa Ardhi yenye Kumb. Na. MUD/ASF/VOL.VI/35 ikipendekeza kumegwa kwa shamba hili na kugawiwa kwa wananchi wa vijiji jirani kutokana na uendelezaji wake kuwa mdogo sana na kodi kutolipwa. Hata hivyo, maombi haya hayakuwahi kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili linapakana na kijiji cha Mbambakofi chenye takribani kaya 500 zenye jumla ya wananchi wapatao 3,173. Mbambakofi ni kijiji pekee katika Wilaya ya Mkinga ambacho kimekosa hata eneo la kujenga huduma muhimu za kijamii kama shule ya msingi na zahanati. Aidha, shamba hili linapakana na Mji Mdogo wa Maramba ambao unakua kwa kasi kubwa, ukiwa na takribani watu 30,000 na kuzungukwa na mashamba ya Maramba JKT hekta 2445, *Lugongo Estate* hekta 6040, *Kauzeni Estate* hekta 189.66, *Mtapwa Estate* hekta 476.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kutelekezwa kwa shamba hili imezidi kuwa mbaya sana sasa kuliko ilivyokuwa mwaka 2007, wakati Halmashauri ya Wilaya ilipoomba mara ya kwanza kumegwa kwa shamba hili. Kwa sasa hali imekuwa mbaya kiasi kwamba hata majengo mengi yaliyokuwepo yameanguka na machache yaliyosalia yamekuwa magofu, mashine na mitambo yoyote ya kilimo iliyokuwepo shambani hapo imeharibika na

michache iliyosalia imehamishiwa Morogoro. Kwa sasa shamba limebaki na wafanyakazi wasiozidi watano kutoka waliokuwepo miaka ya 1990.

(iv) Shamba la Maramba JKT - ukubwa wake ni hekta 2,445 na linamilikiwa na Jeshi. Eneo kubwa halitumiki na halilipiwi kodi. Barua iliyoandikwa kuhusu *Mwele Seed Farm* iliunganishwa pia mapendekezo ya kumega shamba hili ili wananchi wa Mji Mdogo wa Maramba waweze kupata eneo la kujenga makazi yao.

(v) Shamba la Segoma - msitu wa Segoma wenye ekari 2,311 upo ndani ya shamba la Sigi Segoma lenye ukubwa wa ekari 2829. Shamba hili lilimilikishwa kwa Shirika la Uchumi la Wilaya ya Muheza (SHUWIMU) kwa hati Na. 7675 ya tarehe 01/04/1990 ya miaka 33. Kutokana na kukosa mtaji na kuzorota kwa SHUWIMU, hati hii ilibadilishwa umiliki kuwa *Muheza District Council* kuanzia tarehe 16/02/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 SHUWIMU kwa kukosa mtaji na utaalam iliingia ubia na *M/s Sigi Agricultural Co. Ltd.,* na SHUWIMU ilipovunjwa shamba lilimilikiwa na *Muheza District Council* ambayo ilifuta ubia uliokuwepo na kuingia ubia na *SWIFTCOM* ya Tanga. Hii ilisababisha *M/s Sigi Agricultural Co. Ltd.* kufungua kesi namba 18 ya 1996 kupiga kupinga kufutwa kwa ubia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 hukumu ya kesi hii ilitolewa na Halmashauri ya Muheza kupewa ushindi. Mwaka 2007 Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ilianzishwa kwa kumegwa toka Muheza. Katika zoezi la kugawana mali, shamba hili liligawiwa kwa Halmashauri ya Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hukumu kutolewa, Halmashauri kwa ufadhili wa *Tanzania Forest Conservation Group (TFCG)* ilifanya ukaguzi wa uhalisia wa wakati huo na kutoa taarifa katika kikao kilichofanyika tarehe 08/10/2012 kikihusisha viongozi wa kijiji cha Songea, Kata, wataalam wa Halmashauri, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - Kanda ya Kaskazini na wataalamu wa Mkoa. Aidha, kikao kilitoka na mapendekezo kwa kuwa na kijiji cha Segoma kina tatizo kubwa la uhaba wa ardhi, ekari 518 za shamba zigawanywe kwa wananchi kwa shughuli za kilimo na makazi na ekari 2,311 zitengwe kuwa eneo la hifadhi ya msitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 15/12/2012 kikao cha Baraza la Madiwani kama wamiliki halali wa rasilimali hii kiliridhia mapendekezo haya na kuagiza ekari 518 zigawiwe kwa wananchi wa kijiji cha Segoma kwa shughuli za makazi na kilimo na ekari 231 zimilikishwe kwa kijiji cha Segoma kuwa msitu wa kijiji. Ili kutekeleza agizo la Baraza la Madiwani, Menejimenti iliwasiliana na Meneja wa Kanda wa Wakala wa Huduma za Misitu kwa makabidhiano. Hata hivyo Meneja wa Kanda wa Wakala wa Huduma za Misitu aliomba kuonana na

uongozi wa Halmashauri kwa majadiliano juu ya kijiji kumilikishwa misitu. Taarifa ya ombi hilo ilipofikishwa kwenye kikao cha Baraza cha tarehe 16-17/07/2014, Baraza liliagiza kuwa wataalam wa Ardhi na Misitu wa Wilaya watekeleze Azimio la Baraza la tarehe 05/12/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Menejimenti kutekeleza agizo hilo, tarehe 28/11/2014 kwa mshangao mkubwa Halmashauri ilipokea barua kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ikiamuru kusitishwa kugawa ardhi kwa wananchi kwa ajili ya kilimo na makazi na hali kadhalika kukabidhi msitu kuwa wa kijiji cha Segoma. Jambo hili limeleta taharuki kubwa kwa wananchi kiasi kwamba walikuja Dodoma wakati wa vikao vya bajeti kuwasilisha malalamiko yao. Aidha, wakati wa kuhitimisha mjadala wa bajeti nililazimika kuomba ufafanuzi kuhusiana na jambo hili na Naibu Waziri alikiri kuwa wananchi wa Segoma wanayo haki ya kupatiwa ardhi tajwa na kwamba atatembelea Mkinga ili kulipatia ufumbuzi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiendelea kusubiri utekelezwaji wa ahadi ya Naibu Waziri kutembelea Mkinga kuja kuupatia ufumbuzi mgogoro huu, Halmashauri ilipokea barua toka kwa Katibu Tawala wa Mkoa yenye Kumb. Na. BF 174/314/02/35 ya tarehe 02/12/2015 ikiagiza eneo la ekari 518 likabidhiwe rasmi kwa kijiji na eneo la msitu lenye ukubwa wa ekari 2311 kuwa chini ya usimamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu hadi hapo uamuzi mwingine utakapotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi haya ya kuinyang'anya Halmashauri ya Mkinga rasilimali yake siyo tu kwa nia ya uonevu mkubwa bali pia yanakinzana na Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 ambayo inabainisha wazi kuwa jamii inaweza kulinda, kuhifadhi, kusimamia na kutumia kiuendelevu misitu katika ardhi ya kijiji ili kukidhi mahitaji yao ya kimaendeleo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikimbukwe kuwa zaidi ya hekta milioni mbili za misitu hapa nchini zinasimamiwa na Serikali za vijiji zaidi ya 1000. Hivyo kijiji cha Segoma kukabidhiwa kusimamia msitu wao wa asili haitakuwa mara ya kwanza. Tungependa kuona busara iliyotumika mwaka 2015 kuruhusu Kata ya Enguserosambu katika Wilaya ya Ngorogoro kusimamia msitu wa Longido II ikitumika hata kwa msitu wa Segoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na ukweli kuwa wananchi hawa ndiyo wameutunza msitu wa Segoma na kuwajibika kuhakikisha msitu unabaki salama pasipo kuombwa wala kukukabidhiwa na Serikali. Inasikitisha kuona leo wananchi hawa wakiporwa rasilimali hii kwa mabavu, kejeli na udhalilishwaji kuwa wao ni wavamizi. Halmashauri ya Mkinga na wanakijiji wa Segoma wanataka kunufaika na umiliki wa rasilimali yao kupitia mapato yatokananyo na

mavuno ya msitu huu ili kuboresha huduma za kijamii na kuleta maendeleo ya kijiji.

(vi) *Kwamtili Estate* - shamba hili lina ukubwa wa hekta 1,150 na lina milikiwa na *Kwamtili Estate Ltd.* yenye *certificate of Incorporation No*. 2649 iliyosajiliwa tarehe 09/01/1961 ikiwa na wanahisa wafuatao:

| S/N | JINA LA MWENYE HISA | ANAPOISHI | MAELEKEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Dennis Martin Fielder | 4 Market Square Tenbury, Wells Worcestershine – UK | Amerudi Uingereza |
| 2 | National Agriculture & Food Corporation (NAFCO) | Box 903 DSM | Shirika limefutwa |
| 3 | Handrik Tjails Scheen | C1/30 Algami nes Bank, Amsterdam, Netherland | Amefariki |
| 4 | Louis Van Wagenburg | Layscian Ag Vaghel, Holland | Amefariki |
| 5 | Schoonmarkers Bart Venderburg | De Conqabsen, 163 Schlkher, Holland | Amefariki |
| 6 | Tracey Elan Allison | The Willos Terrigton, Herefordenshire, UK | Amefariki |
| 7 | Juvent Magoggo | 42 Block S. Mikanjuni Box 5855 Tanga | Anaishi Tanga |
| 8 | W.J. Tame Ltd | Box 118 Tanga | Amefariki |
| 9 | Jacobus Cornelius Josephus Moris | Logtanburg Vaghel, Holland | Amefariki |

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili lililopo katika eneo la Kwamtili, Kata ya Bosha, Wilaya ya Mkinga lilitumika kwa kilimo cha kibiashara cha zao Kakau. Hata hivyo kwa muda wa miaka takribani 26 saa shughuli za kilimo cha zao la Kakau zimesimama baada ya aliyokuwa Menejiment ya Kampuni chini ya Ndugu Dennis Fielder kutelekeza shamba. Aidha, baada ya shamba kutelekezwa, mmoja wa wanahisa Ndugu Juvent Magoggo amekuwa akifanya shughuli ndogo ndogo ikiwemo kuvuna miti ndani ya shamba hili kwa lengo la kupata fedha za kufanyia uzalishaji mdogo mdogo; na hali kadhalika kuruhusu wananchi wanaozunguka shamba hilo kulima mazao ambayo siyo ya kudumu. Hata hivyo, kwa sasa ndugu Magoggo ameshindwa kuendelea kufanya shughuli hizo baada ya kunyimwa vibali vya kuvuna miti na kusafirisha magogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa ombwe la umiliki wa shamba hili yamezuka makundi ya watu yanayodai kuwa na haki ya kumiliki shamba hili na hivyo kuwakodisha wananchi wanaozunguka shamba hili maeneo ya kulima kwa kuwalipisha sehemu ya mavuno yatokanayo na matumizi ya ardhi hiyo. Aidha, kumekuwa na wimbi la kujitokeza raia wa kigeni kwa kutumia kivuli cha aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa shamba na kulitekeleza Ndugu Dennis Fielder kufanya uharibifu wa mali za kampuni,

ikiwemo upasuaji wa mbao na kuanzisha michakato ya kujimilikisha ardhi hii. Katika hili, wananchi wanainyooshea kidole ofisi ya Wakala wa Hifadhi ya Misitu - Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kwamtili na Kata ya Bosha kwa ujumla wamebaki katika umaskini wa kutupa baada ya shughuli za kilimo cha Kakau katika shamba la Kwamtili ambacho kilitoa ajira kwao kusitishwa. Nusura kwa wananchi hawa ni kupatiwa maeneo katika shamba hili ili kwa kutumia utaratibu wa wakulima wadogo waweze kufanya shughuli ya kilimo na hivyo kujikimu kimaisha. Naiomba Serikali ifanye uamuzi wa kufuta hati ya shamba la Kwamtili na kisha kuligawa kwa wananchi kwa ajili ya kilimo, na sehemu nyingine kutengwa kuwa hifadhi ya msitu wa kijiji.

(vii) *Mjesani Sisal Estate* - shamba hili lenye hati Na. 48108 na ukubwa wa ekari 22,725 lilitelekezwa kwa muda mrefu na hali iliyosababisha ardhi kumegwa na kuanzishwa vijiji vinne ndani ya shamba ambalo ni Kwangena, Mchangani, Bomba Mavengero na Mnyenzani. Aidha, Kampuni ya *Mohamed Ltd.* ya S.L.P 20600 Dar es Salaam imejitokeza na kuanza kuendeleza baadhi ya maeneo ya shamba hili. Hali hii imeleta changamoto kubwa hasa ikizingatiwa kuwa tayari vijiji vilivyomo ndani ya shamba hili vimepatiwa usajili na TAMISEMI. Mfano kijiji cha Kwangena chenye ukubwa wa hekta 300 kimepewa hati ya kuandikishwa kwa kijiji Na. TA/KIJ/603 ya tarehe 03/01/1997, aidha, upimaji wa vijiji ulifanyika na ramani za upimaji kupata vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mkanganyiko huu wa umiliki wa ardhi katika vijiji tajwa, wananchi wa vijiji husika wamekuwa na kilio cha muda mrefu kuiomba Serikali iingilie kati ili kuondoa utata wa umilikishwaji wa maeneo ya vijiji vyao. Mfano, Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Kwangena ulikaa na kuomba kupewa ardhi kwa mujibu wa ramani ya kijiji aliyoidhinishwa. Baraza la Madiwani iliyobariki ombi hilo na Halmashauri kupitia barua yenye Kumb. Na. HW/MKG/D.35/138/5 ya tarehe 17/072012 iliwasilisha ombi hilo kwa Kamishina wa Ardhi, mnamo mwaka 2015 Wizara ilituma wataalam wake kuja kufufua mipaka ya shamba na kwa mshangao mkubwa wananchi wa Kwangena wakamegewa ekari 216 tu. Aidha, ndani ya kipindi kifupi sana ramani ya upimaji ikisajiliwa kwa namba 82741, na wakaandaliwa hati nyingine yenye LONO. 560486 na hati ikasajiliwa tarehe 26/11/2015. Tunaomba Serikali iangalie upya suala hili ili wananchi wa vijiji vya Kwangena, Mchangani, Bamba, Mavengero na Mnyenzani waweze kupatiwa ardhi itakayowawezesha kuishi kwa fahari katika nchi yao huku wakiweza kukidhi mahitaji yao ya kimaisha.

(viii) Mgogoro wa Kijiji cha Mkota na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi - wananchi wa Kitongoji cha Kimuuni katika Kijiji cha Mkota Kata ya Mwakijembe wamekuwa wakiishi katika eneo hilo tangu kabla ya uhuru. Kitongoji hiki kina takribani kaya 170 na wakazi wapato 530. Wananchi hawa wa muda wote

wamekuwa msaada mkubwa kwa ulinzi na rasilimali za nchi yetu hasa ikizingatiwa kuwa eneo hili linapakana na nchi jirani ya Kenya. Wananchi hawa wanalalamika kuwa eneo lao limechukuliwa na hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Pori Tengefu la Umba na kwamba sasa wanatakiwa kuondoka kwenye eneo hilo licha ya kufanya uwekezaji mkubwa kwa kutumia nguvu zao kuchimba mabwawa makubwa ya kunywesha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu nimeufikisha Serikalini na nimelizungumzia jambo hili mara nyingi sana katika Bunge la Kumi, lakini hadi sasa halijapatiwa ufumbuzi. Mheshimiwa Anna Tibaijuka wakati akiwa Waziri wa Ardhi akiongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, alifanya ziara katika Wilaya ya Mkinga na kufanya mkutano wa hadhara katika kijiji hiki. Katika mkutano ule, Mheshimiwa Waziri aliwaahidi wananchi kuushughulikia mgogoro huu. Aidha, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mahmood Mgimwa akiandamana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa naye alifanya ziara katika eneo la mgogoro (Kimuni) na kufanya mkutano wa hadhara ambapo alipokea ombi la wananchi kwa eneo hili kupewa hadhi ya kuwa *Wildlife Management Area (WMA)* na kuahidi Wizara kuanzisha mchakato wa kulitanga eneo hili kuwa *WMA*. Tunaamini kuwa suluhisho la mgogoro huu ni Serikali kukamilisha mchakato huu ili wananchi waweze kuishi kwa amani.

(ix) *Manza Bay Sisal Estate* - ni mkusanyiko wa mashamba manne yenye ukubwa wa jumla ya ekari 2,217.6 shamba na. 273 hati na. 7047 LONO. 124814 ekari 461, shamba Na. 196 hati Na. 14275 LONO. 12621 ekari 498.6, shamba Na. 272 hati Na. 3576 LONO. 642 ekari 507 na shamba hati Na. 14322 ekari 764. Mmiliki wa mashamba haya ni *Mbegu Technologies Inc. Ltd.* wa S.L.P 173 Moshi. Mashamba haya yote yameingia katika eneo la Mji wa Kasea ambao ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga. Kwa muktadha huu naiomba Serikali ione umuhimu wa kufuta hati hizi ili eneo hili liweze kufanyiwa matumizi ya kuendeleza mji wa Kasera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na migogoro hiyo hapo juu, ipo migogoro mingine iliyoibuka kutokana na zoezi la upimaji wa vijiji mwaka 2007 lililohusisha wataalam wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na wataalam wa Halmashauri ya Mkinga. Kiini cha migogoro hii ni zoezi kufanyika bila kuhakikisha ushiriki wa viongozi wa pande zote za vijiji husika katika kubainisha mipaka, jambao ambalo limepelekea vijiji ambavyo havikuwa na uwakilishi kugomea kutambua mipaka iliyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti orodha ya vijiji vyenye migogoro hii ni kama ifuatavyo:-

(a) Kijiji cha Daluni Kibaoni na Kijiji cha Ng'ombeni;

(b) Kijiji cha Daluni Kibaoni, Kijiji cha Mgambo Shashui na Kijiji cha Movovo;

(c) Kijiji cha Mnyenzani na Kijiji cha Jirihini;
(d) Kijiji cha Magodi na Kijiji cha Mwanyumba;

(e) Kijiji cha Dima na Kijiji cha Mazola Kilifi;

(f) Kijiji cha Doda na Kijiji cha Magaoni;

(g) Kijiji cha Monga Vyeru na Kijiji cha Kichalikani;

(h) Kijiji cha Mwakijembe na Kijiji cha Mkota;

(i) Kijiji cha Msimbazi na Kijiji cha Dima; na

(j) Kijiji cha Bosha na Kijiji cha Churwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa sasa changamoto za muda mrefu za uwepo wa migogoro ya mipaka ya vijiji umiliki wa ardhi na uwepo wa mashamba yaliyotelekezwa kwa muda mrefu katika Wilaya ya Mkinga yatapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja ya bajeti hii atueleze nini kauli ya Serikali kuhusiana na changamoto hizi, na tunamuomba atoe kipaumbele cha kuitembelea Mkinga ili kuja kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchangia hoja iliyopo mezani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya ujenzi wa nyumba, mfano Shirika la Nyumba *(NHC)* nyumba zao ni gharama kubwa sana kuanzia shilingi milioni 50 mpaka milioni 270 na kuendelea. Nyumba hizi kimsingi hazimnufaishi Mtanzania wa kawaida mwenye kipato cha chini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inapunguza gharama hizi ambazo kimsingi zinatokana na Serikali kutokuchangia gharama za miundombinu kama barabara, maji na umeme, gharama ambazo sasa zinatolewa na *NHC* kupitia mikopo ya ujenzi wa nyumba hizi, hali inayosababisha gharama ya ujenzi kuwa kubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na miundombinu hii kumekuwa na suala la *VAT* ya asilimia 18 katika kununua nyumba hizi ambazo kimsingi *VAT* zimelipwa kwenye vifaa vya ujenzi. Ninaitaka Serikali itoe tamko kupitia Wizara hii ni lini itatoa *VAT* hizi kwa nyumba zote za Shirika la Nyumba ambalo ndilo mkombozi wa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo mikopo ya magari, ningeshauri Serikali itoe mikopo ya nyumba za *NHC* kwa watumishi ili waweze kukatwa fedha kiasi. Hii itaondoa hali ngumu za wastaafu wetu ambazo wanapata baada ya kustaafu katika utumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Ardhi imekuwa ikifanya kazi bila kuwa na bajeti. Tatizo la Tume hii inafanya kazi ya kuangalia eneo baada ya shughuli kubwa ya upimaji. Ningeshauri kama Tume hii itaendelea kuwepo ipewe bajeti ya kutosha na itoe ushauri kabla ya eneo kupimwa. Ninaitaka Serikali itoe majibu ya kina kuhusiana na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ninaitaka Serikali itoe tamko kuhusu wananchi wanaovamia vyanzo vya maji (waliopo ndani ya mita 60) ambazo wanatakiwa kuondoka. Mfano mzuri ni vyanzo vya maji vilivyopo Mkoa wa Arusha ambako kuna tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya maziko hasa ya mijini yamekuwa na changamoto kubwa sana. Ninamtaka Waziri anipe majibu kuwa Wizara yake imejipangaje kukabiliana na tatizo hili la maziko katika maeneo ya miji kama Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Kilimanjaro ambazo ardhi ni changamoto kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bomoa bomoa ninamtaka Waziri aniambie Serikali imejipangaje katika kulipa fidia kwa wananchi hawa ambao wanaendelea kubomolewa nyumba zao na fidia zinazotolewa haziendani na hali halisi ya gharama za ujenzi wa nyumba? Ni kwa namna gani wananchi hawa watafidiwa kulingana na hali halisi ya maisha ya leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ukurasa wa 31 – 32 amezungumzia jukumu la kuanzisha na kusimamia Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Wizara ya mwaka 2011/2012 Bunge lilipitisha matumizi ya kuanzisha Mabaraza matano ya Ardhi na nyumba ya Wilaya na Tunduru ikiwa ni mojawapo. Hadi sasa Halmashauri imetoa jengo

miongoni mwa majengo ya Idara ya Ujenzi na samani japo chache ili angalau Baraza lianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anapohitimisha michango mbalimbali ya Wabunge naomba mambo yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iajiri Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Tunduru kwa sababu kwa sasa mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Songea Mheshimiwa Norbet Ndimbo ndiye anayetembelea Baraza la Tunduru kila baada ya mwezi mmoja na mara nyingine baada ya miezi miwili. Hili halileti tija kwa wananchi wa Tunduru.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iajiri watumishi na wahudumu wa baraza; kwa sasa kuna mtumishi mmoja tu Bi Vumilia Chipasura, anafanya kazi kama kibarua, hajaajiriwa na anafanya kazi zote za uhudumu, ukarani na uchapaji, ikiwezekana hata huyo aajiriwe.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijenge jengo la kudumu kwa ajili ya Baraza la Ardhi badala ya kuazima jengo Halmashauri, hii iendane na ununuzi wa samani za ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa si vizuri kuendelea kuanzisha mabaraza mengine ya ardhi na nyumba ya Wilaya ikiwa haya yaliyopitishwa na Bunge hayajakamilika.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji na mikakati mizuri inayomkomboa Mtanzania wa hali ya chini. Niombe mambo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za upimaji ardhi zipungue zaidi ili kumuwezesha mwananchi kuweza kumiliki ardhi. Niiombe Serikali itusaidie kupima ardhi ya maeneo yaliyo pembezoni ya Singida Mjini, karibu kata nane, mfano, Mwankoko, Uhamaka, Kisaki na kwingine ili kuwezesha mwananchi kukoposheka na kuinua uchumi wa maeneo hayo, hali hii itatusaidia kuwa na mpango mzuri wa ujenzi na makazi.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono kwa asilima mia moja hoja ya Mheshimiwa Waziri ya Bajeti ya mwaka 2016/2017. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna unavyomsaidia Mheshimiwa Rais kuikuza nchi hii kupitia utatuzi wa migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri anisaidie katika Jimbo langu la Namtumbo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezindua mji mdogo wa Lusewa tarehe 4/4/2016 kwa kumteua *TEO* na Maafisa Ardhi wapime. Tunahitaji mji huo mdogo upimwe na kuainisha maeneo ya matumizi mbalimbali. Mchango wenu unahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali namba 138 la hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa 144 inayosema Shirika la Nyumba limenunua ekari zao katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo si sahihi, *NHC* ilitengewa viwanja 40 katika eneo linalopakana na *TANESCO,* viwanja vya *low density,* lakini *NHC* hawajatoa fedha za fidia na kwa sababu *NHC* hawatoi ushirikiano wowote kuhusu fidia na mpango wao wa kujenga nyumba hizo, Halmashauri inakusudia kugawa viwanja hivyo kwa wahitaji wengine watakaokuwa tayari kutoa fedha za fidia. Masharti ya kuitaka Halmashauri izinunue nyumba zitakazojengwa na *NHC* na kulipa fidia hayajakubalika na kwa kweli hayatekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya hifadhi ya Sebu inapanuliwa bila ya taarifa kwa vijiji husika vinavyoguswa na upanuzi. Vijiji vinavyohusika ni vya Kitanda, Mpuka, Luhangano, Mhangazi, Nangero, Nambecha, Likuyu mandela na kadhalika. Vijiji hivyo vitatenga sehemu ya ardhi yao kama Hifadhi ya Jamii (*WMA)* chini ya umoja wao wa Mbarang'andu. Hivi sasa wanavijiji husika wanataka kurekebisha mpaka wa *WMA* waliojiwekea mwaka 1992 ili kupata eneo zaidi la kilimo kufuatia kuongezeka kwa wakazi wa upande mmoja na upanuaji wa mipaka ya hifadhi za kitaifa za *Selous Game Reserve* na *Undendeule Forest Reserve;* upanuzi huo unaochukua maeneo ya *WMA* kwa upande wa pili. Mazingira haya yanaleta mgogoro unaoanza kukiathiri CCM kwa kupoteza kata ya Mputa na vurugu za wakulima kuchomewa nyumba zao na kufyekwa mazao yao mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Isimani na Waziri mahiri tusaidie kuituliza Namtumbo na Halmashauri yake kwa kurekebisha kasoro hizo hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii ya Ardhi katika Jimbo langu la Kibiti. Kwanza napenda kuipongeza Wizara hii kwa ujumla pamoja na Waziri mwenye dhamana baba yangu Mheshimiwa William Lukuvi kwa anavyochapa kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ni Wizara mtambuka kwani ardhi ni muhimu sana katika shughuli za kila siku za mwanadamu. Hatuwezi kujenga viwanda bila ya kutenga ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Kibiti lina ardhi ya kutosha lakini naiomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kutoa msisitizo kwa watendaji wetu wa Halmashauri kuwajibika katika shughuli zao za kujenga Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la Ardhi na Mahakama ya Ardhi; Baraza la Ardhi katika maeneo yetu tunapoishi ni muhimu sana, kama Baraza la Ardhi la Kata. Napenda kuishauri Serikali yangu sikivu itoe semina elekezi ya Baraza hili la Ardhi ili liipe uwezo wa ufahamu katika shughuli zake za kutatua migogoro ya ardhi katika kata zetu. Mahakama ya Ardhi nayo iwe inatoa lakini kwa muda mfupi; hii itachangia kupunguza dhana potovu ya rushwa kwa wananchi wenye migogoro katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa hati za kimila katika Jimbo langu la Kibiti bado ni tatizo, naomba Wizara yenye dhamana ambayo inaongozwa na Waziri wetu mchapakazi na mwenye weledi mkubwa, Mheshimiwa Willium Lukuvi ahakikishe Jimbo langu la Kibiti sasa wananchi wanapata hati za kimila kama kauli yake Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Magufuli ya Hapa Kazi Tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi katika Jimbo la Kibiti ipo migogoro kadhaa ambayo inahitajika kupatiwa utatuzi kama kata ya Mlanzi na Mahenge. Maeneo mengine ni ya Kibiti na Bumba Msoro; mgogoro wa mpaka kati ya kijiji cha Msafiri, Nyambili, Uponda na maeneo mengine. Katika Jimbo langu pia ipo migogoro ya wakulima na wafugaji. Hii inatokana na kutopanga matumizi bora ya ardhi kama kutenga maeneo ya kilimo, ufugaji, benki ya ardhi pamoja na maeneo ya kujenga viwanda. Migogoro hiyo ipo kata ya Matunda na maeneo mengine. Hapa jimboni kwangu kuna watu wasiojulikana wamechukua maeneo ya Nyatanga, Nyale, Ngambuni, Kisima, Nananyumbani, wananyanyasa wananchi wangu wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuuliza swali Waziri mwenye dhamana, kwa nini hadi leo Songa hawajapata kijiji ikiwa vigezo vyote vya kupata kijiji cha Songa umekamilika lakini hadi leo Serikali bado haijakitangaza kijiji hicho cha Songa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika Idara ya Ardhi Jimboni kwangu Kibiti ni kutokuwa na vitendea kazi vya kisasa ili kuhakikisha wanapima kwa haraka, usafiri wa uhakika, Afisa Ardhi Mteule, fedha ndogo inayotokana na kodi ni vizuri ingebaki asilimia 50 badala ya asilimia 30 ya sasa. Kuongeza watumishi, kwa sasa wapo wachache, kuwalipa posho za kujikimu kwa wakati, kuwalipa posho za masaa ya ziada na hili inatokana na upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji tunawapenda na tunawahitaji katika Jimbo letu la Kibiti; lakini angalizo langu ni kwamba hawa wawekezaji wasipewe ardhi kwa kulipia fidia badala yake wafanye kama ifuatavyo:-

(i) Wanakijiji watoe ardhi na wawekezaji watoe mtaji ili pande zote mbili wawe wamiliki wa kiwanda hicho husika, hii itasaidia kutatua migogoro na dhana potovu ya mwekezaji kuwa kama mnyonyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na taasisi za fedha, napenda kusema Waziri mwenye dhamana atoe tamko maalum juu ya kuzitaka taasisi za fedha zote hapa nchini kutambua hati miliki za kimila nazo ni dhamana ya wananchi kupata mikopo katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja mia kwa mia, Hapa Kazi Tu.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie migogoro ya ardhi iliyopo, moja kwenye Bonde la Mwakaleli kati ya *TANAPA* na wananchi wa Bonde la Mwakaleli katika Kata za Kandete, Luteba na Isange. Tunaomba irudishwe mipaka ya zamani ili wananchi hawa wapate nafasi za kufuga na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa Kyeruku uliopo Kata ya Kisegese, Kijiji cha Ngeleka, kwa sababu shamba hili wananchi wanalihitaji kulilima ili wajikomboe kwenye umaskini na kwa sasa shamba hili lipo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Busokelo tumetenga maeneo tayari kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za *NHC*, wananchi hawa wapo tayari kununua nyumba hizo.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu upo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ukosefu wa mfumo wa kimenejimenti ambao ni unganishi *(Integrated Land Management System)*. Mfumo huu utashirikisha Wizara karibu zote ambazo majukumu yao yanategemea kuwepo kwa ardhi ya kutosha. Kwa mfano Wizara ya Kilimo na Uvuvi, Nishati na Madini, Uchukuzi na Ujenzi, Viwanda na Biashara, Mazingira, Maji, Elimu na Afya. Mpango jumuishi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama kubwa za upimaji wa ardhi wakati teknolojia imeimarika, kuna haja ya kupunguza gharama ili watu wengi wapime ardhi, kwa hili itasaidia kuifanya ardhi kuwa mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukua kwa miji bila ya mpangilio mzuri, hii inaleta bomoa bomoa katika maeneo mengi. Pia kuna haja ya kuongeza kasi ya kupima miji yetu.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yale niliyochangia kwa kuongea, naomba kwa sababu ya muda haya nayo yaunganishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imesababisha migogoro ya ardhi katika vijiji vinavyowazunguka. Mipaka ya *NCAA* iliyowekwa miaka ya 1950 inafahamika na alama bado zipo na pia *GN* inaonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2002 Mamlaka ya Hifadhi ilifanya uhakiki wa maeneo yake na hapo ndipo migogoro ilipoanza. Mamlaka ilichukua maeneo ya wananchi ya kufugia mifugo katika vijiji vya Endramaguang na kijiji cha Lositete bila ya kuwashirikisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *NCAA* inahakiki mipaka yake kazi inayofanywa na Wizara ya Ardhi. Naomba kutahadharisha kuwa haki itendeke na uhakikiwe mpaka wa zamani na si ule wa mwaka 2002 ambao *NCAA* walijiwekea. Najua uhakiki huo umelipiwa na *NCAA* na isije kuwa sababu ya kupindisha haki. Hatutakubali hata mita moja ya ardhi ya wananchi wetu ipotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utata wa mipaka halisi kati ya Wilaya ya Karatu na Wilaya za Ngorongoro Monduli na Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu iligawanywa kutoka Wilaya ya Mbulu na wakati huo mpaka ulikuwa pale juu *view point.* Eneo la msitu wa *Great Northern Forest* lilikuwa Mbulu. Baadaye eneo hilo la msitu lilipandishwa hadhi na kuwa msitu ndani ya hifadhi ya Ngorongoro. Hili haliondoi mpaka wa Karatu kuwa pale juu *view point*. Naiomba Wizara ilete majibu ya mpaka sahihi kati ya Wilaya za Karatu na Ngorongoro na pia kuleta timu ya wataalam ili kuonyesha mpaka sahihi kati ya Wilaya za Karatu na Monduli na pia Karatu na Mbulu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji anayemiliki shamba kubwa Kijiji cha Senzaya amewakosesha wananchi maeneo ya kulima. Eneo analomiliki ni kubwa na ameshindwa kuliendeleza kwa miaka mingi sana. Naomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati ili wananchi waweze kurejeshewa eneo la kulima. Jambo baya zaidi ni kwamba sehemu ya eneo hilo lilichukuliwa kinyemela bila kufuata taratibu/sheria za umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia shamba kubwa na *NAFCO* - Magamba zaidi ekari 12,000 limechukuliwa hivyo wananchi hawana maeneo ya kulima. Ni vyema Serikali ikarejesha sehemu ya shamba hilo ili kuwasaidia wananchi wa maeneo yanayozunguka mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba yote mawili (Isenzanya na *NAFCO*) yapo Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na kwa kunipa fursa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mheshimiwa Lukuvi kwa kazi nzuri na inayoendana na wakati, lakini la muhimu kwa kuwa muwazi kabisa. Sifa yake imemtangulia. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzuri kwa kazi nzuri na kurudisha matumaini ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri maeneo machache ili kuboresha huduma hiyo ya Wizara. Ardhi ndiyo kila kitu, hakuna jambo linaloweza kufanyika bila ardhi, uwazi katika kazi ya Wizara ndiyo mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwanza Wizara iangalie namna ya kudhamini Halmashauri zetu kupata vifaa vya kupima ardhi na kuandaa hati za kimila. Maeneo mengi nchini ujengaji holela unaendelea kwa sababu ya uwezo wa Halmashauri zetu kutokuwa na vifaa vya kisasa vya kupimia viwanja na miji pamoja na mashamba. Pia vifaa vya ofisini ili kuwa na uwezo wa kutoa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itafanya tupate hati kwa wakati na pia kuongeza mapato ya tozo la ardhi *(land rent)*kwa kila mtumiaji.

Pia naomba nishauri Wizara iweze kutumia mfumo ule wa kutumia *satellite imaging* kwenye hati. Pia elimu zaidi itolewe kwa umma juu ya *satellite imaging* ili kuondoa fidia Serikali inayolipa bila sababu kwa wanaojenga maeneo tunapotaka kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze jitihada ya Wizara kumaliza mgogoro. Naomba iunde sheria ya kulinda ardhi ya kilimo bila ya kuwa chini ya mikono ya Halmashauri zetu.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwanza kwa kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara yao kwa ufasaha mkubwa na pili kwa kusimamia utekelezaji wa shughuli

za Wizara kwa ujasiri mkubwa. Hivyo bila kigugumizi chochote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii vilevile kuipongeza Wizara hii kwa kuitikia kilio changu cha muda mrefu cha kuanzisha Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kyela. Kilio changu kiliitikiwa mwezi Julai, 2014 kwa kuanzisha Baraza hilo lakini kwa kutumia Mwenyekiti na Maafisa wengine wa Baraza ambao huazimwa kutoka Mbeya zaidi ya kilometa 100 kutoka Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo sasa umegeuka kero kubwa kwa wananchi kukosa huduma ya uhakika ya Baraza kutokana na Mwenyekiti na Maafisa wake kushindwa kufika Kyela pale inapobidi na kuwaacha wananchi wengi wakisubiri, wakienda na kurudi bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanipatie uongozi/uendeshaji wa Baraza wa kudumu badala ya kusubiri maafisa wa kuazima kutoka Mbeya ambao hawafiki Kyela kwa sababu wanazozijua wenyewe. Nina uhakika, timu hii imara ya uongozi wa Wizara itasikia ombi langu na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Lukuvi na Naibu Waziri Angeline Mabula pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri, Hifadhi ya Kitulo imechukua hata eneo ambalo kimsingi halitumiki kwa utalii wa maua. Kwa hiyo hifadhi imepora eneo ambalo ndilo tegemeo kwa kilimo cha wananchi wa Tarafa za Matamba, Ikuwo, Lupalilo na Magoma, hasa kata zifuatazo Mfumati, Itumbu, Kigala, Ipelele, Mlomwe na Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri ashirikiane na Waziri mwenye dhamana ya Utalii kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Kitulo ili kuondoa malalamiko ya wananchi na kuwasaidia kuendeleza mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri ifahamike kuwa ulinzi wa Hifadhi ya Kitulo unategemea wananchi hawa. Ni muhimu wailinde huku wakiwa na eneo lao kwa ajili ya kulima. Mheshimiwa Waziri alishughulikie jambo hilo hasa miezi ya kuanzia Juni mpaka Septemba wakati wa kiangazi. Nawasilisha.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza kwa dhati Wizara katika mikakati yake ya utekelezaji wake wa bajeti ya mwaka 2016/2017. Lengo kubwa la kutaka Serikali kuendeleza ardhi ni kwamba ardhi ni muhimu sana ndiyo inayokuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa MWenyekiti, Lindi Manispaa eneo la Mkwaya kuna ardhi kubwa inayomilikiwa na Mhindi mmoja. Ni shamba kubwa haliendelezwi, wananchi wa kijiji cha Mkwaya wanakosa eneo la kulima na mmiliki huyo hafanyi chochote. Ninaiomba Serikali kuona kwa namna gani wananchi wa kijiji cha Mkwaya watasaidiwa kupata ardhi hii ambayo haitumiki waweze kutumia kwa ajili ya kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu ni mita ngapi toka katikati ya hifadhi ya barabara mpaka kwenye barabara kuu? Je, wananchi wa Lukuledi, Naditi, Chikunja watalipwa fidia ya nyumba zao zilizowekwa alama ya "X"?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Nyumba *(NHC),* Shirika hili lilianzishwa kwa nia njema ya kusaidia wananchi kujenga nyumba za bei nafuu lakini kwa sasa hivi Shirika hili limekuwa ni la kibiashara zaidi. Hivi huko vijijini hata mijini wananchi wa kipato cha chini wawezaje kumiliki nyumba hata ya milioni 30? Ni vizuri *NHC* wakijenga nyumba wazipangishe kwa bei nafuu na zile kodi zikishalipwa kwa kipindi cha kutosha kulipia deni la ujenzi ndipo mmiliki apewe *offer* ya kununua nyumba hiyo kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi zinazotozwa na *NHC* kwa sasa ni za juu sana na baadhi ya nyumba za biashara hazijakarabatiwa lakini kodi zipo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni *master plan* ipi inayotumika katika Jiji letu la Dar es Salaam? Wananchi wanajenga kama wanavyotaka, lakini ikumbukwe mifumo ya maji taka ni ile ile iliyojengwa enzi ya mkoloni, wakati huo wakazi waliokuwepo walikuwa ni wachache. Sasa hivi Jiji la Dar es Salaam lina wakazi zaidi ya milioni tano wanatumiaje mitandao ile ile ya kupitisha maji machafu? Je, ni kwa kiasi gani Wizara zinashirikiana ili kutatua tatizo hili? Je, Serikali haioni kwa Jiji la Dar es Salaam haiwezi ni wakati muafaka sasa kusitisha ujenzi wa maghorofa makubwa mpaka pawepo na *master plan* ili mji ujipange? Hakuna hata viwanja vya wazi, viwanja vya michezo nyumba zinasongamana hata *emergency* ikitokea katikati ya mji siyo rahisi *fire brigade* kuweza kupita na kuokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi za majengo. Kodi hizi ni kubwa sana kwa wananchi wa kawaida kuzilipa, nikiungana na Kambi ya Upinzani, kodi hizi zilikuwa zinakusanywa na Halmashauri na hii ilisaidia sana kuweza kuleta maendeleo katika Halmashauri husika. Ni sababu zipi zilipelekea Serikali kuamua kodi hizo zikusanywe na kupeleka Hazina?

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia. Uendelezwaji wa Mji wa Kigamboni uendelee kwa kuwa Serikali imeshaanza ujenzi wa Daraja la Nyerere basi na mji ule uendelezwe ili kuleta faida ya lile daraja.

Kuhusu ujenzi wa majumba mapya *(NHC)* na kuyauza yaliyopo katikati ya mji uangaliwe. Ardhi ikishatumika basi, sasa mwaka 2016 tunauza ardhi, je, kizazi cha miaka 50 ijayo watajenga wapi? Nashauri tukodishe tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upimaji Viwanja Kiholela. Serikali imeshindwa nini sasa viwanja vinapimwa hovyo na watu kisha wananchi wanadai huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vipya vinapimwa lakini mradi wa viwanja 20,000 mpaka sasa watu wamewekeza viwanja vimekuwa mapori hakuna uendelezwaji. Mfano Toangoma, Kisota, Gezaulole na Somangira – Temeke, Serikali inasema nini? Gharama kubwa za *rent* za nyumba za *NHC* wakati nyumba hazina ukarabati, maji yamekatwa, umeme wa mashaka lakini *rent* shilingi 320,000 mpaka 280,000. Hizi sio fedha ndogo kwa mtumishi wa kima cha chini vijana wetu wanashindwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kununua nyumba ni kubwa sana na nyumba ni ndogo sana huku familia nyingi zikiwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia.

**MHE. WILLIAM T. OLENASHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpongeza Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri pamoja na watumishi wa Wizara ya Ardhi kwa kutayarisha hotuba nzuri iliyosheheni mikakati mizuri ya kuondoa changamoto ya sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutumia fursa kutoa changamoto kadhaa za ardhi kwenye Jimbo la Ngorongoro ambayo ningeomba Wizara ya Ardhi iangazie mwanga ili kutafuta suluhu ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya vijiji na vijiji. Ngorongoro kuna migogoro mingi ya ardhi inayohusu mipaka. Kutokana na kukosekana mipaka ya kisheria kati ya kijiji kimoja na kingine migogoro hii mara nyingine

imesababisha mauaji na uharibifu wa mali. Mifano ya migogoro ni kama ile kati ya vijiji vya Naar na Kisangiro Maaloni na Yasi Ndito, Sale na Malambo, Ngarwa na Oloipiri na Kirtalo Oldoinyosamba na Pinyin na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwasihi wenzetu wa Wizara ya Ardhi washirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ili kupima mipaka ya vijiji. Ili kuondoa migogoro isiyokuwa ya lazima na kuokoa maisha na mali za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kati ya hifadhi na vijiji. Wilaya ya Ngorongoro ina mgogoro mkubwa kati ya vijiji na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti *(Serengeti National Park)*. Vijiji hivyo ni pamoja na Ololosokwari, Kiitalo, Oloipiri, Oloiriori, Lopulun, Loosoitik, Arrash, Piyaya na kadhalika. Kukosekana kwa mpaka unaoeleweka kwa alama kunaleta mgogoro mkubwa sana kwani mara nyingi wananchi wanakamatwa na kutozwa *fine* kwenye eneo ambalo wao wanafahamu kuwa ni eneo la vijiji toka siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa rai kwa Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana Wizara ya Maliasili na TAMISEMI kupima na kuweka bayana mipaka ya hifadhi ili kuondoa migogoro isiyokuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kati ya vijiji na wawekezaji. Migogoro mingine ambayo ningependa Wizara ya Ardhi iitazame na kutatua kwa kushirikiana na wadau wengine ili ipatikane suluhu ya kudumu ni migogoro kati ya kampuni ya uwindaji ya *Orthelo Business Cooperation (OBC)* na vijiji vilivyopo ndani ya Pori Tengefu la Loliondo *(Loliondo Game Controlled Area)*. Migogoro hiyo ni dhahiri kuwa inasababishwa na mgongano wa Sheria za Ardhi (Na. 4 na 5 za mwaka 1999) na Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009, ambazo zinatoa ardhi kwa vijiji na hapo hapo kuweka mamlaka ya rasilimali za wanyamapori chini ya mamlaka nyingine na hivyo kuleta mgongano wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Wizara ya Ardhi ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kutengua na kufuta mapori tengefu yaliyopo ndani ya ardhi ya vijiji vya Loliondo ili wananchi waweze kupata mamlaka kamili ya kusimamia ardhi zao kama vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mwingine kati ya vijiji na wawekezaji ni kati ya vijiji na wawekezaji, ni ule kati ya kampuni ya kitalii ya *Thompson Safaris* na vijiji vya Sukenya, Mundorosi, mgogoro ambao umezuka baada ya *TBL Ltd.* kuuza ardhi ya shamba la Sukenya ambalo kwa miaka mingi lilitelekezwa na wananchi kulitumia zaidi ya miaka 20. Aidha, wananchi wamefungua kesi mahakamani ya kupinga shamba hilo kuuzwa kwa kile wanachosema kuwa wameporwa na *TBL* bila kufuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro kati ya Wilaya/Mkoa. Ningependa vilevile kati ya mipaka ya Wilaya/Mkoa. Kuna migogoro ya mipaka kati ya Wilaya ya Meatu (Simiyu) na Ngorongoro (Arusha), Longido (Arusha) na Ngorongoro (Arusha) na Karatu (Arusha) na Ngorongoro (Arusha). Mgogoro kati ya Meatu na Ngorongoro umechochewa zaidi na wawekezaji wa *Mwiba Holdings* ambao wanasemekana kusogeza mpaka wa Meatu na Ngorongoro na kumega ardhi ya kijiji cha Kakessio ili kunufaika na rasilimali ya wanyamapori waliopo ndani ya hifadhi. *Mwiba Holdings Ltd.* inasadikika kuwa wanamiliki ardhi ya kijiji cha Makao kinyume na sheria kwani kampuni ya nje ya kijiji mwekezaji hawezi kumiliki ardhi ya kijiji bila ardhi hiyo kuhuishwa na kuwa ardhi ya jumla na hati kutolewa na kamishina wa ardhi. Aidha, kampuni hiyo inafanya ufugaji wanyama pori pembezoni mwa Hifadhi ya Ngorongoro na Pori la Akiba la Maswa kinyume cha Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai kwamba Wizara ifute miliki ya *Mwiba Holdings* kwenye ardhi ya kijiji cha Makao, lakini vilevile Wizara ishirikiane na TAMISEMI kupima mipaka ya Wilaya zenye mgogoro. Naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea bajeti ili tuweze kuijadili. Yapo mambo ambayo nilikuwa nataka kuishauri Serikali pia na mengine kupatiwa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni ya makazi, wananchi wengi sana wanaoishi katika maeneo yasiyopimwa Serikali iliweka mpango wa kuwapatia leseni za makazi ili waweze kutumia ardhi yao kupata mikopo ya benki au taasisi mbalimbali za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini muda wa miaka mitatu ni kidogo sana, ni kwa nini Serikali isiweke angalau hata miaka mitano mpaka kumi ili kusiwepo na usumbufu wa mkopaji kama anachukua mkopo wa muda mrefu? Naomba hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za pango la nyumba za Shirika la Nyumba. Nimpongeze Waziri mwenye dhamana. Tulishawahi kumsikia katika vyombo vya habari akizungumza kuhusu wananchi wa kipato cha chini kushindwa kumiliki nyumba za kuishi au nyumba za biashara. Kama kweli Serikali inataka na ina dhamira ya kweli ya kuwasaidia wananchi wake ingeangalia upya hizi gharama za pango la nyumba za *National Housing* kwa sababu wananchi wengi wana kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hizi nyumba za gharama nafuu ziangaliwe upya, bei ni kubwa sana, watu wenye kipato cha chini si rahisi kuzinunua. Kama

tatizo ni kodi ya vifaa vya ujenzi Serikali ingeondoa ili kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi nchini. Nimpongeze Waziri kwa kuanza kupita katika maeneo yenye migogoro ya ardhi, kwasababu migogoro mingi ni kati ya wakulima na wafugaji, hifadhi na wananchi na mingine ni kati ya wawekezaji na wananchi. Ni kwanini Serikali isiwe na mpango wa kutenga kabisa maeneo kabla ya kuyagawa? Ni kwa nini yasitengwe maeneo ya wakulima ili Serikali iweze kuweka mahitaji yote katika maeneo hayo ili kuondoa hii migogoro? Serikali ina wataalam wa mipango miji, ni kwa nini miji yetu haina mipango? Kumekuwa pia na migogoro hata katika miji yetu sababu wananchi hawajengi majengo kwa mpango. Ni vema Serikali kabla ya kugawa viwanja ingetengeneza mpango mji na baada ya kugawa viwanja basi wasimamie majengo yanayojengwa ili kusiwepo na migogoro ya uvamizi hata ya viwanja vya wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi. Serikali ilijitahidi kufanya maboresho katika Mabaraza haya ya Ardhi ili mabaraza haya yaweze kutenda haki kwa wananchi. Mara nyingi kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya mabaraza kulalamikiwa kutotenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mabaraza haya kumekuwa na changamoto nyingi sana, ni vema Serikali ingeanza kutatua baadhi ya changamoto zinazoyakabili Mabaraza haya.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua juhudi za Serikali katika kuwamilikisha wananchi ardhi. Aidha, natambua kwamba kwa kuwamilikisha wananchi ardhi na kuwapatia hati miliki tunaipa thamani ardhi hiyo na kwa maana hiyo wananchi wanaweza kuitumia ardhi hiyo kama dhamani na kukopa katika taasisi za fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo za Serikali, bado kumekuwa na uelewa mdogo miongoni mwa wananchi juu ya taratibu za kufuata hadi kuweza kumilikishwa ardhi. Kwa sababu hiyo, napenda kujua katika mchakato wa kuwamilikisha wananchi ardhi kwa kutumia hati za kimila, kutafanyika upimaji wa ardhi hiyo au mwananchi atamilikishwa moja kwa moja sehemu hiyo aliyokuwa akiishi au kuitumia tangu mwanzo? Aidha, napenda kujua ikiwa upimaji utafanyika, mwananchi atatakiwa kulipia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya upimaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeshaanza utekelezaji wa zoezi la kupima na kumilikisha ardhi katika Wilaya tatu za mfano; za Ulanga, Kilombero na Malinyi mkoani Morogoro, nadhani ingekuwa vyema Serikali

ikatoa mrejesho wa maendeleo ya mchakato huo ili tuweze kujua mafanikio ni kiasi gani au kuna changamoto kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya upimaji na umilikishaji wa ardhi, ni kwa nini Serikali isiziagize Halmashauri za Wilaya husika kufanya kazi hiyo? Nadhani Wizara ikizipa Halmashauri ruhusa ya kufanya hivyo zoezi hilo litakwenda kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa viwanja vya makazi katika Manispaa ya Morogoro eneo la kutoka Nane Nane hadi Mkambarani katika barabara ya Morogoro – Dar es Salaam katika Manispaa ya Morogoro ni shamba la katani ambalo kwa muda mrefu sasa haliendelezwi licha ya kwamba shamba hilo halina tija kwa kilimo cha katani kutokana na kutoendelezwa, lakini lipo mijini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ingekuwa vyema sasa Serikali ikabadili matumizi ya ardhi ile ili vipimwe viwanja vya makazi katika eneo lile ili kupanua mji wa Morogoro. Nasema hivi kwa sababu sera yetu ya mipango miji hairuhusu kuwa na mashamba makubwa katikati ya mjini, lakini pia ni mpango wa Serikali kubadili matumizi ya ardhi ikiwa ardhi hiyo haitumiki kikamilifu kwa shughuli iliyokusudiwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, ipo migogoro mingi ya mipaka ya ardhi kati ya wananchi na Jeshi la Wananchi (JWTZ). Hali hii imesababisha wananchi wengi kubomolewa nyumba zao na kuondolewa kwa nguvu bila hata ya kulipwa fidia. Aidha, wananchi wanaokumbwa na madhila haya hawajui wapate msaada wapi kati ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi au Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 Kikosi cha Anga Namba 671 cha JWTZ kiliweka mabango katika makazi ya wananchi wa Mtaa wa Makoka, Uluguruni katika Kata ya Makuburi Dar es Salaam ya kuwataka wananchi hao wasifanye chochote katika eneo hilo kwa kuwa ni la Jeshi. Cha kushangaza ni kwamba eneo hilo lina shule za Serikali mbili; ya msingi na sekondari, lina huduma za jamii kama umeme, maji na barabara. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni bado inakusanya kodi ya ardhi na majengo katika eneo hilo. Napenda Serikali itoe kauli kwa wananchi hao ili wajue hatma yao kwa kuwa wamechanganyikiwa kutokana na mkanganyiko kuhusu umiliki wa ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kama wananchi hao hawana haki katika eneo hilo waambiwe mapema ili wasije wakashtukizwa kuambiwa kuhama na kuwasababishia maafa makubwa. Aidha, kama wana haki ya kumiliki eneo hilo, basi Serikali iagize kikosi hicho kiondoe mabango yake ili wananchi hao waweze kuishi kwa amani na kuendeleza makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi naomba nichangie haya yafuatayo:-

(a) Mashamba pori na kutapeli ardhi ya watu ambao hawakuridhia; na

(b) Makazi, ujenzi wa *NHC* na tatizo la mishahara midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba pori na ulaghai kupitia Wenyeviti. Kuna mashamba pori Simanjiro naomba utusaidie kwani wananchi wanateseka na mifugo yao na hivyo kusababisha migogoro kati ya wananchi na mbuga za wanyamapori *(National Park)*. Shamba Namba 24 linasumbua wananchi wa kijiji cha Lobosoit 'A'. Mheshimiwa Waziri anafahamu tatizo hili na tayari maelekezo yale tumeshaanza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa zaidi ya miaka mingi shamba hili halitumiki na halilimwi na juzi kwenye Kikao Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro Bwana Brown Ole Suya alileta barua ya kubatilisha matumizi ya ardhi kutoka kwenye kilimo na mifugo kwenda mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba siyo suala la mazingira na wananchi wa kijiji cha Lobosoit "A", siyo tu hawakumpa mtu huyu hiyo ardhi ya kilimo na mifugo lakini hawapo tayari ardhi yao ihalalishwe ili mtu huyu aiuze ardhi hii kwa wageni (wazungu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wa Vijiji Simanjiro ambao sio waaninifu wameuza ardhi ya wanakijiji bila ridhaa yao na hili limepelekea mpaka wao kupata hati miliki. Waliomilikishwa kimakosa wamepewa mpaka hati miliki na Wizara ya Ardhi. Tutasaidikaje ili wale Wenyeviti wa Vijiji ambao sio waaminifu wachukuliwe hatua na wananchi warudishiwe ardhi yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Laangai, mbali na tamko la mahakama la kuzuia ardhi ya wafugaji isiibiwe na isigeuzwe kuwa eneo la mapambano kama ilivyotokea Kiteto, naomba Wenyeviti na Serikali za Vijiji vya kitapeli zichukuliwe hatua. Iandaliwe orodha ya Wenyeviti wezi wa ardhi ili wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya ardhi inapandisha bei za nyumba; riba za kibenki ni tatizo kubwa la bei ghali za nyumba hizi. La pili, mwanafunzi aliyepata kazi/ajira mwaka huu atapataje nyumba iwapo mshahara wake ni mdogo sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Angola wana mpango mzuri wa kuiwezesha jamii yake kupata makazi bora. Naomba mkajifunze hayo ili wananchi wasaidiwe kupata nyumba bora na nzuri kwa mishahara yao midogo. Hawawezi kukodi nyumba za *NHC* kwa bei za sasa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, nashauri niseme machache**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Wilaya ya Kasulu kuanzisha Baraza la Ardhi tangu mwezi Aprili, 2016. Nashauri basi wataalam hao wafike haraka Kasulu ili Baraza lianze kazi mara moja. Ni hatua nzuri yenye manufaa kwa Wilaya za Kasulu na Buhigwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo uhaba mkubwa sana wa Maafisa Ardhi na Maafisa Mpango Miji. Ni vizuri Serikali iliangalie jambo hili ili wahitimu wa vyuo vyetu vya ardhi waajiriwe moja kwa moja bila kusubiri nafasi hizo eti zitangazwe, ni jambo muhimu sana. Kama walimu wanaajiriwa moja kwa moja, kwa nini isiwe hivyo kwa wapimaji wa ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara sasa iongeze hoja hii Serikalini ili mwaka huu shida hii kwenye Halmashauri, Wilaya, Manispaa na Miji imalizike. *Kasulu Town Council* ina uhaba mkubwa wa upimaji ardhi, *valuers* na Afisa Mipango miji yupo mmoja. Hatuna muda wa kusubiri, wakati ni sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu zoezi hili hati za ardhi za kimila limefanyika nchi nzima, Wilaya ya Kasulu na hasa vijiji vinavyounda Halmashauri ya Mji bado hati hazijatolewa, licha ya baadhi ya vijiji kupimwa. Ni muhimu sasa zoezi la kutoa hati za kimila lihamie Wilaya ya Kasulu na hasa vijiji vya Nyumbigwa, Mhunga, Malumba Herujuu, Karanga, Mpanza na Masambara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Kasulu *(Kasulu Town Council)* tumetenga ardhi, viwanja kwa ajili ya wawekezaji wa nyumba na hasa nyumba za gharama nafuu za *NHC*. Tafadhali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, aagize *NHC* waje sasa Kasulu, soko ni zuri kwa sababu sasa Kasulu ina Halmashauri mbili; Kasulu *DC* na Kasulu *TC,* nyumba zinahitajika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mahitaji ya nyumba za walimu na waganga ni kubwa, mfano Wilaya ya Kasulu, Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Wilaya, mahitaji ya nyumba ni zaidi ya nyumba 2000. Kwa nini *NHC* wasiagizwe kufanya kazi hiyo badala ya Halmashauri ya Wilaya kujenga nyumba chache chache kwa kipindi kirefu? Hii inaweza kufanywa kwa uamuzi wa Serikali na hasa Wizara yako ili *NHC* wasijikite mijini tu na waelekezwe kupeleka nguvu maeneo ya vijijini wakajenge nyumba za gharama nafuu.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi yanachelewesha kesi hivyo kuchochea migogoro ya ardhi. Kesi inachukua miaka kumi; nini matokeo yake kama siyo kukuza migogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro kati ya wananchi wa Mwanalugali - Kibaha Mjini na Halmashauri Kibaha Mjini ambao wameporwa ardhi tangu mwaka 2004 kwa madai ya kufidiwa mpaka leo, nini maana yake? Mgogoro kati ya wananchi wa Bagamoyo na *EPZ* katika shamba ardhi ya Bagamoyo; mgogoro wa ardhi kati ya wafugaji na Vigwaza na wakulima, nashauri wafugaji watengewe maeneo ya mifugo ili kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la *CDA* ni kubwa. Wafanyakazi wa *CDA* kupora ardhi za wananchi na kujimilikisha. Mhudumu ana viwanja kumi eti kwa sababu wanapopima wanajipa viwanja na kuviuza kwa bei nafuu. Ushauri wangu ni kwamba mambo ya ardhi yarudi mamlaka ya Mji wa Dodoma. Wananchi wamechoshwa na *CDA* kwa jinsi inavyofanya kazi kwa maslahi ya wafanyakazi wenyewe.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mufindi Kusini tuna mgogoro wa ardhi kati ya Wizara ya Maliasili na wananchi wa kijiji cha Kitasengwa, Ihomasa, Udumuka na Kilolo, Iyegeya na Mninga. Kufuatana na ongezeko la watu, wananchi wamekosa maeneo ya kujenga nyumba na shughuli za kilimo. Mawaziri waliopita walifika katika vijiji hivi ni Mheshimiwa Maige na Mheshimiwa Ole-Medeye; walifika katika vijiji vya Ihomasa na Kutasengwa. Pia waliahidi kuwa maeneo ambayo yanatumika na wananchi wataachiwa maeneo hayo, lakini mpaka leo hii maeneo haya bado hayajaachiwa wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sasa Waziri wangu wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi atafika katika Jimbo la Mufindi Kusini na kuwaachia ardhi hiyo ili waweze kuendelea na shughuli za kilimo na kujenga nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Njombe na hasa Halmashauri ya Mji wa Njombe kumekuwa na changamoto nyingi sana kuhusiana na ardhi pamoja na nyumba. Changamoto ya kwanza ni upimaji wa ardhi. Maafisa Ardhi wamekuwa wakimilikisha viwanja kwa zaidi ya mteja mmoja. Maafisa wamekuwa wakipima viwanja ambavyo ni ndani ya mita 60 na mwisho wa siku wamejikuta wanawekewa alama ya "X" kwenye nyumba hizo na hatimaye kuwatia hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wakichukuliwa ardhi bila kujadiliana na wenye maeneo husika. Mfano, Mtaa wa Kambarage na Mji

Mwema, hadi sasa hivi kuna mgogoro unaoendelea kati ya mwekezaji na wananchi. Naitaka Serikali ifanye maelewano na wenye ardhi kabla ya kuchukua ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kutoka kwa Waziri wa Ardhi; je, mashamba, majengo na rasilimali nyingine za Njodeko na Njoruma anamiliki nani? Kwa sababu mashirika hayo yalianzishwa na wananchi ili kuleta maendeleo katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua nini kinaendelea kwenye maeneo ya utafiti Igeli na Ichenga yaliyokuwa kwa ajili ya kuwasaidia vijana? Naiomba Serikali kuona namna ya kutumia maeneo hayo kwa ajili ya vijana kujifunza na hatimaye kuwa wakulima wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali watendaji walikuwa wanakusanya kodi za majengo, asilimia 80 ilikuwa inakwenda Halmashauri na asilimia 20 ilikuwa inarudi kwenye Serikali za Mitaa. Baadaye utaratibu umebadilika, wameweka mawakala ambao wamekuwa wakikusanya asilimia 60 kwenda Halmashauri, asilimia 20 wanachukua mawakala, asilimia 20 inarudi kwenye Serikali za Mitaa. Tunapoteza mapato hayo. Nashauri Serikali kuwa kodi hizo zikusanywe na watendaji kusudi asilimia 70 iende Halmashauri, asilimia 30 irudi kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya ujenzi ndani ya mita 60, napenda kuishauri Serikali kwa Mkoa wa Njombe wawekewe utaratibu wa mita 30 badala ya 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii juu ya mambo muhimu matatu yanayohitajika ndani ya Wilaya ya Tarime na hasa Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tarime kwa kiasi kikubwa haijapimwa. Mfano, Halmashauri ya Mji wa Tarime kwenye kata nane, ni kata mbili tu ndiyo zimepimwa. Hilo eneo lingine halijapimwa licha kuwa sasa hivi vijiji na vitongoji vyote vimekuwa mitaa na tuna idadi ya mitaa 81. Hivyo upangaji wa mitaa ni muhimu na uhitaji wa kupanga mitaa ni lazima ili tuweze kupima viwanja na kupandisha thamani ya ardhi yetu. Tunaweza kutumia ardhi ile ili kukopa katika taasisi za kifedha; vilevile mji ukipangwa vyema utavutia wawekezaji mbalimbali kuja katika Halmashauri yetu na kuwekeza kwenye sekta mbalimbali kama vile viwanda, ufugaji, uwekezaji kwenye majengo ambapo tunahitaji *strategic master planning* ya mji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ni Kata ya Bomani kwa sababu tu ndiyo zimepimwa. Tunahitaji upimaji wa haraka kwenye Kata za Turwa, Nyamisangura, Nkende, Kenyemangori, Ketare na Nyandoto ziweze kupimwa ili kuweza kuruhusu utoaji mwingine wa huduma za kijamii kama umeme, barabara, shule, vituo vya afya, vituo vya biashara, maeneo ya viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za upimaji wa ardhi ni ghali sana kwa Mtanzania wa kawaida kuweza kumudu, maana ni kuanzia shilingi milioni moja na kuendelea. Vilevile taratibu hizo zinachukua muda mrefu sana na zina mlolongo na urasimu. Hivyo tunaomba sana upimaji wa viwanja kwenye Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa kipindi cha mwaka huu. Hii itaweza kupunguza kasi ya migogoro kama ule uliopo kwa wananchi wa Mtaa wa Mafarasini, Kata ya Bomani ambapo walipimiwa ardhi kwa ada (gharama) ya shilingi 20,000, shilingi 40,000, shilingi 70,000. Cha kushangaza baada ya muda Serikali inawaambia walipie tena upya gharama za kumiliki ardhi kuwa ni kuanzia shilingi 2,000,000 na kuwaambia kuwa wanaoshindwa kulipia gharama hizo watanyang'anywa ardhi hizo na kupewa wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki kwa maskini wale waliomilikishwa ardhi kwa kufuata sheria na walilipia. Iweje leo tena mnawapoka? Hadi sasa wananchi hawa wa Mafarasini wanashindwa/huogopa kuendeleza makazi yao kwa kuhofia kupokwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni juu ya waraka ambao umetoka Serikali Kuu (Wizarani) kwenda kwenye Halmashauri ya Mji ikitaka kutokutumia matumizi ya ardhi pale inapoona inafaa. Hili kiukweli limekuwa kikwazo kikubwa sana na ukizingatia Halmashauri yangu ni changa na hivi katika upangaji wa mji kuna maeneo yanaweza kubadilishwa matumizi ili yaweze kutumika katika shughuli za kijamii kama vile mashamba na hata viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inarudisha nyuma maendeleo ya Tarime Mjini. Mfano Ofisi ya Mbunge iliandika barua kwenda Halmashauri ya Mji kuomba eneo ambalo litatumika kujenga maktaba ya umma ambayo itasaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi wetu. Vilevile kuongeza idadi ya Watanzania wanaosoma vitabu ili kupanua uelewa. Cha kushangaza na kwa masikitiko, Mkurugenzi wa Halmashauri wa Mji kasema kwamba Serikali imezuia ubadilishwaji wa matumizi ya ardhi. Hii inarudisha nyuma maendeleo ya Tarime Mjini. Naomba Wizara ione umuhimu wa kupatiwa eneo la kujenga maktaba ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni tatizo sugu ni juu ya kucheleweshwa kwa malipo ya fidia kwa wananchi ambao ardhi yao imepokwa na JWTZ. Wananchi hawa walifanyiwa tathmini tangu mwaka 2012

hadi leo hawajalipwa na walizuiliwa kufanya shughuli za maendeleo tangu mwaka 2007 na wakapora hadi mkataba wa mnara wa *Airtel*, kinyume kabisa na sheria za nchi hii. Je, katika tathimini itakayofanywa tena itafidia mkataba wa mnara pamoja na uhalisia wa mali tangu mwaka 2007? Kutakuwa na riba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawataka Serikali imalize malipo ya Ranchi wa Ronsoti, Msati (Nyamisangura) Kenyambi (Nkende) na nyinginezo. Ni aibu kuwapoka wananchi ardhi kinyume na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 lakini mkashindwa kulipa fidia. Vilevile Serikali ione umuhimu sasa ya kuhakikisha Bodi ya Mifuko ya Fidia inaundwa mwaka huu ili tuepushe ucheleweshaji wa malipo ya fidia. Tunaomba *NHC* waje kuwekeza Tarime, maeneo tutawapatia ili kuweza kupunguza adha ya malazi na kukuza mandhari ya mji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile fidia za wananchi wa Nyamoyo ambao walifanyia tathmini tangu mwaka 2011/2012 waweze kulipwa fidia zao maana waliondolewa na kwenda kutafuta makazi mengine ambapo ilibidi wakope fedha benki waweze kuanzisha makazi mengine. Hivyo wameshindwa kulipia mkopo na kubaki na adha kubwa sana. Hawa sasa ni wakazi wa mji wa Tarime, hivyo tufuate Sheria za Ardhi bila kunyanyasa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inachukua muda mrefu kweli kurejesha *retentions* katika Halmashauri husika, mfano Halmashauri yangu ya Mji wa Tarime ambayo haina mapato ya kutosha. Hivyo hizo fedha za upimaji ardhi ni vyema ziwe zinapelekwa mapema kuliko kucheleweshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Ardhi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri Mheshimiwa William Lukuvi kwa kuchaguliwa tena kuongoza Wizara hii, hakika anaweza. Nampongeza pia na kumshukuru kwa ziara aliyoifanya Jimboni kwetu kwani ilitupa mwanga wa utatuzi wa migogoro mingi ya ardhi iliyotuzunguka. Bado tunamhitaji Mheshimiwa Waziri Arumeru ili tuweze kumaliza kabisa changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya sababu ambazo zinasababisha migogoro ni Serikali kuwapa wawekezaji maeneo makubwa mno kuliko uwezo wao na kuyaendeleza. Hii hupelekea wawekezaji kufanya biashara kukodisha ama kugawia wananchi mashamba hayo ambayo baadaye hushindwa kuwaondoa pindi wanavyotaka kufanya shughuli nyingine katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo kama haya hasa katika shamba ya *Fill Estate* na *Tanzania Plantation* yote katika Jimbo la Arumeru Magharibi, Kata ya Bwawani. Wananchi wameumizana sana na vyombo vya dola na zaidi ya watu 11 wapo rumande kwa miezi miwili sasa kwa kubambikiziwa kesi ya wizi wa kutumia silaha eti kwa sababu tu wanagombania shamba na askari polisi ambao wawekezaji wakawakodisha katika shamba ambalo wananchi tayari walikuwepo kwa lengo la kuwatoa kwa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Arumeru karibu sasa yote inakuwa mji, hivyo mashamba mengi ya wawekezaji yamemezwa na idadi kubwa ya wananchi wanaoongezeka kila kukicha na hivyo mashamba haya yanalimwa mjini na bado hayajaendelezwa vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali huchukua muda mrefu sana kubatilisha haki za umiliki za wawekezaji zilizopita muda wake na kupelekea wananchi kuvamia mashamba hayo na kuanza kujigawia. Serikali sasa ichukue hatua madhubuti kutengua hati za ardhi ambazo muda wake umeisha. Hii ni pamoja na kuwatafutia maeneo mengine wawekezaji ambao mashamba yao yameingia ndani ya miji kuepusha migongano zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu linaelekea pabaya hasa jinsi suala la migogoro ya ardhi inavyoshughulikiwa, Taifa linaelekea Zimbabwe. Kwa Mkoa wetu wa Arumeru hali siyo shwari kwa wawekezaji na hivyo wapo kwenye hofu kubwa sasa, wananchi kila wanapoona shamba kubwa basi hulazimisha wanasiasa kufanya liwezekanalo ili wanyang'anywe na wapewe wao, jambo ambalo siyo zuri kwa ustawi wa Taifa letu ambalo bado linahitaji wawekezaji kwa ustawi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwa Serikali, hasa kwa Mkoa wa Arusha kuboreshewa miundombinu inayounganisha mikoa mingine hasa Manyara, Wilaya ya Simanjiro ili kuwaunganisha wananchi hawa na maeneo hayo ambayo bado ardhi ni *virgin*. Mashamba yaliyo mjini na muda wake umekaribia kwisha, Serikali iyatwae na kufanya mipango mipya ya ardhi/mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanasiasa siyo rahisi kutoa elimu ambazo siyo rafiki kwa wananchi kuhusu umiliki wa mipango ardhi, Serikali kwa kutumia vyombo vyake, elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi kuhusu sera za ardhi na umiliki mashamba ili wananchi waache tabia ya kuvamia mashamba ambayo nyaraka zake ziko thabiti/*genuine* ili kuhakikisha kwamba wawekezaji ambao Serikali inahangaika kuwaalika wanakuwa salama na wanafanya kazi zao kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninamwalika tena Mheshimiwa Waziri Jimboni Arumeru Magharibi ili tumalizie migogoro iliyopo *once and for all.* Ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu, kwa kunijaalia uzima na afya njema na leo naomba kuchangia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya Mtwara Mjini hayapapimwa. Katika kikao cha kwanza Bunge lako hili la Kumi na Moja nimeuliza maswali juu ya upimaji na urasimishaji wa ardhi Mtwara Mjini ambalo mpaka sasa halijajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuja kujumuisha hoja yake aje na majibu stahiki, ni lini maeneo mengi ya Mtwara Mjini yatapimwa na kurasimishwa? Swali hili ni muhimu sana kwa kuwa mtu akimiliki kipande chake cha ardhi kisheria anaweza kukopa benki kwa kutumia dhamana ile na kuweza kumsaidia kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara Mjini kuna migogoro ya ardhi mingi sana. Nashangaa Mheshimiwa Waziri ameweka/ametaja mgogoro mmoja tu ambao ni wa Libya. Siyo kweli kwamba Mtwara Mjini kuna mgogoro huu tu. Ipo mingi sana ambayo Serikali inakwepa kwa makusudi kabisa kupitia Maafisa wake wa Ardhi Mtwara Mjini wakiongozwa na Afisa Mipango Miji. Kuna eneo la Mji Mwema na Tangla, maeneo ambayo yalikuwa ya wananchi Serikali, imechukua tangu mwaka 2013 mpaka leo Serikali haijalipa fidia kwa wananchi wale. Wananchi hawana sehemu ya kulima na wengine wamebomolewa makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tathmini iliyofanyika kila *squire meter* moja walilipia shilingi 250 tu. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kwa nini Serikali hii inawadhulumu na kuwanyanyasa wananchi wa Mtwara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kwa kuwa ni miaka mitatu sasa tangu wananchi wamenyang'anywa maeneo yao na hawajapewa fidia, je, Serikali ipo tayari kulipa fidia ya miaka mitatu ili ilingane na thamani ya ardhi ya sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wameibiwa katika tathmini iliyofanywa na watendaji wa Halmashauri na kupewa shilingi 250 - 450 kwa *square meter* moja, Serikali ipo tayari hivi sasa kufuta bei hii na kufanya tathmini upya kwa maeneo hayo ya Mji Mwema na Libya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mgogoro huu ni mkubwa sana Mtwara Mjini na wananchi wamemwelezea mpaka Waziri Mkuu na kuahidi kuutatua, Mheshimiwa Waziri Lukuvi lini atakuja Mtwara Mjini ajionee mwenyewe kuliko kutegemea taarifa za uongo za Maafisa Ardhi ambao ndio wahusika wakuu wa utapeli huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *Plot* Na. 99 ya Mzee Mayunga ekari 15 ambazo amenunua tangu miaka ya 1980 na amekuwa akilipia kila mwaka, leo Maafisa Ardhi wameshirikiana kuficha *file* la huyu mzee na wamemwambia kiwanja hicho hakitambuliki ili wauze eneo hilo kwa mtu mwingine. *Plot* hii Na. 99 anayonyang'anywa ili wauze na wamethubutu mpaka kuficha *file* la mzee huyu ambalo lilikuwa Halmashauri, hii ni dhuluma ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri Lukuvi ahakikishe anamrudishia mzee huyu *plot* yake Na. 99 ambayo wameitisha watendaji wa Halmashauri na Mkoa wa Mtwara. Watendaji wa Ardhi Mtwara Mjini ni majipu makubwa yaliyoiva, tafadhali uje Mtwara kuyatumbua au mnasubiri mpaka watu waandamane na Mheshimiwa Rais aje kutumbua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo unaosemwa sana Mtwara kuwa kutokana na sakata la gesi Mtwara, viongozi wengi wamenunua viwanja kupitia hawa Maafisa wa Ardhi. Naomba sana msipokuja kuwatumbua watu hawa, usemi huu tutauamini sana kwamba mnawalinda kwa kuwa mnawatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba zinazoitwa za bei nafuu siyo kweli kwani bei yake ni ya juu sana. Mwalimu mwenye mshahara wa shilingi 100,000 kwa mwezi kama *basic salary* hawezi kununua nyumba hizi kwa shilingi milioni 40, shilingi milioni 50 na kuendelea, mnasema ni za bei nafuu? Hapana, hizi ni nyumba za wale wale wenye fedha nyingi ambazo sitaki kutumia jina maarufu sana lililopita mtaani kuwa ni nyumba za mafisadi. *NHC* iwezeshwe kujenga nyumba za bei nafuu.

**MWENYEKITI:** Tumemaliza uchangiaji na sasa nianze kuwakaribisha wahitimisha hoja hatua kwa hatua. Nianze na Mheshimiwa Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, dakika zako kumi atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Mheshimiwa Mwijage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea hotuba yangu ya Wizara ya Viwanda, Waziri wa Ardhi nilimshukuru kwa kumtaja jina na hii ni kutokana na namna Wizara hiyo inavyoshirikiana na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna moja napenda niliweke wazi, wawekezaji njoo muwekeze Tanzania na ninyi Watanzania mchangamkie kuwekeza, hatuna tatizo la ardhi. Mama mwenye nyumba wangu alipata nafasi ya kuzungumza akasema viwanda mtavijenga wapi, viwanda tuna maeneo ya kutosha. Ukisoma ukurasa wa 135, jedwali namba 11 la bajeti hii, miji kumi tu imeeleza maeneo yaliyopangwa lakini hayo ni hayo tu. Pia ukienda kwenye jedwali la *TIC (land bank)* kuna hekta 500,900 zinazoonyesha maeneo yaliyotengwa mahsusi kwa ajili ya kilimo na hasa kilimo cha miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumueleza Mheshimiwa Kamanda Silinde kwamba mwekezaji niliyekuwa namwambia ameshaweka timu Songwe, anakwenda jimboni kwake, anakwenda kulima miwa na anategemea kuzalisha tani 120,000 za sukari. Nayasema haya kuwatoa wasiwasi watu wasije wakadhani kwamba nchi ya Tanzania haina ardhi na Wizara ya Ardhi haijanitengea ardhi. Niwashukuru sana, nikushukuru na mueleze bosi wako kwamba Mwijage amekushukuru sana ulipokuwa haupo kwenye kiti chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenga ardhi ya kutosha kwa ajili ya kujenga viwanda vya sukari na kilimo cha miwa**.** Mbunge wangu wa Temeke leo asubuhi aliniuliza swali likanipa shida juu ya hali ya sukari nchini. Niwahakikishie tunayo sukari ya kutosha.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Tumechukua jitihada za kawaida za kutenga maeneo, kwa mfano lipo eneo la Kigoma ambapo hekta 47,000 zitatengeneza kiwanda cha *Kigoma Sugar,* nimelizungumza hili la Songwe, tutaendelea na Songwe, lakini *Kagera Sugar* wanaozalisha tani 60,000 wanapanua eneo la Kitengule wazalishe tani 60,000 nyingine. Aidha, watu wa Oman wataingia ubia na *Kagera Sugar* ili kuzalisha tani 300,000 kutoka pale. Kwa hiyo, hii adha tunayopita ni kwamba tuliamua kudhibiti uingiaji wa sukari ili kuwajengea hamu wawekezaji waweze kuingia katika shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha iliyokuwepo sasa inakwenda kuisha, tunayo sukari ya kutosha, kuna maeneo yana matatizo, kuna Mbunge wa Mwanza ameniuliza kwamba Mwanza sukari iko wapi? Leo Mwanza hali ni mbaya, kilo moja ya sukari shilingi 4,000. Baada ya kunieleza, Bukoba wanapakia tani 600 kwenda Mwanza na kiwanda cha *Kagera Sugar* kimeanza kuzalisha leo, ni tani 250 zinazalishwa. Tarehe 25 Mei, Kilombero *(K1)* inaanza

kuzalisha na wakimaliza kuzalisha *full swing* ni tani 600 kwa siku. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuwe na imani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yaliyochukuliwa yalijenga imani na kuwaleta wawekezaji hapa ndani.

**MBUNGE FULANI:** *(Aliongea nje ya kipaza sauti).*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Ngoja nitoe maelekezo mama unielewe, niko kazini hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa maelekezo wafanyabiashara wote mnaoshughulika na sukari mkajitambulishe kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili sukari mnayopewa Dar es Salaam muifikishe kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waione.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Tayari zimeshatoka tani 10,000 kwa ajili ya kusambazwa, lakini kuna tani 31,000 ziko njiani zinakuja. Ngoja niwaeleze jambo moja, matumizi ya nchi ni tani 1,200 kwa siku, *Kagera Sugar* inazalisha tani 250, Mtibwa inazalisha tani 600, *deficit* ndiyo hiyo niliyowaeleza iliyoagizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba maeneo ya ujenzi hayana shida. Nichukue fursa hii kuwapongeza tena wale viongozi mnaokwenda mbele zaidi kutambua maeneo yenu na kuyapeleka Wizara ya Ardhi ili yapimwe. Nichukue fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wa Tabora. Wabunge wa Tabora walinipa ardhi, nikatafuta mwekezaji, mwekezaji alipokuwa anapanda ndege akazuiliwa asiende Tabora. Niliwaambia wakati wa bajeti yangu kwamba ujenzi wa viwanda ni vita, kwa hiyo, vita hiyo nitaishinda, nitawasaidia watu wa Tabora, nitamleta hata kwa baiskeli huyo mwekezaji ili twende Tabora tuweze kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu ambalo kimsingi halitafanikiwa kama sisi Waheshimiwa Wabunge hatutalisimamia. Tumeagizwa au imekubalika na Serikali kwamba katika maeneo ya vijiji na kata, tutoe maeneo tuyarasimishe, twende tuyapatie hati ili vijana wetu waweze kuanzisha shughuli na biashara ndogo ndogo. Kuna fursa zinakuja za ujenzi wa *silos (godown),* maeneo mtakayoyatoa kama alivyozungumza Mbunge mmoja yataweza kutoa nafuu katika ku-*acquire* ile *land* na kuweza kuweka *infrastructure* bila kutumia gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyotengwa yapo kama nilivyowaeleza, yapo maeneo ya Mkurazi yameelezwa na nimeiona Momba hapa nimeiona imetengwa. Niwaeleze ukweli, nimepewa jukumu lingine bahati mbaya, nimsemee Mheshimiwa Mwigulu. Mheshimiwa Mwigulu maneno anayozungumza siyo hadithi za kufurahisha watu. Tuombe Mwenyezi Mungu atusaidie kabla ya mwaka huu kuisha nitakuwa na mtambo tayari wa kuunganisha matrekta 2,500 hapa Tanzania na matrekta hayo yatakwenda kulima ardhi hizi. Kwa hiyo, tunachopaswa kufanya Watanzania wenzangu, unapopata ardhi isalimishe kwa Mheshimiwa Lukuvi, Wizara ya Ardhi ili ardhi hiyo tuweze kuifaidi Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo mimi niseme Wizara yangu iko vizuri lakini niwatoe wasiwasi wawekezaji, msiwe na wasiwasi ardhi ipo. Nimetoa mfano wa Nzega, Maswa na Kagera ambako wananchi wametoa maeneo. Hata hivyo, mnapotoa maeneo nendeni mkayarasimishe Wizara ya Ardhi ili mpate *title* ili mwekezaji anapokuja iwe rahisi kuwekeza. Napozungumzia wawekezaji sizungumzii wa kutoka nje, mwekezaji ni pamoja na wewe. Tujenge kiburi, tujiaminishe na sisi tuanze kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya masuala haya ya ardhi, ndugu yangu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, kwa kazi yake nzuri anayoifanya pamoja na Naibu Waziri wake. Niseme tu kwamba sisi kama Serikali tutaendelea kushirikiana nao ili haya yote yanayojiri kwenye migogoro ya ardhi yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kusema kwamba yale yote ambayo yanafikiriwa kwamba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ingeyachukua na kuyashughulikia kwa uzito, Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni yupo na ameya-*note* vizuri. Mimi pia kama Waziri mwenye dhamana chini ya ofisi hiyo basi niseme kwamba tunayachukua yote. Waheshimiwa Wabunge tuwahakikishie kwamba tutayafuatilia na tutayatekeleza na tutashauriana na ninyi ili kuboresha haya yote yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na hapa leo wamewakilishwa vizuri sana na Mheshimiwa Felister Bura, amezungumza vizuri sana habari ya *CDA* na Mheshimiwa Kunti

naye amezungumza vizuri sana habari ya *CDA*. Niseme Wabunge hawa wawili wamewawakilisha Wabunge wenzao wa Mkoa wa Dodoma lakini naamini kabisa Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde naye amekuwa mstari wa mbele sana kushughulikia masuala haya yanayohusiana na *CDA*. Wote kwa ujumla wao mara nyingi wamekuwa wakinieleza habari moja ama nyingine kuhusiana na *CDA*. Kwa hiyo, naomba tu niwahakikishie Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na Wabunge wengine wote na Watanzania kwa *interest* ya kuhamishia makao makuu yetu ya nchi hapa Dodoma tuko pamoja na tutashirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge wote wa Mkoa wa Dodoma na hasa Mbunge mwenyeji wa Jimbo la Dodoma Mjini, nadhani itapendeza sana kama tutapata nafasi kabla Bunge hili halijaisha tungekutana ili tutizame haya yote ambayo yamekuwa yakijiri kwa *CDA* hapa Dodoma. Pia tutathmini kwa pamoja umuhimu wa kuhamishia makao makuu ya nchi hapa Dodoma na hii itakuwa pia kwa faida ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma.

Kwa hiyo, naomba tu nichukue nafasi hii kuwahakikishia Wabunge wa Mkoa wa Dodoma kwamba tuko tayari sisi kama Serikali na mimi Waziri niko tayari kukutana nao na tukatathmini haya matatizo ambayo wanafikiri kwamba yamekuwa yakijitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili kuwapa matumaini vizuri naomba niwathibitishie kwamba tumeanza kujipanga na *CDA* na hasa baada ya Mkurugenzi wa *CDA* kuthibitishwa rasmi na Mheshimiwa Rais, mwezi Februari, 2016, kuona kwamba tunarudisha mahusiano mazuri kati ya *CDA* na wananchi wa Mji wa Dodoma na kumaliza ile migogoro yote ambayo ilikuwa ikijitokeza kwa namna moja ama nyingine. Ijumaa nilianza kwa kufanya kikao na wafanyakazi wote wa *CDA*, tumekutana kwa pamoja, tumejitathmini kwa pamoja na tumejenga mkakati wa pamoja wa kuhakikisha kwamba tunapohamia hapa Dodoma kwa kweli wao wana wajibu mkubwa wa kusimamia mambo na mipango yote itakayowekwa. Kwa hiyo, naomba tu niwathibitishie kwamba tuko pamoja na tutaifanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini jambo lingine naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ili kuondoa kutokuelewana kwenye masuala haya kati ya *CDA* na wananchi wa hapa Dodoma tumefikiri ni lazima tuharakishe sana kuleta ile sheria ambayo itaitambulisha vizuri Dodoma kama *capital city*. Kwa hiyo, sheria ile tumeanza kuitengeneza na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba sheria ile iko mbioni kabisa kuletwa na niwaombe tutakapoileta ndani ya Bunge basi mtusaidie kuipitisha. Tukiipitisha sheria hiyo itasaidia sana kupunguza migongano na migogoro mingi ambayo inajionyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ile pia itasaidia kusimamia azma ya Serikali ya kuhamia hapa Dodoma. Niwathibitishie tu kwamba ni lengo hasa la Serikali kuhamia Dodoma na iko pia kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ni lazima tuone kwamba katika kipindi hiki tunajitahidi kuhamisha makao makuu na kuyaleta hapa Dodoma na hilo tutalisimamia na sheria itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini sheria hii pia itaondoa migongano ya kisheria kati ya taasisi mbalimbali ambazo pia zinasimamia matumizi ya ardhi katika makao makuu haya yanayotarajiwa kwenye mji huu wa Dodoma. Vilevile itaondoa pia migongano ya kisheria kwa sababu pia zipo sheria nyingine mbalimbali kwa mfano Sheria ya *Local Government Authority* na sheria nyingine. Tutakapoileta sheria hii itakuwa ni mwarobaini, itatusaidia sasa ku-*define* mipaka ya *CDA* lakini kutoa tafsiri halisi ya majukumu ya kila chombo ili migongano hii yote iweze kuondoka na azma hii ya Serikali ambayo ni njema iweze kutekelezeka ikiwa imefanikiwa kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee kutoa rai kwa wananchi wote wa Dodoma waamini Serikali yao inafuatilia kwa karibu sana kwanza kuhakikisha azma hii inatekelezeka lakini vilevile kuona kwamba migogoro inaisha kwa kufuata sheria na taratibu tulizojiwekea. Niwaombe wananchi wa Dodoma pale wanapoona kuna matatizo waamini kwamba sisi kwa kushirikiana nao tunaweza tukafanya vizuri sana na siyo vinginevyo. Sisi tuko tayari na tumeanza kufanyia kazi changamoto zilizopo na juzijuzi tu tumemaliza migogoro kadhaa ambayo ilikuwa inawakabili wananchi wa Dodoma. Kwa hiyo, waamini ile migogoro iliyobaki tutaendelea kuumaliza mmoja baada ya mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile waelewe kwamba na wao wanatakiwa kufuata sheria na kuzingatia sheria, kila jambo ni lazima litaenda kwa kuzingatia sheria. Pale ambapo tutaona kwamba wana haki watapewa haki yao na pale ambapo wao wanaona kabisa sheria inawataka watekeleze majukumu mengine naomba watupe ushirikiano. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ameamua kabisa kufanya kazi na sisi ili kuhakikisha kwamba tunamaliza matatizo haya yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa sheria hii pia itatufanya tuweze kuwa na mji wa kisasa, makao makuu ya nchi ambayo yatafanana na hii azma ya Serikali yetu tuliyonayo. Waheshimiwa wengi wamezungumza hapa, Mheshimiwa Shally ametuuliza mnakwenda kutembea huko hamuoni miji ya wenzenu ilivyo? Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Shally tumeona, tumejifunza miji mingi jinsi ilivyo mizuri na hivyo tunataka kuujenga Mji wa Dodoma uwe nao una picha ambayo itaweza kupeleka ujumbe wa namna nchi yetu ya Tanzania ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi mkiangalia jinsi Mheshimiwa Rais wetu sasa hivi hata ukienda kwenye mataifa mengine amekuwa akitambulika kwa sifa na heshima kubwa sana. Kwa hiyo, tutakapoujenga mji huu katika kipindi hiki cha kwake pia itabidi uendane na hadhi ya nchi yetu na vilevile uendane na kile tunachokifikiri kitakuwa ni sura ya Taifa letu katika mataifa mengine katika ulimwengu mzima. Naomba tu niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge tumeanza kufanya kazi ya kutosha ya kujenga miundombinu na tutaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naomba niwahikikishie tuko tayari tutafanya kazi pamoja na ninyi na *CDA* kujenga makao makuu ya nchi hapa Dodoma. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kunitunzia muda. Anayefuata ni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, Mheshimiwa Mabula, una dakika zako 20.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge lako Tukufu, naomba nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa fursa aliyonipa ya afya njema na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kusema yale nitakayoyasema ikiwa ni katika hali ya kujibu baadhi ya hoja za Wabunge ambazo wamezitoa na nyingi tutazijibu kwa maandishi na watapata nakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nichukue fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameniamini na kunipa fursa ya kuweza kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na niseme sitamuangusha. Kwa kupitia kwake pia niwashukuru sana wananchi wa Ilemela ambao wamenipa dhamana hii ya kuwawakilisha Bungeni na hatimaye Mheshimiwa Rais akanipa wadhifa mwingine wa kuweza kumsaidia katika Wizara niliyoitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mwanamke wa kwanza kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais. Ni wazi atatuwakilisha vizuri na ameonyesha njia kwa namna alivyoanza. Nimpongeze pia Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na hasa wananchi wa Jimbo lake la Ruangwa kwa kumchagua kuwa Mbunge na hatimaye akateuliwa kuwa Waziri Mkuu na Bunge hili likamthibitisha. Niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao wamechaguliwa. Nimpongeze Spika pamoja na Naibu Spika na Wabunge wote kwa nyadhifa zenu ambao mnategemewa sana na wananchi

kwa sababu ya kuwapa ridhaa kwa hiyo wana matumaini makubwa kutoka kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani zangu pia zimwendee sana Waziri na mtani wangu Mheshimiwa William Lukuvi kwa ushirikiano anaonipa katika kufanya kazi. Ni muda mfupi tu ambao tumekuwa pamoja naye lakini najisikia kuwa na faraja kubwa kwa sababu ni *mentor* mzuri ambaye anaweza kukuelekeza, akakushirikisha na ukaweza kufanya kazi vizuri. Na mimi nasema nitatoa ushirikiano kwake wakati wote kwa namna ambavyo anaelekeza nadhani imenifanya pia nitambue na nielewe Wizara kwa muda mfupi, nasema tutafanya kazi vizuri.

Pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi na mashirika yaliyoko chini ya Wizara wamekuwa na ushirikiano mzuri katika kufanya kazi hizi na hatimaye kwa muda mfupi sana huduma katika Wizara zimeboreka na watu wanahudumiwa vizuri na mrejesho tunaupata. Kwa hiyo, namshukuru sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote walioko katika idara nilizozitaja.

Aidha, pia nishukuru sana Ofisi ya TAMISEMI ambayo nayo tumekuwa tukishirikiana sana katika kutatua kero mbalimbali. Ardhi ni suala mtambuka na mambo mengi yanaletwa ardhi lakini yanagusa Wizara nyingi, kwa hiyo, nishukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shukrani zangu nisisahau familia yangu, namshukuru sana mume wangu Julius Mabula, watoto wangu David, Javine, Diana na Dorothy, baba na mama wazazi Silvester Lubala ambao wameweza kunilea na kunifanya niwe kama nilivyo. Nashukuru ndugu, jamaa na marafiki ambao wote wamekuwa karibu sana katika kunitia moyo na kuweza kufanya kazi kwa umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza ambao tunashirikiana sana katika kazi zetu kuhakikisha kwamba Mkoa unakwenda vizuri. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru viongozi wa dini madhehebu yote Mapadri, Mashehe, Maaskofu katika madhehebu mbalimbali ambao kwa muda wote wamekuwa wakiniombea na kunipa ushauri wa kimwili na kiroho na wamenifanya kwa kweli nisimame imara katika kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie shukurani zangu si kwa umuhimu kwa kukishukuru sana Chama changu ambacho kimeniamini kikaniteua na kunifanya nigombee katika Jimbo ambalo kwa miaka mitano tulikuwa tumepangisha lakini mpangaji akashindwa masharti ya upangaji tumemwambia apumzike ili tuweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani zangu naomba sasa nianze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Wabunge katika michango yao ya maandishi na wengine kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia ile taarifa ya Kambi ya Upinzani ambayo Waziri Kivuli aliiwasilisha hapa na nimshukuru tu kwamba taarifa yake ilikuwa ni nzuri kwa jinsi alivyoileta ina changamoto na mambo ambayo ameyasema hapa tutakwenda kuyatolea taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Upinzani imezungumzia suala la uporaji holela wa ardhi katika maeneo mbalimbali, wamezungumzia ufisadi wa ardhi unaofanywa na viongozi na hakuna hatua zinazochukuliwa na wamezungumza kuhusu watu wa chache kuhodhi ardhi. Katika haya yote niseme utoaji wa ardhi kwa wawekezaji unazingatia zaidi sheria za nchi. Wizara inaelekeza mamlaka ya ugawaji kuzingatia sheria hiyo na Wizara imekuwa ikilisimamia hilo na imetoa mwongozo kwa Wakuu wote wa Wilaya ili kupitia katika vikao vyao ili ardhi isitolewe kiholela kama ambavyo imekuwa ikileta migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hatua zinachukuliwa kwa ardhi ambayo inapatikana kinyume na utaratibu. Wizara imeagiza Halmashauri zote nchini kufanya ukaguzi na uhakiki wa mashamba pamoja na viwanja ili kuweza kuratibu na kuona yapi ambayo yanamilikiwa isivyo kihalali ili hatua ziweze kuchukuliwa. Katika kutekeleza hilo pia ni wazi wote ni mashahidi tumeandaa kitabu ambacho kila mmoja anacho kimeainisha migogoro yote ambayo ipo. Mingine kweli inatokana na watu kukiuka taratibu, lakini mingine pia ni kwa utendaji pengine ambao umekiuka maadili ya kazi kwa watendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la fidia ambalo amelizungumzia. Sheria ya Ardhi na kanuni zake zimeweka utaratibu wa kukadiria na kulipa fidia ya ardhi na fidia yake inatofautiana kutegemeana na eneo ambapo ardhi ipo. Kwa hiyo, kuna ardhi nyingine unakuta bei yake iko juu na nyingine iko chini. Pia hapa tutambue kuna wengine ambao wanalalamika lakini ardhi zao zilitwaliwa kabla ya ile sheria ya mwaka 2002 ambayo imeingiza ardhi pia kuweza kuthamanishwa. Kwa hiyo, wengi wanarudi kudai kuongezewa fidia lakini wakati huo huo walishathaminishwa kwa sheria ya kabla ya sheria mpya ambayo imeingiza na ardhi kuwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ukaguzi wa ardhi ambalo limetolewa na Mheshimiwa Mdee, lakini na hapa mmeliongelea. Niseme Wizara ilishaanzisha kitengo kinachoshughulikia ardhi kwa ajili ya uwekezaji na pia imeziagiza Halmashauri zote nchini kufanya ukaguzi wa mashamba. Hii tunayofanya katika kunyang'anya baadhi ya mashamba ambayo yametelekezwa sehemu kubwa pia tutachukua ili kuweza kuwa na akiba ya

ardhi katika mtazamo huo kwa sababu siyo yote itakayogawiwa kwa wananchi na siyo yote ambayo watapewa tena wawekezaji lazima tutakuwa na sehemu ambayo itakuwa ni kwa ajili ya akiba kwa matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutolipwa fidia ambalo limezungumziwa na hasa wamezungumzia pia maeneo ya jeshi, walizungumzia maeneo ya Kaboya na maeneo mengine yako Mwanza, Ilemela na mengine yametajwa eneo la Kusini. Niseme Waziri wa Ulinzi wakati anazungumzia aliainisha vizuri kabisa namna ambavyo wanakwenda kulipa fidia katika ile migogoro ambayo wanatofautiana sana kati ya jeshi na watu. Kwa hiyo, niseme jeshi limeweka utaratibu wa kutambua mipaka yao na kujipanga katika kulipa fidia. Wameliweka wazi hili na nisingependa kulirudia kwa sababu tayari iko kwenye hotuba ya Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumziwa suala la wananchi wa Kata ya Kahororo kutolipwa fidia. Tukumbuke kwamba maeneo mengi ambayo yanachukuliwa na wawekezaji au taasisi mbalimbali suala la kulipa fidia linakuwa siyo suala la Wizara ya Ardhi ni la mwekezaji au taasisi inayochukua. Hili suala la Kahororo ni suala la Mamlaka ya Maji ya Bukoba ambapo thamani yake ni shilingi 1,961,609,000. Kwa hiyo, hizi zinatakiwa kulipwa kwa wale wananchi kwa kadri walivyothaminishwa katika uthamini uliofanyika mwaka 2014 kwa wananchi 186 na kiasi hiki kinatakiwa kulipwa.

Kwa hiyo, suala la ulipaji wa fidia lazima pia tuangalie ni nani anayehusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara ilishatoa Waraka kwamba hatutapokea jedwali lolote linalotaka watu waliofanyiwa uthamini kwa ajili ya kulipwa fidia kama hatutaridhishwa au kuhakikishiwa kwamba kuna pesa iliyotengwa. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Halmashauri zote wakileta madai yoyote ya fidia na wakitaka wathamini waende ni lazima tuwe tumejiridhisha kwamba kuna pesa imetengwa na watu watalipwa ili tuweze kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna maeneo ya *EPZ* ambayo nayo yanadaiwa fidia. Kuna baadhi ambayo yalichukuliwa na yalikuwa yanalipwa fidia kulingana namna fedha zinavyopatikana. Maeneo ambayo yamecheleweshewa fidia kwa muda mrefu Serikali itaangalia uwezekano wa kuyarejesha mikononi mwa wananchi ili yaweze kutumika kwa kazi nyingine kwa sababu imekuwa ni kero kubwa na wananchi wamekuwa wakilalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makampuni makubwa ya nje kuhodhi maeneo sehemu mbalimbali. Niseme tu Serikali inafanyia kazi orodha ya mashamba kama tulivyosema tayari tumeshaliweka katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia pia suala la Mabaraza ya Ardhi na hili limezungumzwa na Wabunge wengi kwa uchungu sana. Naomba niseme tu kwamba ni wazi kama ilivyozungumziwa Mabaraza ya Ardhi hayako ya kutosha lakini hayana watendaji wa kutosha na kesi zake zinakaa kwa muda mrefu. Niseme tu kwa mwaka huu tumepeleka maombi maalum kwenye Wizara inayohusika kuomba tupatiwe Wenyeviti kwa ajili ya Mabaraza hayo yatakayofunguliwa. Tutafungua Mabaraza 47 na tutaanza na matano. Katika kuyafungua Mabaraza hayo kuna maeneo mengine ambayo yanahitaji ushirikiano wa Wilaya husika kwa sababu shughuli ya kuwa na maeneo na ofisi kila mahali inakuwa na ugumu wake kulingana na rasilimali zilizopo. Hata hivyo, tumebaini mahitaji halisi ya Mabaraza haya kwa lengo la kuboresha na tayari vifaa mbalimbali vimeanza kupelekwa katika maeneo kusudiwa. Aidha, kuhusu watumishi kama nilivyosema tumewakilisha ombi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme katika suala la Mabaraza ya Ardhi naomba tu tuwe na imani kwamba tunakwenda kulitatua tatizo hilo muda ambao si mrefu kuanzia sasa ili wananchi waweze kupata haki kwa wakati. Pia tutaangalia katika zile Wilaya kama watakuwa hawajapangiwa kuwekewa Baraza ambapo unakuta Wilaya moja inahudumia Wilaya zaidi ya tatu au nne, tutaangalia ni Wilaya gani ambayo ina kesi nyingi na inahitaji huduma hiyo kwa haraka. Kwa hiyo, tutaangalia badala ya Mwenyekiti kuwa katika eneo ambalo halina kesi nyingi basi itabidi tumhamishie katika eneo ambalo lina kesi nyingi ili aweze kuhudumia na atakuwa anakwenda kama *visiting chairperson* kwenye lile eneo kwa maana ya Mwenyekiti wa Baraza. Kwa hiyo, tuseme tu kwamba hili tutalifanyia kazi kulingana na namna ambavyo tutakuwa tumeyapata. Kwa hiyo, tunaanza na hayo ambayo tayari yapo matano, lakini yale mengine 47 yote yako katika mchakato mzuri wa kuweza kuyaanzisha, kote tutakwenda kuanzisha kama ambavyo tumesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *National Housing*. Kambi ya Upinzani kwenye hotuba yao nao wamelizungumza, lakini wachangiaji wengi sana pia wamezungumzia suala hili na wamezungumza kwa uchungu sana. Niseme walikuwa na haki ya kuyasema hayo yote kwa sababu *National Housing* ni kioo cha jamii na ni shirika pekee baada ya uhuru linafanya vizuri zaidi kuliko mengine yaliyoanzishwa kipindi hicho na mtakumbuka lilianzishwa mwaka 1962 baada tu ya uhuru. Kazi wanayoifanya sasa na wote ni mashahidi, mmeweza kusifia msimamizi wa shirika hilo lakini tuseme pongezi hizo zinaenda kwa watumishi wote katika idara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamezungumza sana kwamba nyumba zinazosemwa ni za gharama nafuu si za gharama nafuu. Naweza kukubaliana na wanachozungumza kwa sababu ya hali halisi ya namna ambavyo *National Housing* wanavyopata maeneo yale na namna wanavyohangaika na miundombinu. Kama Wizara tumetoa maelekezo,

tumesema kama *National Housing* sasa wanataka kujenga nyumba za gharama nafuu ni lazima waendelee kuwa wabunifu, waendelee kufanya utafiti kuweza kujua ni kwa namna gani watajenga nyumba za gharama nafuu kwa kuangalia vifaa. Achilia mbali lile suala la *VAT* ambalo tumelizungumzia, hili bado tunalizungumza Kiserikali kuweza kuona ni jinsi gani *VAT* itakuwa *waved* ili waweze kupata nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa sasa hivi tunaloangalia ni namna ya kushirikisha taasisi zingine kama *TANESCO*, Idara ya Maji, Idara ya Ujenzi (barabara) ambao ni Halmashauri zenyewe, waweze kufanya maandalizi ya ile miundombinu mapema ili *National Housing* wanapokwenda kule basi waweze kufanya kazi kwa pamoja. Lingine pia Halmashauri zetu pamoja na kwamba tunalalamikia *National Housing* kutowafikia, lakini bado hatujawapa fursa ya kuweza kuja kupata maeneo ambayo yatapunguza gharama. Kwa sababu wakija pale *NHC* wanatakiwa walipe fidia, watengeneze miundombinu hiyo, tumewaambia wajipange vizuri na wafanye *networking* na mashirika mengine ambayo yanashughulika na huduma nilizozisema ili waweze kuona ni jinsi gani hizo nyumba zitapungua gharama kulingana na namna ambavyo wamejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa *NHC* wameshafikia Halmashauri 25 na wameshajenga nyumba ziipatazo 1,076 kwa maana ya zile za gharama nafuu. Kwa hiyo, niseme kwamba wapo katika utaratibu ambao unakwenda sambamba na mahitaji jinsi yalivyo ili kuweza kuona wanafikia wananchi kutegemeana na hitaji la Halmashauri. Niwaombe Halmashauri ambazo ziko tayari katika hilo basi waweze kuwapa nafasi ya kuweza kufika katika maeneo haya na kuwapa maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia hati za kimila kutotambulika. Naomba niwataarifu tu Waheshimiwa Wabunge kwamba hati za kimila kuna Benki ambazo tayari zinazitambua na zinapokea. Ttunayo benki ya *CRDB, TIB, Exim Bank, NMB, Meru Community Bank* ambazo tayari zimeshazitambua hizi hati za kimilila na zinatoa mikopo. Niseme haya yote yanafanyika na bado Serikali inaendelea kuongea na taasisi za fedha ili waweze kuthamini na kutambua kwamba zile hati ni hati ambazo zinahitaji kutambulika kama ambavyo benki zingine zimeanza kuzitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia masuala ya upangaji miji na huduma za jamii katika maeneo mbalimbali. Uvamizi wa maeneo bila kuwa na mipango mizuri ya matumizi bora ya ardhi hatutafika. Kama tulivyosema ni asilimia 15 tu ya ardhi ambayo imepangwa lakini ni jukumu pia la Halmashauri zetu kupima ardhi. Halmashuri zetu zinapaswa kutenga bajeti kidogo kidogo angalau wakapima kwenye maeneo yao. Tukikaa tukisubiri Wizara tutafanya kazi hiyo lakini itatuchukua muda mrefu.

Kwa hiyo, niombe Halmashauri zetu ziweze pia kuchukua wasaa wa kuweza kuyapima yale maeneo na kuweka matumizi bora ya ardhi ili kupunguza migogoro hii ambayo ipo. Kwa sababu kama tutaachia Wizara, kazi itafanyika kama tulivyoanza katika Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi lakini tumeona kwamba huu ni mradi wa miaka mitatu ambayo ni mingi sana tutafikia vipi maeneo yote kama mlivyosema. Niseme hilo ni la kwetu sote tushirikiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutokuwa na Maafisa Ardhi Wateule, Halmashauri pendekezeni majina ya wale ambao wamefikia sifa hizo, mlete kwa Kamishina. Kwa sababu tayari tunao Makamishna Wasaidizi kwenye Kanda nane, watafanya kazi ya kuwateua watumishi hao ili waweze kufanya kazi hiyo.

Suala la upungufu wa watumishi bado tunalifanyia kazi kama nilivyosema pia tumeomba watumishi wengine waweze kuongezwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mambo yaliyozungumzwa ni mengi ambayo yanahitaji pia kuwa na utulivu katika kuweza kuyapitia moja baada ya lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo nataka kusema ni kwamba masuala haya na hasa ya upimaji na mipango miji, tuna *master plan* ambazo zimeandaliwa katika miji yetu ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam ambao ulikuwa umeharibika sana unaandaliwa upya kwa kuzingatia mpango kabambe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana tuwaelimishe wananchi wetu wasiwekeze katika maeneo ambayo watakuja kupata shida baadaye kwa sababu *master plan* zinakuwa zimeandaliwa lazima waangalie waweze kujua katika eneo lake katika mpango uliopo panatakiwa kujengwa nini? Kwa hiyo, kama ni suala la umilikishaji na uendelezaji aweze kuendeleza katika hali halisi ambayo ndiyo mpango uliopangwa ili asijepata hasara baadaye anaambiwa abomolewe kwa sababu amejenga kinyume na taratibu au hakuzingatia mpango mji kwa kule ambako tayari mipango miji imeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge wa Misenyi amezungumzia habari ya kupanga mji mzuri kule kwao. Eneo lolote ambalo wamejiandaa katika kuweka kamji kadogo kazuri katakakofuata sheria na taratibu walete, Wizara ipo tayari tutasaidiana pia na wenzetu wa *National Housing* kuhakikisha kwamba huo mji unapangika vizuri na unajengwa majengo mazuri. Hata kama siyo *National Housing* tutaangalia pia nani anaweza akafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge walilalamikia kuhusu ubovu wa majengo yanayojengwa na kulazimu kubomolewa. Naomba niwaambie, katika jengo lililobomolewa pale Dar es Salaam *National Housing* hakuwa amejenga yeye lilijengwa na mtu mwingine, majengo yote ya *Nationa Housing* yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, wale wanaotaka kuwa na miji mizuri bado msisite kutumia Shirika la Taifa ambalo linaweza likafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamejadiliwa lakini niseme haya ambayo nimeyadodosa tu kwa kuyapitia moja moja, kidogo kidogo bado niseme kwamba tutayajibu yote na Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa na yeye atajibu baadhi ya hoja. Niseme kwa wale wanaojenga maeneo yasiyofaa na kupatiwa huduma za maji, umeme na kadhalika, utoaji wa huduma kwa wakazi waliojenga maeneo hatarishi unafanywa na mamlaka na taasisi kwa kutoa huduma kwa msingi wa kibiashara na hata wale waliobomolewa ambao pengine walikuwa wana hati, Wizara ilishawaambia walete ili tuweze kutambua. Kama alikuwa na hati halali ya Wizara, tunajaribu kupitia na kuweza kuona tutawapa *alternative* ipi ya kuweza kuwapatia viwanja vingine. Habari ya kuwekewa maji, umeme isiwe ni sababu ya kujenga kwenye maeneo ambayo ni hatarishi. Wale wanafanya kazi zao kibiashara ukimwambia alete maji analeta kwa sababu anajua tu kwamba ni eneo ambalo anapeleka huduma. Kwa hiyo, niseme tupo pamoja katika kuhakikisha tunapanga miji yetu ili tuweze kuona kwamba ni jinsi gani tutakwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima ambalo tumesema ni la utatuzi wa migogoro ambalo Waziri wangu atalizungumzia kwa kirefu. Hili suala ni mtambuka na kama ambavyo tumelieleza tutakwenda kukaa pamoja na Wizara zinazohusika ambazo ni Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Maliasili na Utalii, Kilimo, Uvuvi na Mifugo na Maji tuweze kuona kwa sababu migogoro mingi imekuja kwenye Wizara lakini ukiangalia kitabu chetu tulikuwa tunaainisha pia kuona kwamba mgogoro huu utatatuliwa na Wizara ngapi, kama ni ya kwetu tumeonesha na Wizara nyingine anayofuatia tumeionesha. Haya yatafanyika katika utaratibu ambao utakuwa umewekwa vizuri ambao utatusaidia sisi sote kuepuka hiyo migogoro ambayo inajitokeza mara kwa mara na si lengo la Serikali kuweza kusema kwamba tuweze kuhatarisha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba haya yote tunayokwenda kuyafanya tunategemea zaidi ushirikiano wa Wabunge. Tayari kama Wizara tumeshawezesha kwa maana ya kupata zile nyaraka muhimu. Kwa hiyo, tunategemea pia mtakuwa ni sehemu ya utoaji wa elimu. Kwa sababu siku zote tunasema ardhi ni mtaji bila kufahamu sheria na kanuni zinazotawala ardhi bado itakuwa ni shida. Kwa hiyo, nyaraka hizo ni nyenzo mojawapo ambayo tumeitoa itakayotusaidia sisi sote, Wabunge pamoja na Waziri mwenye dhamana katika maeneo hayo ili kuweza kuona kwamba kazi hii tunaifanya

katika muda muda mfupi kwa kusaidiana na hatuzalishi migogoro mingine kwa sababu taratibu tutakuwa tumezizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kuwashukuru sana Wabunge kwa ushirikiano wao na Wizara. Baada ya kuwa tumepokea hoja na migogoro, Wizara itaishughulikia yote na baadaye tutaona namna bora ya kuweza kuona kwamba Taifa ambalo halina mgogoro linapatikana. Kwa sababu kazi tuliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha migogoro iliyopo inakwisha na tusizalishe mingine lakini ni mimi na wewe ambao tutakwenda kuhakikisha migogoro inakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimuachie Mheshimiwa Waziri aweze kuendelea kwa sababu najua kila ambalo limeandikwa litafanyiwa kazi na litakwenda kutolewa ufafanuzi kama ambavyo tumepanga. Nashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja mwenyewe una dakika zako 30.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe, lakini nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii kuanzia Jumamosi hadi leo. Najua kungekuwa na muda kwa hoja hii kila mtu angependa kusema. Kama wengi mlivyosema mtu unaweza ukachagua ukalala barabarani, unaweza kachagua nguo, chakula lakini hakuna mbadala wa ardhi. Kwa mujibu wa Katiba yetu na maisha yetu kila mmoja anahitaji ardhi kwa matumizi yake ya kawaida. Ndiyo lengo la Wizara yangu na Serikali kuhakikisha kwamba katika mpango kazi wetu wa miaka kumi ijayo tunataka nchi hii iwe imepangwa, imepimwa na imemilikishwa. Kila mtu anayestahili kuwa na ardhi awe amemilikishwa ili ardhi yake iwe salama, hilo ndio lengo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru sana na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Nataka niwaambieni msingi wa kazi yetu sisi kama Wizara tunaanzia pale kwenye kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais. Kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi alikuwa anasema na hata sasa anasisitiza kwamba kazi yetu sisi watumishi na viongozi wa Serikali ni kuwahudumia Watanzania wote bila ya ubaguzi. Hiyo ndiyo kazi yetu ya msingi na huo ndiyo msingi uliyojikita katika Wizara hii.

Kwa hiyo, mimi najua na ninyi wenzangu leo mmechangia vizuri mkijua ardhi haina ubaguzi. Ndugu zangu wapinzani mmechangia vizuri sana kuanzia Waziri Kivuli, wenzangu wa Chama Tawala wamechangia vizuri sana, kwa

msingi huo kwamba tunatambua na wote tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwamba tunatakiwa tutekeleze majukumu yetu bila ubaguzi na sisi kama Wizara ya Ardhi ndio *motto* wetu. Kwa hiyo, matatizo yenu yote mliyoyasema bila kujali yanatoka upande gani, sisi kama Wizara tutayafuatilia huko huko yaliko bila kujali ni Jimbo au Wilaya ya nini ili kuyatolea ufafanuzi, kote tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza zimetolewa hoja hapa kutoka kwenye Kamati yangu ya Maliasili na Utalii, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Injinia Nditiye ameunga mkono hoja na ametoa hoja nyingi sana hapa.

Moja, imetolewa hoja juu ya mfumo mpya ambao wengi mmeuzungumzia hapa wa *Integrated Land Management Information System*. Ndugu zangu katika menejimenti ya ardhi kisayansi ndiyo maana tumeamua kuingia kwenye mfumo huu ili kuondoa kasoro zote ambazo tumeziona na tumekuwa nazo katika miaka yote juu ya usimamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa taarifa kama ile niliyoitoa hapa kwamba mfumo huu siyo kwamba umekwama maana wengi nafikiri sikuwapa taarifa mapema kwamba hata yule mtekelezaji wa programu hii ameshapewa barua yaani ameshakuwa *awarded* na baada ya wiki mbili watakuja hapa Dodoma kusaini. Nimeagiza waje wasaini hapa mbele ya Mwenyekiti na Kamati yangu ili tuanze kazi ya kufunga mfumo huu ambayo itachukua si chini ya mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya kabrasha nililowapa kuna kakitabu kadogo, kameandikwa Mradi wa Kuboresha Sekta ya Ardhi. Wale waliopata nafasi bila shaka wamefunuafunua kidogo. Ukija kwenye ukurasa wa mwisho huku ndio unaonesha mfumo wenyewe utakavyokuwa. Kwa hiyo, tutaachana kabisa na mfumo tuliouzoea na makaratasi mengi na mafaili ya hovyo hovyo kwenye Wilaya, Wizarani na Mikoani, tutaingia kwenye masuala ya kisasa.

Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia wote wengi ambao wamezungumza kuanzia Kamati yangu na hasa Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa amezungumza sana kwa sababu alikuwepo kwenye Kamati iliyopita na wale waliosema tulikwenda nao Uganda na Ethiopia ni kweli lakini sasa zamu yetu imefika kwa hiyo nataka kuwatoa wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote wanaozungumza kwamba fedha haziko kwenye bajeti hii, someni hii, humu ndani mna dola zaidi ya milioni 25 kwenye miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezungumza habari ya upimaji na tatizo tulilonalo la vifaa vya upimaji kwenye Halmashauri, ukisoma hapa tuna fedha

nyingi, tumeshaagiza vifaa vya upimaji lakini hatutavipeleka Wilayani, tutavipeleka kwenye Kanda nane, tunataka Halmashauri zenye kazi ya kupima zikachukue pale kwenye Kanda wakapime bila malipo yoyote. Kwa hiyo, vifaa tunanunua na fedha ziko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezungumza habari ya *master plan* hasa ya Jiji la Dar es Salaam, ilikuwa mwezi uliopita ile ndege ya kupiga picha ya anga itusaidie katika kutengeneza *master plan* ingekuwa tayari, sasa hivi kwa sababu ya hali ya hewa wanategea tu. Hata hivyo, fedha ziko hapa kama dola milioni tatu hivi, tumeshamlipa *contractor* na hiyo ndege itapita angani kupiga picha za anga ambazo ndizo zitatusaidia kwa sababu hizi ndio *base map* za kutusaidia kutengeneza *master plan,* fedha ziko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ununuzi wa vifaa hata magari yako hapa. Huo mtandao wenyewe wa *ILMIS* mnaousema ni dola milioni 12, hamtaziona kwenye bajeti yangu kwa sababu hizi fedha zilionekana kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ukiacha hizi zinazosomwa, nataka kuwaondoa wasiwasi na dola zaidi ya milioni 25, ziko kwenye mfuko mwingine na siyo za leo ni kweli ziko kwa miaka miwili iliyopita lakini zitatumika kwa mafao ya Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaendesha zoezi la kukusanya maoni ya Sera ya Ardhi. Waheshimiwa Wabunge, katika kabrasha langu hilo nimewapeni bahasha fulani ina *flash*, ndani ya *flash* mle kuna barua nimeweka inayoonesha kwamba ndani ya barua ile kulikuwa na sera tatu.

Moja ya sera muhimu ambayo inazaa mikingamo yote ya haya mliyozungumza tangu asubuhi ni Sera ya Ardhi kwa sababu ndiyo imezaa Mabaraza ya Ardhi, sheria na kila kitu. Kwa hiyo, ili kuondoa mzizi wa fitina yote haya, ni muda mrefu sana kwa sababu tulianza kutengeneza sera ndiyo iliyotuelekeza kuwa na Sheria Na.4 na 5 ambayo wengine hapa wametoa mawazo kwa nini tuwe na Sheria mbili za Ardhi tuwe na sheria moja. Ndiyo iliyoanzisha hati za kimila na hati za kawaida na ndiyo iliyoanzisha Mabaraza ya Vijiji, Kata na Wilaya hayo yanayosiganasigana. Kwa sababu tunajua sasa ni muda mrefu umepita ndiyo maana tumeamua kuanzisha kazi ya kutafuta maoni ya wananchi juu ya Sera ya Adhi kuona ni namna gani leo baada ya miaka 50 hii tuweze kumiliki na kusimamia rasilimali ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndani ya bahasha ile kwenye kile wanachoita *flash disk* (kinyonyi), nawaombeni mnipe muda wenu kidogo Waheshimiwa Wabunge na ninyi nimewaleteeni *questionnaire* kubwa kidogo, dodoso kwenye kinyonyi nawaombeni sana, ninyi ni wadau muhimu sana katika marekebisho, shida zenu zote hizi zitakwisha tu kama tukishiriki kurekebisha sera halafu baadaye tupitie marekebisho ya sheria zetu. Kwa hiyo, naomba ndani

ya kinyonyi nimewapa dodoso m-*print* ili msumbuke kidogo mtoe maoni yenu humu mkipata nafasi. Nitafurahi Bunge likiisha mwezi wa sita mwishoni kila mmoja wenu anipe maoni yake juu ya anavyofikiri turekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimewapeni sera zote, ndani ya *flash* kuna sera tatu zote tulizonazo na tunatengeneza kwa mara ya kwanza Sera ya Nyumba. Hatukuwa nayo, tunarekebisha Sera ya Makazi na tunatengeneza na Sera ya Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani nimewapeni na Sera ya Nyumba na Sera ya Ardhi ili mpate nafasi Waheshimiwa Wabunge, najua mna majukumu mengi, lakini mtafunuafunua kidogo ili angalau m-*print* mtoe maoni, maana nyie ndio wadau muhimu. Ndani ya *flash* humo pia nimewapeni sheria 15 ambazo ndiyo zinasimamia utawala mzima wa ardhi, naomba mzisome.

Humu ndani kuna wasomi wengi, wengine wanasheria, wengine wazoefu tu, mambo ya ardhi, vita hizi na migogoro hii imetufundisha kusoma vitu vingi. Kwa hiyo na zenyewe kama mnafikiri kuna sheria fulani fulani zinakinzana au haziendi vizuri, someni tupate msingi wa kuzibadilisha. Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge na nitawashukuru sana kama mtanisaidia kurekebisha haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda hautoshi lakini nije kwenye suala la ujenzi holela limezungumzwa sana. Najua Serikali peke yake zamani ndiyo ilikuwa na jukumu la upimaji na upangaji hatukupanga na kupima vya kutosha. Kwa hiyo, wananchi wametutangulia na wamejenga wanavyotaka kwa sababu hawawezi kutusubiri. Sasa tumeanzisha programu ya kupanga na kupima kwenye miji na vijiji, lakini kazi hii lazima tushirikiane kwa sababu ni kazi ya msingi ya Halmashauri zetu, ndiyo wenye ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi mmezungumza habari ya kupanga hata kwenye vimji vidogo, anayeamua mji mdogo upangwe ni ninyi Halmashuri ya Wilaya, mnaamua kwamba mji huu tunataka tuupange, mnaniletea mimi natangaza kwenye Gazeti la Serikali kwamba sasa Waziriameridhia kaeneo fulani ka Tarime kapangwe kama mji mdogo; kama Mheshimiwa Esther anavyoomba, kwa hiyo leteni maombi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hamna uwezo wa kupanga sisi tutawasimamia na kuwasaidia watu wenye uwezo wa kupanga tunao wasomi wengi mitaani. Hivi sasa tumeanzisha kampuni 58 za wataalamu. Tuna wataalamu waliobobea kwenye masuala ya mipango miji wapo mitaani, tumeamua waanzishe kampuni za wataalamu wa kupanga na kupima tumezi-*register* ili ziwe mbadala ya shida ya wapangaji, wapimaji wa Halmashauri,

ambao kwanza ni wachache lakini uzoefu wangu nao mara nyingi sana wapimaji wa Halmashauri hawafanyi vizuri kwa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mahali popote kwenye mchoro ambao tumeupitisha sisi ambao una viwanja 1,000 ambapo Wapimaji wa Ardhi wa Halmashauri yoyote wamepima wakavikabidhi Halmashauri viwanja 1000, lazima 100 watavikata. Kuondoa shida hiyo, kwa sababu vifaa tunavyo vitakuwa kwenye Kanda, tumeamua kushirikisha makampuni binafsi yatakuja kupanga, yatapima, umilikishaji utakuwa jukumu lenu Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda hautoshi kueleza, lakini *concept* hii nitaieneza nitakapopita mikoa yote mikoa yote kuelezea juu ya migogoro na namna ya kutatua na tutapanga hizi kampuni kwa mikoa ili zisaidie katika kupanga miji midogo midogo ili nayo isianze kujitanua kama *squatter* hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunao mpango mwingine wapangaji hawa watakuja kuwafundisha zaidi; tumeshawafundisha, lakini Halmashauri tunataka sasa zijikite katika urasimishaji wa maeneo ambayo tayari yameshakuwa *squatter.* Hatuwezi kuyavunja yale watu wameshajenga. Kwa hiyo tunakuja kuwafundisha tunawaelimisha na tutatumia kampuni za watu binafsi kurasimisha makazi ili watu wanaoishi kwa makazi yanayoitwa si salama waweze kumilikishwa hati zao, miundombinu ipite wapate hati zao waweze kukopesheka. Kwa hiyo hayo ni mambo tunayokuja kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa hati. Hati za kimila zinakopesheka kwenye kitabu changu nimesema na ninawashukuru sana benki ya *TIB, Exim, CRDB* na *NMB* wanakopesha na *NMB* ndiyo benki iliyopo kila mahali. Niambieni kama kuna mahali wamekataa kukopeshea kwa hati ya kimila, wanakopesha. Sasa nasema ushauri wenu nitaongeza nguvu ili mabenki mengine mengi yaweze kukopesha kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutaongeza kasi vilevile ya upimaji na upangaji kwa kushirikiana na Halmashauri lakini kushirikisha kampuni nyingine ambazo hazitatoza hale kubwa, kwa sababu utozaji wa makampuni hawa mengine yanayoingia mikataba kama ya Bukoba na mahali pengine wameingia mikataba hata Lindi na wapimaji binafsi matokeo yake viwanja havinunuliki. Kwa hiyo Wizara yangu vile vile itajikitakatika kutoa bei elekezi ya upangaji wa bei za viwanja ili watu wasijiuzie wanavyotaka. Leo tumesimamisha uuzaji wa viwanja vya Temeke kwa sababu tumekuwa nao, Mheshimiwa Mbunge yupo hapa; yaani mtu anapima tu ardhi gharama ni shilingi 2000 kwa upimaji wa kiwanja halafu wanauza shilingi milioni 27. Haiwezi kuwa, ardhi hii haiwezi kuwa mbadala wa shida zenu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutasimamia upangaji lakini tutasimamia na kuelekeza viwango vya kuuza bei vinginevyo mnalilia tu miji ipangwe nani atanunua kiwanja shilingi milioni 27. Ikiwa Wizara ya Ardhi inakopesha milioni 20 kwa mfanyakazi wa kawaida kukopa, kiwanja milioni 27 utapata wapi?

Kwa hiyo, nawaomba tusimamie. Wenzenu kule Halmashauri wana ingiza vitu ingawa hapa nimeona wengi mnasema gharama ya viwanja ni kubwa upimaji na hela zinakwenda wapi, hizi hewa zinajazwa kule. Kwa kuwa huwa hamshiriki mshiriki vizuri kuhoji gharama hasa hasa mliyoingia Halmashauri ya kupanga ni shilingi ngapi, kupima ni shilingi ngapi. Basi hata faida weka *ten percent, twenty percent*.

Mtu mmoja Halmashauri ya Jiji mmoja ambaye tumemfukuza, ananiambia mzee hapa bwana tumepata katika hii orodha ya viwanja hivi tumepata faida shilingi bilioni saba. Unawezaje kupata bilioni 7 kwa viwanja vya mkupuo 1500 ulivyopima kwa wakati mmoja? Lazima hizi shilingi billioni saba umewanyonya sana wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kuwaagiza halmashauri zote msifikiri ardhi ni suala la kujitajirisha tu. Na hata sasa nimezuia, ni marufuku kwa kampuni binafsi kwenda kununua mashamba na kujipimia viwanja, marufuku, haiwezi kuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani leo Bagamoyo unaenda unanunua shamba heka kumi, kesho umebadilisha matumizi viwanja haiwezi kuwa. Kwanza ukibadilisha shamba kwenda matumizi ya viwanja umepandisha hadhi halafu unapima viwanja. Leo kuna mtu pale wamempa hati 600 za kwake binafsi kwa jina lake kwa sababu ni shamba lake amepima ameweka majina yake. Sasa ni marufuku mtu yeyote aliyenunua shamba litabaki shamba, ukitaka viwe viwanja kabidhi Halmashauri ndio wata *deal* na mimi kubadilisha matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu binafsi umenunua shamba ukilenga kwamba unataka kupima viwanja imekula kwako. Kabidhi hilo shamba Halmashauri itapanga, itapima, itamilikisha yenyewe, kwa sababu nimeona sasa watu wanakuja na *briefcase* zao wanatajirika kwa mashamba yetu kwa kupima viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie kidogo aliyoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya fidia. Jamani fidia ipo kwa mujibu wa sheria, someni sheria sitaki kufafanua zaidi na tumeshasema kwamba ukiukwaji huo basi. Kama kuna mtu anataka kuchukua ardhi hata kwa maendeleo tenga fedha kwenye bajeti. Huo ndio msimamo wa sheria ambao hauna pande mbili ni upande moja tu,

iwe ni kwa maendeleo au kwa huduma. Tenga fedha kwenye bajeti, nunua hilo shamba, fanya unachokitaka, huo ndio msimamo wa sheria. Mkitaka basi njooni mbadilishe sheria hapa ili iseme kwamba ardhi ichukuliwe bure kwanza au ikopwe halafu ndipo ifanye shughuli, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo msimamo wa sheria ni huo na wote mnaochukua hayo ni lazima mfuate sheria. Mimi najua Halmashauri nyingi zimechukua maeneo ya watu wamepima viwanja, wanauza viwanja. Lakini angalau huyo mtu uliyechukua shamba ajue atalipwa kiasi gani aishi kwa matumaini. Lakini msiwe na hofu hata hao wanaocheleweshwa kulipwa fidia inabadilika kwa mujibu wa sheria kwa sababu ukichukua eneo la mtu bila kulipa fidia kwa miezi kadhaa inatozwa *interest*. Kwa hiyo, wale wote ambao wanafikiri hawajalipwa fidia kwa sababu maeneo yao yamechukuliwa na taasisi fulani fulani wajue wameweka fedha benki watalipwa na *interest.* Kwa hiyo, wasikate tamaa siku ambapo watalipwa, watalipwa pamoja *interest* kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Ndugu zangu mmezunguza sana habari ya migogoro ya ardhi. Kwa ufupi sana nataka niseme wale ambao wameniandikia nawashukuru na wengine wameboresha, tutajipanga. Wizara yangu peke yake haiwezi tutajipanga ndani ya Serikali Wizara zote zinazohusika na Maliasili, maana mimi sisababishi migogoro wanaosababisha ni watumiaji wa ardhi yangu. Kwa hiyo, tutajipanga na wenzangu TAMISEMI, Maliasili, Kilimo ili angalau tushirikiane tujipange tuifikie mpaka migogoro ya mipaka ya kijiji na kijiji. Tutajipanga na tutakuja kwenu, nataka kuwahakikishieni tutafika kote tutajipanga na wataalamu wetu ili tufike tuisome. Kama ni marekebisho ya mipaka tutafanya, kama ni ramani tutasoma, kama ni marekebisho ya jambo lolote tutafanya, kwa sababu Serikali ni moja na Mheshimiwa Rais ameagiza katika miaka mitano hii lazima tuwaondolee machungu wananchi, tuondoe migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, kwa *motto* huo tutafika huko kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lwakatare amezungumza mengi sana lakini asishike shilingi yangu. Najua matatizo yake ya Bukoba ni makubwa, lakini kama tulivyoongea *Chief Valuer* wa Wizara yangu Evelyine baada ya Bunge hili pamoja na Kamishna wa Ardhi wa Kanda wanakuja Bukoba. Kuna mgogoro wa viwanja 5,000, sasa wanakuja kwa sababu tulishaelekezwa na Waziri Mkuu, wewe umeandika lakini sisi tulishaelekezwa na Waziri Mkuu kwamba lazima TAMISEMI na mimi nipeleke. Kwa hiyo, mimi napeleka watu wawili, lakini atakwenda na mtu wa TAMISEMI kuhakikisha kwamba mgogoro wa Bukoba sasa tunautafutia dawa *once and for all,* kwa hiyo, tunakuja huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nassari kwanza yale uliyoyasema naomba radhi sana, yale yalioandikwa kwenye kitabu wamekosea, yale mashamba yote yalishafutwa.

Sasa wewe na mimi tunajua, nimehangaika sana ili mradi sasa unataka nije nikae nyumbani kwako wiki mbili nitakuja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulishahangaika sana nimetumia fedha zangu mpaka nimetoa shilingi milioni 271 za kuja kupanga vipande vidogo vidogo kwa kumilikisha wananchi wako wenye shida kutoka kwenye mashamba hayo. Lakini watendaji wangu wa upande ule wameniangusha, hawajafanya. Nimefanya sana na *Arusha DC* anajua nimempa watu wake 4,000 nimewapa vipande kwenye mashamba ambayo tumefuta, lakini hawajapanga kwa sababu sielewi wamenipa taarifa na fedha zangu za kupanga walikuwa hawana Halmashauri ya Arumeru na *DC* nimewapa 271 ya kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Ndugu zangu, Chuachua wa Masasi kwanza ngoja nijipongeze mwenyewe pale unaposema tumejenga nyumba za *National Housing* nilikupa na *bonus* ya zahanati ila haukusema.

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Eee! Chuachua pale, nilikupa *bonus* ya zahanati lakini hukuisema, wewe umezungumzia fidia tu. Lakini nataka kuwahakikishia watu wote, wa Dar es Salaam mmezungumza kwa uchungu sana juu ya migogoro yenu yote, Kazimzumbwi tunaenda kuimaliza Alhamisi, tumeshaelekezwa na Waziri Mkuu mimi na Mheshimiwa Maghembe tunakwenda Dar es Salaam tunaenda kumaliza shughuli ya Kazimzumbwi haitakuwepo tena, tunamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumza, rafiki yangu wa Siha naye amezungumza sana, lakini wewe mambo yako lazima tufike kule tumalize. Mzee wa Karagwe nakumbuka umezungumza sana, Mzee wa Efatha kule Malocha, wazee wa Sumbawanga kule wamezunguza sana habari ya Efatha. Efatha jamani sio jina la mtu maana mnazunguza hapa ni taasisi ya dini naona mmezungumza Efatha sana. Lakini nataka kuwahakikishia ndugu zangu wa Mkoa wa Rukwa, *issue* ile ya Efatha ipo mahakamani, siwezi kuizungumza sana, mimi nitakacho kifanya nitaimarisha nguvu ya mwanasheria wenu wa Sumbawanga ili kumsaidia ili kuharakisha ile kesi iishe haraka. Lakini dhamira ya Serikali ya kutwaa lile shamba iko pale pale, na madhumuni yake ni yale yale. Kwa hiyo, Mzee Malocha nafikiri umenisikia hapo. *(Makofi)*

Ndugu zangu mmechangia watu wengi waliochangia kwa maandishi mpo 57 naomba sana niwashukuru katika hoja hizi mbalimbali nilizozungumza hizi za mwanzo, Waheshimiwa waliochangia hasa hasa kwa kusema ni wengi lakini namkumbuka zaidi ndugu yangu Julius Laizer ambaye alifoka sana.

Nataka kukuhakikishia kwamba yale uliyoyasema nakubali kwamba lile shamba la Makuyuni lazima lirudi kwa wananchi. Lile shamba lilipangwa liende kwa wananchi na litarudi kwa wananchi. Ila ujue inakula kwako kwa sababu aliyejimilikisha hili shamba ni Edward Lowassa, nilitaka kukupa hiyo taarifa tu hapo umeingia pagumu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili lilidhamiriwa na Rais Mkapa wapewe wananchi, lilikuwa shamba la Stein Seed Vallay wanaokumbuka historia ile aliyefukuzwa na ndege na kila kitu..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wasiliana na kiti.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Naam, Mheshimiwa Waziri wakati ule akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alisisitiza kwa Mheshimiwa Mkapa kwamba shamba hili naomba sana wapewe wananchi na vijiji vile wameshaniandikia mimi. Lakini bahati mbaya sana hati niliyonayo hapa imesainiwa na Mheshimiwa Lowassa. Kwa hiyo, mimi nakusaidia wewe kwamba hati hii tutairekebisha yeyeto aliyesaini hapa tutarekebisha na ardhi hii itarudi kwa wananchi. Nakushukuru sana tumeshirikiana kwa mengi na hili tutalimaliza na lazima tushirikiane mimi na Halmashauri ya Monduli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa amezungumza kwa uchungu sana, Mheshimiwa Augustino Masele huyu leo amefunga bao la pili maana hata Jumamosi alichangia. Mheshimiwa Chatanda nasema hawa wote ambao wamezungumza hoja zinazofanana Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mheshimiwa Rashidi Mohamed Chuachua, Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mheshimiwa Sixtus Mapunda, Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mheshimiwa Riziki Mngwali, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mheshimiwa Maulidi Mtulia, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Massay, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mheshimiwa Kiteto Koshuma,

Mheshimiwa Kunti, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Dkt. Godwini Mollel, Mheshimwia Zainab Katimba, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Emmanuel Papian, Mheshimiwa Agustino Masele *again*, Mheshimwia Rose Tweve na Mheshimiwa Juliana Shoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia waliochangia hoja hizi, Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Sixtus Mapunda, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hizi nimezijumlisha zote na majibu yake ndiyo hayo kwamba ndugu zangu hawa ndio wamechangia kwa kusema, lakini wapo waliochangia kwa maandishi na hoja zinafanana. Ninachoomba tu Waheshimiwa Wabunge mnivumilie. Najua hata mdogo wangu pale Mbunge wa Mikumi ananiangalia hajasema sana lakini huko nje anasema sana. Najua ndugu zangu mnaniangalia sana, lakini mengi mnasema hata nje huko tumeongea mengi sana. Nimewataja majina hapa ili wajue wananchi huko kwamba hawa wamechangia kwa kusema. Lakini pia zipo hoja hapa ambazo nitazizungumza zimezungumzwa na hawa wafuatao lakini kwa kuandika, wasije wakasema hawa wabunge wetu ni mabubu hawakusema, hapana upo utaratibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo waliochangia hapa kwa kuandika vilevile. Hoja hizi ni hizi ambazo nitazisoma baadae lakini waliochangia ni Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Mussa Sima, Mheshimiwa Juma Hija, Mheshimiwa Silafu Maufi, Mheshimiwa Halima Mohamedi, Mheshimiwa Risala Kabongo, Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani, Mheshimiwa Aida Joseph, Mheshimiwa Shabani Omary na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni, Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Paschal Yohana Haonga, Mheshimiwa Saumu Sakala, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa William Olenasha, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Haji Kai, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Bhagwanji, Mheshimiwa Frank George, Mheshimiwa Mbarouk Salim, Mheshimiwa Maftaha, Mheshimiwa Gibson, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Daniel Nicodemus, Mwenyekiti pia umechangia na lile shamba lako nitalifuatilia. *(Makofi)*

Waliochangia wengine ni Mheshimiwa Daniel Nicodemus, Mheshimiwa Constantine Kinyasi, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Ally Ungando, Mheshimiwa Joseph Haule, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Willy Qambalo, Mheshimiwa Pascal Yohana, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Esther Matiko, masuala yako ya upimaji wa Mji wa Tarime nimeyazungumza hapa.

Wengine ni Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Mpakate Daimu Iddi, Mheshimiwa Davidi Silinde, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kuwashukuru sana benki ya dunia kwa msaada mkubwa sana wa fedha nyingi ambazo hazikuoneshwa hapa lakini zilipitia Ofisi ya Waziri Mkuu ambazo matumaini yangu ni kwamba mwakani mnaweza mkaona vitu fulani fulani kwa macho ambavyo vimefanywa kutokana na fedha ambazo hazikuombwa kwenye bajeti yangu. Bajeti yangu inaonekana nyepesi sana, lakini kuna fedha ambazo zipo kule kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama nilivyosema zaidi ya dola milioni 25, hazijafanya kazi ya kutosha lakini katika kipindi cha mwaka huu wa fedha mtaona matokeo yake. Nawashukuru sana Benki ya Dunia.

Katika mradi huu wa awali wa kupanga, kupima na kumilikisha Wilaya tatu wenzetu wa Denmark, Sweden na Uingereza wanatusaidia sana nawashukuru sana nao. Lakini nawashukuru sana watu wa Benki Kuu ya Tanzania ambao wanasimamia sana masuala ya *mortgage finance,* tunashirikiana nao nazishukuru na benki zote 29 ambazo zinashiriki katika utoaji wa mikopo ya nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa uchache niwashukuru hao na kwamba tutaendelea kushirikiana nao. Kuna hoja nyingine ambayo imetolewa hapa kuanzia Bunge lililopita la uanzishwaji wa *Real Estate Development Authority.* Tunajua ujenzi wa majumba sasa na biashara ya majumba imekuwa kubwa, kwa hiyo tumeamua sasa tutaleta sheria hapa Bungeni. Imeulizwa sana kuanzia Bunge lililopita Bunge hili la mwaka huu tutaleta sheria ili angalau nchi iweze kutambua na kusimamia sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naommba nirudie tena kuwashukuru kwanza Kamati yangu nataka kusema Kamati yangu kama wenzangu mmepata Kamati mimi nimepata yakwangu nzuri sana, ina watu waliotulia, ingawa wengi wageni lakini ni watu wenye uzoefu na waliotulia wanatoa ushauri mzuri, nawashukuruni sana. Sikusema mengi kwa sababu ninyi mkisema

kwangu ni maagizo, kwa hiyo maagizo yenu na maelekezo yenu nitayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la *KDA* ndugu zanguni mnajua tulikotoka, tulikofikia, sasa naomba ushauri wenu huo, nimeupokea lakini narudi ng'ambo kule Kigamboni nikakae na wadau wa *KDA,* wananchi wa Kigamboni ili tuzungumze tuelewane alafu tunashauriana ndani ya Serikali *the way forward.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwahahakishieni, hakuna pesa humu lakini mimi ninazo shilingi bilioni saba tulikuwa hatujazitumia kwenye bajeti hii kwa ajili ya kuanza kulipa fidia ya watu wachache ambao wapo barabarani. Haziko hapa kwa sababu ziko kwenye bajeti hii ninazo ziko kwenye Mfuko wa Amana na Waziri wa Fedha anajua tunazo sio kwamba, pale hatufanyi, hatufanyi tu kwa sababu hatujamaliza kazi ya kuainisha lakini hatujaenda kujadiliana na wananchi wa Kigamboni juu ya utaratibu wa ulipaji wa fidia na kiwango cha fidia maana huwezi kuwashtukiza. Kwa hiyo kuna kazi inaendela kule. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na kwa watu wa kigamboni; madiwani wote wa Kigamboni wameshaniandikia barua niende kwao kwa sababu mambo haya huwa tunaenda hatua kwa hatua, tunazungumza na tunaelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo nataka kuwahakikishia wenzangu wote wenye hofu ya Kigamboni muondoe hofu. Lakini ushauri wenu tumeuchukua. Ikiwa kunahitajika marekebisho fulani kwa sababu mlitunga sheria ya kuanzisha mamlaka hii tutairudisha hapa ili mfanye marekebisho. Hata kama ikiwa ni kufuta tutairudisha ili tuifute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishieni kwamba, tunazo fedha tutafanya mambo machache. Kuanzini sasa kama nilivyoagiza, masuala ya utoaji wa hati katika eneo lile nimeyafungulia, wataanza kupata hati. Kwa sababu kwa miaka yote hii watu walikuwa hawaruhusiwi kupata hati na kupata vibali vya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, midhali sasa michoro imekamilika na yale wanayotakiwa kujenga kwenye *site* yao yanajulikana kwahiyo nimeshawaagiza wangu tuanze kutoa vibali vya ujenzi kwa watu wanaojenga kulingana na michoro inavyoelekeza katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wenye ardhi yao wapewe hati ili wapate nguvu ya ku-*bargain* na hao wawekezaji ambao watawekeza fedha katika maeneo hayo. Kwa hiyo, haya mawili nitayafanya lakini naomba nisiwapotezee muda mrefu nitazungumza na wadau wa Kigamboni kwa niaba

yenu nafikiri tutaelewana maana tumeshaelewana mambo mengi hapa nafikiri tunaenda vizuri.

Kwa hiyo, ndugu zanguni nataka nikiri kwa mbali, mambo mlioniandikia ni mengi, mambo mlionishauri kwa mdomo ni mengi lakini mengi ni migogoro. Msingi wa migogoro kwanza nataka mnisaidie marekebisho ya sera, ambayo itarekebisha hata sheria zijazo, lakini pili maana yake naomba mnikaribishe tunapiga hodi tutakuja Mkoa kwa Mkoa kusimamia utatuzi wa migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mniunge mkono mnipe pesa hizi ili angalau nianze safari hata kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu!

**NDG. CHARLES J. MLOKA – KATIBU KAMATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 3 - Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi**

Kifungu 1001- *Finance and Administration Division*…...........Sh. 1,511,244,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uwe unawahi mna uzoefu, haya Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru mimi nilihitaji kupata ufafanuzi wa kijifungu kidogo cha 220700 cha *Rental Expenses* ambacho kimetengewa shilingi milioni 240. Kama kuna mahali tunapoteza fedha nyingi ni katika kulipa pango, ofisi mbalimbali na Wizara hii ni ya Ardhi ambayo Mheshimiwa Waziri ana ardhi ni kiasi cha kujenga, na hizi ofisi zisipoteze fedha nyingi sana ilhali tuna pesa nyingi za fidia tunazitafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini fedha hizi bado zinatengwa shilingii milioni 240 kwa ajili ya pango, ni pango la namna gani hamuwezi mka-*accommodate* hii ofisi katika majengo yenu ambayo sasa yapo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ushauri huo alitupatia kwenye Kamati na tumekubaliana tutazingatia kuanzia mwakani, tumeamua tutafute fedha hata kwa kushirikiana na *National Housing* watujengee jengo moja ili angalau tuendelee kutenga bajeti katika Idara mbalimbali zinazokaa nje tulipe mpaka jengo liwe letu, kwa hiyo tutatekeleza katika bajeti ijayo. (*Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Physical Planning Division*...........Sh. 143,655,000
Kifungu 2002 - *Landuse Coord,*
*Comm. and Policy Division*..............Sh. 45,912,000
Kifungu 2003 *Research and*
*Documentation*………….………..Sh. 46,090,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kifungu 1001- *Administration and*
*HR Management*……………..…...Sh. 6,755,910,000

**MWENYEKITI:** Ninaelewa nina majina hapa kulingana na uwiano wa vyama. Ninao Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Richard Ndassa. Tuanze na Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali, Shirika la *National Housing* ni shirika la Serikali ambalo linatakiwa kuwahudumia wananchi wote bila kubagua uwezo wao wa kifedha, na mimi nalipongeza sana kwa huduma nzuri na kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba Waziri leo aniambie kwamba Shirika hili linajenga nyumba kwa gharama nafuu kwa ajili ya kuwakopesha wafanyakazi wa hali ya chini, wafanyakazi wa ngazi ya chini ambao pia wanatamani kuwa na uwezo wa kumiliki nyumba. Lakini nyumba za *National Housing* zinauzwa kwa bei ghali sana. Na nyumba ya vyumba viwili maeneo mengine wanauza shilingi milioni 52, mwalimu anayepata mshahara wa laki nne

atamiliki nyumba ya shilingi milioni 52 lini? Nadhamiria kutoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri kama sitapata majibu ya uhakika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru muuliza swali Mheshimiwa Bura kwa swali lake. Ni kama wakati tunatoa maelezo, ni kweli kuna malalamiko mengi kuhusiana na bei hiyo, lakini tunayo ile taasisi yetu pia ambayo inafanya kazi ya utafiti kwa ajili ya gharama ya vifaa vya ujenzi ili kuweza kurahisisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hiyo itashirikiana na *National Housing* kuweza kuona ni jinsi gani gharama zitapungua. Lakini hata *National Housing* wenyewe tumewaambia wafanye kazi ya ziada kuweza kuangalia kwa sababu hali halisi inavyoonyesha mtu wa kawaida kama alivyomtolea mfano hawezi kumudu kwa sababu ya bei ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, ukiangalia bei ya nyumba za *National Housing* ukilinganisha na mashirika mengine yanayofanya biashara hiyo bado za *National Haousing* ziko chini. Hiyo kama haitoshi Wizara bado tunaongea na Serikali kupitia kwa maana ya Wizara nyingine hasa Wizara yenye dhamana ya fedha, Wizara ya Fedha tuweze kuona ni jinsi gani *VAT* kama itaondolewa. Lakini pia tunataka kuangalia namna ya kuangalia angalau kifaa kimoja kimoja cha ujenzi kama mabati pengine yaweze kuwekewa alama maalum yasiwe na *VAT* na yauzwe kwa ajili ya kujenga nyumba za gharama nafuu tu itakuwa ni rahisi. Kwa hiyo, hiyo ni sehemu mojawapo ambayo tunajaribu kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia taasisi nilizozitaja kama *TANESCO*, Mamlaka ya Maji na Halmashauri wenyewe, wakiweza kuchukua dhamana ya kuhudumia zile huduma zao za kupeleka umeme, kupeleka maji, kutengeneza barabara na kutoa maeneo ambayo angalau *National Housing* watalipa *premium* wasilipe fidia basi itakuwa imepunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo tuseme tunaliona hilo na tunalifanyia kazi na tayari tumeshawapa kazi hiyo *National Housing* waweze kulishughulikia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bura umeridhika?

**MHE. FELISTER A. BURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kwa sababu wanaposema kwamba wanafanya mazungumzo na Idara zingine wakati kuna walimu wanaokaribia kustaafu, kuna makarani wanaohitaji nyumba, kuna Maafisa Wauguzi wanaohitaji nyumba, lakini mishahara yao haiwaruhusu kukopa *National Housing* na shirika hili ni la umma kila mtu afaidi.

Sasa hivi nyumba zinauzwa pale Dar es Salaam shilingi milioni 300. Lakini ziko za *low cost* shilingi milioni 52 haiwezekani halafu Waziri ananiambia anatafuta sijui ujenzi wajenge barabara, umeme, madini wafanye hiyo ni kazi ya Serikali sio kazi yetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono, naomba kutoa hoja. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nitachukua wawili upande huu, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa John Heche. Tuanze na Mheshimiwa John Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na bahati mbaya mambo muhimu kama haya tunayajadili humu baada ya dakika mbili tunasema tumeondoa hili, tumeacha shilingi ipite *but* sina nia mbaya na kaka yangu Lukuvi anajua ninamheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kifupi utu wa mtu ni mahali anapoishi. Watu wetu wanaishi katika mazingira mabaya sana, walimu wanaishi katika mazingira magumu wanalitumikia Taifa hili kwa miaka mingi mishahara yao haiwawezeshi kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli ni sahihi kwa Serikali kuja na majibu rahisi kwamba tunaongea na Halmashauri sijui tunaongea na umeme, sijui tunataka kupeleka *subsidy* kwenye mabati, hivi hamjaona ili mpaka viinchi vidogo vinajengea watu wao nyumba, matokeo yake ni kudhalilisha watumishi na wanawatumikia ninyi watu ambao mko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwakweli mimi ninaomba Waziri toa *commitment* kwa mwaka huu mnampango wa kufanya nini ili shirika hili la kwetu lisiwe shirika la kibiashara liwe shirika kwa ajili ya kusaidia watu wetu kuishi. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kuna msemo unaosema kula nimekula lakini pa kulala wapi, nyumba ndio utu wa binadamu. Suala la hizi nyumba za *National Housing* tumelizungumza kwa kirefu, tukapendekeza walau vifaa vile viondolewe *VAT* ili basi gharama za nyumba hizo ziwe chini. Si leo ni miaka nenda rudi bado Wizara haijazingatia chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa nyingi alizopewa Mzee Lukuvi lakini kwa kweli suala la nyumba, suala la kuwezesha *National Housing* ni la msingi kuliko mambo mengine yote kuliko la Kigamboni, kuliko sijui la wapi, nyumba ndio uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba najua Mheshimiwa Lukuvi anafanya kazi lakini hili la nyumba bado hujatendea haki Watanzania. Kwa hiyo naunga mkono hoja ili Wizara sasa ijipange vizuri na itoe *commitment* ni kwa kiasi gani itahakikisha wananchi wake wanalala kwenye nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizi nyumba hata za bei nafuu wanaozinunua ni wale wenye fedha nyingi wanazi- *sublet,* hakuna Mtanzania wa kima cha chini ataweza kununua. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Felister Bura.

Mimi nataka kusema kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu amesema kwamba, ni kwa sababu ya *VAT*. Mimi ni mteja wa nyumba za *National Housing,* ninafahamu hata ubora na ukubwa wa nyumba zile ni tofauti kabisa na bei zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ukisema kwamba *VAT,* ukiondoa ile *VAT* bado gharama yake ni kubwa, kwa hiyo tunachosema suala la *VAT* ni lingine, lakini suala la kuwauzia wananchi wa kipato cha kawaida bado. Mwalimu angalia pale Singida nyumba zimejengwa hazina watu wa kwenda kuingia mle kwa sababu ya ile gharama, gharama ni kubwa Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona ukienda unataka kulinganisha na mashirika mengine, *is it* kwamba *National Housing* mnajenga kutoa huduma kwa wananchi au mnafanya biashara ili tujue moja. Hebu naomba utusaidie kama kweli mnataka kuwasaidia wananchi, hata ukienda Medeli pale huwezi kumkuta mwananchi wa kipato cha chini anakaa pale, tunakaa sisi Wabunge na wafanyabiashara wenye vipato vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba Mheshimiwa Waziri liangalie vizuri hili, ili tuwasaidie wananchi asante. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi labda nianze kusema kwamba namuunga mkono mama yangu Bura kwa hoja yake na nitumie fursa hii; mimi ni mmoja kati ya Watanzania ambao sikubaliani na dhana inayoitwa kwamba *National Housing* wanajenga nyumba za bei nafuu, hii ni *political statement* ambayo haina ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubali na sisi Waheshimiwa Wabunge tukiri kwamba *National Housing* ime-*turn around* kwa sababu inafanya biashara. Kwa hiyo, wanafanya biashara ni lazima walipe kodi, ni lazima walipe mikopo kwa hiyo *at the end of the day* hawa watu wana wajibu wa kutafuta faida ili wajiendeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tuwe wakweli, *I am against the business model* ya *National Housing* lakini *that is the reality* kwamba hiyo ndio hali halisi. Kwa hiyo, umewadia wakati sasa Wizara ya Ardhi ilete ndani ya Bunge hili *model* ambayo wataitumia kuifanya *National Housing* iweze ku-*provide* hiyo *service* ya nyumba za bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwalazimisha leo *National Housing* wauze hata hivyo hii *VAT* anayosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye nyumba ya shilingi 55,000,000 ukitoa asilimia 8 umetoa shilingi 9,000,000, kwahiyo ni nyumba ya shilingi 45,000,000 bila *VAT*. Lakini ili ainunue huyu mtu anakuwa *connected* na *commercial bank* akakope ambako huyu mtu atalipa *with interest,* kwa hiyo hakuna *civil servant* atakayefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ningeomba mama yangu Bura ili ni jambo sio la siku moja. O*n the other hand* Waziri atupe *commitment* ya kuja na majibu juu ya *mechanism* gani Serikali itamfanya Mchechu na timu yake waweze kujenga nyumba za bei rahisi kwa ajili ya *civil servant. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, lazima tuelewe hii ni hoja nzito lakini maana yake ni kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kutoa ruzuku, Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali hoja hii tunaitenganisha mara mbili. Hapa kuna hizo zinazoitwa *affordable house,* lakini pia kuna la pili la kumuwezesha Mtanzania kujijengea nyumba zake kwa gharama nafuu, yaani kupunguza bei au kupunguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi, kuna hoja mbili. Na katika ilani yetu tuna mambo mawili. Tumesema na tumeahidi kwamba tutahakikisha tunapunguza bei ya vifaa vya ujenzi, lakini pia tutajenga nyumba zisizopungua 50,000 za gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze hili la *affordable*. Kama si hili Bunge, sijipendekezi kwenu hii lugha mnayoizungumza ndiyo ambayo siku zote mimi huwa ninaizungumza. Kwa wale ambao mmewahi kunisikia kwenye kipindi chao kile kinaitwa sijui nini na nyumba, lakini huwa nawapasha humo humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshawakatalia kwamba achene kutumia *terminology* ya *affordable house* wakati hizi nyumba *is not affordable*, nimeshawaambia. Yaani lugha yenyewe inafurahisha *affordable, affordable* lakini *is not affordable*. Mimi nimewaambia ukinipa shilingi milioni 52 najenga nyumba mbili. Kwa hiyo nataka kuwahakikishieni ndugu zangu, kilichonifanya mimi kwenda kuzuia kuendesha miradi mingine mikubwa mpaka wanipe jibu wanakwendaje kujenga nyumba za gharama nafuu, *real* ni kwa sababu hiyo.

Kwa sababu nilitaka sasa Shirika la Nyumba lisijihusishe sana kwenye ajenda B, lijikite kwenye ajenda ya msingi ambayo ni ujenzi wa nyumba za maskini.

Kwa hiyo ndugu zanguni, Mheshimiwa naomba uniunge mkono. Bahati mbaya hatukuelewana tu lakini lugha unayozungumza na mimi huwa nazungumza hiyo hiyo. Mimi naamini, nimewaambia *National Housing* na nimewapa *time frame,* duniani wamebuni *technology* nyingi tu za ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Tusinag'ang'anie hizi *technology* za kufyatua matofali mpaka yaive kwa mkaa. Nimefanya maonyesho Dar es salaam ametokea mjasiriamali wa Babati ambaye anajenga nyumba ya shilingi milioni tisa, ametuonyesha pale. Nimeona *models* ndani ya nchi kuna nyumba zinajengwa shilingi milioni 11, shilingi milioni 20. Kwa hiyo, hii *assignment* nimeshawapa nataka kuwaambia niko makini sana katika hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tupe *commitment.*

**WAZIRI WA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwamba lazima watafute *technology* kokote duniani itakayoshusha gharama na mimi ni miongoni mwa watu ambao hawajali habari ya *VAT* kwamba itashusha gharama peke yake, haiwezi. Utajuaje kwamba hiyo *VAT,* vitu vingapi hapa nchini tumeviondolea kodi lakini bei hazijashuka?

Kwa hiyo, mimi siamini katika hilo, mimi nimesema naamini katika *technology* na ubunifu. Na nimewaambia mradi wa kwanza wa Luguruni nitakwenda kuuangalia hivi karibuni wameniambia wataanza kutekeleza zoezi hili na maagizo yangu, pale Luguruni Dar es salaam. Nisiporidhika nitaacha hizo nyumba zisijengwe mpaka niridhike nyumba kwa ubora lakini kwa *technology* na bei, hilo wanaliweza na wanakiri wameliweza. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Bura uniamini. Hili la vifaa vya ujenzi, bado tunalifanyia kazi ndani ya Serikali ili tuone tutatimizaje matakwa ya ilani yetu.

**MWENYEKITI:** Umetoa *commitment* hapo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani hii si bajeti huwa inakwenda miezi 12? Mpaka niseme tu. Mimi naomba tu Mheshimiwa Bura mwenye hoja, wewe rafiki yangu tumekaa Dodoma miaka yote unaniamini sana. *(Kicheko)*

Mimi nikisemanamaanisha na ndiyo maana mmenisikia hata kabla hamjasema mmeshanisikia nikienda mikoani huwa nalalamika na mimi hizo nyumba. Lugha yenu ndiyo lugha yangu na mimi ningependa maskini wa Tanzania wafaidike na Shirika hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia maelezo ya Mheshimiwa Waziri na nadhani kule kwake Isimani wako wafanyakazi wa ngazi za chini wanaotamani kukopa hizo nyumba, lakini wameshindwa kutokana na ughali wa nyumba zinazouzwa na *National Housing* ambazo ni *low cost* na kwa sababu Waziri amekubali kwamba atafuatilia, lakini hizi ambazo zimeshajengwa, kwa mfano, Kongwa zimesimama pale hazina mnunuzi naamini pia atatafuta namna ya kushusha bei ili wananchi waweze kununua hata Halmshauri zetu ziweze kununua nyumba hizo kwa ajili ya wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea utekelezaji na kwa sababu tuko wote hapa Bungeni, nafuatilia kwa makini sana suala hili, Mheshimiwa Lukuvi nakuaminia lakini nitaendelea kufuatilia, narudisha shilingi yako na naunga mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi niwapongeze *National Housing* kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini kubwa limesemwa na Mheshimiwa Bura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, na bahati nzuri Naibu Waziri amesema kwamba *National Housing* ni kioo cha jamii, lakini Mheshimiwa Waziri akaja akaongezea akasema ni vizuri kuhoji gharama, ametuagiza tukahoji gharama huko.

Sasa mimi natala kujua, kati ya miradi hii 64 ambayo iko katika mikoa 24, zimejengwa nyumba 4,990 lakini kati ya nyumba hizo *National Housing* wameuza nyumba 1,483 kwa gharama ya shilingi bilioni 133.84. Ningependa kujua, gharama ya uwekezaji katika nyumba hizo zote 4,990 ni kiasi gani maana yake tunalalamika kwamba gharama ni kubwa lakini kama uwekezaji ni mkubwa, huwezi kupata bei nafuu hata kidogo, sasa ningependa kujua, gharama ya uwekezaji hasa kwenye nyumba hizi 4,990 shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sijui, Waziri!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndassa naomba niombe radhi, kwenye kitabu hiki kuna maelezo mengi. Nataka kukwambia tu kwamba hizo nyumba 4,000 si nyumba zote za gharama nafuu, ni *units* zote zilizojengwa kwa ujumla na *National Housing*. Sisi tunahesabu hata *apartment* ni nyumba kwa sababu sasa hivi tunatoa *unit tittle* hata kwenye *apartment.* Kwa hizi 4,000 ni pamoja na zile za biashara kubwa kubwa na zile ndogo ndogo, siyo kwamba hizi zote ni

nyumba za gharama nafuu. Na hayo mauzo ni ya pamoja, hatuna mfuko wa nyumba za shilingi milioni 52 na nyumba za shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kutenganisha hapa hiyo si rahisi sana kwasababu kazi hii tunafanya pamoja, na ni kweli kwamba ujenzi wa nyumba zile za gharama kubwa ndio unatoa faida ya ku-*subsides* hizi ndogo. Yaani ile faida wanayoipata kutokana na zile nyumba wanazouza kwa gharama kubwa pale mjini Dar es salaam ndiyo inatoa faida ya kuja kupunguza gharama ya hizi ndogo; kwa sababu tofauti ya *National Housing* na mashirika mengine kama *NSSF* na *PPF,* wale wengine wanajengea pesa zao wanazo, hawa wanakopa benki. Wale wanakusanya kila mwezi wanajenga, hawa wanakopa benki, kwa hiyo, wanakopa benki kwa *interest* ile ile ambayo hata mtu ungetaka kujenga kwa mkopo ungekopa. Kwa hiyo, lazima wakope benki warudishe mkopo sasa ule mkopo wanahamisha tu kwenda kwa mteja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Ndassa hili swali, nitashindwa kutenganisha hapa mahesabu lakini nataka nimhakikishie kwamba hizi *units* 4,000 ni zote pamoja, zile za maghorofa, zile *apartment*s zote pamoja na nyumba za chini. Kwa hiyo, hata gharama ya uwekezaji wa hizi Nyumba ndogo ndogo hapa sinayo lakini akipenda zaidi baadae kwa ufahamu wake naweza nikamjulisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waziri, Mheshimiwa Ndassa umeridhika?

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nimuombe mbele ya safari kwa sababu katika maelezo yake hizi shilingi bilioni 133.82 amejumuisha katika nyumba 1,483 na hakusema katika nyumba hizi ni zile za bei ya chini au za bei ya kati au namna gani kwa hiyo ni vizuri siku nyingine Mheshimiwa Lukuvi, ili kuondoa maswali basi mchanganuo uwepo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, mimi niliuliza kuhusu suala la vifaa vya kupimia ardhi. Mimi nimpongeze Waziri kwamba katika maelezo yake na vile vitabu alivyotupa imewekwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado naendelea kusisitiza ni muhimu sana vifaa hivi vya kupimia ardhi badala ya kukaa tu kwenye Kanda, iangaliwe namna kwa Halmashauri kwa mfano ya kwangu ambayo ina migogoro mingi sana, iweze kupatiwa kwa dhamana tutumie ili tumalize migogoro iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulikuwa na mradi ule wa kupima hati miliki za vijiji; zile za kimila, hati nyingi tumeshindwa kutoa kutokana na vile vifaa vya ofisini vya ku-*print* na kuandaa zile hati kuwa ni tatizo. Lakini pia tukitaka kutoa ramani kubwa leo watu wa Babati inabidi waende Arusha kwenye ofisi za watu binafsi kwa ajili ya kwenda kutoa zile ramani kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekeza kwamba kuwe na *set* nzima, hii ya kupimia pamoja na hizi za ofisini ili kuongeza ile kasi ya kwenda kupima viwanja, hii miji tunayosema, pamoja na kuwa tutakuwa na mpango wa kutumia watu binafsi inawezekana Halmashauri zingine hatutakuwa na uwezo wa kulipia gharama hizo, kwa hiyo yale maeneo ambapo Halmashauri itaweza au watu binafsi twende kwa kasi ya pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti lakini muhimu pia kutumia *satellite imaging*, tukitumia *satellite imaging* hata ule udanganyifu uliopo pia utakuwa unapotea. Na elimu hiyo ikitolewa kwa wananchi migogoro mingi; na leo Serikali inatoa mabilioni ya shilingi kwenda kulipa fidia katika maeneo ambapo tunatarajia kuweka miundombinu kwa mfano, barabara au ujenzi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakishasikia jambo hilo linakuja wanaenda kujenga nyumba na wanaweka miradi huko Serikali inakuja kulipa fidia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa *speculators* tukishakuwa na hii *satellite imaging* na zile picha wananchi wakishaelimishwa suala hilo la fidia pia itakuwa tunapunguza gharama kubwa.

Kwa hiyo, mimi naomba suala hili la vifaa pamoja na kwamba mtaweka kwenye kanda mimi naamini kwamba ikija kwenye Kanda hii ya kwetu ya Kaskazini, Wilaya ya Babati ikishaenda kuazima vile vifaa wengine hawatapata fursa kwasababu zitakaa muda mrefu sana Babati kwenda kumaliza ile migogoro baina ya wawekezaji na wananchi, vijiji na vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ipo mingi lakini pia kama tunavyosema hii miji midogo tunataka kupima, hata kwenye vijiji wanastahili kupimiwa.

Kwa hiyo, tunaomba kwamba suala la vifaa lipewe kipaumbele na wale amba watakuwa na nia ya kukopa basi Wizara itudhamini ili tuweze kununua vifaa vya kisasa. Leo hii hata ule upotoshaji unaofanywa na watu wengi kwamba *GPS* ipo tu hata kwenye sehemu zetu kuna *GPS* pia elimu itolewe, *GPS* hizi hakuna namna unatumia kwenye kupima viwanja, ile ni *end to end* lazima…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jitu Soni alikuwa anachangia, *anyway*, Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa kwa hoja zake. Ni kweli kama walivyozungumza wachangiaji wengi. Gharama ya upimaji ni kubwa sana na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi zilikuwa kubwa, lakini kama mnavyokumbuka mwaka jana tulipunguza gharama za upimaji kwa zaidi ya asilimia 60. Mnajua mwaka jana ilikuwa shilingi 800,000 kupima ekari moja, lakini tumepunguza sasa ni shilingi 300,000, hiyo ni hatua ya kwanza lakini bado tunaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmshauri nyingi hazina uwezo wala hazina hivi vifaa lakini hata wapima wenyewe sehemu nyingine hakuna. Mkiangalia kwenye hiki kitabu kidogo mtagundua sasa hata namna ya upimaji tumerahisisha sana. Wizara yangu imeshaweka alama nyingi sana katika maeneo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkisoma hivi vitabu mtajua kila Wilaya na vijijini huko kuna alama nyingi tumezijenga ambazo zitasaidia sana upimaji na kurahisisha kwa kutumia *GPS*. Mkiangalia hapa mtagundua kwenye kitabu hiki, kiasi cha fedha ambazo tumepewa na aina ya vifaa tumeainisha humu tunavyonunua na kuweka kwenye Kanda. Itarahisisha sana kwa sababu vituo ambavyo vitawasiliana na hivi vipimo katika kurahisisha upimaji tumeshaviweka katika kama Wizara nchi nzima, kitabu hiki mikikisoma vizuri mtaona alama za msingi zinavyoonekana nchi nzima katika mikoa yenu ambazo zinasaidia katika upimaji.

Kwa hiyo, tumeamua kuweka hivi vifaa kwenye Kanda kwa sababu tunajua kwenye Halmashauri nyingine hata wapima hawapo, lakini sisi kwenye kanda tumeweka wapima. Pia sasa hivi tunataka kushirikisha na wataalam vijana binafsi wanaojiajiri. Tuna vyuo vya Tabora, Morogoro tunafundisha *techniacians*. Vikundi hivi wanaweza kufanya kazi hizo lakini kununua hivi vifaa hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo vifaa hivi tutawaazimisha Halmashauri bila malipo, lakini tutawapa na vikundi vyote ambavyo vinataka kuharakisha upimaji wa halmashauri kwa kadri ya maombi ya Halmashauri, ili mradi tu kwamba vifaa hivi vipatikane kwenye Kanda na Halmashauri zinazohudumiwa na Kanda hiyo zisikwame. Tunafikiri ni haua moja kubwa Mheshimiwa Jitu Soni ungetuunga mkono; hii ni hatua kubwa kwamba sasa angalau vifaa viko pale karibu. Kwa mfano, Kanda hii ya hapa Dodoma inahudumia mikoa miwili, Dodoma na Singida. Vifaa vitakuwa hapa, kwa hiyo, Wilaya yoyote itakayohitaji

vifaa vya upimaji, hata kuazima kuazima wapimaji wa Kanda waje kwenye hiyo Wilaya tutafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Jitu Soni nataka kukwambia kwamba hatua ya kwanza ni hii lakini vifaa hivi vitatumika. Tuliona si busara sana kupeleka mpaka Wilayani, kwanza ni hela nyingi lakini pia hatuna uhakika na Halmashauri zetu kama zina wataalum wa kutosha, sisi kwenye Kanda tunao. Kwa hiyo, tumieni huduma hii na sisi itatusaidia kwasababu kadri tunavyozalisha zaidi viwanja na maeneo yaliyopangwa ndivyo Serikali inavyopata mapato. Kwa hiyo, na sisi tuna *interest* ya kuzalisha maeneo mengi yaliyopangwana kupimwa ili Serikali iendelee kumilikisha na kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hayo yote tunafikiria sasa, ni kweli pale Babati kwa mfano, unapotoka, tumechelewa sana mpaka sasa tumepewa karibu hati 2,000 lakini watu wameshalipia zaidi ya 5,000. Kuna masuala ya *Deed Plan* na mengine. Tunajirekebisha kidogo kuweka utaratibu ambao utaharakisha utoaji wa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambieni kwenye kitabu changu nimeandika, siku ambapo wewe umepewa kiwanja, umelipia ada zako zote, nataka baada ya siku 30 uwe umepeta hiyo hati na waliokwa wanabisha sasa nimetangaza nimewaandikia kwenye kitabu, nina majina 4,800 kwenye mtandao watu waliokuwa wanatupa hizi hati Wizarani pale halafu wanakuja kusubiri baada ya mwaka, sasa nawatangaza kwenye mtandao waje wachukue hati zao, mimi sina pa kuziweka ziko 4,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale sasa hivi kuna chumba nimekifunga kuna hati watu wametoka wameenda Ulaya huko, wanakuja likizo ya mwakani kuulizia hati maana walizoea hati ni miaka miwili, leo ni mwezi mmoja. Mahali popote Wilayani itatoka na mambo yote yanaishia kwenye Kanda. Kanda pale ndiyo kuna Kamishna ndiyo anayegonga muhuri, pale kuna Msajili. Kwa hiyo, ndugu zangu hizi hatua tutazichukulia maanani na naomba mtuunge mkono.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu umeridhika?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimshukuru Mheshimiwa Waziri, na mara nyingi kwasababu yale ambayo huwa anayasema huwa anatekeleza. Muhimu tu nataka *commitment* moja kwamba hajajibu suala la juu ya Halmashauri zetu kupatiwa vifaa vya ofisini, hata kwa mkopo. Hati miliki hamtatoa ninyi Wizara, hati miliki tunatoa sisi Wilayani. Sasa mngetupatia vile vifaa vya ofisini. Mimi kwangu nadaiwa hati zaidi ya 19,000, ni kutoa zile *copy*. Sasa mngetudhamini tu hiyo tupate vile vifaa nina uhakika kazi yetu itakuwa ni nafuu na siyo Wilaya yangu tu Wilaya nyingi zina matatizo hayo.

Kwa hiyo mbali na ile moja ya kupima ninaamini utatufanikishia, lakini pia katika ofisi zetu mtusaidie ili kazi hii iende kwa haraka na pia mapato ya Halmasahauri zetu na Serikali Kuu itaongezeka. Nikipata hiyo *commitment*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya kutolea hati, hati zile vifaa ghali zaidi ni karatasi hizi ambazo zinaitwa *crested papers* tunatoa sisi nchi nzima bure, wala hamnunui ninyi. Ninyi pale mnaandika tu yale majalada vifaa muhimu kama hivi tunawasaidia, hata kupata *Deed Plan.* Mtaalam wangu alikuja Babati pale kushirikiana na Halmashauri yako ya Babati ili kuhakikisha kwamba zile *Deed Plan,* vile vikaratasi vile vya *blue* vile vya mchoro ndiyo vinavyochelewesha lakini hivyo navyo dawa yake inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mtu yoyote, mahali popote, Halmashauri isikwame kwa sababu ya vifaa vya kutolea hati, hivi vifaa tunavyo Wizarani, tunavichapa wenyewe, tunavisafirisha wenyewe, tunavileta kwenye Halmashauri na havilipiwi. Sawa sawa na hizo *computer* na *printer* tulizozileta kwa ajili ya kuweka mtandao wa ulipaji wa kodi, tumegharamia wenyewe. Kwa hiyo, kama unazungumzia vifaa hivi tunaimarisha zaidi ili angalau tufanye kwa haraka zaidi utoaji wa *Deed Plan* lakini hizi karatasi tunazitoa, rasilimali zipo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea, Mheshimiwa Lwakatare Wifred Muganyizi.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiwasilisha hoja ya Kambi ya Upinzani nilielezea tatizo la fidia kwa wananchi ambao wananyang'anywa ardhi au ardhi inachukuliwa kwa ajili ya miradi au *projects* mbalimbali za maendeleo ambazo zinakuwa zimebuniwa. Na nilitoa mfano wa matatizo ambapo na Mheshimiwa Waziri wakati akijumuisha hapa na Naibu wake nilitoa mfano wa eneo la Kifungwa katika Kata ya Kahororo kule Bukoba Manispaa. Lakini pia nilitoa mfano wa Burugu katika Mkoa wa Manyara na maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wameyazungumzia ambayo yana matatizo ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika majibu na maelezo yaliyoelezwa hapa nakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri amesema jukumu la kulipa fidia si la Wizara ya Ardhi, bali kuna mamlaka husika ya maji inapaswa kulipa fidia. Lakini pia Mheshimiwa Waziri akaeleza kwamba kuna wataalam wake ambao

wanaondoka hivi karibuni kwa ajili ya kwenda kutatua matatizo ya viwanja 5,000; pia naamini na tatizo hili la uthamini wa watu wa Kifungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningeomba kabisa Mheshimiwa Waziri anifafanulie na anitolee maelezo yafuatayo, ili tuondoke katika mgogoro huu:-

Kwanza nataka kujua kwamba ni lini hasa tatizo hili la fidia litamalizika na watu kulipwa pesa yao? Isije ikawa hata hao anaowatuma wanakwenda kule kupiga bla-bla wanakwenda na pesa? *(Makofi)*

Pili, sheria imetueleza hapa haipaswi kuzidi miezi sita, watu walipwe. Sasa mimi ninafikiri ili niweze kuruhusu huu mshahara wa Mheshimiwa Waziri anipe majibu yaliyojitosheleza, yasiyo ya kupindapinda. Nadhamiria kutoa shilingi iwapo kwa kweli majibu hayatanitosheleza.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ni mdogo wangu na anatoka katika eneo nililoanzia kazi za Serikali. Nilikuwa Mkuu wa Wilaya pale na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare akiwa Afisa Utumishi wangu wa Halmashauri ya Mji wa Bukoba, kwa hiyo, anazungumza anachokijua. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Wilfred Lwakatare nataka nikuhakikishie kwamba, ninachokwenda kukifanya mimi, nimekwambia, kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu amepata malalamiko ya watu 5,000 wananchi wako wa Bukoba ambao katika mradi wenu ninyi mlishirikisha *UTT* mkapima viwanja, nasikia fidia hawajaridhika na *CAG* alifanya ukaguzi na taarifa zilikuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunakuja sisi, tumetumwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kufanya hayo, kuhakiki hawa 5,000 wana haki au hawana haki? Na kama walikuwa na haki watalipwa lini na mamlaka iliyowakopa ni Halmashauri. Maana Halmashauri imeshauza viwanja na ni kiasi gani wanatakiwa walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, timu yangu na ndiyo maana nimemtuma *Chief Valuer,* halafu ni kijana wa kwenu, huyo mama ni wa kwenu. Kwa hiyo, aje huko awaambie wale wananchi wana haki, hawana haki, wana haki kiasi gani? Na wale waliouza viwanja waseme watawapa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la Kahororo rafiki yangu huu uthamini kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, hili eneo lilitwaliwa na Mamlaka ya Maji ya Bukoba. Na kwa wakati huo ilikuwa fidia inatakiwa shilingi bilioni moja na milioni mia tisa. Tutakuja, nitamuagiza *Chief Valuer* akaangalie hali halisi ya sasa, fidia ni kiasi gani na ni watu wangapi. Sasa wewe sijui ni Mjumbe wa Bodi ya Maji, lakini kwa sababu ni shirika lenu tutazungumza nao watupe ratiba ya

kulipa kwa sababu sio mimi nitakayelipa, watalipa Shirika la Maji la Bukoba, ila mimi nitakuja kuwahakikishia wale wananchi hesabu gani wanaidai kwa uhakika. Lakini wewe na mimi sasa tushirikiane tuwabane, *Chief Valuer* atakuja kuwabana Halmashauri yenu ili waweke tarehe na *commitment* kwangu kwamba, watalipa lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo katika maeneo mbalimbali, huko unakosema Babati ulikotolea mfano ni Halmashauri vilevile imechukua viwanja, lakini angalau wao wameweza kulipa fidia kwa wakati. Na ndiyo maana nimetoa *a blanket statement,* nimesema kwa mujibu wa sheria mamlaka yoyote inayochukua ardhi kwa ajili ya maendeleo, kama eneo lina wenyewe inatakiwa ilipe fidia. Na baadaye nikawapoza kidogo wananchi ambao hawajalipwa fidia katika maeneo mbalimbali, wajue kwamba wameweka hela benki kwa sababu sheria yao hii inawalinda, kila baada ya miezi kadhaa kama hawajalipwa watalipwa pamoja na *interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Lwakatare wale watu watakuja. Kwa hili la viwanja 5,000, watakuja kuangalia hili eneo lililochukuliwa na *BUWASA*, lakini kama kuna mambo mengine mna mashaka nayo watumieni kwa sababu na Mkurugenzi wa TAMISEMI anakuja, Kamishna wa Ardhi anakuja, *Chief Valuer* anakuja. Kama kuna migogoro mingine pale Bukoba inayohusiana na ardhi watumieni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombo langu la mwisho, ushauri wa bure ambao hukuniuliza, Mji wa Bukoba umejaa. Unasikia Mheshimiwa Lwakatare, Mji wa Bukoba umejaa, zungumza na Dkt. Haule ile Bukoba Vijijini na ile Wilaya nyingine mkubaliane namna ambavyo Bukoba inaweza ku-*expand.* Miji yote inameza vijiji kwa hiyo, tafuteni vijiji vya jirani vile mtengeneze mpango tuwatengenezee mpango mwingine, ile Bukoba mmebanana mno haitoshi. Huo ni ushauri wa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado shilingi nimeishikilia katika mfuko wa mkono wa kulia kwa sababu gani, mimi namshukuru kwa hatua na jitihada ambazo amezielezea hapa ambazo Serikali na Wizara yake inataka kuzichukua. Lakini katika hoja yangu sikuzungumzia Bukoba tu, nimezungumzia maeneo mbalimbali ambayo yamekumbwa na kadhia hii ya kutolipwa fidia. Na hoja yangu hapa, inaonekana Wizara mfumo wake wa kutatua matatizo ni wa kuchukua vipande vipande, hakuna *policy* ambayo imesimama ambayo itawahakikishia watu kuwa wanalipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo Arusha kuna matatizo ya *compensation* kwenye barabara. Hata ile barabara inayojengwa na *East*

*African Community* kule Arusha kwa Mheshimiwa Nassari, bado watu wanadai fidia yao.

Sasa mimi nataka kujua Wizara imejipangaje katika kukabiliana na hili? Kwa hiyo, mimi naendelea kutoa shilingi, *unless* ananieleza kwamba inakwendaje? Na ninatoa hoja, Waheshimiwa mniunge mkono katika kushikilia shilingi hii. Natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ametoa hoja, imeungwa mkono. Tuchukue wachache tu. Tunaanza na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, niiunge hoja ya Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. Anachokiongea Mheshimiwa Lwakatare sio cha Bukoba Mjini na Mheshimiwa Waziri umeelekeza eneo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nitolee tu mfano, suala la fidia limekuwa ni changamoto kubwa sana. Hata wakati natoa mchango wangu hapa nimesema, fidia hazilipwi! Lakini kwenye Wizara mbalimbali nayo imekuwa changamoto, kwa mfano tu, uwanja wa ndege hapa Msalato, watu walifanyiwa tathmini mwaka 2011 wananchi 980 wanadai shilingi bilioni tatu, hawajawahi kulipwa mpaka leo, halafu mnakuja tu na maneno hapa mepesi mepesi ya bla-bla kwa nini mnatufanyia hivi? Tunataka kauli ya Serikali, ni nini mkakati wenu wa kulipa fidia ya Watanzania nchi nzima na sio maneno yasiyokuwa na maana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MH. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Suala hapa inaonekena kuna tatizo kubwa la kutokuwa na sera endelevu na za uwazi. Itikadi wakati wa Mwalimu Nyerere, ukirejea hotuba ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 1974, *May Day* siku ya Jumatano, anawaambia Watanzania kwamba wafanyakazi mnamgomea nani wakati mali hizi, ardhi na mashirika ya umma yote ni ya wakulima na wafanyakazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ubinafsishaji kulikuwa hakuna sera ya uwazi na endelevu ambayo inatoa haki kwa wote. Sasa itikadi ni ipi hapa, ni ya ujamaa au ni ya ubepari kwamba kila Mwenyezi Mungu ni wetu sote na kila mtu ni wake. Sasa kwa kuwa Serikali haina sera ambayo ni endelevu ya kutoa fidia na huku wanazungumzia uwekezaji, huku wanazingumzia haki kwa Watanzania, mnasimamia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, afadhali muwe wa kweli, muwe wawazi kwamba hakuna sera na ndio maana migogoro ipo nchi nzima. Kwa hiyo, ni vyema sasa mkawa na sera endelevu ambayo ni ya uwazi na mnasimamia nini

ili Watanzania wajue wanasimamia lipi, kama ni mashirika, kama ni biashara, kama ni nini la sivyo, itakuwa mahali popote migogoro, migogoro, migogoro tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana naunga hoja ya Mheshimiwa Lwakatare mkono, ili mambo haya yawe wazi kabisa na sasa ni lini sera hiyo itakuwepo na Watanzania wote ambao wanahitaji fidia ambayo ni haki yao kwa maendeleo ya Taifa letu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kabla hatujaendelea nitumie mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 104(1), niongeze muda wa nusu saa tuweze kuendelea na shughuli muhimu hii. Tunaendelea, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri amesema maelezo yafuatayo, nanukuu; "Mamlaka yoyote inayochukua ardhi wametakiwa watoe fidia."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli nzuri sana kwa Mheshimiwa Waziri. Lakini kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, kwamba fidia ni lazima mamlaka ambayo inachukua ardhi iweze kutolewa na kwa wakati, lakini kinachosikitisha ni kwamba Serikali kwanza imekuwa na mtindo wa kuwanyang'anya tu ardhi wananchi, huo ndio ukweli ulivyo. Kwa sababu wananchi hawana ubavu, hawana uwezo. sisi ndio wawakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano mdogo tu, mimi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mwinyi yule yuko pale mbele, unamuona pale anachekacheka, Serikali haitoi fedha, maeneo kadhaa yamechukuliwa na Jeshi la Wananchi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahonda na wewe unajua, mpaka leo wanaogopa hata kwenda. Na baadhi ya wananchi na watoto wao wameshakufa miaka na miaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itwambie sasa, itoe *commitment* hapa, ina mkakati gani wa ziada wa kutoa fidia kwa maeneo ambayo wameyachukua? Mtuambie sasa, mbali ya sera, fedha mnazo, mambo ambayo ninyi mnazihitaji mbona mnatoa fedha? Toeni fedha za fidia.

Mheshimiwa Wilfred Lwakatare umetoa hoja nzuri, hoja safi kabisa. Naungananae Mheshimiwa Lwakatare. Serikali mtuambie mkakati wenu wa ziada wa kutafuta fedha mahali popote kuweza kutoa fidia kwa maeneo mnayoyachukua kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe fedha, wasibabaishe. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lwakatare katika mambo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza Mheshimiwa Waziri ni suala la ninyi Wizara ya Ardhi kukaa na Wizara ya Maliasili kuona ni jinsi gani na kuangalia mipaka ile ya wananchi. Mfano suala la Tarangire nimelisemea muda mrefu sana, lakini *solution* ilikuwa rahisi kwamba ukae na Mheshimiwa Maghembe mmalize lile suala kwa sababu hata kwenye vitabu vyako ulivyoviandika hapa suala la *Galapo Estate* ni ekari chache sana kati ya ekari 17,000 ambazo zinatakiwa, lakini hamkai. Siku nyingi mmesema mnakaa, hamkai na ninaamini maeneo mengi kuna matatizo ya hifadhi na wananchi, mngekaa mngemaliza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la *retention* ya asilimia 30. Katika Halmashauri zetu hata zile pesa ambazo zinakusanywa na maeneo ya kwenye Idara ya Ardhi, zile pesa Wizara yako pia hairudishi kule. Unasema kwa kauli yako, mamlaka ambayo imesababisha hayo ilipe, Halmashauri walipe. Hivi inawezekanaje waliosababisha matatizo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, tunaongelea fidia. Hoja ya Mheshimiwa Lwakatare…

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niliweke sawa tu. Ninazungumzia Kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba mamlaka husika walipe, lakini hao ndio wamesababisha hawajalipa na mfano mzuri unafahamu Halmashauri yangu ya Babati tunadai kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifikiri Mheshimiwa Waziri, atuambie kwamba, pamoja na mpango mzuri alionao wa kwamba kuanzia sasa hakuna maeneo ambayo yatatwaliwa bila fidia, uwaambie Watanzania, wale ambao wanasubiri fidia kwa muda mrefu wanalipwaje? Hapo hujasema! Kwa sababu Halmashauri hawawezi kulipa walishashidwa.

Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lwakatare, Mheshimiwa Waziri kuna kitu bado hujatwambia. Unafanya nini kuhusu hizi pesa zilipwe na Halmashauri wameshashindwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwathibitishia Watanzania kwa ujumla kwamba kila miradi tunayoijenga iwe ya barabara, viwanja vya ndege, bandari au reli, suala la fidia ni la lazima kwa mujibu wa sheria. Kinachotokea kama ambavyo fedha hizi zinatokana na kodi zetu, tunajenga kutokana na kodi zetu, kama ambavyo tunashindwa kumaliza barabara zote kwa wakati mmoja

ndivyo hata suala la fidia tunashindwa kulimaliza kwa wakati mmoja na hilo ndio tatizo linalotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kila mwaka tunakuwa na bajeti ya kulipa fidia. Hakuna mahali ambapo tunajenga barabara, viwanja vya ndege, bandari ama reli bila kulifikiria suala la fidia, isipokuwa kwa mfano kwa upande wa barabara, tulijiwekea sheria wenyewe kwamba kuna kiwango ni cha hifadhi ya barabara na tunawaomba wananchi wasiingie katika hifadhi ya barabara. Eneo hilo ndilo tulilo na tatizo kubwa. Kwamba, kuna wengi wanaifuata barabara ndani ya hifadhi, hao hawastahili kulipwa fidia kwa mujibu wa sheria tuliyokubaliana sisi wenyewe humu. Lakini mara nyingi sisi wawakilishi wao tunakuwa mstari wa mbele kuwaombea walipwe fidia wakati hawastahili kulipwa fidia na hapo ndipo migogoro mingi katika suala la barabara ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nilieleze hilo na kwa kweli, mpango upo kwa maana ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kumsihi kaka yangu *entare ya kibeta* Lwakatare urudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri tufanye kazi. Mojawapo ya Wizara zinazodaiwa ni Wizara yangu, inadaiwa karibu shilingi bilioni 200 kulipa fidia. Lakini nikubali nukuu aliyoisema Mheshimiwa Mbatia alipomkumbuka Baba wa Taifa kwamba unagoma unamgomea nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba tunataka uwekezaji, ningependa kutengeneza maeneo ya uwekezaji nchi nzima, sasa unaponinyang'anya eneo akija mwekezaji nimuweke wapi? Unagoma unamgomea nani? Na ndiyo maana tunahangaika, sera inasemaje? Sera inasema tutakulipa. Kama sikukulipa leo, baada ya miezi sita nitakulipa *eight percent,* lakini gharama ikiwa kubwa unagoma unamgomea nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sera endelevu tunayo, lakini wawekezaji tunawataka, maendeleo tunayataka. Sisi wenyewe vijana wetu tunataka kuwapa maeneo, umenipa eneo niweke eneo la uwekezaji, anatoka sekondari mwanao, Mujulizi anatoka sekondari utamuweka wapi? Lazima tumpe eneo. Ukisema ooh, bei ni kubwa liondolewe, litaondolewa, utamuweka

wapi? Atacheza *pool,* ataendesha pikipiki. Nichukue fursa hii Mheshimiwa Lwakatare, *entare ya kibeta,* nikuite tena ndugu yangu rudisha shilingi twende mbele, aje atutengenezee *Special Economic Zone* Omukajunguti na yenyewe msidai fidia.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena kumsihi Mheshimiwa Lwakatare, mimi najua kwenye kile kinyonyi *(flash disc)* nimewapa Sheria ya Ardhi, zote mbili. Eeh, kinyonyi, kwa kiswahili nimeambiwa inaitwa kinyonyi *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Eeeh, kweli!

**MWENYEKITI:** Sema *flash,* inatosha. Tuendelee *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeandikiwa hapa, kinyonyi! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tuendelee. Mheshimiwa Waziri endelea!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti sasa kwenye *flash* mle nimewapa Sheria Namba 5 na 4 za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ile namba 4; *section* ya 3 utaona kabisa masuala ya fidia yamejieleza wazi. Hakuna ubishi, inaeleza kabisa utaratibu unapochukua ardhi ya mtu ufanyaje. Sasa jambo hili Mheshimiwa Lwakatare unasema utaratibu gani na sera gani; tulikuwa hatujalifikisha mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo ambacho kilipaswa kusimamia utaratibu na kujenga nidhamu ya utoaji na ulipaji wa fidia tulikuwa hatujakiunda. Hatujaikamilisha ile sheria kwa kuunda Bodi ya Fidia. *This time around* kwenye *budget speech* yangu nimesema sasa naunda chombo huru, Bodi ya Fidia ambayo itaratibu na kusimamia utaratibu wote wa fidia, na ndiyo maana kwa mara ya kwanza tumeitengea shilingi bilioni tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi hii kwanza itaratibu madeni yote hayo na fidia yote inayodaiwa lakini ndiyo itakayosimamia kazi za kila siku za Mdhamini Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba hakuna tena watu kutwaa maeneo ya maendeleo au ya shughuli nyingine bila kulipa stahili kwa mujibu wa sheria hii ya ardhi kifungu kidogo cha tatu. Kwa hiyo, ninachosema tunachokuahidi Mheshimiwa Lwakatare ni kwamba kile kitu kilikuwa kinakosekana ni chombo kilichoundwa kwa sheria ile cha kuratibu na kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama bodi itakataa kuidhinisha fidia hii mpaka wale waliofanyiwa tathmini walipwe, bodi hii ndiyo yenye meno na yenye madaraka, ilikuwa haijawahi kuundwa. Ukisoma kitabu changu safari hii ndiyo nimeamua kuiunda. Kwa hiyo, bodi hii itanisaidia sana katika kusimamia haki na kuratibu shughuli zote za fidia katika nchi hii.

Kwa hiyo, ndugu yangu pamoja na sera ya ardhi, kama kuna udhaifu wa kisera ambao Mheshimiwa Mbatia umeuona tuweke kwenye sera hii ya ardhi kwa sababu sera hii ndiyo iliyozaa sheria hii na iliyotunga Sheria hii ya Fidia, kifungu hiki cha tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kwanza uamini bodi inaundwa *immediately* kwa sababu safari hii nina fedha. Tangu kifungu hiki kilipoanza mwaka 1999 hatujawahi kuunda bodi, mwaka huu ndio tunaunda bodi, na kwa nini tumeweka na pesa? Tunataka sasa bodi hii isimamie ili mambo haya yasiendelee. Kwa hiyo, ndugu yangu ninakuambia tutaitimiza sheria hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare unarejesha shilingi?

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu na kumpenda sana kaka yangu Waziri Lukuvi. Lakini hivi vinyonyi inategemea vina maziwa kiasi gani, vinginevyo tunaweza tukajikuta tunanyonya damu. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa mimi niseme hivi, kimsingi hapa tunachozungumzia ni mfumo endelevu. Leo anaongea Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake, kesho kutwa huyu anakuwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingi inayozungumzwa hapa na mbwembwe, na nini na kinyonyi chake na kabrasha la mabegi ni mikakati binafsi inayoonekana kufanywa na Mheshimiwa Lukuvi. Hapa tunachohoji ni mfumo endelevu ulioandaliwa kwa mapana yake sio kwa Lukuvi tu, na anavyoongoza Wizara kama Lukuvi. Ni mfumo ambao umepangwa kisera na ni mfumo endelevu ambao ni wa kinchi ambao hata mwingine akija kesho na kesho kutwa ni kwamba tunapita katika *roadmap* hiyo hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili hapa suala la fidia ni suala la sheria na miongozo mbalimbali inayotolewa. Sheria ipo ya kwamba watu wafidiwe ndani ya kipindi cha miezi sita. Na katika mwongozo wake imeelekezwa kwamba taasisi yoyote, kampuni yoyote, Wizara yoyote inapopanga *project* lazima ihakikishe ina pesa ya kulipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kwamba bodi anazungumza itakuwepo lakini sasa Wizara hii ndiyo wakati wote watu wakivunja sheria na kuvunja miongozo wanatangulia kubomoa, wanabomoa tu. Sasa mnataka na wananchi miezi sita ikipita nao watafute lami ya kubomoa? Na kitu watakachotumia ni kuibomoa Serikali kwa kura zao kwa kutotekeleza kile ambacho wanaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa mimi nimependa na nimefurahi pamoja na kwamba *tv* haioneshi lakini watu hawalali wanafuatilia hoja hii, sasa wamewaona Wabunge wa CCM wanaolia kwa machozi ya mamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote katika kuchangia hapa kila mmoja amedai matatizo ya fidia kwa watu wake, lakini watu hawakuunga mkono hoja hii sasa nataka, Watanzania wanakuambia ukielezwa na wewe tumia akili ya kwako kichwani, mmewaona walivyo! *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi niombe tu kwamba nimuombe Mheshimiwa waziri na watu wake, hebu jaribu kuturidhisha ili tusimamie suala hili kwa misingi ya mfumo endelevu ambao utawahakikishia watu kwamba wanalipwa pesa zao. Na kwa kuanzia watu wote wanaodai hivi sasa hebu huu mfuko wako wa fidia uanze kuwaona kwa jicho la kutimiza haki ili waweze kulipwa fidia yao. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru kwa kurudisha shilingi. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze tu kwa kusema kwamba nchi yetu hii haina matatizo ya sheria, nchi yetu hii haina matatizo ya sera, lakini kila mwaka Bunge linapitisha bajeti zake na kila bajeti inayopita imeeleza mambo mengi sana mazuri. Tatizo sio sera, tatizo sio mambo mazuri, tatizo sio maelezo mazuri ya Waziri, tatizo la nchi hii ni kutekeleza yale ambayo yanaandikwa na yale ambayo yanaahidiwa, hilo ndilo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hapa wakati anahitimisha hoja zake amezungumza mambo mengi sana mazuri. Na miongoni mwa mambo hayo amesema ya kwamba Serikali kama Serikali hivi sasa ina mkakati wa kuhakikisha kwamba inapanga maeneo yote ya miji lakini sio tu kupanga, maeneo yote yanapimwa lakini kubwa zaidi maeneo yote yanamilikishwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri anipe ni lini Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi itarasimisha rasmi maeneo mengi ya miji ambayo yanaitwa *squatter* ambayo wananchi wameachwa wakijenga maeneo yale, lakini mwisho wa siku yanakuja yanabomolewa na Halmashauri ama na Serikali?

Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni lini utaratibu huu utaanza kutekelezwa kwa vitendo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu Mbunge wa Mtwara Mjini nataka nikuhakikishie kwamba tumeshaanza. Nimezindua programu ya kitaifa ya urasimishaji pale Kimara, lakini Mheshimiwa Halima Mdee umesikia hapa leo akisema na ni mwenzako yule wa UKAWA kwamba niko Chasimba kule, watu ambao walikuwa wamekaa hawana matumaini kwa miaka yote sasa wameanza kuona matumaini, wameanza kumilikishwa hati zao lakini nilikwambia hata wewe nje nakuja na Mtwara. Sasa unapotoa shilingi unataka unitolee nauli yangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimesema hapa; ninao mkakati wa kurasimisha nchi nzima. Wataalam wa kurasimisha ni wa Halmashauri, hamna uwezo kwa sababu wataalam hao hawapo. Mimi nafundisha vikundi kazi na kampuni zile binafsi tuje kupanga na kupima lakini na urasimishaji ili twende kwa kasi.

Pili nimeomba hapa kila mji unaoiva iva vimji vidogo vidogo hivyo mvipangie mipango ili nivitangaze tuviwahi, tuvipime na kuvipanga mapema badala ya kuacha watu mpaka wame-*squatter* halafu ndiyo tunakuja kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini nataka kuhakikishia nimeshaanza na nitapiga hodi na Mtwara nije niwafundishe watu wako na watu wangu wapima wako pale, unaye mpima mzuri pale, ili niwafundishe watu wa Mtwara na Mtwara ni mji pekee nataka kurasimisha haraka kwa sababu hata ile *master plan* naizindua hivi karibuni na mimi nimekusaidia hapa fedha kumalizia ile *master plan* ya Mtwara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Nachuma!

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Kazungumza hilo suala zima la *master plan* lakini Mtwara Mjini kwa kiasi kikubwa maeneo yamejengwa bila kufuata utaratibu kwa maana ya kwamba wananchi wameachwa wakijenga, lakini

Halmashauri hii hii ambayo ni mwakilishi wa Serikali ndio wanaokuja na kuwaambia wananchi kwamba wamevamia maeneo yale wakati wamewaacha wakijenga bila kuwapa utaratibu na bila kuwapimia yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazungungumza hapa juu ya *master plan,* lakini nisikitike tu kwamba niliuliza swali hapa katika Bunge hili la Kumi na Moja katika Kikao kile cha Kwanza, swali linalohusu kwamba ni lini Mtwara Mjini watafanya huu urasimishaji. lakini nasikitika mpaka leo swali langu hilo halijajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe tu kwamba na nipate majibu ya kutosha kutoka kwa Waziri na kama sipati kwamba Mtwara Mjini ni tarehe ngapi wataanza urasimishaji huu, kwa sabau wananchi wamekuwa wakiishi katika mazingira ambayo ya kiutata na wanaambiwa siku yoyote wanaweza wakabomolewa. Naomba nipate majibu ya uhakika kwamba ni tarehe ngapi urasimishaji huu utaanza kwa sababu amezungumza tu juu ya *master plan...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante! Hujatoa shilingi, tunataka maelezo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *master plan* na urasimishaji ni vitu viwili tofauti. Nimekuhakikishia kwamba nakuja Mtwara lakini nakuja miji yote kwa sababu si Mtwara tu iliyoharibiwa, miji yote imeharibiwa, ina *squatters* kila mahali. Lakini nimekuahidi Mbunge wa Mtwara Mjini nakuja Mtwara kwa sababu hatuwezi kuwa na *master plan* pale halafu kunakuwa na *squatter.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimekuhakikishia yote mawili. *Master plan* itaanza kutumika lakini zoezi la urasimishaji tunakuja kuanza kufanya. Hata hivyo ujue kwamba kazi hii ni kazi yako wewe na Halmashauri yako. Sasa ungefurahi tu kwamba mimi Waziri sasa nachukua hela yangu ya Wizarani kuja Mtwara kuja kukusaidia kazi ya urasimishaji. Ila kukuondoa hofu nawaagiza watu wa Mtwara wasiendeleze hilo zoezi la kuvunja mpaka nitakapofika mimi kuwafundisha namna ya kurasimisha hayo maeneo. Hilo nakusaidia. Sasa usiondoe shilingi! *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*………...Sh. 777,092,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud!

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina jambo dogo tu kwa rafiki yangu Waziri Lukuvi. Kwenye kifungu hicho, *item* ya 221400 – *Hospitality Supplies and Services* ambayo kwa mara hii kuna shilingi 37,570,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2015/2016 ilikuwa ni shilingi 17,200,000 mara hii kuna ongezeko la shilingi 20,000,000. Na utetezi wa randama wa Serikali unasema fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017 itatumika kuhudumia vikao vya kazi vinavyoratibiwa na kitengo na kutoa zawadi kwa wafanyakazi bora ongezeko la tengeu limetokana na fedha za *Food and Refreshment* zilizokuwa zikitengwa kupitia kifungu fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa yote haya ongezeko la shilingi 20,000,000 zote hizi na mambo na makando kando mengine yote, na mnasema kwamba mnapunguza matumizi, hebu tuambie Mheshimiwa Waziri ambaye leo naona haujapata kazi kubwa kutokana na kazi yako iliyo na nafuu. Tuambie shilingi 20,000,000 zote hizi za *Food and Resfreshment* ni za nini?. Naomba ufafanuzi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, za nini? Si imeelezwa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza msemaji alivyouliza, kifungu hiki ni kweli kimetengwa kwa ajili ya shughuli zlizozitaja na ukiangalia kwa mwaka 2015/2016 ilikuwa ni shilingi 17,200,000 lakini fedha zilizotengwa kwa mwaka huu ni shilingi milioni 37 kwa sababu pia ongezeko sasa hivi litatumika katika vikao vya kazi. Na hapa tunapongalia shughuli zilizoko mbele yetu ni kubwa zaidi ambazo zinahitaji kuwa na vikao vya mara kwa mara kuhakikisha tunayoyapanga, migogoro inayokwenda kufanyika lazima watu wakae, wafanye maandalizi kwa ajili ya kwenda kuhudumia. Kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba ongezeko hili linategemeana pia na kazi ambayo iko kubwa mbele yetu kwa ajili ya kuweza kushughulikia masuala yaliyoko katika ufumbuzi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 – *Policy and Planning*……..............Sh. 653,380,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 – *Management Information System*……..................Sh. 641,120,000

**MWENYEKII:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kupata ufafanuzi kwenye *item* 221200 – *Communications and Information.* Kwa mwaka huu kuna shilingi 204,400,000 mwaka uliopita, mwaka 2015/2016 kulikuwa na shilingi 245,000,000. Na randama inasema hizi fedha zitatumika kulipia huduma ya mawasiliano ya *internet* pamoja na kulipia huduma ya simu, tengeu hili limeongezeka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya vituo makusanyo vitakavyounganishwa kwenye mtandao wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati kwenye makusanyo hayo na maeneo ambayo yataunganishwa kwenye mtandao wa Wizara, ongezeko la maeneo na shilingi 60,000,000 mimi nataka kujua tu ni maeneo yapi? Tuambie zaidi tu, utupe ufafanuzi, ni maeneo yapi ambayo mtandao wenu mtakwenda na ongezeko la shilingi 60,000,000 hizo ambazo tayari zimeongezeka. Ni hilo tu, dogo tu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu kama aliyosema tutaongeza maeneo yapi nadhani katika hotuba ya Waziri amezungumzia pia tuna panua wigo kwenye maeneo ya kanda na huu mradi ambao tunakwenda kuufanya utakwenda kufunga vifaa kwa ajili ya mawasiliano hayo ambayo yataongeza pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa vyovyote vile ili uweze kuwa na uhakika na kile kinachofanyika na hasa katika usimamizi mzima wa utawala wa ardhi lazima mfumo huu uweze kupanuka kwenda kwenye Halmashuri zetu lakini katika ngazi ya Kanda na itashuka pia katika Halmashauri kwa sababu mwanzo tunaanzia kwenye Kanda. Kwa hiyo, lazima gharama itakuwa kubwa tu kwa sababu ni vifaa ambavyo ni vya gharama na viko *more technical* katika utumiaji wake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*……………..Sh. 364,388,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management unit*……………………..Sh. 434,060,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*……………….Sh. 352,120,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*…………...........Sh. 432,820,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 – *Land Administration Division...*Sh. 13,348,824,000

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti mimi nadhani sisi wajibu wetu ni kuishauri na kuisimamia Serikali na kwenye kifungu hiki *item* ya 220100 fedha hizi ambazo zimetengwa mara hii ni shilingi 29,800,000, fedha za mwaka jana 2015/2016 ni shilingi 282,800,000.

Sasa Mheshimiwa Waziri wakati akijibu akasema *crested papers* ni jambo dogo tu lakini kwenye maelezo ya ziada mtanunua *computer*, kuna *stationery* na mambo mengine. Sasa ongezeko la shilingi milioni 140; hasa Mheshimiwa tuambieni, Serikali itupe ufafanuzi wa ziada kwamba baada ya *crested papers* na *stationeries* na *computers* na uchambuzi wake shilingi milioni 140, hebu Waziri tutoe wasiwasi hapa la ongezeko hili la shilingi milioni 140. Tupe ufafanuzi wa kina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kama inavyoonekana hapo kwamba hivi vifaa vitanunuliwa, lakini tukumbuke pia wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha, lengo pia la idadi ya hati ambazo tunategemea kwamba zitatolewa kwa kipindi hiki zimekuwa nyingi zaidi. Tumeweka lengo kubwa la kama 400,000 lakini pia tujue kwamba tulikuwa na lengo la 40,000 kipindi kilichopita, lakini sasa hivi zitakuwa nyingi zaidi. Kwa hiyo gharama pia hata hiyo ya *crested paper* na hizi *cartridge* zinazoongelewa zitakuwa ni nyingi, na hivi vifaa vyote vina bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata alivyozungumza kwamba kwenye Halmashauri vinakwenda bure, si bure kwa maana hiyo kwa sababu huku tayari tutakuwa tumeshaingia gharama. Kwa hiyo, unapoongeza idadi ya hati na gharama zinakuwa ni kubwa na vifaa hivi vyote ni kwa ajili ya utoaji wa hati pia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Kifungu kinaafikiwa?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Haimuhusu hiyo.

**MWENYEKITI:** Kifungu hicho kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 – *Survey and Mapping Division*…………………..............Sh. 4,310,060,000
Kifungu 2003 – *Registration of Titles Unit*…..........Sh. 980,774,000

Kifungu 2004 – *Valuation Unit*……….............Sh. 830,518,000
Kifungu 2005 – *Dar-es-Salaam*
*Zone*…………………….……..........…Sh. 505,000,000
Kifungu 2006 – *Eastern Zone*………..…............Sh. 400,000,000
Kifungu 2007 – *Central Zone*……..………...........Sh. 365,000,000
Kifungu 2008 – *Western Zone*……………............Sh. 410,000,000
Kifungu 2009 – *Lake Zone*………….……..……...Sh. 685,000,000
Kifungu 2010 – *Nothern Zone*…….………..........Sh. 595,000,000
Kifungu 2011 – *Southern Zone*…..………............Sh. 270,000,000
Kifungu 2012 – *Southern Highlands*
*Zone*……….……….......................Sh. 480,000,000

Kifungu 3001 – *Rural and Town Planning*
*Division*……..................................Sh. 2,721,571,000
Kifungu 3002 – *Housing Division*…….…….........Sh. 2,039,646,000
Kifungu 3003 – *District Land and*
*Housing Tribunal Unit*……….....Sh. 3,521,666,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati, sasa tunaingia kwenye kipindi cha *guillotine.*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 – *Administration and HR*
*Management*……….................Sh. 800,000,000
Kifungu 2001 – *Land Administration*
*Division*……………..…............Sh. 18,200,000,000
Kifungu 2002 – *Surveys and Mapping*
*Division*…….……........…….......Sh. 1,000,000,000
Kifungu 3002 – *Housing Division*……………....................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, mtoa hoja, taarifa!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limepitia Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kifungu kwa kifungu bila mabadiliko yoyote. Naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2016/2017 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nathibitisha kwamba Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 yamepitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ndio tumefika mwisho wa safari yetu tuliyoianza tangu jana kwenye Mafungu haya mawili… aah, Jumamosi kweli!

Niwashukuruni sana kwa kazi nzuri muliyofanya kuanzia mtoa hoja mwenyewe, Naibu Waziri na timu yao ya wataalam, lakini pia sasa na michango yenu iliyowezesha hayo yote leo kuhitimishwa kwa sura tuliyoiona.

Mheshimiwa Waziri na timu yako mmepewa idhini ya Bunge ya kwenda kutumia. Ahadi ni nyingi, lakini kipindi cha miezi 12 sio kipindi kirefu. Niwatakie kila la heri katika utekelezaji wa shughuli zenu.

Sina matangazo na kwa vile tumefanya kazi vizuri, mimi sina la ziada isipokuwa kutamka kwamba sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.25 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 24 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*